# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Office of the Controller and Auditor General, Samora Avenue, P.O. Box 9080, DAR ES SALAAM.
Telegram: "Ukaguzi", Telephone: 255(022)2115157/8, Fax: 255(022)2117527,
E-mail: ocag@nao.go.tz, Website: www.nao.go.tz

Kujibu tafadhali taja ;
Kumb. Na.FA.27/249/01/2016/2017 Tarehe, 27-03-2018

Mh. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 9120,
1 Barabara ya Barack Obama,
**11400 DAR ES SALAAM.**

**YAH: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, ninayo heshima kuwasilisha kwako taarifa yangu ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali ya Mitaa kwa mwaka 2016/2017 kwa taarifa na hatua zaidi.

Naomba kuwasilisha,
Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu Za Serikali,**
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vimeainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) kama ilivyofafanuliwa zaidi na vifungu vya 45 na 48 vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

**Dira ya Ofisi**
Kuwa kituo cha ubora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma.

**Lengo La Ofisi**
Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji ili kupata thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Misingi ya Maadili**
Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

- ✓ **Kutopendelea:** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
- ✓ **Ubora**: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
- ✓ **Uadilifu:** Ofisi ya Taifa ya kaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
- ✓ **Zingatio kwa Wadau**: Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamanduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo, weledi na ari ya kazi.

- ✓ **Ubunifu:** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo kutoka ndani na nje ya taasisi.
- ✓ **Matumizi bora ya rasilimali**: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake

# YALIYOMO


Orodha ya Majedwali ........ 5
Orodha ya Viambatisho ........ 9
DIBAJI ........ 11
SHUKRANI ........ 13
MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA TAARIFA YA JUMLA YA UKAGUZI ........ 14
SURA YA KWANZA ........ 24
1.0 USULI ........ 24
SURA YA PILI ........ 30
2.0 HATI ZA UKAGUZI ........ 30
SURA YA TATU ........ 37
3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA ........ 37
SURA YA NNE ........ 43
4.0 MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE ........ 43
SURA YA TANO ........ 54
5.0 UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ........ 54
SURA YA SITA ........ 62
6.0 TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI NA MASUAL YA UTAWALA ........ 62
SURA YA SABA ........ 69
7.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA ........ 69
SURA YA NANE ........ 86
8.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO NA MIRADI MINGINE ........ 86
**SURA YA TISA** ........ 102
9.0 USIMAMIZI WA MIKATABA NA MANUNUZI ........ 102
SURA YA KUMI ........ 163
10.0 USIMAMIZI WA MATUMIZI YA UMMA ........ 163
SURA 11 ........ 201
11.0 USIMAMIZI WA MAPATO ........ 201
SURA YA KUMI NA MBILI ........ 221
12.0 USIMAMIZI WA MALI ........ 221
SURA YA KUMI NA TATU ........ 227
13.0 UKAGUZI MAALUM ........ 227
SURA YA KUMI NA NNE ........ 247
14.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 247
VIAMBATISHO ........ 268

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1-1: Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa mwaka wa Fedha 2016/2017 .... 25
Jedwali Na. 2-1: Mamlaka za Serikali za Mitaa na aina ya Hati ya ukuguzi ............. 34
Jedwali Na. 2-2: Muhtasari wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa katika makundi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ............................................................................ 34
Jedwali Na. 2-3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne mfululizo ............................................................ 35
Jedwali Na. 2-4: Halmashauri zenye hati yenye mashaka kwa zaid ya miaka mitatu mfululizo ........................................................................................ 36
Jedwali Na. 3-1: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka iliyopita. .................................................. 39
Jedwali Na. 3-2: Orodha ya Halmashauri zenye Mapendekezo yasiyotekelezwa yaliyotolewa wakati wa Ukaguzi Maalum kwa kipindi cha miaka mitano iliyofuatana .. 39
Jedwali Na. 3-3: Mwenendo wa Majibu ya Serikali Kuhusiana na Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ......................... 40
Jedwali Na. 3-4: Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Halmashauri ........................................................................................ 40
Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa makusanyo ya mapato ikilinganishwa kulingana na bajeti ........................................................................................ 44
Jedwali Na. 4-2: Mwenendo wa Makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ........................................................................ 45
Jedwali Na. 4-3: Mwenendo wa fedha za maendeleo ambazo hazikupokelewa .......... 49
Jedwali Na. 4-4: Mwenendo wa fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikupokelewa ........................................................................................ 49
Jedwali Na. 4-5: Mwenendo wa Ruzuku ya matumizi ya kawaida isiyotumika ........... 51
Jedwali Na. 4-6: Mwenendo wa Ruzuku ya maendeleo isiyotumika ....................... 51
Jedwali Na. 4-7: Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 zilizokuwa na bajeti ya ziada ........ 52
Jedwali Na. 5-1: Mwenendo wa Wadaiwa na malipo ya kabla ya huduma ya muda mrefu kwa miaka Minne mfululizo ........................................................... 55
Jedwali Na. 5-2: Mwenendo wa madeni ya muda mrefu .................................... 56
Jedwali Na. 5-3: Mapato yaliyoonekana katika daftari la mapato na matumizi lakini hayakuonekana katika taarifa za kibenki ................................................... 58
Jedwali Na. 5-4: Makosa yaliyoonekana katika Taarifa ya Fedha .......................... 59
Jedwali Na. 6-1: Ubadhirifu uliobainishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ........... 68
Jedwali Na. 7-1: Mwenendo wa idadi ya watumishi kwa miaka mitatu mfululizo. ...... 70
Jedwali Na. 7-2: Idadi ya maafisa waliokuwa wakikaimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mpya ambazo zimeanzishwa ........................................................ 71
Jedwali Na. 7-3: Orodha ya Halmashauri na idadi ya wafanyakazi wanaolipwa mishahara chini ya 1/3 ya mshahara wa kila mwezi ...................................................... 73
Jedwali Na. 7-4: Mwenendo wa watumishi waliopokea mshahara chini ya 1/3 ya mshahara wa kila mwezi kwa miaka mitatu iliyopita ................................................... 74
Jedwali Na. 7-5: Upimaji usioridhisha wa utendaji wa watumishi wa umma katika Namlaka za Serikali za Mitaa ............................................................... 75
Jedwali Na. 7-6: Taarifa za watumishi zisizo timilifu katika mfumo wa utumishi (HCMIS) ........................................................................................ 77

Jedwali Na. 7-7: Madai ya mishahara na Madai mengine ya wafanyakazi wa halmashauri ........ 78
Jedwali Na. 7-8: Kuchelewa uidhinishaji wa wafanyakazi wenye sifa za kupanda madaraja na uboreshaji wa mshahara ........ 80
Jedwali Na. 7-9: Makato ya kisheria kwa wafanyakazi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ........ 81
Jedwali Na. 7-10: Tozo kutokana na kutowasilisha makato ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ........ 82
Jedwali Na. 7-11: Mishahara imelipwa kwa watumishi ambao hawapo kazini. ........ 83
Jedwali Na. 8-1: Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo .... 87
Jedwali Na. 8-2: Fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo hazikutumika ........ 88
Jedwali Na. 8-3: Miradi ambayo haijakamilika ........ 90
Jedwali Na. 8-4: Kiasi ambacho hakikuchangiwa kwenda katika mifuko ya Wanawake na Vijana ........ 93
Jedwali Na. 8-5: Mikopo Iliyotolewa kwa wanawake na vijana ambayo Haijarejeshwa 95
Jedwali Na. 8-6: Ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu ambayo haikupelekwa ngazi za chini ........ 98
Jedwali Na. 8-7:Muhtasari wa hali ya miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari ........ 100
Jedwali Na. 9-1: Gharama za manunuzi zilizofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitatu ........ 103
Jedwali Na. 9-2: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikufuata Sheria ya Manunuzi .... 104
Jedwali Na. 9-3: Kiwango cha uzingatiaji wa sheria ya manunuzi kwa kipindi cha miaka miwili ........ 105
Jedwali Na. 9-4: Udhaifu katika Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Manunuzi ... 106
Jedwali Na. 9-5: Mapungufu yaliojitokeza kwenye vitengo vya manunuzi na Bodi ya Zabuni ........ 107
Jedwali Na. 9-6: Orodha ya Serikali za mitaa zilizofanya manunuzi pasipo ushindani. 110
Jedwali Na. 9-7: Mwenendo wa manunuzi pasipo ushindani ........ 111
Jedwali Na. 9-8: Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni ........ 111
Jedwali Na. 9-9: Mwenendo wa manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni kwa miaka mitatu inayofuatana ........ 112
Jedwali Na. 9-10: Halmashauri zilizofanya Councils that Procured Goods and Service from Unapproved Supplier ........ 113
Jedwali Na. 9-11: Mwenendo wa manunuzi yaliyofanyika kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa ........ 114
Jedwali Na.9-12: Mamlaka za serikali za mitaa zilizofanya manunuzi kwa njia ya masurufu ........ 115
Jedwali Na.9-13: Ununuzi wa bidhaa na huduma kwa fedha taslimu ........ 116
Jedwali Na.9-14: Serikali za Mitaa zilizopokea bidhaa bila kukaguliwa ........ 117
Jedwali Na.9-15: Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizonunua bidhaa, kazi na huduma nje ya mpango wa manunuzi ........ 118
Jedwali Na.9-16: Mwenendo wa manunuzi nje ya mpango kwa miaka mitatu ........ 119
Jedwali Na.9-17: Halmashauri zilizolipia bidhaa ambazo hazijapokelewa ........ 120
Jedwali Na.9-18: Matengenezo ya magari bila idhini ya TEMESA ........ 121

Jedwali Na. 10-1: Mapungufu katika matumizi yanayojirudia kwa miaka miwili inayofuatana ........ 164
Jedwali Na. 10-2: Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mara ya kwanza zinazohitaji kuboresha mifumo ya udhibiti ya ndani ........ 167
Jedwali Na. 10-3: Orodha ya aina ya matumizi yasiyofaa ........ 169
Jedwali Na. 10-4: Malipo yasiyostahili Sh.Tz 769,479,797 ........ 171
Jedwali Na. 10-5: Malipo batili na yasiyokuwa na manufaa Sh.Tz 1,011,974,990 ........ 172
Jedwali Na. 10-6: Halmshauri ambazo zilitolewa taarifa ya kukosekana kwa hati za malipo. ........ 176
Jedwali Na. 10-7: Halmashauri zilizofanya manunuzi bila yasiyoambatana na risiti za kieletroniki ........ 177
Jedwali Na. 10-8: Kodi ya zuio ambayo haikukatwa Sh.Tz 156,244,852 ........ 178
Jedwali Na. 10-9: Madeni ya Miaka Iliyopita Ambayo Hayakulipwa Katika Mwaka Husika ........ 179
Jedwali Na. 10-10: Halmashauri zilizofanya matumizi nje ya bajeti na zilizobadilishiwa matumizi ya fedha kwa kiasi kikubwa ........ 181
Jedwali Na. 10-11: Uhamisho wa ndani wa Fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa ........ 182
Jedwali Na. 10-12: Halmashauri zenye kiasi kikubwa cha madeni kwenye akaunti za amana ........ 183
Jedwali Na. 10-13: Malipo yaliyofanyika bila kibali sahihi ........ 184
Jedwali Na. 10-14: Halmashauri zenye malipo makubwa yasiyo na viambata muhimu 186
Jedwali Na. 10-15: Matumizi yaliyolipiwa kwenye vifungu visivyo ........ 187
Jedwali Na. 10-16: Malipo yaliyofayika bila ukaguzi wa awali. Sh. Tz 2,182,095,636 . 188
Jedwali Na. 10-17: Mapungufu katika kutoa na kurejesha masurufu ........ 191
Jedwali Na. 10-18: Mamlaka zenye matumizi Zaidi ya mafuta ........ 193
Jedwali Na. 10-19: Changamoto za mfumo wa usimamizi wa fedha ........ 195
Jedwali Na. 10-20: Mapato ya ndani ambayo hayakupelekwa kutekeleza miradi ya maendeleo ........ 197
Jedwali Na. 10-21: Fedha zisiohamishwa kwenda idara husika ........ 200
Jedwali Na. 11-1: Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuwasilishwa na Mawakala ........ 201
Jedwali Na. 11-2: Mwenendo wa makusanyo ya mapato ambayo hakuwasilishwa na mawakala kwa miaka minne mfululizo ........ 203
Jedwali Na. 11-3: Mwenendo unaoonesha vitabu ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi kwa miaka minne mfululizo ........ 206
Jedwali Na. 11-4: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye vitabu vilivyokosekana ........ 206
Jedwali Na. 11-5: Leseni za biashara ambazo hazikukusanywa ........ 207
Jedwali Na. 11-6: Maduhuli ambayo hayakupelekwa Benki kwa wakati Sh.Tz 296,798,267 ........ 208
Jedwali Na. 11-7: Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zisizo na Daftari la mapato ........ 210
Jedwali Na. 11-8: Fedha ambazo hazikukusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ........ 211
Jedwali Na. 11-9: Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki ........ 212
Jedwali Na. 11-10: Orodha ya Makusanyo ya ardhi yasiyopelekwa Wizarani ........ 214
Jedwali Na. 11-11: Mwenendo wa kodi iliyokusanywa bila kuwasilishwa Wizarani ........ 215

Jedwali Na. 11-12: Orodha ya idadi ya kampuni zisizokusanya kodi ya huduma........ 215
Jedwali Na. 11-13: Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zisizokuwa na sheria ndogo za mapato........................................................................... 216
Jedwali Na. 11-14: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye mfumo wa LGRCIS usio na Ufanisi ........................................................................................ 218
Jedwali Na. 11-15: Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye upungufu wa machine za kieletroniki (POS) ............................................................... 220
Jedwali Na. 12-1: Idadi ya Halmashauri zisizotunza daftari la mali la kudumu ......... 223
Jedwali Na. 12-2: Ardhi na Majengo yasiyo na Nyaraka za Umiliki ........................ 224
Jedwali Na. 12-3: Idadi ya Halmashauri zenye magari yasiyokua na Bima ............... 225
Jedwali Na. 12-4: Orodha ya halmashauri zenye mali zisizo na namna ya utambulisho ........................................................................................ 226
Jedwali Na. 13.0-1: Kiasi ambacho hakikusuluhishwa kwenye vitabu vya hesabu kufikia 30 Juni, 2017 SH.TZ 3,075,198,442.10 ........................................................ 237
Jedwali Na. 13.0-2: Tofauti kati ya salio halisi la Benki Kuu na salio kwa mujibu wa barua ya OR-TAMISEMI kwenda kwa Mamlaka za serikali za mitaa ................................ 238
Jedwali Na. 13.0-3: Masuala ambayo hayakufanyiwa usuluhishi katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki ............................................................................ 240

## Orodha ya Viambatisho


Kiambatisho Na.2:1: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Hati inayoridhisha .......... 268
Kiambatisho Na.2:2: Halmashauri zenye hati yenye shaka na isiyoridhisha pamoja na misingi ya hati hizo .......... 270
Kiambatisho Na 2:3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne mfululizo .......... 293
Kiambatisho Na.2:4: Mamlaka za Serikali za Miataa yenye masuala mengine yanayoambatana na hati ya Ukaguzi .......... 303
Kiambatisho Na.3:1:Utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya jumla .......... 306
Kiambatisho Na.3:2: Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyosalia kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa .......... 307
Kiambatisho Na.3:3: Hali Halisi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa .......... 312
Kiambatisho Na.4:1: Ulinganishi wa mapato ya ndani dhidi Bajeti iliyoidhinishwa .... 317
Kiambatisho Na.4:2:Makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na matumizi ya kawaida .......... 323
Kiambatisho Na.4:3: Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani .......... 328
Kiambatisho Na.4:4: Mchanganuo wa makusanyo ya mapato unaoonesha ziada ya mapato yakilinganishwa na bajeti .......... 334
Kiambatisho Na.4:5: Fedha za ruzuku ya maendeleo zilizopokelewa zaidi ya bajeti .. 335
Kiambatisho Na 4:6: Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa zaidi ya bajeti .......... 336
Kiambatisho Na 4:7: Fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo hazijapokelewa .......... 337
Kiambatisho Na 4:8: Fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazijapokelewa .......... 343
Kiambatisho Na 4:9: Fedha za ruzuku ya kawaida ambazo hazikutumika .......... 347
Kiambatisho Na.4:10: Fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo hazikutumika .......... 349
Kiambatisho Na.5:1: Wadai na malipo yaliyofanyika kabla ya huduma yaliyokaa muda mrefu SH.TZ 138,907,446,027.......... 356
Kiambatisho Na 5:2: : Mamlaka za Serikali za mitaa zenye madeni ya muda mrefu SH.TZ 165,562,212,375 .......... 359
Kiambatisho Na 5:3: Idadi ya kesi zilizo mahakamani kwa kila Halmashauri .......... 362
Kiambatisho Na 5:4: Bakaa ya fedha na thamani ya mtandao wa barabara zilizochukuliwa na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini .......... 369
Kiambatisho Na 6:1:Mapungufu katika mifumo ya TEHAMA na Uhasibu .......... 377
Kiambatisho Na 6:2: Mapungufu katika Mazingira ya Jumla ya Mfumo wa Teknolojia ya Habari .......... 378
Kiambatisho Na.6:3: Utendaji usioridhisha wa Kamati za Ukaguzi .......... 381
Kiambatisho Na 6:4: Mapungufu katika utendaji kazi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani .......... 384
Kiambatisho Na 6:5: Mapungufu katika uanzishwaji wa Kitengo cha Kusimamia Vihatarishi. .......... 389
Kiambatisho Na.6:6: Mapungufu katika mpango wa kuzuia na kukabiliana na ubadhirifu .......... 391
Kiambatisho Na 7:1:Upungufu wa watumishi .......... 395
Kiambatisho Na.7:2: maafisa wanaokaimu nafasi za uandamizi kwa muda mrefu ..... 399
Kiambatisho Na 8:1: Miradi ambayo haijatekelezwa .......... 401

Kiambatisho Na 8:2: Miradi iliyokamilika lakini haitumiki TZS 782,468,997 ............ 404
Kiambatisho Na 8:3: Mapungufu yaliyoonekana wakati wa utekelezaji wa miradi ..... 406
Kiambatisho Na 8:4: Mamlaka za serkali za mitaa zilizobainisha changamoto katika kutekeleza sera ya elimu bila malipo ........................................................ 409
Kiambatisho Na 9:1: Manunuzi ya bidhaa, ushauri na huduma ............................ 412
Kiambatisho Na 9:2: Orodha ya Halmashauri zenye mapungufu katika uzingatiaji wa sheria za manunuzi. ............................................................................ 416
Kiambatisho 10:1:Madhaifu katika matumizi yanayojirudia kwa miaka miwili inayofuatana ................................................................................... 419
Kiambatisho Na 10:2: Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa stakabadhi za mfumo wa kieletroniki Sh. 7,421,735,182 ................................. 422
Kiambatisho Na 10:3: Matumizi yasiyokuwa katika bajeti na fedha zilizobadilishiwa matumizi Sh. 4,658,384,441 ................................................................ 423
Kiambatisho 10:4: Mikopo kutoka akaunti ya Amana isiyorejeshwa Sh. 5,611,768,190 ..................................................................................................... 424
Kiambatisho Na 10:5: Malipo yasiyotambulika katika Akaunti ya Amana Sh. 8,388,155,073 ..................................................................................................... 425
Kiambatisho Na 10:6: Malipo bila kuwa na viambata muhimu Sh. 5,362,908,811 ...... 427
Kiambatisho Na 10:7: Utunzaji wa Rejesta za Amana na Masurufu wenye Mapungufu 429
Kiambatisho 10:8: Mapungufu yaliyobainishwa katika kutunza masurufu Sh. 2,081,629,305 ...................................................................................... 433
Kiambatisho Na 10:9: Mapungufu katika matumizi ya mafuta Sh. 685,641,980 ......... 436
Kiambatisho Na 10:10: Mapokezi Pungufu ya Fedha za Ruzuku za Shule Sh. 1,930,944,815 ..................................................................................................... 437
Kiambatisho Na 11:1: : Fedha ambazo hazikukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani Sh. 12,191,753,217.78 ............................................................... 439
Kiambatisho Na 13:1: Kiasi ambacho hakikusuluhishwa kwenye vitabu vya hesabu kufikia 30 Juni, 2017 ....................................................................... 446
Kiambatisho Na 13:2: Kiasi ambacho hakikusuluhishwa kwenye kiasi salia cha benki kwa mamlaka za serikali za mitaa ..................................................... 451

## DIBAJI




Ninawasilisha ripoti hii kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2005) inayonitaka nifanye ukaguzi angalau mara moja kwa kila mwaka na kutoa ripoti katika masuala ya hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na maafisa wote wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na hesabu zote zinazosimamiwa na karani wa Bunge. Kifungu Na. 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma wa mwaka 2008 na Kanuni Na.88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma wa mwaka 2009 vinanitaka niwasilishe ripoti jumuifu ya Ukaguzi kwa Rais kufikia tarehe 31 Machi kila mwaka, ambapo, baadaye huwasilishwa Bungeni kupitia Waziri mwenye dhamana (mwenye dhamana ya tawala za mikoa na Serikali za Mitaa).

Ripoti hii imejumuisha matokeo muhimu ya Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za mitaa, hasa kwenye tathmini na uchunguzi wa taarifa za fedha pamoja na kumbukumbu zake, udhibiti wa mifumo ya ndani taratibu, pamoja na michakato ya manunuzi na kufuata sheria na kanuni. Pia, inajumuisha matokeo ya Ukaguzi Maalumu uliofanywa na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka ya nyuma na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2016/2017.

Kufuatia Ukaguzi uliofanyika, maoni ya ukaguzi yametolewa kwa Mamlaka za serikali za mitaa zipatazo 185 ambazo zilikaguliwa, na nimeweka wazi katika maoni hayo kama taarifa za kifedha zinaonesha mtazamo wa kweli na wa haki kwa mujibu wa viwango vilivyopitishwa vya kimataifa vya mfumo wa uaandaaji taarifa wa hesabu katika sekta ya umma.

Ukaguzi ulifanyika kulingana na Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) iliyotolewa na Viwango Mahususi kwa Ukaguzi wa Taasisi za Umma vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC) ambazo ni muhimu kwa ajili ya ukaguzi wa sekta za umma. Ofisi yangu

imekuwa ikifanya kazi kitaalamu ili kuonesha umuhimu wake kwa wananchi, Bunge na wadau wengine.

Ninaamini kwamba, Matokeo na mapendekezo yaliyojumuishwa katika ripoti hii, yakitekelezwa yataboresha sana shughuli za serikali katika utoaji wa huduma, hivyo kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika serikali na sekta za umma.

Prof. Mussa Juma Assad,
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**
**Machi, 2018**

## SHUKRANI

Ofisi mbalimbali, watu binafsi na wafanyikazi wamechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha kufikia malengo ya Ofisi yangu kutimiza mamlaka ya kikatiba kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake ya kila mwaka kwa Rais kabla ya mwisho wa mwezi Machi kila mwaka.

Mahsusi nathamini mchango mkubwa na endelevu toka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli kwa Ofisi yangu.

Rasilimali; fedha, mfumo na watu ni muhimu sana kufanikisha jitihada za taasisi nzima, hivyo imenilazimu nitoe shukrani zangu kwa Bunge na kamati zake kwa jitihada za dhati kuhakikisha rasilimali zinapatikana kwenye Ofisi ya Ukaguzi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/18. Kwa hali yoyote ile mafanikio yasingepatikana bila kuwepo kwa ushirikiano na juhudi zilizoratibiwa na Wizara ya Fedha na Mipango, mimi ni nani napaswa kushukuru.

Pia, natoa shukrani kwa uongozi wa taasisi zilizokaguliwa kwa ushirikiano wao wakati wa kipindi cha ukaguzi, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Washirika wa Maendeleo katika kuhakikisha kuwa ofisi inapata fedha ili iweze kutimiza majukumu yangu ya kikatiba.

Mwisho, ni lazima nitambue kazi kubwa iliyofanywa na wafanyakazi wangu kwenye ngazi zote kuanzia wakaguzi hadi wafanyakazi wasio wakaguzi. Kwamba ninaweza kusimama na kuzungumzia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ni kwa sababu tu wakaguzi walioenda kwenye ukaguzi walipata msaada mkubwa kutoka kwa wafanyakazi wasio wakaguzi, wakati mwingine hufanya kazi katika mzingira magumu sana na kufanya kazi yao kwa kiwango cha juu na kuwasilisha rasimu ya taarifa yao kwa wakati.



Prof. Mussa Juma Assad

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**MACHI, 2018**

## MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA TAARIFA YA JUMLA YA UKAGUZI

### Utangulizi

Ripoti hii ni tamko langu juu mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 , Ukaguzi maalum uliofanyika katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya pamoja na ukaguzi maalum unaondelea wa usuluhishi wa kiasi salia na kiasi sawa cha fedha za Mamlaka za serikali za mitaa 46 zilizounganishwa na mfumo wa malipo ya TISS uliopo TAMISEMI-DODOMA Muhtasari huu unaangazia mambo yalitokana na ripoti zangu pamoja na barua za mapungufu nilizozitoa kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### Hati za Ukaguzi

Inatia moyo kwamba idadi ya Hati za Ukaguzi zinazoridhisha imeongezeka kutoka 138 sawa na asilimia 81 kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia 166 (90%) kwa mwaka 2016/2017 na idadi ya Hati zenye shaka imepungua kutoka 32 (19%) mwaka 2015/2016 mpaka 16 (8%) kwa mwaka 2016/2017. Ingawa, idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati zisizoridhisha imeongezeka kutoka moja sawa na asilimia 1 mwaka 2015/2016 mpaka tatu sawa na asilimia 2 mwaka 2016/2017. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata Hati isiyoridhisha ni Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Hatua za haraka zinahitajika kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ambayo imepata Hati Isiyoridhisha kwa miaka mitatu mfululizo. Aidha, kuwapo uangalizi wa karibu kwa Halmashauri za Wilaya za Longido, Rombo, Korogwe na Ukerewe ambazo zimepata hati yenye shaka kwa miaka mitatu mfululizo au zaidi.

### Mambo muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi

Kwa muhtasari, nimebainisha maeneo muhimu yanayohitaji kutazamwa kwa ukaribu na Umma, Serikali, Bunge na uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ambapo mapendekezo katika kasoro zilizobainika na athari zilizobainishwa na kufafanuliwa kwa

kina katika Sura za ripoti hii zirekebishwe kwa juhudi na kwa wakati.

i. **Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa miaka ya nyuma**

Taarifa ya Jumla ya Ukaguzi ya mwaka 2015/2016 ilikuwa na jumla ya mapendekezo 14 yaliyokuwa yakihitaji ufuatiliaji wa Serikali tangu 2013/2014. Majibu ya Serikali yalipokelewa tarehe 10/07/2017 kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali; ambapo, hakuna mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu, mapendekezo tisa (64%) yalikuwa yanaendelea kutekelezwa; na mapendekezo matano (36%) hayakushughulikiwa kabisa.

Sambamba na hilo, kati ya mapendekezo 12,703 niliyoyatoa kwenye ripoti 171 za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2015/2016, mapendekezo 4,262 (34%) yalitekelezwa; 3,024 (24%) yalikuwa yakiendelea kutekelezwa; mapendekezo 3,206 (25%) hayakushugulikiwa kabisa na mapendekezo 2,211 (17%) yalipitwa na wakati.

Hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika ripoti iliyopita inaonesha kwamba; kati ya maagizo 748 yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, maagizo 233 (31%) yalitekelezwa, maagizo 256 (34%) yapo katika hatua za utekelezaji na maagizo 259 (35%) hayajatekelezwa. Aidha, sijapokea taarifa ya Serikali ya utekelezaji wa maagizo ya LAAC katika mwaka 2015/2016.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yanayohusiana na Kaguzi maalum umebaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 39 zilizofanyiwa kaguzi maalum bado hazijatekeleza mapendekezo 628 yasiyo na thamani na mapendekezo yenye thamani ya jumla ya Sh. Tz 172,322,765,827; baadhi yake ni yaliyoibuliwa toka katika ripoti ya jumla ya mwaka 2013/2014.

Maelezo ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yapo katika Sura ya tatu ya ripoti hii.

ii. **Uchambuzi wa Hali ya Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Mapitio ya hali ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yalibainisha mapungufu yafuatayo:

- Mapitio ya jumla ya utekelezaji wa bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 yameonesha kupungua kwa makusanyo ya mapato ya ndani kwa Sh. Tz 126,428,328,985 sawa na asilimia 20 ya bajeti. Makusanyo halisi yalikuwa Sh. Tz 519,863,656,618 wakati jumla ya matumizi ya kawaida yalikuwa Sh. Tz 4,656,643,395,963. Hii ina maana kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa haziwezi kutekeleza shughuli zake bila ya kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wafadhili.
- Ruzuku ya miradi ya maendeleo ilitolewa zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa Sh. Tz 18,074,193,265 (41%) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 14. Aidha, ruzuku ya matumizi ya kawaida ilitolewa zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa Sh. Tz 82,484,838,958 (9%) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 39.
- Ruzuku ya miradi ya maendeleo ilitolewa pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa TZS 532,214,628,377(51%) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 167. Aidha, ruzuku ya matumizi ya kawaida ilitolewa pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa Sh. Tz 389,708,969,984(15%) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 146.
- Ruzuku ya matumizi ya kawaida ambayo haikutumika hadi mwishoni mwa mwaka ni Sh. Tz 270,132,243,323 (14%) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 75. Aidha, ruzuku ya miradi ya maendeleo ambayo haikutumika hadi mwishoni mwa mwaka ni Sh. Tz 260,847,695,932 (36) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 168.

iii. **Ukaguzi wa Taarifa za Fedha**

Sura tano ya ripoti hii inaangazia kwa muhtasari hoja na mapendekezo yatokanayo na ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kama ifuatavyo:

- Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa sita zilipotoshwa kwa Sh. Tz 50,090,445,925; kwa ujumla wake pamoja na sababu

nyingine. Hii imesababisha kutoa Hati tatu zisizoridhisha na Hati tatu zenye shaka.

- Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mbili, nilibaini mapokezi ya fedha ambazo hazijapelekwa benki kwa kipindi kirefu kiasi cha Sh. Tz 279,707,282.
- Nilibaini miundombinu ya barabara yenye thamani ya Sh. Tz 622,778,967,107 pamoja na bakaa ya fedha taslimu ya Sh. Tz 68,294,093,494 ambayo imetolewa taarifa katika Hesabu za Mwaka 2016/2017 lakini taarifa hizo hazitaonekana katika taarifa za fedha za mwaka 2017/2018 za Mamlaka husika.
- Pia, ilibainika kuwa kuna mashauri 1,111 katika mahakama mbalimbali dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 116 yenye jumla ya madai ya Sh. Tz 186,443,100,559. Kesi nyingi kati ya hizo zinatokana na uvunjwaji wa mikataba kati ya Mamlaka husika na Wakandarasi, kesi za watumishi na migogoro ya ardhi.
- Nimebaini uwepo wa madai kiasi cha Sh. Tz 138,907,446,027 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 161 ambayo hayajakusanywa kwa muda mrefu.
- Pia nimebaini uwepo wa madeni kiasi cha Sh. Tz 165,562,212,375 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 158 ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu ikiwa ni ongezeko la Sh. Tz 9,758,056,955 ikilinganishwa na madeni ya Sh. Tz 155,804,155,420 yaliyoripotiwa katika Taarifa za fedha za mwaka 2015/2016.

**iv. Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na utawala bora**

Hii inaangazia mapungufu yaliyobainika wakati wa tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani ikijumuisha ufanisi mdogo katika Mfumo wa Hesabu (Epicor 9.05), Mazingira yasiyoridhisha ya udhibiti wa mfumo wa TEHAMA, utendaji usioridhisha wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani, utendaji usioridhisha wa Kamati za Ukaguzi, mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi na ukosefu wa tathmini ya masuala ya udanganyifu.

**v. Mapungufu katika malipo ya mishahara na usimamizi wa rasilimali watu**

Udhibiti wa mishahara na usimamizi thabiti wa rasilimali watu ni nguzo muhimu itakayoongeza uwezo na ufanisi wa Mamlaka za

Serikali za Mitaa kuhudumia jamii, ingawa bado kuna kasoro mbalimbali ambazo ni kikwazo kwa Mamlaka hizo kufikia malengo hayo. Yafuatayo ni mapungufu niliyobaini wakati wa ukaguzi:

- Pamoja na juhudi za Serikali za kuhuisha taarifa za mishahara, bado kiasi cha TZS 406,248,481 kililipwa kwa watumishi hewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 29.
- Ilibainika uwepo wa madai mbalimbali ya watumishi kiasi cha TZS 9,868,633,522 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 ambayo hayajalipwa.
- Watumishi wapatao 4,830 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 58 wanapokea chini ya theluthi moja ya mshahara stahiki.
- Hadi kufikia tarehe 30/06/2017, watumishi 8,369 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 hawakupadishwa madaraja licha ya kuwa na sifa zilizotajwa katika Kanuni za Kudumu za Utumishi Umma.
- Tathimini yangu ilibaini upungufu wa Watumishi 155,013 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 161 sawa na asilimia 32 kati ya Watumishi 477,829 wanaohitajika.

**vi. Mapungufu yaliyoonekana katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitekeleza miradi na kazi mbalimbali kupitia ruzuku ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGCDG), Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), Mpango wa Kuimarisha Mamlaka za Miji (ULGSP), Programu ya Kuboresha *Elimu* (EQUIP), Idara ya Kimataifa ya Maendeleo (DFID), Shirika *la* Umoja wa Mataifa *la* Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Elizabeth Glasier la Kupambana na Virusi vya Ukimwi kwa Watoto (EGPAF), Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (P4R) na Programu ya WALTER REED. Mapitio ya utekelezaji huo ulibaini mapungufu yafuatayo:

- Mamlaka za Serikali za Mitaa 4 hazikutekeleza miradi ya maendeleo 50 iliyopangwa kutokana na kupokea fedha pungufu ya bajeti ambapo ni asilimia 49 tu ya Sh. Tz 1,034,122,816,044 zilizoidhinishwa ndizo zilizopokelewa katika Mwaka 2016/2017.
- Miradi ya Maendeleo 25 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 yenye thamani ya Sh. Tz 7,793,272,396 haikutekelezwa licha ya

fedha za miradi hiyo kupokelewa na Mamlaka husika za Serikali za Mitaa.

- Nilibaini miradi 60 iliyokamilika yenye thamani ya Sh. Tz 782,468,997 katika Mamlaka ya serikali za mitaa 13 ambayo haitumiki ipasavyo.
- Katika mwaka huu wa fedha (2016/2017) nimeendelea kubaini kujirudia kwa mapungufu ya miaka ya nyuma ambapo asilimia 10 ya mapato kutoka vyanzo vya ndani kiasi cha Sh.Tz 53,222,719,138 hakikuchangwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 143 kwenda katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Kwa kipindi cha miaka mitano, jumla ya Sh. Tz 149,082,304,735 bado hazijachangwa.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa 76 zilikuwa na jumla ya Sh. Tz 130,684,657,588 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Lakini hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 jumla ya Sh. Tz 48,473,335,881 zilitumika na kusalia bakaa ya Sh. Tz 82,461,355,743 sawa na asilimia 63.
- Nimebaini kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa 37 hazikuchangia asilimia 20 ya ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu kwenda ngazi za chini kiasi cha Sh. Tz 1,733,581,179

**vii. Mapungufu yaliyobainika katika usimamizi wa manunuzi na mikataba**

Katika kuzingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi nilibaini mapungufu yafuatayo:

- Malipo yenye thamani ya Sh.Tz 251,171,899 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa tano kwa ajili ya huduma na bidhaa ambazo hazikupokelewa.
- Manunuzi yenye thamani ya Sh.Tz 644,312,449 yalifanyika na Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 bila kukaguliwa na Kamati ya Ukaguzi wa bidhaa kinyume na Kanuni ya 244 na 245 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.
- Malipo yenye thamani ya Sh.Tz 1,413,388,622 yalifanyika na Mamlaka za Serikali za Mitaa 32 kwa manunuzi ambayo hayakushindanisha wazabuni.

- Manunuzi yenye thamani ya Sh.Tz 2,703,509,121 yalifanyika bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
- Manunuzi yenye thamani ya Sh.Tz 936,775,623 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 27 kwa Wazabuni ambao hawakuidhinishwa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali.
- Manunuzi yenye thamani ya Sh.Tz 2,384,412,108 yalifanyika na Mamlaka za Serikali za Mitaa 21 wakati hayakujumuishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka

**viii. Mapungufu katika usimamizi na udhibiti wa matumizi**

Nilibaini mapungufu yenye kila dalili ya ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha za umma, upotevu wa fedha za Serikali na matumizi yasiyolingana na thamani ya fedha:

- Licha ya msisitizo wa kudai risiti za kielektroniki kwa kila manunuzi yanayofanyika, bado Mamlaka za Serikali za Mitaa 93 zilifanya malipo ya jumla ya Sh.Tz 7,421,735,182 bila kudai risiti za kielektroniki.
- Malipo ya jumla ya Sh.Tz 769,479,797 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 36 kwa manunuzi ambayo hayakuwa halali.
- Malipo ya jumla ya Sh.Tz 792,674,230 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 kwa matumizi yasiyo na tija ambayo yalitokana na madai kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania ikiwa ni kodi ya zuio ambayo haikuzuiliwa na Mamlaka husika huko nyuma.
- Malipo ya jumla ya Sh.Tz 5,362,908,811 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 114 yakiwa na nyaraka pungufu.
- Malipo ya jumla ya Sh.Tz 4,658,384,441 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 63 nje ya bajeti.

**ix. Mapungufu katika usimamizi na udhibiti wa mapato ya ndani**

Nimebaini mambo mbalimbali yanayohusiana na usimamizi wa mapato ya ndani katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:

- Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 41, nimebaini kwamba jumla ya Sh.Tz 3,538,329,470 hazikuwasilishwa na Wakala wa kukusanya mapato.

- Katika ukaguzi, nimebaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 21 hazikuwasilisha jumla ya vitabu vya kukusanyia mapato 349 kwa ajili ya ukaguzi licha ya kuombwa kufanya hivyo.
- Nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 32 zilishindwa kukusanya jumla ya Sh. Tz 12,191,753,218 kutoka katika vyanzo vyake.
- Nilikosa udhibitisho kama kiasi cha Sh. Tz 2,411,293,357 kilichokusanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 39 kilipelekwa benki.

x. **Mapitio ya ruzuku za shule na changamoto zinazohusiana na sera ya Elimu bila Malipo katika shule za msingi za Tanzania**

Nimebaini mapungufu yanayohusiana moja kwa moja na ruzuku za shule na changamoto za utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo katika shule za msingi na sekondari za Tanzania. Kwa muhtasari napenda kuangazia mambo yafuatayo:

- Kwa mujibu wa viwango vya ruzuku za shule, nilibaini kwamba jumla ya Sh.Tz 1,930,944,815 zilitolewa pungufu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 kwa ajili ya shule za Msingi na Sekondari.
- Changamoto za utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo katika shule za msingi na sekondari za Tanzania ni:
  - Mtizamo potofu wa jamii kuhusiana na Sera ya Elimu Bila Malipo.
  - Fedha zilitolewa bila kuzingatia uhalisia wa idadi ya wanafunzi. Hii ilisababisha utumaji shuleni wa fedha pungufu au zaidi.
  - Shule nyingi hazina wahasibu au watumishi wenye uelewa wa uhasibu.
  - Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari wakati miundombinu ya shule hizo haitoshi ukilinganisha na ongezeko hilo.
  - Kukosekana kwa fedha za kulipa walinzi, walimu wa muda mfupi wa sayansi (kwa shule zenye upungufu), gharama za ukaguzi wa shule kikanda, vitambulisho, madeni ya nyuma ya wazabuni, maji, umeme na gharama za mitihani ya kujipima.
  - Manunuzi kufanyika bila kufuata sheria na kanuni za manunuzi.

xi. **Usimamizi duni wa mali**

Mapitio ya usimamizi wa mali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 nilibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanapaswa kufuatiliwa kwa ukaribu;

- Kuna jumla ya Magari, Pikipiki na Mitambo chakavu 693 yaliyotelekezwa muda mrefu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 92 lakini menejimenti zao hazikuchukua hatua zozote za kutathimini uchakavu ili kubaini ni kwa kiasi gani Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kupata faida kutokana na mali hizo chakavu.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa 13 hazikuwa na rejista za rasilimali mali za kudumu na Mamlaka za Serikali za Mitaa 12 zina rejista za mali lakini hazikuhifadhi taarifa muhimu za mali hizo kwenye rejista za mali za kudumu.

xii. **Hasara ya fedha za Umma iliyobainika katika ukaguzi maalum wa Soko la Mwanjelwa**

Ninatoa muhtasari wa mambo muhimu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusiana na ujenzi wa soko jipya la Mwanjelwa ambalo liliungua tarehe 12/12/2006 na kusababisha hasara kubwa ya mali. Ukaguzi maalum uliombwa baada ya wadau kubaini kasoro mbalimbali. Ufuatao ni muhtasari wa masuala yaliyobainishwa ambayo yalipelekea hasara ya fedha za Umma:

- Ongezeko la gharama za ujenzi baada ya mkataba ulioingiwa na mkandarasi Tanzania Building Works Ltd kuvunjwa SH.TZ 5,816,523,388
- Hasara iliyosababishwa na kutomshirikisha Mshauri Mwelekezi katika mchakato wa kumpata mkandarasi wa pili SH.TZ 682,798,733
- Malipo ya awali yalilipwa kwa Tanzania Building Works Ltd zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa na mkataba SH.TZ 1,000,000,000

- Madai ya dhamana ya utekelezaji No: 109/2012 dhidi ya M/s Jubilee Insurance Company of Tanzania Limited ambayo hayakulipwa Sh.TZ 1,067,007,292
- Tozo za ucheleweshaji kazi ambayo haijalipwa na Tanzania Building Works Ltd kwa H/Jiji la Mbeya kwa kuchelewa kumaliza kazi kwa wakati Sh. Tz 1,033,912,388
- Hasara ambayo Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipata kwa kuchukua mkopo benki ya CRDB badala ya NSSF Sh. Tz 5,138,762,054
- H/Jiji la Mbeya kushindwa kukusanya kodi ya pango SH.TZ 1,225,158,063 baada ya wapangaji kushindwa kufanya biashara katika soko hilo kutokana na bei za juu za kodi ya pango ikilinganishwa na zile za soko katika eneo hilo.
- Hasara iliyotokana na kuchukua mkopo kutoka Benki ya CRDB kabla shughuli za ujenzi hazijaanza rasmi SH.TZ 3,360,423,611
- Hasara iliyopatikana kutokana na nyongeza ya muda kwa Mkandarasi mjenzi M/s Tanzania Building Works Ltd SH.TZ 1,633,524,526
- Malipo kwa Mkandarasi M/s Tanzania Building Works Ltd yanayozidi kazi alizofanya SH.TZ 1,140,288,750
- Mabadiliko na nyongeza za kazi zilizotokana na uzembe na kukosekana weledi katika usanifu wa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mwanjelwa SH.TZ 3,161,636,499

# SURA YA KWANZA

## 1.0 USULI

Kama ilivyoelezwa kwenye muhtasari, ripoti hii inaonesha matokeo, hitimisho na mapendekezo kutokana na ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa[1] kwa mwaka wa fedha ulioshia Juni 30, 2017. Ripoti hii pia inajumuisha matokeo ya kaguzi maalum zilizofanywa mwaka 2016 /2017. Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005).

## 1.1 Malengo ya Ukaguzi

Kupata uhakika wa kutosha kwamba taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina kasoro kutokana na ubadhirifu au makosa, na zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika vya utayarishaji wa taarifa za fedha katika Sekta ya Umma. Pia, kuona kama sheria na kanuni husika zimezingatiwa.

## 1.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi na taratibu nyingine za ukaguzi kama zilivyostahili.

Ukaguzi ulifanywa kwa kutumia sampuli; kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yametegemea jinsi nyaraka na taarifa mbalimbali zilivyowasilishwa kwangu kwa ajili ya ukaguzi.

Ripoti hii inaonesha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo kwenye maeneo yafuatayo:

a) Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani;
b) Maandalizi na utekelezaji wa bajeti;
c) Usimamizi wa rasilimali watu na mishahara;
d) Usimamizi wa mikataba na manunuzi;

[1] Mamlaka za Serikali za Mitaa zinajumuisha, Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji, na Wilaya

e) Usimamizi wa matumizi;
f) Usimamizi wa mali na madeni;
g) Masuala yanayoibuliwa kwenye ukaguzi wa taarifa za fedha;
h) Ukaguzi wa miradi ya Maendeleo na miradi mingine;
i) Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa;
j) Kaguzi Maalum; na
k) Utekelezaji wa Mapendekezo zangu na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa miaka ya nyuma

Kaguzi zangu zilipangwa kwa namna ambayo itaniwezesha kuwa na matarajio mazuri ya kubaini kasoro kwenye taarifa za fedha zinazosababishwa na makosa pamoja na ubadhirifu. Wajibu wa kubaini na kuzuia makosa pamoja na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani unabaki kuwa jukumu la Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ilikagua Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kama zilivyoainishwa katika Jedwali Na. 1-1 hapa chini:

**Jedwali Na. 1-1: Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa mwaka wa Fedha 2016/2017**

| Na. | Hadhi ya Halmashauri | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 1. | Halmashauri za Jiji | 5 |
| 2. | Halmashauri za Manispaa | 21 |
| 3 | Halmashauri za Miji | 22 |
| 4 | Halmashauri za Wilaya | 137 |
| **Jumla** | | **185** |

## 1.3 Mchakato wa Ukaguzi

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwa ni mwanachama wa asasi za kitaaluma yaani INTOSAI,

AFROSAI na AFROSAI-E; inatumia viwango na miongozo inayotolewa na asasi hizi. INTOSAI hutoa viwango vya ukaguzi wa nje (ISSAI) kwa sekta ya umma na Umoja wa Mataifa. Viwango hivi vinahitaji wakaguzi kuzingatia maadili, kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata uhakika kama taarifa za fedha hazina kasoro kutokana na ubadhirifu au makosa.

Mbinu za ukaguzi zilihusisha kukagua taarifa za fedha pamoja na taratibu nyingine ili kufikia malengo ya ukaguzi. Taratibu zangu za ukaguzi zilijumuisha mambo yafuatayo:

- Kuandaa mpango kazi wa ukaguzi ili kubaini na kutathmini vihatarishi vya kasoro katika taarifa za fedha vinavyotokana na ubadhirifu au makosa, kwa kuzingatia kuielewa Halmashauri husika na mazingira yake ikiwa ni pamoja na mfumo wake wa udhibiti wa ndani.
- Kupata vielelezo sahihi vinavyotoa ushahidi wa kutosha kama taarifa za fedha zina kasoro kubwa, kwa kubuni njia sahihi za ukaguzi kulingana na vihatarishi vilivyobainika.
- Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba hatua sahihi zimechukuliwa juu ya mapendekezo yaliyotolewa.

## 1.4 Mchakato wa kuandaa Taarifa

Mchakato wa ukaguzi unatumia mbinu shirikishi, ambapo taasisi zilizokaguliwa zilishirikishwa kikamilifu katika mchakato mzima. Mchakato hujumuisha; Maafisa Masuuli, Wakuu wa Idara, Kamati za Ukaguzi na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani; hii ni kwa sababu ninaamini hawa wapo kwenye nafasi nzuri ya kutoa majibu sahihi kuhusu usahihi wa taarifa za fedha na nyaraka nyingine zinazohusiana na ukaguzi ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria na kanuni.

Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yanatolewa kwa kuzingatia vigezo vilivyopo au namna inayoonekana kuwa bora, ikihusisha visababishi, athari na mapendekezo yanayotolewa kwa Menejimenti za taasisi zilizokaguliwa kwa ajili ya maboresho ya baadaye.
Pia, kutoa hati ya ukaguzi inayoonesha matokeo ya ukaguzi wa taarifa ya fedha, uzingatiaji wa sheria na kanuni husika, pamoja na mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani.

Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Iliyorekebishwa 2005) inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha kwa Rais kila taarifa ya fedha atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya Kifungu kidogo cha (2) cha Ibara hii. Vilevile, Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma 2009 inasisitiza kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali awasilishe Ripoti Kuu zote za Ukaguzi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla au ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka, na hatimaye, ripoti hiyo itawasilishwa Bungeni kupitia kwa Waziri mwenye dhamana. Kwa hiyo, ripoti hii ni utekelezaji wa matakwa haya ya kisheria.

## 1.5 Vigezo vya uandaaji wa Taarifa za Fedha

Aya ya A2 na A3 ya Viwango vya Kimataifa vya Asasi kuu za ukaguzi (ISSAI) Na.1210 inatanabaisha mahitaji muhimu ili kazi ya ukaguzi ifanyike (masharti ya awali ya kufanyika kwa ukaguzi), ambayo ni vigezo vya kuzingatia (mfumo unaokubalika wa kuripoti taarifa za kifedha) hufanya msingi wa maandalizi ya taarifa za fedha kwa menejimenti na huwa ni vigezo kwa wakaguzi kwa ajili ya ukaguzi wa taarifa za kifedha. Kama uongozi hautakuwa na misingi sahihi ya uandaaji wa taarifa za fedha basi wakaguzi hawatokuwa na vigezo vya kukagua taarifa hizo.

Kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinazitaka

Mamlaka za Serikali za Mitaa kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu zinazohusu:

- Mapato na matumizi ya fedha na miamala mingine katika Halmashauri.
- Mali na Madeni ya Halmashauri, na kwa kila mwaka wa fedha kuwapo kwa mizania inayoonesha maelezo ya mapato na matumizi, mali na madeni yake yote.
- Katika uandaaji wa taarifa hizi za fedha, Agizo la 11 hadi la 14 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linazitaka Halmashauri kuanzisha mifumo sahihi ya udhibiti wa ndani na usimamizi ambao ni muhimu ili kuwezesha utayarishaji wa taarifa za fedha zisizokuwa na kasoro kubwa kutokana na ubadhirifu au makosa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaandaa taarifa za fedha kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis). Taarifa zote za fedha zimeandaliwa katika msingi wa mfumo endelevu.

## 1.6 Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha

Agizo la 31 (1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka Afisa Masuuli kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi kabla au ifikapo tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha.

Agizo hilo pia linazipa Mamlaka za Serikali za Mitaa jukumu la kuandaa taarifa za fedha kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

Ninapongeza juhudi za Serikali zilizopelekea maandalizi mazuri na hatimaye, mawasilisho ya taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa

mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

# SURA YA PILI

## 2.0 HATI ZA UKAGUZI

Kama ilivyoelezwa katika sura iliyotangulia, malengo ya kufanya kaguzi hizi ni kupata uthibitisho wa kuridhisha kama taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina makossa makubwa yanayotokana na udaganyifu au makosa ya kawaida, na kutoa ripoti ambayo inajumuisha maoni yangu ya ukaguzi. Nilifanya ukuguzi wangu kwa mujibu wa Viwango vya Ukaguzi wa Hesabu vya Kimataifa vinavyotolewa na Umoja wa Taasisi Kuu za Ukaguzi Duniani (ISSAIs). Kuwa na uhakika usiokuwa na shaka ni kiwango cha juu cha uthibitisho lakini haimaanishi kuwa ukaguzi uliofanywa kwa mujibu wa viwango hivi mara zote utabaini makosa yote yaliyopo kwenye taarifa za fedha. Makosa yanaweza kutokea kutokana na udanganyifu au makosa ya kawaida na huchukuliwa kuwa ni makosa makubwa kama kosa mojamoja au kwa ujumla wake yanatarajiwa kuathiri maamuzi ya kiuchumi ya watumiaji kwa kuzingatia taarifa hizi za fedha.

Ninaamini kwamba ushahidi wa ukaguzi ambao nimepata unatosha na unafaa kutoa msingi wa maoni yangu ya ukaguzi. Katika utoaji maoni ya ukaguzi, nipo huru na taasisi zilizokaguliwa kama inavyotakiwa na Bodi ya Kimataifa ya Maadili kwa Wataalamu wa Uhasibu (Kanuni za IESBA) pamoja na mahitaji ya kimaadili ambayo yanahusiana na ukaguzi wangu wa taarifa za fedha nchini Tanzania.

Kati ya kaguzi 185 ambazo zimefanyika mwaka huu, aina zifuatazo za Hati za Ukaguzi zilitolewa kwa mujibu wa ISSAI 1700[1] na 1705[2].

## 2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi na misingi yake

### 2.1.1 Hati inayoridhisha

Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaporidhika kuwa taarifa za fedha ziliandaliwa kwa kuzingatia viwango vya uandaaji wa hesabu vinavyokubalika kwa kiasi kikubwa. Hii ina maana kuwa, taarifa za fedha hazina makosa makubwa. Hata hivyo, kutolewa kwa Hati inayoridhisha haimaanishi taasisi

iliyokaguliwa ina mfumo wa udhibiti wa ndani wenye ufanisi wa asilimia mia moja, ila inamaanisha kuwa hakuna jambo lolote kubwa lilobainika na mkaguzi kumfanya atoe Hati yenye shaka.

### 2.1.2 Hati yenye shaka

Hati hii hutolewa wakati Mkaguzi anapokuwa amejiridhisha kuwa, taarifa za fedha zina makosa makubwa lakini yasiyoenea na kuathiri maeneo mengine ya taarifa ya fedha. Hii inamaanisha kwamba, kutokubaliana na kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi ni kwa sehemu fulani tu ya taarifa ya fedha lakini sehemu nyingine iliyobaki huonesha uhalisi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa.

### 2.1.3 Hati Isiyoridhisha

Hati hii hutolewa pale mkaguzi anapojiridhisha kuwa kosa mojamoja au kwa ujumla wake ni makubwa na yameenea maeneo mengi ya taarifa za fedha. Hii inamaana kuwa kuna kutokubaliana kwa kiwango kikubwa. Hii inamaanisha pia kwamba, kuna kutofautiana na menejimenti kunakotokana na taarifa ya fedha kutokuwa na ufafanuzi wa kutosha au kuwa na makosa ya kiuhasibu ambayo yanaathiri taarifa nzima ya fedha.

### 2.1.4 Hati Mbaya

Hutolewa wakati Mkaguzi anapokuwa ameshindwa kupata vielelezo sahihi vinavyotoa ushahidi wa kutosha ili kupata msingi wa maoni ya ukaguzi; na Mkaguzi amejiridhisha kuwa makosa ambayo hatoyagundua yatakuwa makubwa na yameathiri maeneo mengi ya taarifa ya fedha.

## 2.2 Masuala mengine yanayoambatana na Hati za Ukaguzi

ISSAIs 1701, 1706 na 1720 zinahitaji Mkaguzi kutoa maelezo ya ziada katika ripoti ya ukaguzi ili kutoa ufafanuzi zaidi kwa watumiaji kuhusu taarifa fedha zilizokaguliwa. Hii hufanywa kwa kuandikwa aya za mambo muhimu yaliyobainika kwenye ukaguzi, masuala muhimu ya msisitizo, masuala mengineyo na taarifa nyinginezo.

Zaidi hayo, Mkaguzi anawajibika kutoa matokeo baada ya kutathmini kiwango cha taasisi kuzingatia mahitaji mbalimbali ya kisheria.
Aina ya masuala ya ziada kuhusiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa mwaka 2016/2017 ni kama zinavyoelezwa kwenye aya zinazofuata.

### 2.2.1 Masuala Muhimu ya Msisitizo

Masuala muhimu ya msisitizo humaanisha mambo yote ambayo yameelezwa au kufafanuliwa vizuri katika Taarifa ya fedha lakini yanadhaniwa kuwa ni muhimu kutolewa tahadhari kwa watumiaji wa taarifa ya fedha ili yaeleweke vizuri kwao.

Nilieleza aya ya Masuala Muhimu ya Msisitizo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 69 kama zilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho 2:4** cha ripoti hii.

### 2.2.2 Masuala Mengineyo

Aya hii inajumuishwa katika taarifa ya ukaguzi pale tu Mkaguzi anapofikiri kuwa ni muhimu kueleza mambo ambayo si yale yaliyoelezwa na kufafanuliwa katika taarifa ya fedha, ambayo, kwa mtizamo wa Mkaguzi, ni muhimu kwa watumiaji kuelewa ukaguzi na wajibu wa Mkaguzi au taarifa ya Mkaguzi.

Kwa mwaka husika wa ukaguzi, ripoti za ukaguzi za Mamlaka za Serikali za Mitaa 22 zilijumuisha aya ya Masuala Mengineyo. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Masuala Mengineyo zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2:4** cha ripoti hii.

### 2.2.3 Mambo muhimu ya ukaguzi

Aya ya Mambo muhimu ya Ukaguzi inajumuishwa katika taarifa ya ukaguzi ili kuongeza uwazi katika mchakato wa ukaguzi na kuwajulisha watumiaji wa taarifa za fedha maeneo yaliyotathminiwa yenye viashiria vya kuwa makosa makubwa na wale wanaohusika na kufanya maamuzi muhimu kwenye taasisi na kufanyia kazi tahadhari muhimu zinazotolewa na mkaguzi.
Mambo haya yalifafanuliwa katika muktadha wa ukaguzi wa taarifa za kifedha kwa ujumla wake na katika kutengeneza maoni ya

ukaguzi. Hakuna maoni ya ukaguzi tofauti yaliyotolewa juu ya mambo hayo yameoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2:4** cha ripoti hii.

### 2.2.4 Taarifa nyinginezo

ISSAI 1720 (ilireyokebishwa) inahitaji ripoti ya ukaguzi kujumuisha aya ya Taarifa nyinginezo. Taarifa nyinginezo zinanajumuisha taarifa ya mkurugenzi, maeleozo ya madiwani na tamko la mkuu wa idara ya fedha zilizojumuishwa katika taarifa ya fedha. Menejimenti ya taasisi iliyokaguliwa inahusika na taarifa nyinginezo. Kama mkaguzi, nilihitajika kusoma taarifa nyingine na kwa kufanya hivyo, nitathmini kama taarifa nyingine haziendani kwa kiasi kikubwa na taarifa ya fedha au kwa uwelewa wangu nilioupata kutokana ukaguzi, au vinginevyo zinaonekana kukosewa kwa kiasi kikubwa nahitajika kutolea taarifa. Maoni yangu juu ya taarifa za fedha hayakuhusisha taarifa nyingine na sijatoa aina yeyote ya uthibitisho wala hitimisho juu ya taarifa hizo zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2:4** cha ripoti hii.

### 2.2.5 Tathmini ya uzingatiwajia wa mahitaji ya kisheria

ISSAI 1700.43 (Iliyorekebishwa) humpa Mkaguzi majukumu mengine ya kuripoti. Lengo ni kuhakikisha kwamba shughuli za taasisi zinafanywa kulingana na sheria na kanuni mbalimbali. Kwa mwaka huu, nilitathmini na kupitia miamala na taratibu za manunuzi za Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza majukumu yangu kama ilivyo katika sheria ya manunuzi.

Tathmini ya uzingatiwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake zimeelezwa vizuri katika sura ya tisa ya ripoti hii.

## 2.3 Hati za Ukaguzi zilizotolewa mwaka 2016/2017

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, nimetoa Hati za Ukaguzi kwa jumla Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 nilizozikagua. Hati hizi zimetolewa baada ya kupata ushahidi sahihi na wa kutosha na ufafanuzi uliotolewa katika taarifa za fedha zilizowasilishwa kwangu tarehe 30 Septemba 2017 na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na aina ya Hati za ukaguzi zilizotolewa ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2-1 hapa chini.

**Jedwali Na. 2-1: Mamlaka za Serikali za Mitaa na aina ya Hati ya ukuguzi iliyotolewa**

| Hati ya ukaguzi iliyotolewa | Mamlaka za Serikali za Mitaa | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Hati inayoridhisha | 166 | 90 |
| Hati yenye Shaka | 16 | 8 |
| Hati Isiyoridhisha | 3 | 2 |
| **Jumla** | **185** | **100** |

Hakukuwa na Hati mbaya iliyotolewa kwa mwaka huu.

Maelezo zaidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Hati inayoridhisha, Hati yenye shaka na Hati isiyoridhisha kama inavyooneshwa kwenye **Viambatisho 2:1** na **2:2** vya taarifa hii.

## 2.4 Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa makundi mbalimbali ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kama ilivyoelezwa katika sura iliyopita uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa umegawanyika katika makundi manne. Jedwali Na. 2-2 hapo chini linaonesha makundi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Hati za ukaguzi zilizotolewa mwaka huu.

**Jedwali Na. 2-2: Muhtasari wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa katika makundi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

| Aina ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | Idadi ya Taasisi | Aina ya Hati za Ukaguzi | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Hati inayorizisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha |
| Jiji | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Manispaa | 21 | 18 | 2 | 1 |
| Miji | 22 | 21 | 1 | 0 |
| Wilaya | 137 | 122 | 13 | 2 |
| **Jumla** | **185** | **166** | **16** | **3** |

## 2.5 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne mfululizo

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa zimeongezeka kutoka 171 mwaka 2015/2016 hadi 185 mwaka 2016/2017. Na pia Hati za

Ukaguzi zimebadilika kama inavyochambuliwa katika Jedwali Na. 2-3 hapa chini:

**Jedwali Na. 2-3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne mfululizo**

| Hati ya Ukuguzi | Hati inayoridhisha | | Hati yenye mashaka | | Hati isiyoridhisha | | Hati mbaya | | Jumla ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | Jumla | % | Jumla | % | Jumla | % | Jumla | % | |
| 2016/17 | 166 | 90 | 16 | 8 | 3 | 2 | 0 | 0 | 185 |
| 2015/16 | 138 | 81 | 32 | 19 | 1 | 1 | 0 | 0 | 171 |
| 2014/15 | 110 | 79 | 28 | 20 | 2 | 1 | 0 | 0 | 140 |
| 2013/14 | 104 | 78 | 29 | 21 | 0 | 0 | 1 | 1 | 134 |

Ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka jana, idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata Hati inayoridhisha imeongezeka kutoka 138 hadi 166 ambalo ni ongezeko la asilimia 20, na pia zilizopata Hati yenye shaka zimepungua kutoka 32 hadi 16 sawa na asilimia 50. Uchambuzi wa mwenendo wa Hati za ukaguzi unaonesha kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeboresha uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

Hata kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji haina mabadiliko kwenye Hati za Ukaguzi zilitolewa kuanzia 2014/2015 hadi 2016/2017. Halmashauri hii imepata Hati isiyoridhisha kwa miaka mitatu mfululizo.

Licha ya hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa Kigoma pamoja na uongozi wa Halmashauri husika wa kusimamisha na kuhamishwa kwa wafanyakazi, uwezo wa Halmashauri kusimamia rasilimali za umma unaendelea kuwa mbaya zaidi. Mnamo tarehe 18-01-2016 Halmashauri, kupitia RAS Kigoma, iliniomba kufanya ukaguzi maalum wa Hesabu zake kwa mwaka ulioishia Juni 2015. Hata hivyo, tarehe 28/08/2017 kwa barua yenye Kumb. Na. A.70 / 10/45 walitengua maombi hayo kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na madai ya kwamba tayari wameboresha mfumo wao wa udhibiti wa ndani, na Kwamba, kasoro ambazo zilipelekea ukaguzi maalum kuombwa kufanyika hazipo tena.

Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya 1982, kifungu cha 71 hadi 78 inamtaka Waziri anaewajibika (OR-TAMISEMI) kutumia mamlaka yake kuboresha utendaji wa Mamlaka yoyote ya Serikali za Mitaa kwa kuchukua hatua za haraka ambazo zinahitajika na zinazofaa kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

Nina wasiwasi na utendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Ninapendekeza Serikali kuchukua hatua sahihi.

Zaidi ya hayo, kutokana na mwenedo wa hati za ukaguzi, nashauri Waziri anayehusika kuchukua hatua kwa Halmashauri zilizooneshwa kwenye Jedwali Na. 2-4 ambazo zimepata Hati yenye shaka kwa miaka mitatu hadi minne mfululizo. Kujirudia kwa Hati yenye shaka kunaashiria kuwa uongozi wa Halmashauri husika haujaboresha uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha zinazoendana na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha katika sekta ya Umma (IPSAS), usimamizi wa rasilmali za Umma na kuzingatia Sheria na kanuni.

**Jedwali Na. 2-4: Halmashauri zenye hati yenye mashaka kwa zaid ya miaka mitatu mfululizo**

| Jina la Halmashauri | Idadi ya miaka |
|---|---|
| H/W Longido | 4 |
| H/W Rombo | 3 |
| H/W Korogwe | 3 |
| H/W Ukerewe | 3 |

Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zote 185 na Hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2:3.**

# SURA YA TATU

## 3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

Sura hii inatoa mwelekeo wa hali ya masuala yasiyoshughulikiwa kutokana na mapendekezo niliyoyatoa mwaka uliopita katika Ripoti ya Jumla, ripoti za kaguzi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na ripoti za ukaguzi maalum na hali ya utekelezaji wa maagizo ya jumla yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Taarifa ya Utekelezaji kwa kila pendekezo inaonesha aidha pendekezo limetekelezwa kikamilifu, bado linaendelea kutekelezwa au halijatekelezwa.

Ripoti hii inatolewa ili kukidhi matakwa ya Kifungu Na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 (iliyorekebishwa 2013) inayomtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa kuandaa ripoti ya mwaka kujumuisha hali halisi ya utekelezaji wa mipango kazi iliyoandaliwa na Maafisa Masuuli na kuunganishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Zaidi ya hayo, Sheria inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilisha nakala ya taarifa jumuifu ya Majibu na Mpango wa Utekelezaji kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa ajili ya uhakiki.

Pia, Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 (iliyorekebishwa 2013) kinampa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum kuhusu jambo lolote linalohusiana na fedha au mali za umma kwa lengo la kulijulisha Bunge pindi atakapoona inafaa.

Ufuatiliaji wa hoja za miaka iliyopita unatoa uthibitisho kwa watumiaji wa ripoti kuwa ni jinsi gani Mamlaka ya Serikali za Mitaa inavyofanyia kazi mapendekezo yangu na maagizo ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Hatua za haraka katika kushugulikia mapendekezo yangu na maagizo ya Kamati ya LAAC itapelekea kuimarika kwa uwajibikaji kwenye usimamizi wa masuala ya kifedha na rasilimali nyinginezo ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kuimarika huko kutapelekea kupatikana kwa huduma bora zinazohitajika kwa jamii.

Kazi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika uchunguzi wa kifedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinategemeana na kukamilishana.

Kamati hutegemea matokeo ya ukaguzi katika kutekeleza majukumu yake. Vivyo hivyo, ninategemea kazi za Kamati ambazo huboresha hatua za utekelezaji wa mapendekezo yatokanayo na kaguzi zangu.

Tarehe 10 Julai 2017 nilipokea majibu ya Serikali yaliyoandaliwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali yanayoonesha utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yahusuyo ripoti ya jumla ya mwaka uliopita kupitia barua yenye Kumb. Na CHA.114 /474/78. Ninatambua jitihada zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuwasilisha mapendekezo ya mpango wa utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Hata hivyo, katika kaguzi zangu za miaka iliyopita, nilionesha kuguswa na utekelezaji usioridhisha na kujirudia kwa hoja za ukaguzi za muda mrefu zinazohusu Ripoti Jumuifu, ripoti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kaguzi Maalumu na Maagizo ya LAAC. Kwa mwaka 2016/2017, nimeendelea kuona marudio ya hoja zinazofanana na zile zilizopita; na hii inanipa wasiwasi kuwa majibu ya Ripoti ya Jumla na mpango kazi ulioandaliwa na Maafisa Masuuli na kuwasilishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali haukuweza kutekeleza kikamilifu mapendekezo niliyoyatoa.

Hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita, hususani Ripoti ya Jumla, ripoti husika za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ripoti za ukaguzi maalum na maagizo ya Kamati ya LAAC inawasilishwa kama ifuatavyo:

## 3.1 Hali halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti ya Jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miaka Iliyopita na Ripoti za kila Halmashauri.

Kati ya mapendekezo 14 niliyoyatoa kwenye Ripoti Jumuifu ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, hakuna mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu, mapendekezo tisa (64%) yalikuwa yakiendelea kutekelezwa na

mapendekezo matano (36%) hayakushughulikiwa kabisa. Sambamba na hilo, kati ya mapendekezo 12,703 niliyoyatoa kwenye ripoti 171 za Halmashauri kwa mwaka 2015/2016, mapendekezo 4,262 (34%) yalitekelezwa, 3,024 (25%) yalikuwa yakiendelea kutekelezwa; 3,206 (25%) hayakushughukiwa kabisa na mapendekezo 2,211(17%) yalipitwa na wakati kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3-1 hapo chini:

**Jedwali Na. 3-1: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka iliyopita.**

| Ripoti | Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Idadi ya mapendekezo yalliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yanayoendelea Kutekelezwa | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Mapendekezo yaliyopitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ripoti ya Jumla | 2015/2016 | 171 | 14 | 0 | 9 | 5 | 0 |
| | 2014/2015 | 164 | 38 | 3 | 19 | 16 | 0 |
| | 2013/2014 | 163 | 16 | 0 | 6 | 10 | 0 |
| | | | | | | | |
| Ripoti za Halmasha | 2015/2016 | 171 | 12703 | 4262 | 3024 | 3206 | 2211 |
| | 2014/2015 | 164 | 11283 | 2914 | 3287 | 3650 | 1431 |
| | 2013/2014 | 163 | 7921 | 2330 | 2241 | 2728 | 622 |

Maelezo ya ziada ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti Jumuifu na ripoti kwa kila Halmashauri yameainishwa kwenye **Kiambatisho Na.3:1** na **Na.3:2** kwa mtawalia.

## 3.2 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi katika Ripoti za Kaguzi Maalum

Orodha ya Halmashauri zenye mapendekezo yasiyotekelezwa yaliyotolewa kwenye ukaguzi maalum imeoneshwa katika Jedwali Na. 3-2 hapa chini:

**Jedwali Na. 3-2: Orodha ya Halmashauri zenye Mapendekezo yasiyotekelezwa yaliyotolewa wakati wa Ukaguzi Maalum kwa kipindi cha miaka mitano iliyofuatana**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Idadi ya masuala yasiyo na thamani | Masuala yenye thamani (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| 2013/2014 | 6 | 111 | 38,725,436,111 |
| 2012/2013 | 6 | 146 | 35,717,988,924 |
| 2011/2012 | 14 | 302 | 66,471,126,999 |
| 2010/2011 | 13 | 69 | 31,408,213,793 |
| **Jumla** | **39** | **628** | **172,322,765,827** |

Hali ya utekelezaji wa Mapendekezo na Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Serikali na Halmashauri.

Nimebaini kuwa, utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamebaki bila kutekelezwa kwa muda mrefu kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 3-3 hapa chini:

**Jedwali Na. 3-3: Mwenendo wa Majibu ya Serikali Kuhusiana na Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa**

| Tarehe yaliyowasilishwa Bungeni | Mwaka wa fedha husika | Idadi ya mapendekezo | Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali |
|---|---|---|---|
| 28 Januari 2015 | 30th Juni, 2015 | 9 | 9/11/2016 |
| 28 Januari 2014 | 30th Juni, 2014 | 12 | Hakuna Majibu |
| 6 Desemba 2013 | 30th Juni, 2013 | 10 | Hakuna Majibu |
| 17 Aprili 2012 | 30th Juni, 2012 | 15 | Hakuna Majibu |
| 04 Aprili 2011 | 30th Juni, 2011 | 7 | Hakuna Majibu |

Aidha, kati ya maagizo 748 yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Halmashauri husika kwa mwaka 2015/2016, maagizo 233 (31%) yalitekelezwa, maagizo 256(34%) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na maagizo 259(35%) hayajatekelezwa kama yalivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 3-4 hapa chini:

**Jedwali Na. 3-4: Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Halmashauri**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Halmashauri | Jumla ya mapendekezo | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea kutekelezwa | Yasiyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 115 | 748 | 233 | 256 | 259 |
| 2014/2015 | 142 | 1094 | 433 | 231 | 430 |
| 2013/2014 | 118 | 900 | 408 | 201 | 291 |

Maelezo ya hali halisi ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa yaliyotolewa kwa kila Halmashauri ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.3:3.**

## 3.3 Kukosekana kwa mfumo rasmi wa ufuatiliaji wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizofanyiwa kazi na taasisi za uchunguzi Serikalini

Kufuatia kuongezeka kwa masuala yanayohusiana na rushwa, udanganyifu, wizi na matumizi mabaya ya mali na rasilimali za umma ambayo yameainishwa katika ripoti za ukaguzi wangu, taasisi nyingine za uchunguzi hutumia ripoti hizi kwa ufuatiliaji zaidi. Katika suala hili, ninatambua juhudi na hatua zinazochukuliwa na taasisi husika katika kufanyia kazi masuala yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu. Hata hivyo, kuna mambo ambayo yanapaswa kuangaliwa ili kuboresha matumizi sahihi ya ripoti ninazozitoa.

Sehemu mojawapo ni utumiaji wa pamoja wa nyaraka na taarifa kutoka kwa wakaguliwa pindi zinapokuwa zinahitajika kwangu na kwa taasisi husika za uchunguzi. Kila Ofisi hujiona kuwa na haki zaidi ya kupewa nyaraka hizo kuliko ofisi nyingine pindi zinapohitajika kwa ajili ya kufanya kazi za uchunguzi. Changamoto hii hupelekea kuchelewesha, na wakati mwingine kuzuia, mawanda ya uchunguzi kwa kila Ofisi kutokana na kuwapo kwa taratibu ndefu za upatikanaji wa nyaraka hizo.

Ushirikiano kati ya Ofisi yangu na taasisi za kichunguzi ni muhimu kwa sababu iwapo kuna suala ambalo nimeliripoti na linachunguzwa na taasisi husika linaweza kukosa sifa za kisheria kutokana na jinsi lilivyoshughulikiwa au kukosekana kwa nyaraka zinazohitajika. Hii inapelekea Ofisi ya ukaguzi kutokuwa na taswira nzuri kwa jamii. Kwa maana nyingine, jukumu langu la usimamizi linaonesha kutokuwa na

matokeo iwapo hakutakuwa na ufuatiliaji kutoka kwa taasisi husika kwenye masuala niliyoyabaini kwenye kaguzi zangu.

Hivyo, ninapendekeza serikali ianzishe utaratibu ambao utaimarisha na kuboresha uhusiano kwa kitendo kati ya taasisi za uchunguzi na ofisi yangu (Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) bila kuathiri majukumu ya kila Ofisi. Serikali inaweza kuanzisha ufuatiliaji shirikishi utakaopunguza muingiliano wa mahitaji ya nyaraka, hivyo kuboresha ukusanyaji wa ushahidi wakati wa kushughulikia masuala ya kiuchunguzi.

Kifungu Na. 2.7 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008 (iliyorekebishwa mwaka 2013) kinahitaji Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa ripoti ya udanganyifu au makosa yoyote yanayobainika wakati wa ukaguzi kwa chombo sahihi cha uchunguzi na kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka ya Umma. Ninashauri serikali izingatie marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008 (iliyorekebishwa mwaka 2013) ili kuingiza kifungu kitakachozipa mamlaka za vyombo vya uchunguzi kuchunguza yatokanayo na ripoti ya CAG mara baada ya kupelekwa Bungeni na kutambua maeneo ambayo yanahitaji ufuatiliaji wa ziada. Kifungu hicho kieleze kwa ufasaha wajibu wa ushirikishwaji katika matokeo ya uchunguzi ndani ya muda uliopangwa kisheria.

## SURA YA NNE

## 4.0 MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE

Sura hii inaelezea juu ya bajeti zilizoidhinishiwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya matumizi dhidi ya fedha zilizotolewa, mapato halisi yaliyokusanywa kutoka vyanzo vya ndani na mwelekeo wa mapato ya mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2017.

### 4.1 Mtizamo wa jumla wa Bajeti

Bajeti ni kipengele muhimu sana katika mchakato wa mipango ya kifedha, udhibiti na tathmini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchini Tanzania, Serikali huandaa bajeti kwa msingi wa uwepo wa fedha taslimu wakati taarifa za kifedha huandaliwa kwa msingi wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual) kama ilivyoelezwa katika Sura zilizopita.

Bajeti iliyoidhinishwa maana yake ni mamlaka ya matumizi inayotokana na sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya serikali, na maamuzi mengine yanayohusiana na mapato yaliyotarajiwa au yatakayopokelewa kipindi cha bajeti.

Kifungu 43(1) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya mwanzo wa mwaka wa fedha, katika kikao maalum, kupitisha bajeti ya makadirio ikionesha: (a) kiasi cha mapato kinachotarajiwa kupokelewa; (b) Kiasi kinachotarajiwa kutolewa na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika, na kukiwa na ulazima, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kupitisha bajeti za ziada katika mwaka wa fedha.

Ukaguzi wa bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umeonesha masuala mbalimbali kama yalivyoelezwa hapo chini:

## 4.2 Mwenendo wa mapato ya ndani yakilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

Mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni mapato yaliyokasimiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo havikusanywi na Serikali Kuu. Mapato haya hubakia katika Halmashauri ili kufidia mapungufu ya ruzuku na kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kujikimu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli zao za kila siku. Mapato hayo ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanajumuisha kodi za ndani, ada, tozo, ushuru, vibali vya ujenzi, na mapato mengineyo ndani ya mipaka ya Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17, Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 zilifanikiwa kukusanya jumla ya Sh.Tz 523,564,835,716 kutoka vyanzo vyake vya ndani ukilinganisha na bajeti ya Sh.Tz 628,045,048,644 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha Sh.Tz 104,480,212,928 sawa na 17% ya bajeti iliyopitishwa kwa mwaka. Kwa maelezo zaidi angalia **Kiambatisho Na. 4:1**.

Jedwali Na. 4-1 hapa chini linaonesha mwenendo wa makusanyo ya mapato ikilinganishwa na bajeti kwa muda wa miaka mitatu.

**Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa makusanyo ya mapato ikilinganishwa kulingana na bajeti**

| Mwaka | Bajeti(Sh.Tz) | Makusanyo Halisi(Sh.Tz) | Tofauti(Sh.Tz) | % |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 628,045,048,644 | 523,564,835,716 | (104,480,212,928) | 17 |
| 2015/2016 | 536,203,527,158 | 482,898,501,332 | (53,305,025,824) | 10 |
| 2014/2015 | 471,192,301,516 | 409,100,130,028 | (62,092,171,489) | 13 |

Jedwali hilo hapo juu linaonesha kuwa, kwa miaka mitatu mfululizo kulikuwa na upungufu wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuja na hatua madhubuti za kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani kwa kuhakikisha kuwa vitu vinavyosababisha mapato yasikusanywe vinaondolewa na udhibiti wa usimamizi wa mapato kuimarishwa ili kupunguza utegemezi kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

## 4.3 Mwenendo wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ikilinganishwa na ruzuku ya matumizi ya kawaida

Ruzuku ya Matumizi ya kawaida ni fedha za uendeshaji wa shughuli za kila siku ikijumuisha malipo ya mishahara kwa watumishi, manunuzi ya vifaa na huduma mtambuka ambapo chanzo cha fedha ni makusanyo ya ndani na ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh.Tz 519,863,656,618 kutokana na vyanzo vya ndani na kufanya matumizi ya kawaida ya jumla ya Sh.Tz 4,656,643,395,963. Ulinganisho wa mapato yake ya ndani na matumizi ya kawaida umebaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 hazina uwezo wa kujiendesha kutokana na mapato ya ndani kwani haziwezi kugharamia matumizi ya shughuli za kawaida bila kutegemea ufadhili kutoka Serikali Kuu na wafadhili wengine. Maelezo zaidi yametolewa katika **Kiambatisho Na. 4:2**

Jedwali Na.4-2 linaonesha mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na matumizi ya kawaida.

**Jedwali Na. 4-2: Mwenendo wa Makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na matumizi ya kawaida**

| Mwaka | Makusanyo halisi (Sh.Tz) | Matumizi ya kawaida (Sh.Tz) | Asilimia ya kujitegemea |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 519,863,656,618 | 4,656,643,395,963 | 11 |
| 2015/2016 | 482,898,501,334 | 4,453,470,809,033 | 11 |
| 2014/2015 | 409,100,130,028 | 3,569,212,750,970 | 11 |

Kutokana na mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani ukilinganishwa na matumizi ya kawaida kwa kipindi cha miaka mitatu (2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017) Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuweza kugharamia shughuli zake za kila siku bila kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha mfumo madhubuti na endelevu wa kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani.

## 4.4 Makusanyo ya mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kiasi cha fedha ambacho kinapangwa na kukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zenyewe kutoka vyanzo tofauti ambavyo havikusanywi na Serikali Kuu. Vyanzo vikuu vya mapato hayo ya ndani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama vile, ushuru wa mazao, tozo za utoaji wa huduma, ada za leseni, ushuru wa soko na tozo, vibali vya ujenzi, na vibali katika shughuli za biashara.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 zilikaguliwa ili kujua kiasi kilichokusanywa na Halmashauri za Majiji, Halmasahuri za Manispaa, Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji na yafuatayo yalibainika:

### 4.4.1 Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani Sh.Tz 115,971,628,729

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 144 zilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh.Tz 516,564,978,035 kutokana na vyanzo vya ndani. Ingawa Mamlaka hizo zilifanikiwa kukusanya Sh.Tz 400,593,349,306 ambayo ni sawa na asilimia 78 hali iliyopelekea upungufu wa Sh.Tz 115,971,628,729 sawa na asilimia 22 ya bajeti yote. Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kiasi ambacho hakikukusanywa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4:3**.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji na Halmashauri ya wilaya ya Siha ndiyo zenye upungufu mkubwa katika makusanyo ya mapato ya ndani sawa na asilimia 68 ikifuatiwa na Halmashauri ya Mji wa Babati ilikusanya mapato pungufu kwa asilimia 63. Hii inaonesha kuwa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa haukuweka mikakati madhubuti katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Ninapendekeza kuwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweke mikakati na endelevu madhubuti ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

### 4.4.2 Makusanyo ya mapato ya ndani zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa Sh. Tz 3,722,046,551

Katika mwaka 2016/2017, Mamlaka ya Serikali za Mitaa 38 zilikusanya jumla ya mapato ya Sh.Tz 111,050,856,796 ikilinganishwa na kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa ya Sh.Tz 107,328,810,245 kutoka vyanzo vya mapato ya ndani yanayoonesha ziada ya Sh.Tz 3,722,046,551 sawa na 4% ya bajeti iliyopitishwa. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato unaoonesha ziada ya mapato yakilinganishwa na bajeti kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 4:4.**

Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo yanayozidi bajeti iliyoidhinishwa yanaashiria ama bajeti iliyopitishwa haikuwa na uhalisia, au vyanzo muhimu vilivyopo katika mamlaka hizo havikuibuliwa vyema ili kukusanya mapato kama ilivyopaswa. Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze iliongoza kwa kuwa na makusanyo zaidi ya bajeti ikilinganishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingine.

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutengeneza Bajeti zinazozingatia uhalisia na kuweka mbinu madhubuti na endelevu zitakazotuhakikishia kupanda kwa makusanyo ya mapato na kupunguza utegemezi wa rukuzu kutoka Serikali Kuu.

## 4.5 Kiwango cha ruzuku kilichotolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa

### 4.5.1 Fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo zilizopokelewa zaidi ya bajeti Sh. Tz 18,074,193,265

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka za Serikali za Mitaa 14 ziliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Sh. Tz 44,446,747,137 kama ruzuku ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kiasi cha Sh. Tz 62,520,940,402 kilipokelewa, hivyo kufanya jumla ya Sh. Tz 18,074,193,265 ambayo ni sawa na 41% ya bajeti kupokelewa zaidi ya bajeti. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopokea fedha za maendeleo zaidi ya bajeti imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4:5.**

### 4.5.2 Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa zaidi ya bajeti Sh. Tz 82,484,838,958

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ya Serikali za Mitaa 38 ziliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Sh. Tz 909,489,550,054 kama ruzuku ya matumizi ya kawaida. Hata hivyo, jumla ya Sh. Tz 991,974,389,012 kilipokelewa, hivyo kufanya jumla za Sh. Tz 82,484,838,958 (9%) kupokelewa zaidi ya bajeti. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopokea fedha za maendeleo zaidi ya bajeti imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4:6**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala iliongoza kwa kupokea ruzuku ya matumizi ya kawaida zaidi ya bajeti. Hii inaashiria kuwa. bila kupitisha bajeti ya ziada, mapokezi ya fedha zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa yanaweza kuchangia kutumika vibaya kwa fedha hizo na watumishi wasio waaminifu.

Ninaishauri Serikali kupitia Hazina kupeleka fedha za maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa, endapo kuna umuhimu wa kupeleka fedha zaidi, Wizara ipate idhini kutoka kwenye mamlaka husika kabla ya kufanyika matumizi ya fedha hizo.

## 4.6 Kiasi cha fedha kilichotolewa pungufu ya bajeti

### 4.6.1 Fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa Sh.Tz 532,214,628,377

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ya Serikali za Mitaa 167 ziliidhinishiwa jumla ya Sh. Tz 1,034,122,816,044 kutumika kama ruzuku ya matumizi ya maendeleo. Ukaguzi niliofanya nilibaini kuwa kiasi kilichopokelewa ni Sh. Tz 501,908,187,667 tu, hivyo kupelekea upungufu wa Sh. Tz 532,214,628,377 sawa na 51% ya bajeti iliyoidhinishwa. Hii inaashiria kuwa, upungufu wa fedha hizo unakwamisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Kwa maelezo zaidi tazama **Kiambatisho Na. 4:7.**

Jedwali Na. 4-3 hapa chini linaonesha mwenendo wa fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikupokelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitatu mfululizo.

**Jedwali Na. 4-3: Mwenendo wa fedha za maendeleo ambazo hazikupokelewa**

| Mwaka wa Fedha | Bajeti ya Ruzuku ya Maendeleo | Kiasi halisi kilichotolewa cha Ruzuku ya Maendeleo (Sh.Tz) | Kiasi pungufu cha Ruzuku(Sh.) | % | Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 1,034,122,816,044 | 501,908,187,667 | 532,214,628,377 | 51 | 167 |
| 2015/2016 | 1,010,650,744,099 | 390,525,992,297 | 620,124,751,801 | 61 | 151 |
| 2014/2015 | 752,832,745,765 | 363,123,775,781 | 389,708,969,984 | 52 | 147 |

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inaongoza kwa upungufu wa bajeti iliyoidhinishwa sawa na asilimia 96 ikifuatiwa na Halmashauri ya Kibondo na Mufindi kwa asilimia 88 na 86.

### 4.6.2 Fedha za ruzuku ya kawaida zilizopokelewa pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa Sh. Tz 581,527,226,466

Katika mwaka 2016/2017, bajeti iliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 146 ilikuwa Sh. Tz 3,989,650,046,115 na kiasi kilichopokelewa ni Sh. Tz 3,408,122,819,649 ambacho ni pungufu ya bajeti iliyopitishwa kwa kiasi cha Sh. Tz 581,527,226,466 sawa na 15%. Hii inaashiria uwezekano wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kumudu kwa uhakika uendeshaji wa shughuli za kila siku: Kwa maelezo zaidi tazama **Kiambatisho Na. 4:8** cha ripoti hii.

Jedwali Na. 4-4 hapa chini linaonesha mwenendo wa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida ambazo hazikupokelewa katika mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitatu mfululizo.

**Jedwali Na. 4-4: Mwenendo wa fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikupokelewa**

| Mwaka | Bajeti ya mwisho ya matumizi ya kawaida (Sh.Tz) | Kiasi halisi kilicho pokelewa (Sh.Tz) | Kiasi ambacho hakikutolewa (Sh.Tz) | % ya upungufu | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 3,989,650,046,115 | 3,408,122,819,649 | 581,527,226,466 | 15 | 146 |
| 2015/2016 | 1,010,650,744,099 | 390,525,992,297 | 620,124,751,801 | 61 | 151 |

| Mwaka | Bajeti ya mwisho ya matumizi ya kawaida (Sh.Tz) | Kiasi halisi kilicho pokelewa (Sh.Tz) | Kiasi ambacho hakikutolewa (Sh.Tz) | % ya upungufu | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2014/2015 | 752,832,745,765 | 363,123,775,781 | 389,708,969,984 | 52 | 147 |

Halmashauri ya Mji ya Kondoa na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo zimepokea Ruzuku ya maendeleo na ya matumizi ya kawaida chini ya bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingine.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia OR– TAMISEMI kuonesha athari itokanayo na kupokea ruzuku chini ya bajeti iliyoidhinishwa na hivyo kupelekea kutokamilika kwa malengo yaliyokusudiwa. Pia ninarudia tena mapendekezo yangu ya miaka iliyopita kwa Serikali Kuu kutoa fedha kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoidhinishwa.

## 4.7 Fedha isiyotumika

### 4.7.1 Bakaa ya fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida Sh. Tz 270,132,243,323

Katika mwaka unaokaguliwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 75 zilitumia Jumla ya Sh. Tz 1,714,044,062,102 ya fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na kiasi cha Sh. Tz 1,984,176,305,424 kilichopokelewa kutoka Hazina, hivyo kuwa na bakaa ya kiasi cha Sh. Tz 270,132,243,323 sawa na asilimia kumi na nne (14%) ya fedha zote za ruzuku ya matumizi ya kawaida ziliyopokelewa. Mchanganuo wa bakaa ya ruzuku ya fedha za matumizi ya kawaida umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4:9**.

Jedwali Na. 4-5 hapa chini linaonesha mwenendo wa bakaa ya fedha za ruzuku ya kawaida kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitatu mfululizo.

**Jedwali Na. 4-5: Mwenendo wa Ruzuku ya matumizi ya kawaida isiyotumika**

| Mwaka | Jumla ya ruzuku iliyopokelewa (SH.TZ) | Ruzuku iliyotumika | Bakaa ya ruzuku (SH.TZ) | % ya bakaa |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 1,984,176,305,424 | 1,714,044,062,102 | 270,132,243,323 | 14 |
| 2015/2016 | 4,523,484,681,888 | 4,350,297,589,014 | 173,327,538,558 | 4 |
| 2014/2015 | 3,482,376,848,057 | 3,388,531,416,909 | 93,845,431,148 | 3 |

### 4.7.2 Bakaa ya fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo Sh. Tz 260,847,695,932

Katika mwaka unaokaguliwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 168 zilipokea jumla ya ruzuku ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 ya Sh. Tz 732,166,960,118. Hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017, fedha zilizotumika kwa mwaka husika ni Sh. Tz 471,319,264,186 na hivyo kuwa na bakaa ya jumla ya Sh. Tz 260,847,695,932 sawa na 36% ya fedha zote za ruzuku ya maendeleo zilizopokelewa. Mchanganuo wa Bakaa ya ruzuku ya fedha za maendeleo umeoneshwa katika **Kiambatisho 4:10**.

Pia, mwenendo wa bakaa ya ruzuku ya maendeleo kwa miaka mitatu mfululizo imeoneshwa katika Jedwali Na. 4-6.

**Jedwali Na. 4-6: Mwenendo wa Ruzuku ya maendeleo isiyotumika**

| Mwaka | Ruzuku iliyo pokelewa (Sh.Tz) | Ruzuku halisi iliyotumika (Sh.Tz) | Bakaa (Sh.Tz) | % ya bakaa | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 732,166,960,118 | 471,319,264,186 | 260,847,695,932 | 36 | 168 |
| 2015/2016 | 586,306,528,447 | 388,699,819,438 | 197,606,709,009 | 34 | 171 |
| 2014/2015 | 550,868,372,532 | 449,532,701,737 | 101,335,670,796 | 18 | 151 |

Kwa bakaa ya ruzuku ya maendeleo na ruzuku ya matumizi ya kawaida, zote zinaashiria kuwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuweza kutekelezwa kwa wakati kutokana na kuchelewa kupokea fedha kutoka Hazina.

Ninaendelea kuishauri Serikali Kuu kupeleka fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa wakati kama zilivyopitishwa katika bajeti ili kuwezesha mamlaka hizo kutekeleza shughuli zake kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## 4.8 Kutothibitika kuidhinishwa kwa nyongeza ya bajeti Sh. Tz 28,168,547,528

Kifungu Na. 43(2) cha Sheria ya bajeti ya mwaka 2015 kinaeleza kuwa, "ongezeko la bajeti linapaswa kuwa ni kwa ajili ya (a) ongezeko lolote au punguzo kutoka bajeti iliyopitishwa, mabadiliko ya malengo, au ongezeko la vifungu vipya ndani ya sheria husika (b) Uhamisho au mabadiliko yoyote ya vifungu vya bajeti kama haviwezi kutekelezeka kupitia mabadiliko ya vifungu vya ndani ya taasisi husika au kubadilika kwa malengo au (c) kuonesha namna ambavyo mfuko mkuu ulivyotumika". Pia Kifungu Na. 43(1) cha Sheria ya Bajeti kinaitaka serikali kuwasilisha nyongeza ya bajeti kwa Bunge kwa ajili ya kuipitisha; bajeti ya ziada kuonesha fedha zilizotumika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa au kutekeleza malengo ambayo hayakuwa yamepangwa kutekelezwa.

Katika kupitia na kulinganisha bajeti na kiwango halisi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 10, imeonekana bajeti halisi iliyopitishwa imerekebishwa kwa Sh. Tz 28,168,547,528, hivyo kupelekea bajeti ya mwisho kuwa Sh. Tz 434,547,765,892 ambayo inaashiria ilitakiwa ipitishwe nyongeza ya bajeti kama Kifungu Na. 43(2) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinavyotaka.

Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na viwango husika ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 4-7.

**Jedwali Na. 4-7: Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 zilizokuwa na bajeti ya ziada**

| Na | Jina la Halmashauri | Bajaeti ya awali (Sh.Tz) | Bajeti iliyo rekebishwa (Sh.Tz) | Bajeti ya Mwisho (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Same | 53,318,890,665 | 3,895,671,264 | 57,214,561,929 |
| 2 | H/W Longido | 24,135,836,000 | 5,146,092,000 | 29,281,928,000 |
| 3 | H/W Hanang' | 31,619,016,000 | 461,973,000 | 32,080,989,000 |
| 4 | H/W Bumbuli | 18,789,164,000 | 121,819,000 | 18,910,983,000 |
| 5 | H/M Kinondoni | 138,556,745,933 | 3,025,302,184 | 141,582,048,117 |
| 6 | H/W Rufiji | 30,384,561,000 | -241,737,000 | 30,142,824,000 |
| 7 | H/W Tandahimba | 30,497,622,806 | 694,734,600 | 31,192,357,406 |
| 8 | H/W Ngorongoro | 22,244,767,700 | 3,380,664,531 | 25,625,432,231 |
| 9 | H/Mji Korogwe | 15,964,458,008 | 8,874,425,634 | 24,838,883,642 |
| 10 | H/W Hai | 40,868,156,252 | 2,809,602,315 | 43,677,758,567 |
| | **Jumla** | **406,379,218,364** | **28,168,547,528** | **434,547,765,892** |

Hata hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuweza kuwasilisha nyongeza ya bajeti kutoka bungeni kuthibitisha uhalali wa matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa au matumizi ambayo hayakuwa yamekasimiwa kama inavyotakiwa na Kifungu Na. 43(1) cha Sheria ya Bajeti, 2015.

Ninapendekeza kwa Menejimeneti za Malaka za Serikali za Mitaa kupata vitabu vya nyongeza za bajeti zilizopitishwa na Bunge kabla ya kuanza kufanya matumizi ya fedha hizo.

# SURA YA TANO

## 5.0 UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA

Sura hii inaonesha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yatokanayo na ukaguzi wa taarifa za kifedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 nilizozikagua katika mwaka husika (2016/2017).

Ukaguzi wa taarifa za fedha huongeza kuaminika kwa taarifa zinazokaguliwa, faraja pamoja na ujasiri zaidi kwa wadau wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Lengo la ukaguzi wa taarifa za fedha ni kuwezesha mkaguzi kutoa maoni, kama taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo yote, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma au mfumo mwingine wa taarifa za fedha unaotambuliwa. Mkaguzi anawajibika kwa kutoa maoni juu ya taarifa za fedha, na kwa upande mwingine, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kuandaa na kutoa taarifa za fedha. Hata hivyo, taarifa hizo haziwezi kuaminika mpaka zitakapokaguliwa.

Mchakato wa ukaguzi unabainisha maeneo ambayo menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kuboresha mifumo yao ya udhibiti, michakato au taratibu, na kuongeza thamani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuongeza ubora wa taratibu zake za uendeshaji.

### 5.1 Wadai wa Halmashauri na malipo kabla ya kupokea huduma yaliyokaa kwa muda mrefu Sh.Tz 138,907,446,027

Madai na malipo kabla ya kupokea huduma ni miongoni mwa vipengele vya Mali zinazotumika kwa kipindi kifupi kama zilivyoainishwa katika Aya 79 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS 1). Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingi, madai na malipo kabla ya kupokea huduma hujumuisha malipo ya awali kwa wakandarasi, mapato yasiyowasilishwa na mawakala wa kukusanya mapato au wakusanyaji wa mapato, karadha, masurufu na mikopo ya Wanawake na Vijana. Ukaguzi wa Mapato yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha pamoja na vielelezo vyake umeonesha kuwapo kwa madai ya Sh.Tz 138,907,446,027 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 161 ambayo hayakuweza kukusanywa kwa muda mrefu kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 5:1** cha ripoti hii.

Ulinganisho wa wadai na malipo yaliyofanyika kabla ya kupokea huduma kwa miaka miwili mfululizo. Unaonesha kuongezeka kwa Sh.Tz 3,980,339,857 kutoka Sh.Tz 134,927,106,170 katika Halmashauri 148 kwa mwaka 2015/16 hadi Sh.Tz 138,907,446,027 katika mwaka 2016/2017 kwa Halmashauri 161 zilizokaguliwa.

Jedwali Na. 5-1 linaonesha mwenendao wa wadaiwa na malipo ya kabla ya uduma kwa miaka mine mfululizo.

**Jedwali Na. 5-1: Mwenendo wa Wadaiwa na malipo ya kabla ya huduma ya muda mrefu kwa miaka Minne mfululizo**

| Mwaka | Kiasi (Sh.Tz). | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 138,907,446,027 | 161 |
| 2015/2016 | 134,927,106,170 | 148 |
| 2014/2015 | 179,026,643,470 | 163 |
| 2013/2014 | 141,648,528,746 | 161 |

Hata hivyo, Halmashauri 7 hazikuandaa mchanganuo wa muda wa madai na malipo yaliyofanyika kabla ya kupokea huduma. Halmashauri hizo ni H/M Iringa, H/W Iringa, H/W Kilolo, H/W Kisarawe, H/W Magu, H/W Meatu na H/W Mwanga. Hivyo, mawanda yangu ya ukaguzi yalizuiliwa kwa kuwa sikuweza kutathmini kiwango ambacho madai haya yameathiri mahitaji ya undeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nina wasiwasi na upatikanaji wa kiasi hiki cha madai kwa sababu bado hakuna dalili kuwa Halmashauri husika zitakusanya kiasi hicho cha madai hivi karibuni au baadaye.

Kwa mara nyingine tena, naendelea kuzikumbusha menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika kuimarisha utaratibu wa kukusanya madai na kuboresha udhibiti katika ukusanyaji wa madeni yaliyokaa muda mrefu. Kuacha madai hayo kwa kipindi hicho cha muda mrefu kunaweza kusababisha ugumu wa namna ya kukusanya na kwa baadhi yake yanaweza kuwa tayari ni madai yasiyolipika tena.

## 5.2 Madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu Sh.Tz 165,562,212,375

Katika vitu vinavyochangia utendaji mzuri katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni jinsi menejimenti zinavyobuni na kutengeneza mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi na kwa wadau wanaoshughulika nao kama vile watoa huduma.

Katika kupitia taarifa ya Hesabu za mwaka unaoishia 30 Juni 2017 nimebaini kuna wadaiwa wa muda mrefu wenye jumla ya Sh. Tz 165,562,212,375, ambapo ni ongezeko la SH.Tz. 9,758,056,955 ukilinganisha na Sh. Tz 155,804,155,420 ilivyoripotiwa katika Taarifa za fedha za mwaka 2015/2016.

Jedwali Na. 5-2 hapa chini linaonesha mwenendo wa madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu kwa kipindi cha miaka minne mfululizo

**Jedwali Na. 5-2: Mwenendo wa madeni ya muda mrefu**

| Mwaka | Kiasi (Sh.Tz) | Idadi ya Halmshauri |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 165,562,212,375 | 158 |
| 2015/2016 | 155,804,155,420 | 154 |
| 2014/2015 | 212,130,677,853 | 163 |
| 2013/2014 | 143,833,939,924 | 161 |

Hata hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa 8 hazikuandaa mchanganuo wa muda wa madeni wakati wa kuwasilisha taarifa zao za fedha ambazo ni H/M Bukoba, H/W Kilolo, H/W Kisarawe, H/W Kwimba, H/W Magu, H/W Meatu, H/W Misungwi na H/W Mwanga. Katika hali hiyo, sikuweza kutathmini ni kwa kiwango gani Mamlaka hizi za serikali za Mitaa zinaweza kulipa madeni hayo na kuweka viwango vizuri vya uendeshaji wa shughuli zao.

Madeni yasiyolipwa yameoneshwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. 5:2** cha ripoti hii.

Ninashauri kuwa, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kulipa madeni wanayodaiwa mapema inavyowezekana. Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa ziandae mchanganuo wa muda wa madeni ili kuwezesha kutambulika muda wa madeni utakaoweza kusaidia kuweka Mikakati ya kulipa. Pia, udhibiti wa kutosha, sera na taratibu zinapaswa kuwekwa na menejimenti ili kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibika kwa miadi yoyote iliyowekwa wakati hawana fedha.

## 5.3 Kesi dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinaweza kuathiri mtiririko endelevu wa kifedha Sh.Tz 186,443,100,559

Ukaguzi wa Taarifa za hesabu za mwaka husika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umejumuisha upembuzi wa kesi zilizoko mahakamani dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ili kuweza kufanya tathmini ya athari inayoweza kupatikana katika kutoa huduma pindi uamuzi wowote wa kimahakama utakaotolewa kulingana na kesi zilizopo kupelekea Halmashauri kushindwa.

Wakati wa ukaguzi nilibaini, kuwa jumla ya kesi 1,111 dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 116 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali. Kesi hizo ni za madai ya jumla ya Sh.Tz 186,443,100,559 ambapo kesi 165 (15%) katika Halmashuari 7 zenye thamani ya sh.Tz 133,526,200,884 ni kiwango kilichotengwa na kutolewa taarifa katika Taarifa za fedha kwa mujibu wa Aya 100 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma Na.19 (IPSAS 19); wakati kesi 46 (4%) katika Halmashauri 6 zenye kiasi cha Sh.Tz 5,380,150,112 zilioneshwa lakini hakuna kiwango kilichotengwa na kuoneshwa katika taarifa za hesabu zilizowasilishwa. Aidha, kesi 900 (81%) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 103 zenye thamani ya Sh. Tz 147,536,749,563 hazikuoneshwa katika taarifa za fedha zilizowasilishwa.

H/M Ilala inaongoza kwa kuwa na kesi 78, ikifuatiwa na H/M Morogoro yenye kesi 45, na H/Jiji Tanga yenye kesi 39. Mchanganuo wa kesi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 5:3** katika ripoti hii.

UlinganishO wa kesi zilizopo mahakamani kwa miaka miwili (2) mfululizo umeonesha kupungua kwa kesi; hadi kufikia kesi 1,111 kwa Mamlaka za serikali za mitaa 116 kwa mwaka 2016/2017 kutoka kesi 1206 za Mamlaka za Serikali za Mitaa 115 kwa mwaka 2015/2016. Vivyo hivyo, jumla ya madai yamepungua hadi kufikia Sh. Tz 186,443,100,559 ikilinganishwa na madai ya mwaka 2015/2016 yaliyokuwa na thamani ya Sh.Tz 264,920,968,506.

Hata hivyo, sehemu kubwa ya kesi hizi imetokana na kuvunjwa kwa mikataba kati ya Wakandarasi na Halmashauri, kesi za watumishi pamoja na migogoro ya ardhi.

Pamoja na kupongeza juhudi zilizofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zimepelekea kupungua kwa idadi ya kesi katika mwaka huu wa ukaguzi, ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa

kuchukua hatua ya kupunguza wingi wa kesi kwa kuzuia matendo yoyote au makosa ambayo yanaweza kupelekea kushtakiwa. Menejimenti zinapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika kutimiza majukumu yao ya kila siku ili kupunguza au kuondoa uwezekano wa matukio yatakayopelekea kushtakiwa. Pale inapowezekana, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuwashawishi washtaki ili yafanyike majadiliano nje ya mahakama ili kupunguza uwezekano wa kulipa fedha nyingi iwapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa zitashindwa kesi hizo.

## 5.4 Mapato yaliyoripotiwa katika daftari la mapato na matumizi lakini hayakuonekana katika taarifa ya benki Sh. Tz 279,707,282

Kulingana na Agizo 29(2) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 2009, linataka waweka hazina wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha usuluhisho unafanyika, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa akaunti mbali mbali sanjari na kufanya usuluhishi kati ya daftari la fedha na taarifa za benki kila mwezi na kufanya masahihisho ipasavyo. Katika kupitia daftari la mapato na matumizi kwa mwaka husika, mapato yenye thamani ya Sh.Tz 279,707,282 kwa mamlaka za Serikali za Mitaa mbili, mapato yameingizwa katika daftari la mapato na matumizi lakini hayakuonekana katika Taarifa za kibenki kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na.5-3

**Jedwali Na. 5-3: Mapato yaliyoonekana katika daftari la mapato na matumizi lakini hayakuonekana katika taarifa za kibenki**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Bukoba | 60,487,040 |
| 2. | H/M KIgoma Ujiji | 219,220,242 |
| | **Jumla** | **279,707,282** |

Kutokuwepo kwa ufuatiliaji katika usuluhishi wa taarifa za benki na taarifa katika daftari la mapato na matumizi kunaweza kupelekea kufanyika udanganyifu au makosa ya kibenki kutokea bila kutambulika mapema. Pia, kutokuandaa usuluhishi wa kibenki kunaweza kupotosha watumiaji wa taarifa ya fedha kuhusu uhalisia wa salio ishia la fedha taslimu katika akaunti za Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi kufikia mwisho

wa mwaka. Zaidi ya hayo, pale masuala yote yanayotakiwa kurekebishwa katika usuluhishi wa kibenki, yakibaki kwa muda mrefu bila kurekishwa yanaweza kusababisha kutumika vibaya kwa fedha za umma kitu kinachoweza kupelekea hasara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakumbushwa kuandaa usuluhishi wa kibenki kila mwisho wa mwezi ikifuatiwa na kuidhinishwa na Maafisa Waandamizi. Pia, hatua madhubuti zinatakiwa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa masula yote yaliyosalia kwa muda mrefu yanashughulikiwa au kurekebishwa katika usuluhishi wa kibenki.

## 5.5 Makosa katika taarifa za fedha zilizowasilishwa Sh. 50,090,445,925

Agizo 31(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, na Kifungu 45(4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) inamtaka Afisa Masuuli kutayarisha na kuziwasilisha taarifa za fedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi kisichozidi miezi (3) baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha kwa maana ya tarehe 30 September ya kila mwaka.

Nimeibaini kuwa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa 6 zina makosa kadhaa ya kitarakimu, kuacha kuonesha baadhi ya taarifa muhimu, na utoaji taarifa usio sahihi uliopelekea taarifa za fedha zilizowasilishwa kukosa usahihi. Thamani ya jumla ya makosa kwa taarifa za fedha zilizowasilishwa ni Sh.Tz 50,090,445,925; kasoro hii pamoja na masuala mengine, imenilazimu kutoa Hati zisizoridhisha tatu na Hati zenye mashaka tatu kama zilivyoainishwa katika Jedwali Na. 5-4 hapa chini.

**Jedwali Na. 5-4: Makosa yaliyoonekana katika Taarifa ya Fedha**

| Jina la Halmashauri | Aina ya hati ya ukaguzi | Jumla ya Makosa (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| H/M Kigoma/Ujiji | Isiyoridhisha | 14,020,977,349 |
| H/W Kigoma | Isiyoridhisha | 29,042,829,125 |
| H/W Pangani | Isiyoridhisha | 5,852,292,654 |
| H/M Tabora | Yenye mashaka | 217,181,426 |
| H/W Ukerewe | Yenye mashaka | 79,488,750 |
| H/W Lushoto | Yenye mashaka | 877,676,621 |
| **Jumla** | | **50,090,445,925** |

Hii imetokana na kuchangiwa na ukosefu wa watumishi mahiri katika kuandaa taarifa za kifedha; pia, kwa kutofahamu Miongozo ya kimataifa katika uandaaji wa taarifa za fedha.

Kama nilivyowahi kushauri mara nyingi, ninaendelea kushauri Maafisa Masuuli wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa wanahitaji kuwahusisha wakuu wote wa idara katika kutoa taarifa zote muhimu kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha. Pia, Maafisa Masuuli wote wanapaswa kuimarisha mchakato wa kudhibiti ubora wa taarifa na ratiba ya uandaaji wa taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa zinazowasilishwa kwa ukaguzi. Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa upande mwingine, inapaswa kuandaa mafunzo ya kujenga uwezo yatakayowahusisha watumishi wanaohusika katika kuandaa taarifa za fedha.

## 5.6 Msisitizo juu wa shughuli za Mfuko wa Barabara ambao kazi zake zimechukuliwa na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikitekeleza shughuli za Mfuko wa Barabara katika ngazi za Wilaya. Hata hivyo, Kifungu Na. 3 (1) cha Sheria ya Wakala wa Serikali (Sura ya 245) kilitangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 211 la tarehe 12, 2017 kuanzisha Mamlaka ya Wakala wa Msimamizi wa Barabara Mijini na vijijini (TARURA), ambayo ilizinduliwa tarehe 2 Julai 2017 na kuchukua shughuli zote zilizokuwa zikitekelezwa na Mfuko wa Barabara rasmi kuanzia tarehe 01 Julai 2017. Matokeo ya kuuchukua Mfuko wa Barabara na kuwekwa kwenye taasisi hii mpya. Maoni yangu ni kwamba, mifumo ya Barabara yenye thamani ya Sh. Tz 622,778,967,107 na fedha taslim kiasi cha Sh. Tz 68,294,093,494 ambazo ziliripotiwa katika taarifa za fedha za mwaka 2016/2017 katika kipengele cha Mfuko wa Barabara, hazitakuwa sehemu ya mali katika taarifa za fedha na za uendeshaji za mwaka 2017/2018 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Mchanganuo umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 5:4**

Kwa mtazamo huo, thamani ya mali za kudumu, bakaa ya fedha taslimu na madeni (kama yapo) kwa Mamlaka za serikali za Mitaa itapungua kiwango cha thamani ya mali, madeni na masuala yote yanayohusiana na mchakato huo kama yapo.

Kwa Hiyo, Ninashauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha utunzaji sahihi wa taarifa za fedha na vitabu vya kumbukumbu kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma ili kuzuia makosa katika kuwasilisha taarifa za fedha za mwaka 2017/2018.

## SURA YA SITA

## 6.0 TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI NA MASUAL YA UTAWALA

Sehemu hii ya utangulizi inaelezea juu ya matokeo yanayohusiana na mambo mbalimbali ya mfumo wa udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na mfumo wa uhasibu, utendaji wa kitengo cha ukaguzi cha ndani, utendaji wa Kamati ya Ukaguzi, tathmini ya viashiria hatarishi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ujumla, na usimamizi wa tathmini ya ubadhirifu.

Ukaguzi wa mfumo wa udhibiti wa ndani unafanyika kwa mujibu wa agizo Na. 25 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linalozitaka Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kupitia kwa Mtunza Hazina, kuhifadhi kumbukumbu za fedha na mifumo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria zilizoandikwa, kanuni na miongozo iliyotolewa na Waziri na Bodi ya Viwango vya Uhasibu wa Kimataifa (IASB) kwa kuwa zinahusiana na uhasibu katika sekta ya umma.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, mapungufu yafuatayo yalibainika:

### 6.1 Mapungufu katika mifumo ya TEHAMA na Uhasibu

Shughuli za kifedha za Halmashauri nyingi huandaliwa kwa kutumia Mfumo wa uhasibu ujulikano kama EPICOR Toleo Na.9.05 na Halmashauri chache hutumia Toleo Na.10 (Mfumo funganishi wa usimamizi wa Fedha). Katika kipindi cha ukaguzi, tathmini ya utayari na ufanisi wa Epicor na mifumo mingine inayotumiwa na Halmashauri 39 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulibaini kujirudia kwa makosa mbalimbali licha ya makosa hayo kubainishwa katika ripoti zangu za kila mwaka kama inavyoainishwa hapa chini; kwa maelezo zaidi tazama **Kiambatisho Na. 6:1.**

Mfumo Funganishi wa Uhasibu (EPICOR-IFMS) haujafungamanishwa na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS); unafanya kazi kama mfumo wa udhibiti wa fedha taslimu ambao unachukua miamala ya fedha taslimu na kuacha miamala inayofanyika pasipo malipo. Kwa hiyo, ili kukamilisha hesabu za mwaka za Halmashauri, marekebisho na ujumuishaji wa hesabu hulazimika kufanywa nje ya mfumo.

- Kutokana na Mfumo wa Uhasibu (EPICOR) kutofungamanishwa na mifumo mingine inayotumiwa na Halmashauri kama vile Mfumo wa Mishahara “LAWSON”, Mfumo wa Mipango “PLANREP” na Mfumo wa Kukusanya Mapato “LGRCIS”, Halmashauri hulazimika kuingiza taarifa kwenye Leja Kuu (General Ledger) iliyo kwenye Mfumo wa Uhasibu (EPICOR) kwa njia za kawaida (manually).
- Baadhi ya moduli (modules) zilizoko kwenye Mfumo wa Uhasibu (Epicor) hazitumiki. Moduli hizo ni kama vile Moduli ya Madeni, Madai, Masurufu, Manunuzi na Usimamizi wa Mali na kusababisha Halmashauri kuandaa taarifa hizo nje ya mfumo.

Ninapendekeza kuwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kuhakikisha kuwa Mifumo ya Uhasibu (Epicor) unalinishwa na ifungamanishwe na mifumo mingine muhimu inayotumiwa na Halmashauri; na kuhakikisha kwa moduli zake zote zinatumiwa kikamilifu, kuimarisha mfumo wa mtandao ili kuboresha mfumo wa uingizaji taarifa na kuongeza ufanisi na upatikanaji wa taarifa za fedha.

## 6.2 Mapungufu katika Mazingira ya Jumla ya Mfumo wa Teknolojia ya Habari

Udhibiti wa teknolojia ya habari ni msingi wa udhibiti wa kimazingira kwa kuwa unatoa uhakika wa mifumo kufanya kazi kama ilivyopangwa, na kwamba, matokeo yake ni ya kuaminika. Udhibiti wa Teknolojia ya Habari upo ndani ya mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri ili kutoa uhakika kuhusu usiri, uaminifu na upatikanaji wa taarifa.

Ukaguzi wa mazingira ya udhibiti wa Teknolojia ya Habari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 91 ulibaini mapungufu yafuatayo; kwa maelezo zaidi angalia **Kiambatisho Na. 6:2**

- Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazina sera ya Teknolojia ya Habari inayoweza kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miundombinu ya Teknolojia ya Habari ikiwa ni pamoja na programu za kompyuta na vifaa vya TEHAMA.
- Kutokuwapo kwa mipango ya kupima na maafa wa TEHAMA katika Mamlaka za Serikali za Mitaa huweza kusababisha upotevu wa data

utakaosababishwa na kushindwa kurejeshwa kwa mfumo endapo mfumo utashindwa kufanya kazi.

- Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazina mikakati ya kulinda vifaa vyote vya kompyuta na programu zake kupitia Teknolojia ya Habari kama vile kupambana na virusi “antivirus”, vyumba maalum kwa ajili ya vifaa vya TEHAMA na mfumo wa kuzuia na kuzima moto.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa hazijajenga uwezo wa kutosha kwa wafanyakazi wake kwa upande wa TEHAMA.
- Kitengo cha Teknolojia ya Habari kuwa na uhaba wa wafanyakazi/watumishi, ambapo hupunguza wigo wa kazi zao zilizopangwa kila mwaka.
- Halmashauri nyingi hazikuandaa mpango mkakati wa Teknolojia ya Habari, hivyo tathmini ya utekelezaji wa mpango wa Teknolojia ya Habari haukufanyika.

Kwa hivyo, ninapendekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuandaa Sera na taratibu za Teknolojia ya Habari ili watumishi wote wafahamu wajibu na majukumu yao katika kulinda na kutumia vyema vifaa na programu za TEHAMA.

## 6.3 Utendaji usioridhisha wa Kamati za Ukaguzi

Agizo Na. 12 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 2009, linazungumzia kuanzishwa kwa Kamati ya Ukaguzi kwa kila Halmashauri, na majukumu ya Kamati. Kamati ya Ukaguzi ina jukumu muhimu katika kujenga mazingira mazuri ya kuimarisha utawala bora. Wakati wa kutathmini utendaji wa Kamati za Ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 140 kwa mwaka wa ukaguzi nilibaini mapungufu yafuatayo; kwa maelezo zaidi rejea **Kiambatisho Na.6:3:**

- Kamati hazikukutana angalau mara moja kwa kila robo mwaka kinyume na Agizo Na. 12 (5a) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009.
- Kamati hazikupitia taarifa za fedha, sera ya usimamizi wa viashiria hatarishi na kuchambua mikakati ya kuchunguza na kuzuia ubadhirifu.
- Wengi wa wanakamati wa Kamati za Ukaguzi hawakuwa na ufahamu wa mambo ya kifedha/kihasibu.
- Kamati nyingi za Ukaguzi hazikuandaa na kuwasilisha ripoti ya majukumu yake ya mwaka.

Ninapendekeza kuwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika zihakikishe Kamati za Ukaguzi zinatimiza majukumu yake kikamilifu katika uangalizi wa mifumo ya utoaji taarifa za kifedha, taratibu za kusimamaia athari zinazotokana na shughuli za kifedha, udhibiti juu ya utekelezaji wa sheria, maadili, kanuni na taratibu.

## 6.4 Upungufu katika utendaji kazi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ni kitengo huru kinachojitegemea katika utendaji kazi za udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kuchunguza na kutathmini ufanisi na utoshelevu wa udhibiti huo. Agizo Na. 13 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 na kifungu Na. 48(1) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa 1982 (Kilichorekebishwa 2000) linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha na kuimarisha Ufanisi wa Ukaguzi wa Ndani kama sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani ya Halmashauri.

Nilifanya tathmini ya ufanisi wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani na kubaini mapungufu yafuatayo; kwa maelezo zaidi rejea **Kiambatisho Na. 6.4:**

- Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani vingi vina uhaba wa watumishi; hivyo havifanyi kazi kufuatana na mpango kazi wa mwaka.
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimetengewa bajeti isiyokidhi mahitaji yake, hivyo hupelekea kushindwa kutekeleza kikamilifu mpango-kazi wake.
- Halmashauri za Serikali za Mitaa kushindwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kama vile EPICOR, LAWSON, PLANREP na LGRCIS.
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakina vitendea kazi vya kutosha kama vile shajara, kompyuta na magari kwa ajili ya kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.
- Baadhi ya vitengo vya ukaguzi wa ndani havikuandaa mpango wa ukaguzi ambao hutoa muongozo wa majukumu ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.

Ninapendekeza kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani vinapatiwa rasilimali watu na fedha za kutosha ili kuviwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na kwa ukamilifu.

## 6.5 Mapungufu katika uanzishwaji wa Kitengo cha Kusimamia Vihatarishi

Menejimenti ya vihatarishi ni mchakato endelevu ambao na hutumika kwa ajili ya kufanya maamuzi katika awamu zote za miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ili kufanikisha hili, Halmashauri zinapaswa kupanga mikakati na misingi ambayo itawezesha kutambua athari na kuzikabili. Barua yenye kumb. Na LH.274/394/03/30 ya tarehe 25.10.2016 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango iliziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vitengo cha kusimamia vihatarishi na kuteua Mratibu. Hata hivyo, nilibaini kuwa Mamlaka nyingi hazikuanzisha Kitengo cha Kusimamia Vihatarishi na Mamlaka chache ziliteua waratibu, lakini waratibu hawa hawakupewa mafunzo yoyote kuhusu majukumu yao.

Wakati wa ukaguzi wa taarifa za kifedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa 71, nilibaini kuwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikutathmini vihatarishi vilivyo katika halmashauri; aidha, hakuna hatua zilizochukuliwa kupunguza athari zilizopo.

Kukosekana kwa waratibu wa vihatarishi na sera ya usimamizi wa athari kunazifanya Halmashauri kutokuwa katika nafasi nzuri ya kukabiliana na athari punde zitakapojitokeza, hivyo kuathiri shughuli zao za sasa na za baadaye. Yafuatayo ni muendelezo wa mapungufu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi; kwa maelezo zaidi **Kiambatisho Na. 6.5**:

- Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazikufanya tathmini ya kutambua viashiria hatarishi kwa maeneo yanayohusishwa na udhibiti wa ndani.
- Sera za vihatarishi zilizopo katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hazihuishwi ili kuendana na athari mpya zinazoweza kujitokeza.
- Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hawana ufahamu juu ya umuhimu wa sera ya kusimamia vihatarishi na udhibiti wa ndani.
- Halmashauri za Serikali za Mitaa nyingi hazina Mpango mkakati unaohusu vihatarishi.

Ninapendekeza kuwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa ziteue waratibu wa kusimamaia vihatarishi na kuwaeleza wajibu na majukumu

yao ya kutambua na kukabiliana na athari ambazo zinaweza kusabisha kutofikia malengo ambayo Mamlaka za Serikali za Mitaa zimejiwekea. Ili kutimiza lengo hili, Mratibu anapaswa kuanzisha utaratibu sahihi wa utambuzi, tathmini, uainishaji, uchambuzi, ufuatiliaji na jinsi ya kukabiliana na athari tarajiwa.

## 6.6 Mapungufu katika mpango wa kuzuia na kukabiliana na ubadhirifu

Dalili za ubadhirifu zinaweza kuelezwa kuwa ni hali ambayo moja kwa moja inatokana na shughuli zisizokuwa za uaminifu au udanganyifu; na hii inaweza kuwa ni udanganyifu wenyewe au jaribio la kuficha udanganyifu.

Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi (ISSAI 1240) vinaelezea "Ubadhirifu" kuwa ni kitendo cha makusudi kinachofanywa na mtu mmoja au zaidi ndani ya menejimenti, wale wanaohusika na utawala, watumishi, au washiriki wengine kwa njia ya udanganyifu ili kupata manufaa au faida haramu.

Lengo la kufanya tathmini ya ubadhirifu ni kuniwezesha kutoa hakikisho Bungeni kwamba Halmashauri zina mfumo unaofaa katika kuzuia na kukabiliana na ubadhirifu. Masuala yaliyobainika yanaashiria kwamba mfumo wa udhibiti wa ndani unaweza kushindwa kugundua na kuzuia ubadhirifu unaohusiana na shughuli au miamala ya kilaghai bila ya menejimenti kuwa na taarifa.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini mapungufu yafuatayo katika tathmini ya kuzuia ubadhirifu; kwa maelezo zaidi rejea **Kiambatisho Na. 6:6:**

- Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazina mipango ya kutambua na kukabiliana na ubadhirifu.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingi hazina nyaraka zozote zinazoonyesha kuwa kuna mifumo maalum ya kutambua na kukabiliana na athari au makosa yanayotokana na ubadhirifu.
- Hakuna taratibu zilizowekwa za kufanyia kazi ubadhirifu ulioonekana.

Mbali na mapungufu ya tathmini, kuzuia na kukabiliana na ubadhirifu yaliyotajwa hapo juu, kuna masuala ya ziada yaliyotokeza katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye thamani ya Sh.Tz 52,514,388

ambayo yanaonesha uwezekano wa kuwepo kwa udanganyifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Jedwali Na. 6-1: Ubadhirifu uliobainishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Ubadhilifu uliojitokeza | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ileje | Matumizi yasiyo sahihi | 15,686,350 |
| 2 | H/W Makete | Makato ya Madiwani kutowasilishwa benki | 15,789,404 |
| 3 | H/Mji Bariadi | Matumizi yasiyo na viambata | 7,769,742 |
| 4 | H/W Morogoro | Kushndwa kuthibitika kwa uhalali wa matumizi ya mafuta yaliyotumika | 13,268,892 |
| Jumla | | | **52,514,388** |

Hivyo, ninapendekeza kuwa manejimenti za Halmashauri ziimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani ili ya kubaini na kuzuia vihatarishi vinavyohusiana na ubadhirifu; pia ziwe na mipango iliyoidhinishwa kwa ajili ya kukabiliana na vihatarishi. Vile vile, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa zinafanya tathmini ya mara kwa mara ya vihatarishi vya ubadhirifu na kuchukua hatua stahiki.

## SURA YA SABA

## 7.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

Malipo ya mshahara ni mchakato unaofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwalipa watumishi wake stahiki zao. Inajumuisha kumbukumbu za mshahara na ujira kwa wafanyakazi, kodi ya mapato (PAYE) na makato mengine. Usimamizi wa orodha ya malipo ya mshahara unahitaji utunzaji sahihi wa kumbukumbu na uhuishaji wa mara kwa mara wa mfumo wa malipo (HCMIS). Hii ni kwa sababu wafanyakazi humakinikia sana na mapungufu mbali mbali makosa mbalimbali katika mchakato wa mishahara. Mfumo wa ulipaji wa mishahara unaosimamiwa vizuri hutoa uhakika wa malipo kwa wakati kwa wafanyakazi. Usimamizi wa ulipaji wa mishahara pia hujumuisha kuhakikisha Sera ya kulipa mishahara ya Serikali inafuata Sheria na Kanuni na Taratibu zinazosimamia ajira.

Menejimenti ya rasilimali watu inajumuisha shughuli, sera, na matendo yanayohusika katika kupata, kuendeleza, kutumia, kutathmini, kudumisha, na kuweka idadi sahihi na ujuzi wa wafanyakazi ili kukamilisha malengo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Malipo ya mshahara na usimamizi wa rasilimali watu ni sehemu muhimu ya mfumo wa jumla wa usimamizi wa kifedha na utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote. Pia, inajulikana kuwa, utawala bora wa malipo na usimamizi wa rasilimali watu ni muhimu sana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwa na matokeo chanya na ufanisi katika kutumikia jamii ingawa bado kuna udhaifu unaozuia Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia malengo yao. Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu niliyobaini wakati wa ukaguzi nilioufanya:

### 7.1 Upungufu wa watumishi 155,013

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, idadi sahihi na ujuzi stahiki wa wafanyakazi ni kitu muhimu sana kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukamilisha malengo yao. Tathmini yangu kuhusu idadi ya watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 161 nilizozichagua

imebaini upungufu wa watumishi 155,013 sawa na asilimia 32 ya idadi inayohitajika ya watumishi ni 477,829 kama ilivyochanganuliwa katika **Kiambatisho Na. 7:1** cha taarifa hii.

Mwenendo wa miaka mitatu mfululizo unaonyesha kupungua kwa rasilimali watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kujali mapendekezo niliyotoa juu ya suala hilo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, upungufu ulikuwa 22% katika Mamlaka 117 nilizokagua, mwaka wa fedha 2015/2016 upungufu ulikuwa 30% kwa Mamlaka 126 na mwaka wa fedha 2016/2017 upungufu uliongezeka hadi 32% kama ilivyo katika Jedwali Na. 7-1 hapa chini

**Jedwali Na. 7-1: Mwenendo wa idadi ya watumishi kwa miaka mitatu mfululizo.**

| Mwaka | Mamlaka zilizojaribiwa | Mahitaji | Upungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 161 | 477,829 | 155,013 | 32 |
| 2015/2016 | 126 | 349,974 | 106,426 | 30 |
| 2014/2015 | 117 | 324,557 | 71,803 | 22 |

Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI hazikuchukua hatua stahiki kujaza pengo la watumishi. Pia, kupunguza watumishi waliokosa sifa za utumishi (vyeti visivyo halali) katika utumishi wa umma bila kuwa na mikakati ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi ndani ya muda mfupi kumesababisha upungufu mkubwa wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa kuzingatia upungufu wa watumishi, ufanisi na matokeo ya utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeathiriwa kwa kiasi kikubwa. Wafanyakazi wachache waliopo wanalazimika kubeba majukumu zaidi ili kukidhi matarajio ya wateja. Hii inaweza kusababisha matatizo ya kiafya, pia kushuka kwa ari ya kufanya kazi na maadili ya kazi. Sekta zilizoathiriwa zaidi ni Afya, Kilimo na Elimu.

Ili Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kufikia malengo yao ya kutoa huduma bora kwa umma, ninapendekeza kwa wahusika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Hazina kuweka utaratibu utakaohakikisha upatikanaji wa

fedha kwa ajili ya kuajiri wafanyakazi wapya kujaza nafasi zilizopo, uhifadhi wa wafanyakazi wenye ujuzi na utoaji wa motisha maalum kwa wafanyakazi kufanya kazi katika Halmashauri zenye upungufu mkubwa.

### 7.2 Kuwapo kwa maafisa wanaokaimu nafasi za uandamizi kwa muda mrefu

Agizo D 24 (3) la Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 ambalo linasisitiza mtumishi wa umma kutokaimu nafasi ya wazi kwa muda unaozidi miezi sita halikuzingatiwa.

Kama afisa anayekaimu hana sifa za nafasi hiyo, mamlaka ya uteuzi inatakiwa kuhakikisha kuwa mchakato wa kuteua mkuu wa kitengo husika unakamilika ndani ya kipindi cha miezi sita.

Katika kupitia majalada binafsi na kufanya mahojiano na Wakuu wa Idara na Vitengo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 113 nilibaini kuwa maafisa 586 walikuwa wakifanya kazi kwa kukaimu ukuu wa idara au kitengo kwa zaidi ya miezi sita kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 7-2** cha ripoti hii. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, wengi wa maafisa waliokuwa wakikaimu hawakuwa na sifa zinazostahili kwa ajili ya nafasi hizo; pia, ilitokana na kuchelewa kwa uteuzi wa watu wanaostahili kutoka kwa mamlaka za uteuzi.

Pia, nilibaini kuwa tatizo la upungufu wa watumishi liliongezeka kwa kuanzishwa kwa Halmashauri mpya bila mikakati ya kuwa na maafisa wenye sifa kabla ya kuanzishwa kwa Halmashauri hizo mpya. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2016/2017, niliangalia Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 ambazo zilikuwa na maofisa 67 wanaofanya kazi kwa kukaimu nafasi za juu kama ilivyoelezwa katika Jedwali Na. la 7-2 hapa chini:

**Jedwali Na. 7-2: Idadi ya maafisa waliokuwa wakikaimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mpya ambazo zimeanzishwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Maofisa waliokaimu zaidi ya miezi sita |
|---|---|---|
| 1. | H/Mji Bunda | 10 |
| 2. | H/W Chalinze | 4 |
| 3. | H/Mji Ifakara | 8 |
| 4. | H/W Kibiti | 2 |
| 5. | H/M Kigamboni | 10 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Maofisa waliokaimu zaidi ya miezi sita |
|---|---|---|
| 6. | H/Mji Kondoa | 7 |
| 7. | H/W Madaba | 8 |
| 8. | H/W Malinyi | 6 |
| 9. | H/Mji Mbinga | 8 |
| 10. | H/Mji Mbulu | 4 |
| **Jumla** | | **67** |

Kufanya kazi katika nafasi ya kukaimu kwa muda mrefu hushusha ari ya kazi. Hii inaweza kusababisha afisa kutumia ofisi ya umma kwa maslahi binafsi au kutoa huduma zilizo chini ya kiwango.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahimizwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI kuharakisha mchakato wa upekuzi kwa maofisa wanaokaimu vyeo ili wathibitishwe au kama itashindikana, basi uteuzi wa maafisa wenye sifa kwenye nafasi hizo ufanyike.

Pia, ninapendekeza kuwa mamlaka za uteuzi ziteua maafisa waliohitimu na wenye uwezo kwa ajili ya Mamlaka Mpya za Serikali za Mitaa zilizoanzishwa hivi karibuni. Kufanya hivyo kutawasaidia kutoa huduma inayotarajiwa kwa muda mfupi.

## 7.3 Kulipwa mshahara ghafi chini ya theluthi moja kila mwezi

Sehemu ya 3 ya Kanuni ya Maafisa Walioainishwa (Urejeshwaji wa Madeni) ya Sheria Na.7 ya mwaka 1970 na kusisitiziwa na Waraka wenye Kumb. Na: CE.26/46/01/1/66 wa tarehe 28 Novemba, 2012 vinaelekeza kwamba, makato katika mishahara ya watumishi yanatakiwa yasizidi theluthi mbili (2/3) ya mishahara yao ghafi.

Katika ukaguzi wa mishahara na nyaraka mbalimbali katika Halmashauri 58 katika mwaka 2016/2017 kulibainika kuwapo kwa wafanyakazi 4,830 ambao walipokea mishahara yao chini ya theluthi moja ya mishahara yao ghafi. Ilikuwa ni matarajio yangu kwamba, makato mengi yangepungua kwa kipidi kirefu kutokana na kuanzishwa kwa udhibiti kwa kutumia mfumo wa LAWSON Serikalini, lakini hali imekuwa sivyo. Ufafanuzi upo katika Jedwali Na. 7-3 hapa chini.

**Jedwali Na. 7-3: Orodha ya Halmashauri na idadi ya wafanyakazi wanaolipwa mishahara chini ya 1/3 ya mshahara wa kila mwezi**

| Na. | Jina la Mamlaka | Watumishi waliohusika | Na. | Jina la Mamlaka | Watumishi waliohusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 147 | 30 | H/W Madaba | 13 |
| 2 | H/W Arusha | 343 | 31 | H/W Mafia | 58 |
| 3 | H/W Babati | 2 | 32 | H/W Magu | 242 |
| 4 | H/W Bariadi | 40 | 33 | H/Mji Makambako | 11 |
| 5 | H/Mji Bariadi | 96 | 34 | H/W Makete | 102 |
| 6 | H/W Buchosa | 38 | 35 | H/W Mbinga | 66 |
| 7 | H/W Bukoba | 146 | 36 | H/W Mbogwe | 17 |
| 8 | H/W Busokelo | 47 | 37 | H/W Meatu | 21 |
| 9 | H/W Chalinze | 63 | 38 | H/W Missenyi | 94 |
| 10 | H/W Chamwino | 211 | 39 | H/W Mkinga | 77 |
| 11 | H/W Chunya | 25 | 40 | H/W Mlele | 25 |
| 12 | H/W Hai | 225 | 41 | H/W Monduli | 136 |
| 13 | H/W Handeni | 59 | 42 | H/W Mpanda | 59 |
| 14 | H/Mji Handeni | 15 | 43 | H/W Mpwapwa | 107 |
| 15 | H/W Igunga | 134 | 44 | H/W Mufindi | 62 |
| 16 | H/W Ileje | 21 | 45 | H/W Muheza | 50 |
| 17 | H/M Ilemela | 69 | 46 | H/W Mwanga | 176 |
| 18 | H/W Iringa | 68 | 47 | H/W Ngorongoro | 11 |
| 19 | H/W Kalambo | 98 | 48 | H/W Nsimbo | 39 |
| 20 | H/W Kaliua | 83 | 49 | H/W Nyasa | 17 |
| 21 | H/W Karagwe | 132 | 50 | H/W Pangani | 65 |
| 22 | H/W Karatu | 94 | 51 | H/W Same | 220 |
| 23 | H/Mji Kibaha | 106 | 52 | H/W Sengerema | 98 |
| 24 | H/W Kilindi | 104 | 53 | H/W Sikonge | 16 |
| 25 | H/W Kilwa | 12 | 54 | H/W Songea | 45 |
| 26 | H/W Kongwa | 41 | 55 | H/M Songea | 59 |
| 27 | H/Mji Korogwe | 89 | 56 | H/W Sumbawanga | 4 |
| 28 | H/W Longido | 40 | 57 | H/M Tabora | 191 |
| 29 | H/W Lushoto | 156 | 58 | H/Mji Tunduma | 45 |
| **Jumla** | | | | | **4,830** |

Mwenendo wa kuongezeka au kupungua kwa makato ya mishahara kwa watumishi kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita unaonyesha kupungua kwa mwaka 2015/2016 ikilinganishwa na matukio yaliyoripotiwa mwaka 2014/2015. Lakini, mwaka wa fedha wa 2016/2017 kulikuwa na ongezeko kubwa la wafanyakazi ambao walipokea mshahara chini ya theluthi moja ya mishahara yao ghafi. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, nilibaini jumla ya watumishi 789 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 16 na mwaka

wa fedha wa 2015/2016 katika Halmashauri 33, wafanyakazi wapatao 625 walilipwa mishahara amabayo ilikuwa chini ya theluthi moja ya mishahara yao ghafi. Jedwali Na. 7-4 linatoa ufafanuzi zaidi.

**Jedwali Na. 7-4: Mwenendo wa watumishi waliopokea mshahara chini ya 1/3 ya mshahara wa kila mwezi kwa miaka mitatu iliyopita**

| Mwaka | Halmashauri | Idadi ya watumishi waliopokea mshahara chini ya 1/3 ya mshahara |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 58 | 4,830 |
| 2015/2016 | 33 | 625 |
| 2014/2015 | 16 | 789 |

Ongezeko hilo limesababishwa na mabadiliko ya kiwango kipya cha asilimia 15 kwa wafanyakazi ambao ni wanufaika wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) badala ya asilimia nane (8%) iliyokuwa ikikatwa awali. Baada ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo (HESLB) ya mwaka 2016, Serikali iliamua kuanza kutumia asilimia 15 kwa ajili ya kupunguza mkopo bila kujali kiasi cha mshahara wa mtumishi kitakachosaidia.

Makato mengi kwenye mishahara ya watumishi yanaweza kuathiri utendaji na ustawi wao, hivyo, kuathiri utoaji wa huduma za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, kiasi kikubwa cha makato ya mshahara kinaweza kusababisha mtumishi wa umma kuingia kwenye majaribu kwa urahisi na kushiriki katika matumizi mabaya ya fedha za umma. Zaidi, huweza kusababisha matumizi mabaya ya ofisi kwa faida binafsi.

Kwa maoni yangu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kwa ujumla zinapaswa kuandaa utaratibu wa motisha ambao utahakikisha kuwa watumishi wa umma wanapata kuridhika kwa kazi bila kujali makato makubwa katika mishahara yao iliyosababishwa na utekelezaji wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Marekebisho ya mwaka 2004. Ninapendekeza kuwa, katika siku zijazo marekebisho yoyote ya sheria yanapaswa kuzingatia mikataba iliyokuwepo awali ili kuzuia madhara kwa pande zinazohusika.

## 7.4 Udhaifu katika ujazaji wa fomu za kupima utendaji kazi kwa watumishi (OPRAS)

Mfumo wa wazi wa upimaji utendaji kazi wa watumishi (OPRAS) ni mchakato ambao hutumiwa kupima utendaji na maendeleo ya mtumishi wa umma. Unalenga kujenga utamaduni wenye tija juu ya utendaji

ambapo wafanyakazi mmoja mmoja, msimamizi na watumishi kwa pamoja wanawajibika kufanikisha malengo ya kutoa huduma kwa umma kwa kuweza kufikia matokeo yake kwa namna nzuri zaidi na ya ufanisi.

Ufanisi katika usimamizi na utendaji wa kila mtumishi ni muhimu kwa utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu huwawezesha wafanyakazi wote kuelewa na kuchangia kufikia malengo ya pamoja. Tathmini binafsi kwa mtumishi wa umma husaidia si tu utendaji wa wafanyakazi katika kazi yao ya sasa lakini pia katika mahitaji ya mafunzo na kupanda madaraja.

Kwa kuzingatia umuhimu wa OPRAS katika sekta ya umma, nilitathmini upimaji wa watumishi katika Mamlaka 36 katika mwaka ulioishia Juni 30, 2017 na kubaini kuwa utendaji haukufanyika kulingana na matakwa ya Kanuni ya 22 (1) ya Kanuni za Huduma za Umma 2003 na Agizo D.42, D.62, D.63, D.67 na D.68 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009. Maelezo ya uchambuzi yanaonyeshwa kwenye Jedwali Na. 7-5 chini:

**Jedwali Na. 7-5: Upimaji usioridhisha wa utendaji wa watumishi wa umma katika Namlaka za Serikali za Mitaa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya watumishi | Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya watumishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Arusha | 10 | 20 | H/W Maswa | 5 |
| 2 | H/W Arusha | 22 | 21 | H/W Mbarali | 21 |
| 3 | H/W Bariadi | 16 | 22 | H/W Mkinga | 39 |
| 4 | HMji Bariadi | 10 | 23 | H/W Mlele | 10 |
| 5 | H/W Bunda | 28 | 24 | H/W Moshi | 33 |
| 6 | H/W Chalinze | 22 | 25 | H/W Mpanda | 12 |
| 7 | H/W Handeni | 15 | 26 | H/M Mpanda | 12 |
| 8 | H/W Ileje | 19 | 27 | H/M Musoma | 299 |
| 9 | H/W Itigi | 4 | 28 | H/W Mwanga | 19 |
| 10 | H/W Kakonko | 10 | 29 | H/W Ngorongoro | 14 |
| 11 | H/W Kalambo | 46 | 30 | H/Mji Njombe | 10 |
| 12 | H/W Karatu | 15 | 31 | H/W Nsimbo | 7 |
| 13 | H/W Kilindi | 37 | 32 | H/W Pangani | 20 |
| 14 | H/Mji Korogwe | 41 | 33 | H/W Rufiji | 10 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15 | H/W Kwimba | 11 | 34 | H/W Same | 8 |
| 16 | H/W Ludewa | 12 | 35 | H/W Singida | 5 |
| 17 | H/W Lushoto | 20 | 36 | H/W Sumbawanga | 11 |
| 18 | H/W Mafia | 7 | **Jumla** | | **892** |
| 19 | H/Mji Makambako | 12 | | | |

Uelewa mdogo kwa wafanyakazi na wasimamizi wao juu ya umuhimu wa OPRAS katika upimaji wa utendaji wa jumla wa mtumishi binafsi katika Halmashauri husika wakati wa kuhudumia umma ndiyo sababu kuu ya changamoto zilizotajwa. Ujazaji na utumiaji wa fomu katika kupima utendaji na uhakiki vinaonekana kama upotezaji wa muda na rasilimali na kuonekana kama shughuli ya kawaida ambayo haina tija kwa kazi zao na ustawi wa kazi.

Pia, nilibaini kuwa malengo ya wafanyakazi na wasimamizi wao hayakuwianishwa na yale ya Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri hazitengi bajeti kwa ajili ya mmafunzo ya ujazaji wa OPRAS kwa watumishi wao.

Tathmini isiyoridhisha ya utendaji kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ina madhara kwa maendeleo ya utoaji wa huduma katika Halmashauri hizo kwakuwa hakuna onyo la awali wanalopewa wafanyakazi ambao hawafikii matarajio na malengo wanayoweka ya utendaji. Kwa upande mwingine, kwa watendaji bora ambao wanapatikana katika kwa kufikia viwango vya utendaji vilivyowekwa, hawataweza kutambuliwa kwa kupewa motisha kama njia ya kuwahamasisha kufanya kazi nzuri zaidi ikiwa OPRAS haifanyiki kila mwaka.

Ili kuboresha utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ninapendekeza kuwa, uongozi wa Serikali za Mitaa husika uhakikishe wanatenga bajeti ya kutosha kwa shughuli za OPRAS.

## 7.5 Udhaifu katika kusimamaia mfumo wa taarifa za usimamizi wa utumishi (HCMIS)

Mfumo wa taarifa wa usimamizi wa utumishi (HCMIS) ni mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu na mishahara ambao ulipitishwa na Serikali

kama chombo cha ufanisi wa usimamizi wa rasilimali watu na malipo kwa watumishi wa umma.

Serikali ya Tanzania ilipitisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu (HCMIS) kwa sababu ya changamoto zilizokuwa zikikwamisha usimamizi wa shughuli za rasilimali watu na malipo kama vile kuchelewesha kutekeleza matangazo, kuhamisha, kulipa na kuondoa majina ya watumishi katika mfumo.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa ulifanyika uhakiki wa taarifa (data cleaning) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 zinazohusisha wafanyakazi 15,690. Pamoja na mapendekezo yangu ya ripoti za miaka ya nyuma, mapungufu yaleyale bado yameendelea kujitokeza. Nayo ni: (i) Kuchelewa kuhamisha taarifa za watumishi waliohamishwa kutoka katika mfumo wa mishahara kutoka Halmashauri ya awali kwenda Halmashauri nyingine; (ii) Kuchelewa kufuta kumbukumbu za wastaafu, wafu, walioacha kazi, kuondolewa na kuacha watumishi kutoka kwenye mfumo mkuu wa ulipaji bila kuhuisha kumbukumbu za watumishi kama vile tarehe ya kuzaliwa na tarehe ya kuthibitishwa kazini. (Angalia Jedwali Na. 7-6)

**Jedwali Na. 7-6: Taarifa za watumishi zisizo timilifu katika mfumo wa utumishi (HCMIS)**

| Na. | Jina la Mamlaka | Idadi ya watumishi | Na. | Jina la Mamlaka | Idadi ya watumishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bahi | 86 | 15 | H/M Moshi | 143 |
| 2 | H/Mji Kasulu | 47 | 16 | H/W Moshi | 199 |
| 3 | H/W Kibondo | 93 | 17 | H/W Mwanga | 135 |
| 4 | H/M Kinondoni | 4,591 | 18 | H/W Bumbuli | 1,273 |
| 5 | H/Mji Kibaha | 129 | 19 | H/M Mpanda | 990 |
| 6 | H/W Mafia | 53 | 20 | H/W Mpimbwe | 798 |
| 7 | H/W Kibiti | 12 | 21 | H/W Ludewa | 26 |
| 8 | H/W Chalinze | 50 | 22 | H/Mji Makambako | 7 |
| 9 | H/Mji Masasi | 104 | 23 | H/Mji Mafinga | 79 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | H/W Arusha | 2,616 | 24 | H/W Mufindi | 172 |
| 11 | H/W Karatu | 1,598 | 25 | H/W Mbarali | 8 |
| 12 | H/W Longido | 945 | 26 | H/W Chunya | 55 |
| 13 | H/W Monduli | 1288 | 27 | H/W Kalambo | 20 |
| 14 | H/W Ngorongoro | 53 | 28 | H/W Nkasi | 120 |
| **Jumla** | | | | | **15,690** |

Natambua juhudi zinazoendelea za Serikali za uhakiki wa taarifa za watumishi na malipo kwa ujumla. Hata hivyo, mapungufu ya mara kwa mara yana athari mbaya juu ya mshahara wa kila mwezi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, bajeti ya mwisho kwa watumishi wastaafu wa sekta ya umma na upandaji wa madaraja kwa wafanyakazi waliopo.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Umma, ufanye jitihada zaidi juu ya uhakiki wa taarifa kwa ufanisi na kuhuisha taarifa mara kwa mara kwenye mfumo wa HCMIS ili kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinalipa mishahara sahihi na kwa wakati. Pia, ninashauri Ofisi ya Raisi – Tume ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kuwa ruhusa ya kuhuisha taarifa kwa haraka inatolewa pale taarifa za mtumishi zinapotakiwa kuhamishwa kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine.

## 7.6 Madai ya wafanyakazi Sh.Tz 9,868,633,522

Mapitio ya majalada binafsi ya watumishi, nyaraka zinazohusiana na madai, mahojiano na maafisa rasilimali watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 yailibaini kuwapo kwa madai yanayofikia jumla ya Sh. Tz 9,868,633,522 ambayo hayakulipwa kama yanavyoonekana katika Jedwali Na. 7-7 hapa chini:

**Jedwali Na. 7-7: Madai ya mishahara na Madai mengine ya wafanyakazi wa halmashauri**

| Na. | Jina la Mamlaka | Madai yaliyo baki | Na. | Jina la Mamlaka | Madai yaliyo baki |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Busokelo | 1,284,448,194 | 11 | H/W Mufindi | 24,552,000 |
| 2 | H/W Hai | 85,440,000 | 12 | H/W Mwanga | 22,800,000 |
| 3 | H/W Ileje | 1,450,166,232 | 13 | H/Jiji Mwanza | 317,729,732 |
| 4 | H/W Iringa | 32,916,000 | 14 | H/W Njombe | 1,155,081,316 |
| 5 | H/W Itilima | 162,815,000 | 15 | H/W Nkasi | 951,329,648 |
| 6 | H/W Karatu | 465,514,122.84 | 16 | H/W Nzega | 24,788,200 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | H/W Kilosa | 894,175,881 | 17 | H/W Rungwe | 124,080,000 |
| 8 | H/M Kinondoni | 1,012,535,551 | 18 | H/M Sumbawanga | 1,447,781,645 |
| 9 | H/W Kondoa | 33,334,000 | 19 | H/Mji Tunduma | 208,500,000 |
| 10 | H/W Moshi | 170,646,000 | **Jumla** | | **9,868,633,522** |
| | | | | | |

Ninatambua juhudi zilizofanywa na Serikali kumaliza tatizo la madai ya watumishi ya muda mrefu. Hata hivyo, wasiwasi wangu ni ucheleweshaji wa kulipa madai ya mfanyakazi pale yanapotakiwa kulipwa.

Fedha zinazotengwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali kwa ujumla kwa ajili ya watumishi wanaopanda madaraja, ajira mpya, posho mbalimbali, na gharama mbalimbali za wafanyakazi ndio sababu kubwa za kuwapo kwa madai haya kwa muda mrefu. Madai yasiyolipwa kwa muda mrefu yanaongeza madeni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na yanaweza kudhoofisha morali wa watumishi katika kutoa huduma bora na kwa ufanisi kwa umma.

Ninapendekeza kwa Halmashauri na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Hazina kuhakikisha kuwa fedha za kutosha zinatengwa kwa ajili ya kulipa madai ya wafanyakazi kwati.

## 7.7 Kucheleweshwa kuthibitishwa kwa watumishi 8,369 waliopanda madaraja na nyongeza za mishahara yao

Agizo Na. D.51 la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 linataka tarehe inayotakiwa kumpandisha daraja mtumishi wa umma kutambuliwa na mamlaka ya uteuzi ambayo haitateua tarehe ya kupanda daraja ambayo ni mapema zaidi ya tarehe ambayo alipata ajira, au tarehe ambayo afisa alipata sifa kuthibitishwa kupandishwa daraja na kuanza kutumikia majukumu ya daraja jipya.

Hata hivyo, mapitio ya majalada binafsi, taarifa za LAWSON na nyaraka nyingine katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18, yamebainisha kuwa watumishi 8,369 waliokuwa na sifa za kupanda madaraja walichelewa kuidhinishwa bila kujali kuwa walikidhi vigezo vyote vilivyoainishwa na Agizo tajwa hapo juu. Pia, nilibaini kuwa ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

waliwasilisha orodha ya watumishi wa umma waliostahili kupandishwa madaraja kwa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kupata idhini kama ilivyo katika Jedwali Na.7-8.

**Jedwali Na. 7-8: Kuchelewa uidhinishaji wa wafanyakazi wenye sifa za kupanda madaraja na uboreshaji wa mshahara**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa | Idadi ya watumishi | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa | Idadi ya watumishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Chemba | 364 | 10 | H/W Mwanga | 637 |
| 2 | H/W Kondoa | 410 | 11 | H/W Same | 577 |
| 3 | H/W Kondoa | 168 | 12 | H/W Muheza | 1335 |
| 4 | H/W Manyoni | 190 | 13 | H/W Mbulu | 50 |
| 5 | H/W Tabora | 272 | 14 | H/W Makambako | 300 |
| 6 | H/W Bagamoyo | 483 | 15 | H/W Iringa | 443 |
| 7 | H/W Rufiji | 83 | 16 | H/W Chunya | 374 |
| 8 | H/W Ulanga | 534 | 17 | H/W Busokelo | 30 |
| 9 | H/W Moshi | 1977 | 18 | H/W Tunduma | 142 |
| | | | **Jumla** | | **8,369** |

Kuchelewa kufanya mabadiliko ya mishahara kunatokana na Waraka No. CFA.26 / 205 / O1 B / 46 wa tarehe 13 Juni 2016 kutoka Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao uliamuru taasisi za umma nchini kote kuahirisha kupandisha madaraja kwa watumishi wa umma wala kuongeza mishahara, kuajiri watumishi wapya na kubadilisha kada hadi uhakiki wa uwepo wa watumishi halali na vyeti vyao halisi vya taaluma utakapokamilika.

Kuchelewa kupandisha madaraja kwa watumishi wa umma wenye sifa hupunguza ari yao ya kazi, ambapo inaweza kusababisha utendaji duni katika huduma zinazotolewa kwa jamii.

Ninapendekeza kuwa, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ziharakishe Mchakato wa vibali vya kupandisha madaraja na kuhakikisha madai yanayoendana na kupanda kwa madaraja yanafanyiwa kazi kwa bila kuchelewa.

## 7.8 Makato ya mshahara ambayo hayakupelekwa kwenye taasisi husika Sh. Tz 963,796,371

Jambo la msingi katika malipo ya mshahara ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wanalipwa kwa usahihi na kwa wakati unaofaa pamoja

na kukata kodi ya mapato na makato mengine. Kodi iliyokatwa na makato mengine hutolewa kwa wakati unaofaa kwa taasisi husika. Ni muhimu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupeleka makato ya mishahara kwa muda mwafaka kwa Taasisi husika.

Kwa mujibu wa sheria zilizopo, kanuni na maagizo mbalimbali, mishahara ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa hulipwa kwa kuzingatia makato ya kisheria na yasiyo ya kisheria kama vile Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PSPF, LAPF, NSSF, PPF, WCSF na NHIF), kodi ya mapato, Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF), ulipaji wa mikopo kwa taasisi za fedha, SAH/JIJIOS na michango kwa Vyama vya Wafanyakazi.

Mengi ya makato haya yamezuiwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye watumishi wanaolipwa kutokana na mapato ya ndani ya Halmasahuri mbalimbali hapa nchini. Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2017, Mamlaka za Serikali za Mitaa 31 hazikupeleka makato ya jumla Sh.Tz. 963,796,371 kwenye taasisi husika.

Mwaka wa fedha 2015/2016 nilibaini kuwa kulikuwa na kutowasilishwa kwa makato ya Jumla ya Sh.Tz. 1,123,229,274 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa 30. Ukaguzi wangu umebaini kuwa kuna upungufu wa wastani wa makato yasiyowasilishwa ya jumla ya Sh.Tz. 37,440,976 katika mwaka huo wa 2015/2016 ikilinganishwa na Sh. Tz 31,090,206 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2017. Rejea Jedwali Na.7-9.

**Jedwali Na. 7-9: Makato ya kisheria kwa wafanyakazi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mitaa | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mitaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bariadi | 78,660,924 | 17 | H/W Muheza | 24,360,782 |
| 2 | H/W Bumbuli | 31,762,612 | 18 | H/W Namtumbo | 12,484,140 |
| 3 | H/W Busega | 7,544,730 | 19 | H/W Ngorongoro | 11,683,800 |
| 4 | H/W Igunga | 40,918,190 | 20 | H/W Nyasa | 6,062,180 |
| 5 | H/W Iramba | 6,477,600 | 21 | H/W Rungwe | 19,988,400 |
| 6 | H/W Itigi | 3,530,649 | 22 | H/W Singida | 30,982,021 |
| 7 | H/W Kibondo | 13,319,898 | 23 | H/M Singida | 6,920,969 |
| 8 | H/W Kilosa | 62,787,964 | 24 | H/W Songea | 19,988,400 |
| 9 | H/W Kisarawe | 75,432,080 | 25 | H/W Songwe | 8,939,713 |
| 10 | H/W Mafia | 32,940,734 | 26 | H/M Tabora | 164,831,128 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | H/MJI Mafinga | 10,500,000 | 27 | H/JIJI Tanga | 38,417,400 |
| 12 | H/W Malinyi | 17,503,954 | 28 | H/MJI Tarime | 4,242,600 |
| 13 | H/W Manyoni | 21,051,888 | 29 | H/W Tunduru | 72,451,160 |
| 14 | H/JIJI Mbeya | 76,310,255 | 30 | H/W Ukerewe | 17,302,571 |
| 15 | H/W Mbulu | 33,670,895 | 31 | H/W Uvinza | 5,843,869 |
| 16 | H/W Morogoro | 6,884,865 | **Jumla** | | **963,796,371** |

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 8 zilitozwa jumla ya Sh.Tz. 774,725,229 kutokana na kuchelewa kupeleka makato ya kisheria. Kuchelewesha kuwasilisha makato ya kisheria kwenye taasisi husika husababisha tozo ambayo, kimsingi, ni matumizi yasiyo na manufaa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jedwali Na. 7-10 inaonyesha maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 7-10: Tozo kutokana na kutowasilisha makato ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

| Na. | Jina la Mamlaka | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Urambo | 23,582,888 |
| 2 | H/M Temeke | 23,787,612 |
| 3 | H/W Tandahimba | 1,371,752 |
| 4 | H/W Maswa | 196,107,960 |
| 5 | H/Mji Kahama | 5,126,190 |
| 6 | H/W Chunya | 290,815,989 |
| 7 | H/W Nyasa | 146,240,201 |
| 8 | H/W Namtumbo | 87,692,637 |
| **Jumla** | | **774,725,229** |

Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatumia fedha za makato ya kisheria kufanyia shughuli nyingine, hivyo, kusababisha madeni na gharama za tozo kwa njia ya adhabu kutokana na matumizi yasiyo na manufaa.

Licha ya mapendekezo yangu ya mwaka uliopita, Mamlaka nyingi bado hazikupeleka makato ya kisheria kwa taasisi husika. Hii ni dalili ya kutokukubaliana na mapendekezo yangu ya ukaguzi kuhusu namna bora kuboresha mfumo wa malipo ya mishahara. Kukosa kupeleka michango ya watumishi kwa taasisi husika kuna madhara kwa watumishi pindi ajira inapokoma.

Ninapendekeza kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali kwa ujumla zihakikishe zinwasilisha wa mapema makato ya kisheria mara yanapokuwa

tayari. Pia, nasisitiza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa makato ambayo hayakupelekwa yanapelekwe haraka kwa taasisi husika.

## 7.9 Mishahara inayolipwa kwa wafanyakazi wasiokuwepo kazini na makato ya kisheria kulipwa kwa taasisi mbalimbali Sh.Tz. 329,383,482

Agizo Na. 79 (6) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linataka mishahara isiyolipwa iliyopelekwa benki kwenye akaunti ya amana ya watumishi waliofariki, waliostaafu, na kuacha kazi kurejeshwa Hazina ndani ya wiki mbili baada ya mshahara husika kulipwa. Pia, msisitizo umetolewa katika Agizo Na.79 (8) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

Nilipitia taarifa za mfumo wa malipo ya mishahara, majalada binafsi, rejista za wafanyakazi waliofariki, wafanyakazi waliostaafu na walioacha kazi, na kubaini kuwa Sh. Tz 329,383,482 zililipwa kama mishahara na makato kwa wafanyakazi hewa katika Mamlaka mbalimbali. Serikali za Mitaa 29 zilihusika. Nilishindwa kuthibitisha namna fedha hizo zitakavyorejewa kutokana na kukosa uthibitisho wa kuwapo kwa kiasi hicho kilicholipwa kwa watumishi wasiokuwa kazini. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 7-11 hapa chini.

**Jedwali Na. 7-11: Mishahara imelipwa kwa watumishi ambao hawapo kazini.**

| Na. | Jina la Halmashauri | Mshahara (halisi) (Sh.Tz) | Makato (Sh.Tz) | Jumla (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/JIJI Arusha | 6,530,545 | 7,881,455 | 14,412,000 |
| 2 | H/W Bumbuli | 2,693,430 | 3,318,570 | 6,012,000 |
| 3 | H/W Chalinze | 1,667,898 | 802,102 | 2,470,000 |
| 4 | H/W Chunya | 1,960,000 | - | 1,960,000 |
| 5 | H/W Handeni | 2,188,792 | 1,656,240 | 3,845,032 |
| 6 | H/W Karagwe | 8,819,267 | 11,820,733 | 20,639,999 |
| 7 | H/W Kibaha | 8,733,825 | 6,537,175 | 15,271,000 |
| 8 | H/W Kilindi | 14,814,234 | 17,835,766 | 32,650,000 |
| 9 | H/W Kilosa | 1,164,085 | 1,305,915 | 2,470,000 |
| 10 | H/M Kinondoni | 22,090,057 | 13,059,943 | 35,150,000 |
| 11 | H/W Korogwe | 13,230,752 | 7,228,249 | 20,459,001 |
| 12 | H/MJI Korogwe | 888,540 | 692,920 | 1,581,460 |
| 13 | H/W Longido | 4,371,364 | 2,716,636 | 7,088,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Mshahara (halisi) (Sh.Tz) | Makato (Sh.Tz) | Jumla (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|
| 14 | H/W Lushoto | 736,062 | 1,376,938 | 2,113,000 |
| 15 | H/W Mafia | 1,212,081 | 2,138,919 | 3,351,000 |
| 16 | H/MJI Masasi | 5,423,585 | 2,091,415 | 7,515,000 |
| 17 | H/W Mbinga | 2,369,928 | 2,200,072 | 4,570,000 |
| 18 | H/W Misungwi | 3,965,468 | 2,209,532 | 6,175,000 |
| 19 | H/W Mkinga | 2,966,153 | 2,903,847 | 5,870,000 |
| 20 | H/W Morogoro | 7,218,293 | 8,137,707 | 15,356,000 |
| 21 | H/M Morogoro | 11,753,305 | 14,670,695 | 26,424,000 |
| 22 | H/M Moshi | 2,572,155 | 2,067,845 | 4,640,000 |
| 23 | H/W Muheza | 4,173,213 | 4,015,788 | 8,189,001 |
| 24 | H/MJI Nanyamba | 3,819,549 | - | 3,819,549 |
| 25 | H/W Ngara | 2,970,680 | 3,118,836 | 6,089,516 |
| 26 | H/W Pangani | 1,983,240 | 1,575,682 | 3,558,922 |
| 27 | H/W Sumbawanga | 2,871,000 | 1,199,000 | 4,070,000 |
| 28 | H/JIJI Tanga | 3,091,349 | 5,260,653 | 8,352,002 |
| 29 | H/W Ukerewe | 29,390,993 | 25,891,007 | 55,282,000 |
| **Jumla** | | **79,145,326** | **73,250,663** | **329,383,482** |

Licha ya juhudi zilizofanywa na Serikali kuhusu uhakiki wa taarifa za mishahara, bado malipo ya mishahara na makato kwa watu ambao si watumishi wa sekta ya umma yanaendelea kulipwa. Matukio ya malipo hayo yanamaanisha kwamba mapendekezo yangu ya awali ya uboreshaji wa mfumo wa ulipaji mishahara hayakutekelezwa.

Moja ya sababu kuu ya suala hilo ni usiri usiofaa kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Hazina, ambapo hakuna taarifa ya mishahara iliyosimamishwa kwa mfanyakazi kulipwa wakati utumishi wake unapokoma. Sababu nyingine ni, upungufu wa uhakiki wa taarifa za malipo pamoja na ucheleweshaji wa mawasiliano kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Hazina kwa kuhuisha taarifa za watumishi mara kwa mara.

Ninasisitiza kuwa, kama Serikali inataka kuona matokeo kuna haja ya pande zinazohusika katika suala la mishahara kutekeleza mapendekezo yangu ya miaka mingi juu ya suala hilo. Uwazi na mawasiliano kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Hazina ni muhimu sana katika kurekebisha shughuli zote za malipo ya mishahara. Taarifa zinapaswa kutumwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu kiasi cha makato kilicholipwa kwa

taasisi mbalimbali na kusimamisha makato ya mishahara kwa kiwango sawa na watumishi wasiostahili kulipwa.

# SURA YA NANE

# 8.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO NA MIRADI MINGINE

## 8.1 Muhtasari wa Miradi ya maendeleo

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea na utekelezaji wa Miradi ya maendeleo kwa kutumia makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, fedha kutoka Serikali Kuu, michango ya jamii, pamoja na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendendeleo.

Miradi na kazi mbalimbali zimetekelezwa kupitia Ruzuku ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGCDG), Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), Mpango wa Kuimarisha Mamlaka za Miji (ULGSP), Programu ya Kuboresha Elimu (EQUIP), Idara ya Kimataifa ya Maendeleo (DFID), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Elizabeth Glasler la Kupambamna na Virusi vya Ukimwi kwa Watoto (EGPAF), Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (P4R) na Programu ya WALTER REED. Ufadhili katika miradi hii ulitofautiana, baadhi ya Miradi ilijumuisha Mamlaka zote za Serikali za Mitaa na mingine ilikuwa ni kwa baadhi tu kutegemeana na malengo ya mradi ikilinganishwa na changamoto za eneo husika.

Miradi iliyotekelezwa mwaka huu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya (HBF), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mfuko wa Barabara (RF) haikujumuishwa katika Sura hii. Hii ni kwa sababu kaguzi zake zilijitegemea hivyo tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo imetolewa kwenye ripoti inayojitegemea ya miradi ya maendeleo.

Mambo yaliyobainika wakati wa mapitio ya matumizi ya fedha, pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:

## 8.2 Matumizi pungufu ya fedha zilizopokelewa

Tathmini ya matumizi ya fedha katika utekelezaji wa miradi na shughuli nyingine za maendeleo zilizopangwa kufanyika mwaka huu imebainisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 76 zilikuwa na kiasi cha Sh.Tz. 130,684,657,588 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Lakini hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 jumla ya Sh.Tz. 48,473,335,881 zilitumika na kusalia bakaa ya Sh.Tz. 82,461,355,743 sawa na asilimia 63 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8-1 hapa chini.

**Jedwali Na. 8-1: Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo**

| Chanzo cha Fedha | Idadi ya serikali za Mitaa | Fedha iliyopokelewa (Sh.Tz) | Chanzo cha Fedha (Sh.Tz) | Idadi ya serikali za Mitaa (Sh.Tz) | Fedha iliyopokelewa |
|---|---|---|---|---|---|
| LGCDG | 34 | 18,770,716,309 | 9,161,503,911 | 9,980,507,377 | 53% |
| ULGSP | 10 | 75,868,080,427 | 26,149,661,913 | 49,718,418,514 | 66% |
| EQUIP | 24 | 24,038,027,105 | 10,055,387,336 | 13,956,218,726 | 58% |
| CDCF | 15 | 1,103,768,479 | 530,521,291 | 573,082,245 | 52% |
| SEDP/P4R | 6 | 3,142,279,046 | 1,315,680,946 | 1,826,598,100 | 58% |
| CHF | 12 | 1,868,372,045 | 794,685,750 | 979,011,337 | 52% |
| SPECIAL FUND | 6 | 5,893,414,177 | 465,894,734 | 5,427,519,444 | 92% |
| **Jumla** | | **130,684,657,588** | **48,473,335,881** | **82,461,355,743** | **63%** |

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa fedha ambazo hazikutumika ni kati ya asilimia 52 na 92. Hivyo kwa wastani, asilimia 63 ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hazikutumika kwa sababu ya ukosefu wa ufanisi katika upangaji na utekelezaji wa miradi au Hazina kuchelewa kupeleka fedha.

Salio kubwa la fedha za miradi ya maendeleo mwishoni mwa mwaka lina maana kwamba baadhi ya Miradi ya Maendeleo haikutekelezwa au

ilitekelezwa kwa sehemu tu, hivyo kuathiri malengo yaliyokusudiwa. Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na.8:1.**

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kutekeleza shughuli zote zilizopangwa, kuandaa mipango mikakati ya kutumia fedha zilizosalia, kutekeleza na kumalizia shughuli ambazo hazikukamilishwa miaka ya nyuma na kujumuisha katika bajeti ya sasa ongezeko la gharama litokanalo na mfumuko wa bei ikilinganishwa na bajeti ya awali.

## 8.3 Miradi Mikubwa ya Maendeleo

Miradi Mikubwa ya Maendeleo inahitaji uwekezaji wa muda mrefu; na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahitaji kiasi kikubwa cha fedha katika kuijenga, kuiboresha na kuikarabati (mfano Ardhi, Majengo, Barabara).
Mapitio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yamebainisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185, zilikuwa na jumla ya Sh. Tz 796,708,520,009 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 kiasi kilichotumika kilikuwa ni Sh. Tz 531,652,643,504 na kuacha bakaa ya kiasi cha Sh. Tz 265,055,876,504 sawa na asilimia 33 ya fedha zote zilizokuwepo kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo kama inavyoonekana katika Jedwali 8-2.

**Jedwali Na. 8-2: Fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo hazikutumika**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Fedha iliyokuwepo (Sh.Tz) | Fedha iliyotumika (Sh.Tz | Bakaa ya Fedha (Sh.Tz) | % ya Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016/17 | 185 | 796,708,520,009 | 531,652,643,504 | 265,055,876,504 | 33 |
| 2015/16 | 171 | 584,417,654,676 | 370,970,071,298 | 212,934,270,535 | 36 |
| 2014/15 | 164 | 582,208,588,668 | 501,334,438,593 | 80,874,150,075 | 14 |
| 2013/14 | 157 | 718,749,785,161 | 532,156,786,062 | 186,592,999,099 | 26 |

Jedwali Na. 8-2 la hapo juu linatoa taswira ya jinsi uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutumia fedha zilizopokelewa ulivyoongezeka

kutoka asilimia 64 kwa mwaka fedha 2015/2016 mpaka asilimia 67 kwa mwaka fedha 2016/2017.

Kuwapo kwa salio kubwa la fedha mwishoni mwa mwaka kunadhihirisha kasi ndogo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha utaratibu utakaohakikisha kuwa miradi yote ya maendeleo inatekelezwa na kukamilika kwa wakati kulingana na mpango kazi ili jamii inufaike na huduma zinazotarajiwa kupatikana kutokana na miradi hiyo.

Taarifa ya mapato na matumizi kwa Miradi ya Maendeleo kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeoneshwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. 8:2.**

## 8.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo niliyoifanya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 imebaini yafuatayo: kuwapo kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye miradi ambayo haikutekelezwa kutokana na kutokupokea fedha za utekelezaji miradi haikutekelezwa au kukamilishwa licha ya kupokea fedha; na miradi mingine imekamilika lakini haitumiki.

Mapungufu haya yana athari kubwa katika utekelezaji, usimamizi na tathmini ya miradi hiyo, na hivyo, kuhitaji hatua za haraka za serikali kama inavyoelezwa katika aya zifuatazo: -

### 8.4.1 Miradi ambayo haijatekelezwa

Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo niliyoifanya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa inaonesha kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikutekeleza Miradi ya Maendeleo 13 kutokana na kutokuletwa kwa fedha ya miradi ya maenedleo ya kiasi cha Sh. Tz 1,052,416,58

Kwa upande mwingine, Miradi ya Maendeleo 25 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 yenye thamani ya Sh. Tz 7,793,272,396 haikutekelezwa licha ya fedha za miradi hiyo kupokelewa na Mamlaka husika za Serikali za Mitaa.

Hii inaashiria kwamba malengo ya miradi hiyo hayakufikiwa hivyo kuathiri malengo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo ni kuhakikisha jamii inanufaika na huduma zinazotarajiwa kupatikana kutokana na miradi hiyo. Miradi ya maendeleo ambayo haijatekelezwa imeainishwa katika **Kiambatisho Na.8:3.**

### 8.4.2 Miradi ambayo haijakamilika

Nimefanya mapitio ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 26 na kubaini kuchelewa kukamilika kwa miradi mbalimbali yenye jumla ya Sh. Tz 3,187,957,259 kutokana na kukosekana kwa usimamizi wa kutosha, kuchelewa kupokelewa kwa fedha na ushiriki hafifu wa jamii katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 8-3.

**Jedwali Na. 8-3: Miradi ambayo haijakamilika**

| Na. | Jina la Serikali ya Mataa | Thamani ya Miradi ambayo haijakamilika (Sh.Tz) | Chanzo cha Fedha | Na. | Jina la Serikali ya Mataa | Thamani ya Miradi ambayo haijakamilika (Sh.Tz) | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 200,000,000 | LGCDG | 14 | H/Mji Mbulu | 51,386,364 | LGCDG |
| 2 | H/Mji Bunda | 84,650,457 | LGCDG | 15 | H/W Misungwi | 117,275,800 | LGCDG |
| 3 | H/W Geita | 164,642,600 | LGCDG | 16 | H/W Mbarali | 392,556,000 | SEDP |
| 4 | H/M Ilemela | 145,067,000 | LGCDG | 17 | H/W Mkuranga | 9,000,000 | LGCDG |
| 5 | H/W Iramba | 20,000,000 | LGCDG | 18 | H/W Mlele | 171,573,068 | LGCDG |
| 6 | H/W Kalambo | 104,704,800 | LGCDG | 19 | H/W Mpanda | 90,864,000 | LGCDG |
| 7 | H/W Karagwe | 108,344,250 | LGCDG | 20 | H/Mji Mpanda | 45,000,000 | LGCDG |
| 8 | H/W Korogwe | 101,000,000 | LGCDG | 21 | H/W Mvomero | 107,000,000 | LGCDG |
| 9 | H/W Kwimba | 179,664,400 | LGCDG | 22 | H/W Rungwe | 33,085,600 | LGCDG |
| 10 | H/W Ludewa | 129,000,000 | LGCDG | 23 | H/W Songwe | 21,000,000 | LGCDG |
| 11 | H/W Magu | 312,067,000 | LGCDG | 24 | H/M Sumbawanga | 48,200,000 | LGCDG |

| Na. | Jina la Serikali ya Mataa | Thamani ya Miradi ambayo haijakamilika (Sh.Tz) | Chanzo cha Fedha | Na. | Jina la Serikali ya Mataa | Thamani ya Miradi ambayo haijakamilika (Sh.Tz) | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12 | H/Jiji Mbeya | 339,715,200 | LGCDG | 25 | H/W Tarime | 17,235,720 | LGCDG |
| 13 | H/W Mbeya | 65,000,000 | LGCDG | 26 | H/Mji Tunduma | 129,925,000 | LGCDG |
| **Jumla** | | | | | | **3,187,957,259** | |

Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya hii kunaweza kupelekea kupitiwa upya kwa Mikataba ya miradi hiyo kutokana na gharama za awali kupitwa na wakati. Kuna uwezekano wa miradi hii kutekelezwa chini ya kiwango kutokana na kukosa usimamizi wa kutosha na nia ya Wakandarasi kujitahidi kumaliza kazi katika muda wa Mkataba licha ya fedha kuchelewa. Aidha, kutokamilika kwa miradi ya maendeleo kwa wakati kunawanyima walengwa wa miradi hiyo kupata fursa ya kunufaika na huduma zitokanazo na miradi hiyo kwa wakati uliopangwa.

Naishauri Serikali kupitia Hazina kupeleka kiasi kilichoidhinishwa cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo mapema ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuboresha huduma za kijamii.

Pia nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha utaratibu utakaohakikisha kuwa miradi yote ya maendeleo inatekelezwa na kukamilika kwa wakati kulingana na mpango kazi ili jamii inufaike na huduma zinazotarajiwa kupatikana kutokana na miradi hiyo.

### 8.4.3 Miradi iliyokamilika lakini haitumiki

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwapo kwa miradi iliyokamilika yenye thamani ya Sh.Tz. 782,468,997 katika Mamlaka ya serikali za mitaa 13 ambayo haitumiki, hivyo kunawanyima wananchi fursa ya kunufaika na miradi husika. Orodha ya Miradi ya maendeleo ambayo imekamilika lakini haitumiki imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 8:4**

Nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa miradi yote iliyokamilika inatumika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kupata thamani ya fedha.

### 8.4.4 Mapungufu katika Usimamizi wa Miradi

Usimamizi wa miradi ni utaratibu mzima wa uibuaji, upangaji, utekelezaji, udhibiti na ukamilishaji wa miradi husika. Madhumuni ya usimamizi wa miradi ni kufanikisha kufikiwa kwa malengo tarajiwa ya miradi yanayozingatia kanuni za mafanikio zinazotambulika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza miradi mbalimbali kutokana na mikataba au kutekelezwa chini ya usimamizi wa Halmashauri moja kwa moja (Force account). Miradi mingi inayotekelezwa katika ngazi ya chini; kama vile Kata, Vijiji na Shule, zinatumia utaratibu wa usimamizi wa moja kwa moja kwa kupelekewa moja kwa moja fedha za miradi.

Wakati wa utekelezaji wa miradi, nasisitiza kuzingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Viwango elekezi bila kujali ni ngazi zipi miradi hii inatekelezwa. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibika kuhakikisha kwamba miradi inatekelezwa kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika.

Tathmini niliyoifanya juu ya usimamizi wa Miradi iliyokamilika na ile inayoendelea kutekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 15 imebaini udhaifu na upungufu mkubwa katika usimamizi na ufuatiliaji katika miradi hiyo kinyume na matakwa ya sheria, kanuni na viwango. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye mapungufu katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ipo katika **Kiambatisho Na. 8:5.**

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na kuhakikisha zabuni zinatolewa kwa wakandarasi wenye uwezo. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wote watakaoshindwa kurekebisha mapungufu yaliyoonekana au kutimiza masharti ya mikataba yao.

## 8.5 Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana

Mwaka 1993 Serikali, kupitia Azimio la Bunge, ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana ikiwa na lengo la kuviwezesha kifedha vikundi vya Wanawake na Vijana kushiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishaji. Hatua hii ilifikiwa baada ya kubainika kwamba vikundi vya aina hii si rahisi kupata mikopo kutoka katika Taasisi za fedha kutokana na wanachama wake kutokuwa na mali ambazo zingetumika kama dhamana ya mikopo hiyo.

Katika ripoti yangu iliyopita niliibua suala la malimbikizo ya michango ambayo haikupelekwa katika Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana kiasi cha Sh. Tz 95,859,585,597 ikiwa ni asilimia 10 kutoka Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi kati ya mwaka 2012/2013 mpaka 2015/2016.

Katika mwaka huu wa fedha, (2016/2017) nimeendelea kubaini mapungufu yaleyale, ambapo asilimia 10 ya mapato kutoka vyanzo vya ndani kiasi cha Sh. Tz 53,222,719,138 hakikuchangwa na Mamlaka za Serikali za Mtaa 143 kwenda katika mifuko hiyo kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.8-4.

**Jedwali Na. 8-4: Kiasi ambacho hakikuchangiwa kwenda katika mifuko ya Wanawake na Vijana**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya mamlaka za serikali za Mitaa | Fedha ambayo haikuchangwa (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 143 | 53,222,719,138 |
| 2015/2016 | 151 | 28,521,878,199 |
| 2014/2015 | 112 | 17,690,754,651 |
| 2013/2014 | 104 | 38,741,094,214 |
| 2012/2013 | 68 | 10,905,858,533 |

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeeleza kwamba kushindwa kuchangia katika mfuko huo kunatokana na upungufu wa fedha unaotokana na Hazina kupeleka fedha pungufu za matumizi mengineyo na ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu ikilinganishwa na

bajeti, huku gharama za uendeshaji wa Mamlaka hizo zikiongezeka. Aidha, makusanyo ya mapato ya ndani yamekuwa hayatoshelezi hata kutoa huduma za msingi katika Mamlaka hizo.

Orodha ya mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazikuchangia mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana imeainishwa katika **Kiambatisho Na.8-6.**

Maoni yangu ni kwamba Serikali iangalie upya namna ya kuendesha mfuko huu ikizingatiwa kwamba kwa hali ya sasa ni vigumu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchangia asilimia 10 ya Mapato yao ya ndani pamoja na kulipa malimbikizo ya michango ya nyuma. Serikali inaweza kuweka kiwango cha juu cha uchangiaji katika mifuko hiyo na kuweka muda maalum wa uchangiaji. Muongozo wa sasa wa uchangiaji wa asilimia kumi kutoka mapato ya ndani haujitoshelezi na hautekelezeki. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano kiasi ambacho hakijachangwa kinafikia Sh.Tz 149,082,304,735. Hii ina maana kuwa fedha nyingi zilitakiwa kuwa zimechangwa tangu mwaka 1993 mpaka leo.

### 8.5.1 Mikopo Iliyotolewa kwa vikundi vya Wanawake na Vijana ambayo haijarejeshwa Sh. Tz 5,809,326,477

Nilifanya tathmini ya ufanisi wa mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana na kubaini kwamba changamoto kubwa inayozikabili Mamlaka za Serikali za Mitaa ni namna ya kurejesha fedha kutoka kwa vikundi vilivyokopeshwa ili kuweza kukopesha vikundi vingine vya Wanawake na Vijana vyenye uhitaji.

Nimebaini kwamba kati ya jumla ya Sh. Tz 9,194,222,623 zilizokopeshwa kwa vikundi vya Wanawake na Vijana mwaka huu, Sh. Tz 3,384,896,146 tu ndizo zilizorejeshwa; na kiasi cha Sh. Tz 5,809,326,477 bado hakijarejeshwa licha ya tarehe za marejesho kwa mujibu wa mikataba kuwa zimeshapita.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilieleza kwamba kushindwa kukusanya marejesho hayo kunatokana na kutokuwapo kwa masharti yenye msukumo wa kisheria katika ukusanyaji wa madeni ya mfuko huo.

Jedwali Na. 8-5 linaonesha kwa muhtasari mikopo iliyotolewa kwa wanawake na vijana ambayo haijarejeshwa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo: -

**Jedwali Na. 8-5: Mikopo Iliyotolewa kwa wanawake na vijana ambayo Haijarejeshwa**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya mamlaka za serikali za Mitaa | kiasi kinachodaiwa (Sh.Tz) | % ya kiasi kinachodaiwa (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 84 | 5,809,326,477 | 63 |
| 2015/2016 | 76 | 4,746,008,627 | 50 |
| 2014/2015 | 52 | 2,003,235,125 | 21 |
| 2013/2014 | 41 | 1,426,955,884 | 15 |

Orodha ya Halmashauri zenye mikopo ambayo haijarejeshwa imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 8:7.**

Naishauri Serikali kuuboresha mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana katika namna ambayo utapata msukumo wa kisheria na kutengeneza mikakati ya urejeshaji mikopo ambayo itahamasisha urejeshwaji mikopo kwa hiari ili ukuaji wa mfuko uwe endelevu.

## 8.6 Changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Elimu bila malipo

Mnamo tarehe 27 Novemba 2015 Serikali ilitoa Waraka Na. 6 kwa ajili ya utekelezaji wa sera ya Elimu na Mafunzo ambao unawataka Walimu Wakuu wa shule zilizo katika Mamlaka za Manispaa, Miji na Wilaya pamoja na Bodi za shule kuhakikisha kuwa elimu ya msingi na Sekondari inatolewa bila malipo kwa wanafunzi wote. Waraka huu unataja kwamba "utoaji wa elimu bila malipo una maana kwamba wanafunzi hawatalipa ada au michango ya aina yoyote

iliyokuwa ikilipwa awali na wazazi kabla ya kutolewa kwa Waraka huu”.

Naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuhakikisha watoto wa Tanzania wanapata fursa ya Elimu, jambo ambalo limekuwa likitiliwa mkazo tangu nchi ipate uhuru. Mipango na sera za maendeleo zinajielekeza katika kuinua elimu ili kuongeza uzalishaji na ustawi.

Tangu kutolewa kwa Waraka huu, Serikali inatenga fedha kila mwezi kwa ajili ya kufidia gharama za uendeshaji na kuzituma moja kwa moja katika akaunti za shule husika.

Mapitio ya nyaraka za matumizi na mchakato wa manunuzi kwa baadhi ya shule zilizotembelewa na Wakaguzi kutoka Ofisi yangu yalibaini mapungufu yafuatayo; -

- Fedha zilitolewa bila kuzingatia uhalisi wa idadi ya wanafunzi. Idadi ya wanafunzi hubadilika mara kwa mara ilhali taarifa zilizotumika kuombea fedha zilikuwa hazihuishwi mara kwa mara. Hii inaweza kusababisha fedha pungufu au zaidi zikatumwa shuleni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 8:8.**
- Shule nyingi hazina wahasibu au wafanyakazi wenye uelewa wa uhasibu, hivyo taarifa nyingi za kihasibu hazitunzwi, vikiwemo vitabu vya kihasibu na taarifa za usuluhisho na benki za kila mwezi kinyume na matakwa ya Agizo Na. 27(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa la Mwaka 2009.

- Kukosekana kwa fedha za kulipa walinzi, walimu wa muda mfupi wa sayansi (kwa shule zenye upungufu), gharama za ukaguzi wa shule kikanda, vitambulisho, madeni kutoka kwa wazabuni wa nyuma, maji, umeme na gharama za mitihani ya kujipima. Hivyo, hakuna masomo ya ziada baada ya muda wa kawaida kumalizika.

- Mtazamo hasi wa jamii kwa kufikiri kuwa sera ya elimu bila malipo inawaondolea kabisa wajibu wa kuchangia elimu, ikiwamo kuwanunulia vifaa vya shule watoto wao.

- Manunuzi kufanyika bila kufuata sheria na kanuni yakiwamo manunuzi kutoka kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA), kukosekana kwa taarifa za ukaguzi wa vitu vilivyonunuliwa na wakati mwingine malipo hufanyika kabla ya kupata huduma.

- Elimu bure imeongeza idadi ya wanafunzi katika shule za msingi wakati miundombinu ya shule hizo haitoshi ikilinganishwa na ongezeko hilo.

- Hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo.

- Wajumbe wa Kamati na Bodi za shule na Walimu Wakuu hawajapatiwa mafunzo kuhusu taratibu za manunuzi na uhasibu kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa weledi.

Naishauri Serikali kuhakikisha kwamba, mpango mkakati kupambana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Elimu bila malipo unaandaliwa. Upungufu wa madarasa, walimu, vitabu and vifaa vingine vya kufundishia unatakiwa kutatutuliwa haraka.

Jamii ina mchango muhimu katika kuinua elimu na kuboresha shule zetu. Hivyo, kusitisha malipo ya ada kusipunguze ushiriki katika kuzisaidia shule; badala yake, iwe chachu kwao kushiriki kwa karibu katika maendeleo ya shule hizo. Jamii isizuiliwe kutoa msaada, ikiwemo ya vifaa inayotokana na juhudi zao bila kuzishurutisha familia zisizoweza kuchangia kama ambavyo amekuwa akisisitiza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli.

## 8.7 Ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu ambayo haikupelekwa ngazi za chini Sh. Tz 1,733,581,179

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato kutoka vyanzo vyao vya ndani. Lakini baadhi ya vyanzo vilivyotajwa katika sheria hiyo vilifutwa kati ya mwaka 2003 na 2004. Badala yake ukaanzishwa utaratibu wa kufidia vyanzo hivyo kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Mwongozo wa OR- TAMISEMI wa Mwaka 2005 unazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kupeleka asilimia 20 ya ruzuku hiyo katika ngazi ya Kata na Vijiji. Matumizi ya fedha hizi ni kuendesha ofisi pamoja na kuchangia miradi mingine ya maendeleo kama vile TASAF.

Katika mwaka huu wa fedha, nimebaini kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa 37 hazikupeleka asilimia 20 ya ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu iliyopokelewa kutoka Serikali Kuu kwenda ngazi za chini kiasi cha Sh. Tz 1,733,581,179 kinyume na Mwongozo uliotolewa. **Jedwali Na. 8-6** linaonesha kwa muhtasari fedha ambazo hazikupelekwa ngazi za chini: -

**Jedwali Na. 8-6: Ruzuku ya fidia kutoka Serikali Kuu ambayo haikupelekwa ngazi za chini**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Babati | 39,210,183 | 20 | H/W Kyela | 14,165,200 |
| 2 | H/W Bahi | 107,898,359 | 21 | H/W Kyerwa | 26,323,600 |
| 3 | H/W Bariadi | 257,675,873 | 22 | H/W Lindi | 193,960,900 |
| 4 | H/Mji Bariadi | 22,307,129 | 23 | H/W Magu | 17,817,600 |
| 5 | H/W Biharamulo | 11,007,897 | 24 | H/W Makete | 20,745,200 |
| 6 | H/W Buchosa | 17,758,400 | 25 | H/W Malinyi | 28,324,600 |
| 7 | H/W Buhigwe | 155,229,618 | 26 | H/W Maswa | 85,136,600 |
| 8 | H/W Bukoba | 20,090,000 | 27 | H/W Mbogwe | 16,625,050 |
| 9 | H/Mji Bunda | 16,957,379 | 28 | H/W Meatu | 23,177,400 |
| 10 | H/W Busega | 159,925,092 | 29 | H/W Meru | 59,600,096 |
| 11 | H/W Butiama | 32,534,000 | 30 | H/W Missenyi | 12,044,400 |
| 12 | H/W Chemba | 36,885,963 | 31 | H/W Muleba | 18,915,600 |
| 13 | H/W Chato | 20,612,400 | 32 | H/W Musoma | 17,944,400 |
| 14 | H/W Ikungi | 15,142,200 | 33 | H/W Ngara | 18,823,600 |
| 15 | H/W Ileje | 16,132,200 | 34 | H/W Ngorongoro | 87,265,140 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | N a. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 16 | H/W Iramba | 20,157,767 | 35 | H/W Rorya | 10,493,200 |
| 17 | H/W Karagwe | 19,735,200 | 36 | H/W engerema | 1,052,000 |
| 18 | H/W Kigoma | 79,147,433 | 37 | H/W Simanjiro | 15,435,800 |
| 19 | H/W Kishapu | 17,323,700 | | **Jumla** | **1,733,581,179** |

Uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ulinitaarifu kwamba kutokupelekwa kwa fedha hizo kulichangiwa na kukosekana kwa uhakika wa utoaji wa fedha hizo. Hii ina maana kwamba ngazi za chini haziwezi kutekeleza shughuli zake za kawaida na zile za maendeleo kama ilivyopangwa, na hivyo, kurudisha nyuma kasi ya maendeleo katika ngazi hizo.

Nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kupeleka mara moja asilimia 20 ya fedha zilizopokelewa ili kuziwezesha ngazi hizo kujiendesha na kutekeleza shughuli nyingine za maendeleo.

## 8.8 Mapungufu katika usimamizi wa Mfuko wa Afya wa Jamii

Mfuko wa Afya wa Jamii ulianzishwa kama mbadala wa gharama za matibabu kwa wananchi hasa waishio vijijini na wasio na bima za afya. Kwa ujumla, Mfuko wa Afya wa Jamii unalenga kuwawezesha wanachama wake kupata huduma za kiafya nzuri na za uhakika kwa kuanzisha mfumo wa malipo wa uhakika na endelevu.

Aya ya 3.3 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Fedha ya Mfuko wa Afya wa Jamii Toleo la Mwaka 2014 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kukamilisha uandaaji wa taarifa linganifu za misaada. Kinyume na matakwa ya aya hiyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 hazikuwa na taarifa linganifu za misaada. Pia, madai kwenda Bima ya Afya [NHIF] hayakufidiwa na wakati mwingine yalikataliwa kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 8:9**.

Nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuata Muongozo wa Usimamizi wa fedha na Uendeshaji wa Mfuko wa Afya wa Jamii.

## 8.9 Upungufu wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari

Upatikanaji wa elimu bora unategemea mazingira bora na miundobinu ya elimu inayojitosheleza inayojumuisha madarasa, maabara, vyoo, migahawa, nyumba za watumishi na viwanja vya michezo.

Nimetathmini utoshelevu wa miundombino katika sekta ya elimu, hasa katika shule za Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 31 na kubaini upungufu mkubwa wa miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri utoaji wa elimu bora kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 8-7.

**Jedwali Na. 8-7:Muhtasari wa hali ya miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari**

| Maelezo | Mahitaji | Iliyopo | Upungufu | % |
|---|---|---|---|---|
| **Shule za Sekondari** | | | | |
| Vyumba vya Madarasa | 24797 | 12001 | 12796 | 52 |
| Maabara | 6772 | 1065 | 5707 | 84 |
| Matundu ya Vyoo | 33652 | 15913 | 17739 | 53 |
| Madawati | 211197 | 28637 | 182560 | 86 |
| Nyumba za walimu | 6879 | 1041 | 5838 | 85 |
| Mabweni | 11461 | 1366 | 10095 | 88 |
| | | | | |
| **Primary school** | | | | |
| Vyumba vya Madarasa | 83369 | 12790 | 70579 | 85 |
| Matundu ya Vyoo | 105776 | 18272 | 87504 | 83 |
| Madawati | 246303 | 212255 | 34048 | 14 |
| Nyumba za walimu | 14257 | 4868 | 9389 | 66 |

Aidha, upungufu huo umepelekea kutokufikiwa kwa wastani unaohitajika wa Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 (1:45). Kwa hiyo:

- Idadi kubwa ya walimu imeshidwa kufika katika vituo vipya vya kazi, hasa maeneo ya vijijini, kutokana na maeneo hayo kukosa miundombinu inayojitosheleza.

- Upungufu wa miundombinu unaweza kuathiri utoaji wa elimu bora na kusababisha matokeo mabaya ya wanafunzi. Aidha, mkakati wa kuondoa wasiojua kusoma na kuandika unaweza kuchukua muda mrefu kufanikiwa kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na serikali kutatua tatizo hilo.

Nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa, OR-TAMISEMI pamoja na Wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wote wa elimu kuweka mikakati inayotekelezeka nay a haraka ili kuweza kutatua tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu iliyopo ili sekta ya elimu nchini iweze kuimarika zaidi.

## SURA YA TISA

## 9.0 USIMAMIZI WA MIKATABA NA MANUNUZI

Kifungu cha 3 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. ya 7 ya mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa 2016 kinafafanua manunuzi kama njia ya kununua, kukodisha, au kukodisha bidhaa yoyote, kazi au huduma kwa taasisi za manunuzi. Hujumuisha kazi zote zinazohusiana na kupata bidhaa yoyote, kazi au huduma, ikiwa ni pamoja na maelezo ya mahitaji, uteuzi na mwaliko wa zabuni, maandalizi, tuzo na usimamizi wa mikataba. Kutokana na ukweli kwamba kiasi kikubwa cha rasilimali za Serikali hutumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma, kuna haja ya kuimarisha nidhamu ya fedha na uwazi katika mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kufikia kiwango cha juu cha thamani ya fedha.

### 9.1 Taswira ya Manunuzi yaliyofanyika Katika kipindi kinachotolewa taarifa

Ukaguzi wa manunuzi ya bidhaa na huduma katika mwaka wa fedha 2016/2017 ulifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185. Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa jumla ya Sh. Tz 1,357,364,182,309 kilitumika kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma ambapo ni ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. Tz 1,059,766,536,340 kilichotumika mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Ongezeko la manunuzi limetokana na kuongezeka la idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 14 (kutoka 171 mwaka 2015/16 hadi 185 kwa mwaka 2016/17) na utekelezaji wa huduma zilizoko kwenye Halmashauri mpya. Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya miundombinu mipya, bidhaa na huduma, pamoja na gharama za matengenezo ili kuendeleza shughuli za kila siku katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mpya.

Uchambuzi wa kiasi kilichotumiwa na halmashauri kwenye ununuzi wa bidhaa, ushauri na huduma kwa miaka mitatu mfululizo 2016/2017, 2015/2016 na 2014/2015 ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-1 hapa chini.

**Jedwali Na. 9-1: Gharama za manunuzi zilizofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitatu.**

| Aina ya manunuzi | 2016/2017 (Sh.Tz) (milioni) | % | 2015/2016 (Sh.) | % | 2014/2015 (Sh.Tz) | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (milioni) | | (milioni) | |
| Manunuzi ya bidha na huduma | 608970 | 45 | 497086 | 47 | 421167 | 39 |
| Manunuzi ya matengenezo mbalimbali | 198961 | 15 | 142946 | 13 | 153413 | 14 |
| Manunuzi ya mali za kudumu na | 549431 | 40 | 419733 | 40 | 518051 | 47 |
| miradi ya maendeleo | | | | | | |
| Jumla | 1357364 | 100 | 1059766 | 100 | 1092633 | 100 |

Kutokana na jedwali hilo hapo juu, inaonekana manunuzi ya mali za kudumu na miradi ya maendeleo yalipungua kwa asilimia 7 mwaka 2014/15. Mwaka 2015/16 hadi 2016/17 kiwango cha manunuzi hakikubadilika, kilibaki kuwa asilimia 40. Gharama za matengenezo zilipungua kwa asilimia 1 kwa mwaka 2014/2015 na 2015/2016. Aidha, gharama hizo ziliongezeka kwa asilimia 2 kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017. Manunuzi ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 8 kwa mwaka 2014/2015 na 2015/2016. Kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017 manunuzi yalipungua kwa asilimia 2. Maelezo zaidi yanaoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 9:1.**

## 9.2 Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013

Kifungu cha 48 (3) cha Sheria za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, kinanitaka kueleza katika ripoti yangu ya mwaka kama taasisi nilizozikagua zimezingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake. Kwa kuzingatia jukumu hili, katika ukaguzi wa manunuzi nimebaini kuwa, kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 185, Mamlaka za Serikali za Mitaa 144, sawa na asilimia 78,

zilifuata Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake wakati Mamlaka za Serikali za Mitaa 41, sawa na asilimia 22, hazikuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Jedwali Na. 9-2 linaonesha Idadi ya Halmashauri ambazo hazikufuata Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2016 na kanuni zake za mwaka 2013.

**Jedwali Na. 9-2: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikufuata Sheria ya Manunuzi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Na. | Jina la Halmashauri | Na. | Jina la Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Kasulu | 15 | H/W Arusha | 29 | H/Mji Mafinga |
| 2 | H/W Nzega | 16 | H/W Karatu | 30 | H/W Kilolo |
| 3 | H/W Urambo | 17 | H/W Longido | 31 | H/W Mbarali |
| 4 | H/M Tabora | 18 | H/W Kiteto | 32 | H/W Busokelo |
| 5 | H/W Bunda DC | 19 | H/W Mbulu | 33 | H/W Momba |
| 6 | H/M Bukoba | 20 | H/M Mpanda | 34 | H/W Songwe |
| 7 | H/W Biharamulo | 21 | H/W Mpanda | 35 | H/M Songea |
| 8 | H/W Muleba | 22 | H/W Nsimbo | 36 | H/W Songea |
| 9 | H/W Ngara | 23 | H/Mji Njombe | 37 | H/W Madaba |
| 10 | H/Mji Kahama | 24 | H/Jiji Arusha | 38 | H/Jiji Dar es salaam |
| 11 | H/W Nyasa | 25 | H/W Kaliua | 39 | H/M Kigoma Ujiji |
| 12 | H/M Ilemela | 26 | H/W Moshi | 40 | H/W Mpwapwa |
| 13 | H/Mji Kondoa | 27 | H/Mji Nzega | 41 | H/Jiji Tanga |
| 14 | H/W Ngorongoro | 28 | H/W Iringa | | |

Kiwango cha kutozingatia sheria ya manunuzi ya mwaka 2011 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2016 na kanuni zake za mwaka 2013 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kishuka kwa asilimia 7 kutoka asilimia 29 mwaka 2015/16 hadi asilimia 22 mwaka 2016/17 kama inavyoonekana hapa chini.

**Jedwali Na. 9-3: Kiwango cha uzingatiaji wa sheria ya manunuzi kwa kipindi cha miaka miwili**

| Uzingatiaji | 2016/17 | | 2015/16 | |
|---|---|---|---|---|
| | Halmashauri | % | Halmashauri | % |
| Kutokuzingatia | 41 | 22 | 50 | 29 |
| Kuzingatia | 144 | 78 | 121 | 71 |
| **Jumla** | **185** | **100** | **171** | **100** |

Ninashauri Serikali iimarishe vitengo vya Manunuzi kwa kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kuwajengea uwezo watendaji wake na kuajiri idadi itakayowatosheleza ili kupunguza mapungufu yaliyojitokeza.

## 9.3 Mapungufu katika kuzingatia Utaratibu wa Ununuzi wa Umma

Nilikagua na kufanya tathmini za uzingatiaji wa sheria za manunuzi, na nilibainisha idadi kubwa ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazikufuata taratibu za manunuzi.

Halmashauri 92 zilikiuka taratibu za manunuzi, katika kipindi cha utekelezaji wa mikataba, kufanya malipo zaidi ya kiasi cha mikataba, marekebisho yasiyo sahihi katika mikataba pamoja na udhaifu katika ufuatiliaji wa mikataba wakati wa utekelezaji. Malipo mengine yalifanyika bila kuwa na ankara za malipo, hati za mapokezi ya bidhaa, hati za kuagiza bidhaa, vocha za kupokelea bidhaa, nukuu za bei, na fomu za uidhinishwaji manunuzi,na baadhi ya malipo yalifanywa kabla ya kupokelewa kwa bidhaa na huduma; hati za mapokezi ya bidhaa kutosainiwa na mpokeaji; ankara za malipo na hati za mapokezi ya bidhaa kutokuonesha tarehe; hati za mapokezi ya bidhaa na ankara za malipo kuonesha kuwa zilipokelewa kabla ya kutolewa kwa Hati za kuagiza bidhaa.Mapungufu mengine ni baadhi ya hati za kuagiza bidhaa kutokuwa na saini ya Afisa Masuuli.

Halmashauri zilizohusika zinaoneshwa kwenye **Kiambatisho 9-2** cha ripoti hii.

Kutokana na kutokuzingatiwa kwa Sheria namba 7 ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016 na Kanuni zake za 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016, orodha ya mamlaka za Serikali za Mitaa hazikubaini thamani ya fedha kwenye manunuzi.

Napendekeza kuwa menegimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuchukua hatua stahiki za kerekebisha mapungufu yaliobainishwa hapo juu pia kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni za manunuzi ili kupata ufanisi na thamani ya fedha.

## 9.4 Udhaifu katika Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Manunuzi

Nilifanya mapitio katika mipango ya mwaka ya manunuzi ili kuangalia kama manunuzi yametekelezwa kwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi; nimebaini madhaifu yafuatayo;

**Jedwali Na. 9-4: Udhaifu katika Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Manunuzi**

| Na | Halmashauri | Maoni |
|---|---|---|
| A | H/W Meru | Mpango wa Mwaka wa Manunuzi haukuandaliwa. Hii ni kinyume na Kanuni ya 69(3-5) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016. |
| | H/W Ngorongoro | |
| B | H/W Kalambo | Halmashauri hazikuandaa wala kuwasilisha ripoti za kila robo mwaka za utekelezaji wa mpango wa mwaka wa manunuzi kinyume na Kanuni Na.38(o) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2011. |
| | H/W Songwe | |
| | H/W Monduli | |
| | H/W Misungwi | |
| | H/W Mbulu | |
| | H/W Bumbuli | |
| | H/Mji Mafinga | |
| | H/Mji Mbulu | |
| C | H/W Magu | H/W hazikutangaza mpango wa manunuzi wa mwaka kupitia tovuti ya zabuni kinyume na kanuni ya 18 ( 1) na 19 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013. |
| | H/W Mbulu | |
| | | |
| D | H/W Magu | Mpango wa Mwaka wa Manunuzi haukuwasilishwa kwenye Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma ndani ya siku 14 baada ya kukamilika kwa mchakato wa bajeti, kama inavyotakiwa na Kanuni ya |
| | H/W Busega | |
| | H/W Momba | |

| Na | Halmashauri | Maoni |
|---|---|---|
| | | 70 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. |
| E | Monduli DC | H/W hazikuandaa na kujumuisha gharama shirikishi kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka wa halmashauri kinyume na Kanuni Na. 39(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. |

Hali iliyoelezwa hapo juu inaweza kupelekea kufanyika kwa manunuzi yasiyo kwenye mpango na yasiyo na ushindani.

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinafanya manunuzi yaliyo kwenye mpango wa manunuzi na kwa mujibu wa sheria za manunuzi.

## 9.5 Tathmini ya Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi na Bodi ya Zabuni

Nimefanya tathmini katika eneo la utendaji la Vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi na Bodi za Zabuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa na nimebaini mapungufu yafuatayo kama yalivyoelezewa kwenye Jedwali Na. 9.5 hapa chini:

**Jedwali Na. 9-5: Mapungufu yaliojitokeza kwenye vitengo vya manunuzi na Bodi ya Zabuni**

| Na. | Halmashauri | Maoni |
|---|---|---|
| a | H/W Ileje | Mamlaka za Serikali za Mitaa tajwa hazikuzingatia kanuni inayotaka kuanzisha vitengo vya Manunuzi vyenye Maafisa Ugavi na wataalamu wengine wa kiufundi pamoja na wasaidizi na wafanyakazi wa kiutawala kinyume na Kifungu Na. 37(1-2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. |
| | H/W Magu | |
| | H/W Mlele | |
| | H/W Mbeya | |
| | H/W Mufindi | |
| | H/W Rungwe | |
| | H/W Songwe | |
| | H/W Hanang | |
| | H/W Chalinze | |
| | H/W Kondoa | |
| | H/W Same | |
| b | H/W Nkasi | |

| Na. | Halmashauri | Maoni |
|---|---|---|
| | H/W Same | Mamlaka za Serikali za Mitaa tajwa hazikuanzisha Bodi ya Zabuni kinyume na Kifungu Na. 7 cha Sheria ya Bodi ya Wazabuni ya mwaka 2014 na Sheria Na. 31 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. |
| c | H/W Mbeya | Bodi ya zabuni kutokuwa na wataalamu wa kutosha kinyume na Kifungu Na. 7 (1)&(2)(c) ya Sheria ya Bodi ya Wazabuni ya mwaka 2014 |
| | H/W Ngorongoro | |
| | H/W Same | |
| | H/W Meru | |
| d | H/W Momba | Bodi ya Zabuni kutotimiza wajibu wake pia bajeti isiyokidhi utekelezaji wa majukumu ya Bodi na Kamati ya Tathimini kinyume na Kifungu Na. 38(i) cha sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 Na. 7 (e) cha sheria ya Bodi ya Wazabuni ya mwaka 2014. |
| | H/W Chalinze | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| e | H/W Maswa | Utunzaji wa daftari za mikataba kinyume na Aya ya 2.4.3 ya LAAM ya mwaka 2009. |
| | H/W Malinyi | |
| | H/W Nzega | |
| | H/W Kilosa | |
| f | H/M Tabora | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi aliingilia kati majukumu ya kamati ya tathimini kinyume na Kifungu cha 41 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma mwaka 2011. |
| | | |
| | | |
| g | H/W Meatu | Utunzaji wa daftari la matengenezo na ukarabati wa magari na mitambo ulikuwa kinyume na kanuni Na. 137(4)(a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. |
| h | H/W Itigi | Mamlaka za Serikali za Mitaa tajwa hazikutekeleza ushauri waliopewa na wanasheria dhidi ya mikataba hii ni kinyume na Kanuni ya 59 (1) & (5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013<br>Kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016. |
| | H/Mji Tunduma | |
| | H/W Mbeya | |
| | H/W Busokelo | |
| | | |

Maoni yangu ni kwamba, kutokuwa na mchanganyiko wa fani mbalimbali kwenye vitengo vya manunuzi na bodi za zabuni ndio sababu inayosababisha manunuzi yasiyokuwa na tija.

Ninashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi vina watumishi wenye uwezo na wenye sifa kama inavyotakiwa na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za manunuzi za mwaka 2011. Hivyo, Bodi za Zabuni zinatakiwa kuwa na wajumbe wenye fani mbalimali ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya umma.

## 9.6 Matokeo ya ukaguzi wa manunuzi katika Serikali za Mitaa

Kanuni Na. 4(1), (2)(a) na(d), na 5(1), (2) (a-c) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016 inazitaka taasisi za manunuzi kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kwa uaminifu na uadilifu wakati wanafanyapo manunuzi.

Nyaraka zilizokaguliwa zinazotokana na manunuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Ukaguzi huo ulilenga kufanya tathmini ya taratibu za manunuzi, menejimenti ya mikataba na udhibiti ili kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata sheria, haki, usawa, uwazi, ushindani, kupunguza udanganyifu, rushwa, upendeleo na vitendo visivyoashiria usawa. Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi:

### 9.6.1 Mchakato usiokuwa na ushindani wa manunuzi SH.TZ 1,413,388,622

Ukaguzi wa nyaraka za manunuzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 umeonesha Mamlaka za Serikali za Mitaa 32 zilitumia jumla ya SH.TZ 1,413,388,622 kwa ajili ya gharama za ujenzi, huduma na bidhaa bila kushindanisha wazabuni kinyume na Kanuni Na. 163 na 164 za Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016.

Hali hiyo inatia shaka kama thamani ya fedha ilipatikana katika Halmashauri zilizofanya manunuzi kwa kutumia manunuzi ya moja kwa moja pasipo kushindanisha.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanya manunuzi ya bidhaa, huduma, kazi na ushauri pasipo kushindanisha wazabuni pamoja na kiasi kilichohusika zimeorodheshwa kwenye Jedwali Na. 9-6 hapa chini;

**Jedwali Na. 9-6: Orodha ya Serikali za mitaa zilizofanya manunuzi pasipo ushindani**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mpwapwa | 27,067,920 | 18 | H/Mji Handeni | 6,694,795 |
| 2 | H/W Manyoni | 17,016,400 | 19 | H/W Kilindi | 6,340,730 |
| 3 | H/W Itigi | 15,996,540 | 20 | H/W Pangani | 16,590,272 |
| 4 | H/W Kigoma/Ujiji | 23,720,000 | 21 | H/W Mbulu | 7,950,000 |
| 5 | H/W Uvinza | 12,867,830 | 22 | H/W Mpanda | 23,072,466 |
| 6 | H/Mji Kasulu | 103,996,600 | 23 | H/Mji Njombe | 9,826,200 |
| 7 | H/W Kigoma | 7,080,000 | 24 | H/Mji Makambako | 23,939,600 |
| 8 | H/W Sikonge | 1,540,000 | 25 | H/Mji Mafinga | 42,446,000 |
| 9 | H/W Mtwara | 8,614,000 | 26 | H/W Kilolo | 11,298,108 |
| 10 | H/W Newala | 25,908,506 | 27 | H/W Busokelo | 14,300,695 |
| 11 | H/Mji Masasi | 56,124,563 | 28 | H/W Songea | 68,764,435 |
| 12 | H/M Ilemela | 315,771,819 | 29 | H/W Madaba | 4,659,900 |
| 13 | H/W Missenyi | 24,500,002 | 30 | H/W Tunduru | 313,589,533 |
| 14 | H/M Kahama | 141,788,976 | 31 | H/W Kalambo | 9,148,433 |
| 15 | H/W Karatu | 10,835,200 | 32 | H/W Nkasi | 30,462,263 |
| 16 | H/W Moshi | 30,162,400 | **Jumla** | | **1,413,388,622** |
| 17 | H/W Bumbuli | 1,314,436 | | | |

Ulinganisho wa manunuzi pasipo ushindani kwa miaka mitatu ni kama inavyooneka katika **Jedwali Na.9-7** hapa chini;

**Jedwali Na. 9-7: Mwenendo wa manunuzi pasipo ushindani**

| Mwaka | Manunuzi pasipo ushindani (Sh.) | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2016/17 | 1,413,388,622 | 32 |
| 2015/16 | 2,120,374,651 | 36 |
| 2014/15 | 337,093,387 | 11 |

Kutokana na Jedwali hilo hapo juu, ninahitimisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye manunuzi yasiyo ya ushindani yamepungua kwa Shilingi 706,986,029 kutoka mamlaka 36 kwa mwaka 2015/2016 hadi 32 kwa mwaka 2016/2017 sawa na asilimia 34.

Napendekeza mamlaka zote kuhakikisha wazabuni wanashindanishwa ili kupata bei shindani na kuzingatia viwango na taratibu za manunuzi. Endapo mzabuni mmoja atatumiwa katika manunuzi, lazima kuwepo sababu na uhalali wa kutosha.

### 9.6.2 Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni Sh. 2,703,509,121

Nimebaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 zimefanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa mwaka wa fedha 2016/2017 bila ya kupata idhini ya Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni Na. 163(4) na 185(1) ya kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Orodha ya Halmashauri na kiasi husika kinaonekana katika Jedwali Na. 9-8 hapa chini.

**Jedwali Na. 9-8: Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi( Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Kigamboni | 159,938,687 | 14 | H/Jiji Tanga | 329,348,438 |
| 2 | H/Mji Kibaha | 48,669,000 | 15 | H/Mji Mbulu | 32,729,500 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi( Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | H/W Mafia | 33,101,300 | 16 | H/M Mpanda | 33,565,473 |
| 4 | H/W Serengeti | 141,273,440 | 17 | H/Mji Njombe | 15,864,000 |
| 5 | H/W Rorya | 7,386,120 | 18 | H/W Ludewa | 15,075,195 |
| 6 | H/Mji Tarime | 12,000,000 | 19 | H/Mji Makambako | 11,056,105 |
| 7 | H/M Ilemela | 59,922,000 | 20 | H/W Makete | 6,334,712 |
| 8 | H/M Bukoba | 164,510,151 | 21 | H/W Kilolo | 7,168,972 |
| 9 | H/W Biharamulo | 68,156,800 | 22 | H/W Mbarali | 56,341,467 |
| 10 | H/W Ngara | 24,920,000 | 23 | H/W Songwe | 102,359,171 |
| 11 | H/Jiji Arusha | 53,490,400 | 24 | H/M Songea | 13,173,188 |
| 12 | H/W Meru | 58,924,602 | 25 | H/W Nyasa | 1,235,200,400 |
| 13 | H/W Kilindi | 13,000,000 | **Jumla** | | **2,703,509,121** |

Ulinganisho wa manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni kwa miaka iliyopita ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-9 hapa chini.

**Jedwali Na. 9-9: Mwenendo wa manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni kwa miaka mitatu inayofuatana**

| Mwaka | Kiasi (Sh.) | Idadi ya serikali za mitaa |
|---|---|---|
| 2016/17 | 2,703,509,121 | 25 |
| 2015/16 | 907,898,325 | 17 |
| 2014/15 | 824,726,260 | 11 |

**Jedwali Na. 9-9** hapo juu linaonesha kwamba, kiasi ambacho hakikupitishwa na Bodi ya Zabuni kimeongezeka kwa kiasi cha Shilingi 83,172,065 kutoka mwaka 2014/2015 hadi 2015/2016 sawa na asilimia 10 na kwa kiasi cha Shilingi 1,795,610,796 kwa mwaka 2015/2016 hadi 2016/2017 sawa na asilimia 198 kinaonesha kuwa

kuna ongezeko kubwa la kiasi na idadi ya Serikali za Mitaa zilizofanya manunuzi bila ya kupata kibali cha Bodi ya Zabuni. Mbali na kutozingatia Sheria na kanuni zilizonukuliwa, thamani ya fedha katika manunuzi haya inaweza isipatikane. Hata hivyo, napendekeza kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata kibali cha Bodi ya Zabuni kama inavyotakiwa na sheria na kanuni zake ili ziweze kupata thamani ya fedha katika manunuzi yanayofanyika na ili mapungufu haya yasijitokeze tena.

### 9.6.3 Manunuzi yaliyofanywa kutoka kwa wauzaji ambao hawakuidhinishwa SH.TZ 936,775,623

Wakati wa ukaguzi wa matumizi na malipo yaliyofanywa katika mwaka wa fedha 2016/2017, nimegundua kuwa Mamlaka 27 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni ambao hawakuidhinishwa kinyume na Kanuni Na. 131(4)(b) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa mwaka 2016.
Maelezo zaidi yanaoneshwa kwenye Jedwali Na. 9-10 hapa chini;

**Jedwali Na. 9-10: Halmashauri zilizofanya Councils that Procured Goods and Service from Unapproved Supplier**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Dodoma | 9,557,100 | 15 | H/W Monduli | 9,801,600 |
| 2 | H/W Itigi | 9,066,480 | 16 | H/M Moshi | 30,162,400 |
| 3 | H/M Kigoma/Ujiji | 51,311,640 | 17 | H/W Moshi | 13,620,000 |
| 4 | H/W Kasulu | 12,222,420 | 18 | H/W Mpanda | 17,250,107 |
| 5 | H/W Mafia | 39,824,158 | 19 | H/W Nsimbo | 17,486,246 |
| 6 | H/W Kisarawe | 31,850,002 | 20 | H/W Mpimbwe | 2,522,439 |
| 7 | H/W Misungwi | 21,420,000 | 21 | H/W Mbarali | 56,341,467 |
| 8 | H/W Magu | 21,197,020 | 22 | H/W Chunya | 23,600,000 |
| 9 | H/M Bukoba | 164,510,151 | 23 | H/W Busokelo | 21,615,000 |
| 10 | H/Mji Kahama | 116,600,257 | 24 | H/W Tunduma | 3,976,000 |
| 11 | H/M Shinyanga | 46,835,015 | 25 | H/W Songwe | 102,359,171 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 12 | H/Jiji Arusha | 9,313,000 | 26 | H/W Madaba | 18,243,500 |
| 13 | H/W Karatu | 19,369,200 | 27 | H/W Mbinga | 41,299,650 |
| 14 | H/W Meru | 25,421,600 | | **Jumla** | **936,775,623** |

**Jedwali Na. 9-11: Mwenendo wa manunuzi yaliyofanyika kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa**

| Mwaka | Kiasi (Sh.) | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 936,775,623 | 27 |
| 2015/2016 | 1,182,526,122 | 27 |
| 2014/2015 | 672,423,123 | 28 |

Jedwali hapo juu linaonesha mwelekeo wa manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa yamepungua kwa Shilingi 245,750,499 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa 27 zilizoripotiwa miaka ya nyuma na mamlaka za serikali 27 zilizoripotiwa mwaka unaotolewa taarifa.

Manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa kinajenga uwezekano wa kununua huduma na bidhaa zisizoendana na thamani ya fedha.

Napendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotajwa kufanya manunuzi kwa kuzingatia kanuni za manunuzi zilizoelezwa hapo juu pia kuzingatia ufanisi na tija katika matumizi ya fedha za umma.

### 9.6.4 Ununuzi wa Bidhaa na Huduma kwa Kutumia masurufu SH.TZ 662,411,904

Tathmini ya ukaguzi wa mfumo wa manunuzi na ukaguzi wa nyaraka zinazohusiana na manunuzi katika Serikali za Mitaa 20 zinaonyesha kwamba, watumishi mbalimbali walipewa masurufu ya jumla ya Sh. 662,411,904 kwa ajili ya ama kununua bidhaa na huduma, kazi na ushauri bila ya kutumia hati ya manunuzi kinyume na Agizo Na. 69(1) ya Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya

mwaka 2009 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-12 hapo chini.

**Jedwali Na.9-12: Mamlaka za serikali za mitaa zilizofanya manunuzi kwa njia ya masurufu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Kigamboni | 90,899,364 | 12 | H/W Longido | 13,734,100 |
| 2 | H/W Mafia | 6,900,000 | 13 | H/M Moshi | 30,162,400 |
| 3 | H/W Kisarawe | 18,260,000 | 14 | H/W Bumbuli | 11,616,500 |
| 4 | H/W Chalinze | 9,613,000 | 15 | H/Mji Makambako | 33,853,920 |
| 5 | H/Mji Nanyamba | 2,500,000 | 16 | H/Jiji Mbeya | 21,958,000 |
| 6 | H/Mji Newala | 4,227,000 | 17 | H/Jiji Mbeya | 70,044,700 |
| 7 | H/W Bariadi | 69,060,600 | 18 | H/W Ileje | 22,590,000 |
| 8 | H/W Busega | 9,092,180 | 19 | H/Mji Tunduma | 2,250,000 |
| 9 | H/Jiji Mwanza | 129,007,740 | 20 | H/M Songea | 27,528,400 |
| 10 | H/W Kwimba | 45,691,000 | | **Jumla** | **662,411,904** |
| 11 | H/W Ukerewe | 43,423,000 | | | |

Kitendo hiki kinakiuka mchakato wa manunuzi ya umma, hasa kanuni za msingi za uwazi, ushindani, ufanisi, usawa na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Napendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa tajwa kuhahikisha kuwa manunuzi yote yanafanyika kwa kutoa hundi kwa wazabuni baada ya kuzingatia taratibu za manunuzi. Na kwa mara nyingine tena nazishauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha Vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi na taratibu za manunuzi ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za umma.

### 9.6.5 Ununuzi wa bidhaa na huduma kwa fedha taslimu Sh.Tz 469,663,282

Agizo Na. 68 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, inaelekeza malipo ya bidhaa au huduma yanayofanywa na taasisi za serikali yalipwe kwa mzabuni kwa njia ya hundi. Kinyume

na agizo hilo, Serikali za Mitaa 14 ziliwalipa wazabuni jumla ya 469,663,282 fedha tasilmu badala ya hundi. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-13 hapo chini;

**Jedwali Na.9-13: Ununuzi wa bidhaa na huduma kwa fedha taslimu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz | Na. | Jina la Halmashsuri | Kiasi (Sh.Tz.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Dodoma | 3,558,500 | 9 | H/M Moshi | 35,774,400 |
| 2 | H/M Singida | 25,837,000 | 10 | H/W Rombo | 22,210,000 |
| 3 | H/M Kinondoni | 102,526,472 | 11 | H/W Muheza | 6,620,000 |
| 4 | H/W Gairo | 2,829,000 | 12 | H/W Pangani | 5,135,000 |
| 5 | H/M Ubungo | 27,519,000 | 13 | H/W Mlele | 14,271,000 |
| 6 | H/Jiji Arusha | 13,550,000 | 14 | H/W Sumbawanga | 189,536,410 |
| 7 | H/W Arusha | 9,990,500 | | **Jumla** | **469,663,282** |
| 8 | H/W Ngorongoro | 10,306,000 | | | |

Kiasi kilichoripotiwa kulipwa kwa kutumia fedha taslimu kimepungua kwa Sh.Tz 592,267,023 sawa na asilimia 56 kutoka mwaka 2015/2016 (Sh.Tz 1,061,930,305) hadi mwaka 2016/2017 (Sh.Tz 469,663,282). Hii inaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanya jitihada ya kutatua tatizo hilo kwa mwaka ninaoutolea taarifa.

Kwa maoni yangu, ununuzi wa bidhaa na huduma kwa fedha taslimu unaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kuwa unatoa nafasi ya kufanyika kwa matumizi mabaya ya fedha.

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Serikali za Mitaa kuanzisha utaratibu sahihi wa kuepuka kulipa fedha taslimu kwa manunuzi ya bidhaa na huduma za umma ili kupunguza athari ya matumizi mabaya ya fedha kwa umma kwa kufuata Agizo Na. 68 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

### 9.6.6 Bidhaa zilizopokelewa bila kukaguliwa na Kamati ya Mapokezi Sh.Tz 644,312,449

Kanuni ya 244 na 245 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 zinamtaka Afisa Masuuli kuunda Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya Bidhaa itakayowajibika kukagua, kupima bidhaa na huduma zilizopokelewa kutoka kwa wazabuni na kubainisha kama idadi ni sawa, ubora na bei stahiki. Kinyume na kanuni iliyotajwa, Mamlaka za Serikali za Serikali za Mitaa 25 zilipokea bidhaa zenye thamani ya SH.TZ 644,312,449 bila kukukaguliwa na Kamati ya Ukaguzi.

Orodha ya Serikali za Mitaa zilizopokea bidhaa bila kukaguliwa ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.

**Jedwali Na.9-14: Serikali za Mitaa zilizopokea bidhaa bila kukaguliwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Singida | 5,231,570 | 14 | H/W Muheza | 24,933,620 |
| 2 | H/W Urambo | 14,040,000 | 15 | H/W Pangani | 13,625,000 |
| 3 | H/W Chalinze | 4,116,000 | 16 | H/Jiji Tanga | 52,434,768 |
| 4 | H/W Kilombero | 44,442,164 | 17 | H/W Kiteto | 20,622,336 |
| 5 | H/W Misungwi | 16,627,500 | 18 | H/W Mbulu | 7,950,000 |
| 6 | H/W Ushetu | 40,402,000 | 19 | H/Mji Makambako | 9,771,105 |
| 7 | H/Jiji Arusha | 23,586,300 | 20 | H/W Mbarali | 29,267,500 |
| 8 | H/W Karatu | 9,617,200 | 21 | H/W Songwe | 102,359,171 |
| 9 | H/W Longido | 7,055,800 | 22 | H/M Songea | 47,926,200 |
| 10 | H/W Meru | 21,920,420 | 23 | H/W Madaba | 4,659,900 |
| 11 | H/M Moshi | 30,162,400 | 24 | H/W Mbinga | 69,624,200 |
| 12 | H/W Rombo | 6,096,000 | 25 | H/W Kalambo | 31,146,500 |
| 13 | H/Mji Handeni | 6,694,795 | | **Jumla** | **644,312,449** |

Idadi ya Serikali za Mitaa zilizokuwa na hili tatizo haijabadilika kwa mwenendo wa miaka miwili mfululizo. Ingawa kiasi kimepungua kwa Sh. Tz 145,511,821 sawa na asilimia 19 kutoka Sh. 789,824,270 kwa mwaka 2015/2016 hadi Sh.Tz 644,312,449 kwa mwaka 2016/2017.

Kwa mtazamo wangu, Kuna uwezekano wa kununua bidhaa zenye ubora hafifu na kwa bei ya juu pia haziendani na vigezo vilivyowekwa katika mkataba.

Napendekeza kwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya Bidhaa zinaanzishwa na zinakagua na kutoa taarifa kama bidhaa zilizonunuliwa zina viwango na ubora unaotakiwa.

### 9.6.7 Manunuzi yaliyofanywa nje ya Mpango wa Mwaka wa manunuzi Sh. 2,384,412,108

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 inataka taasisi inayofanya manunuzi kukadiria mahitaji yake ya bidhaa, huduma na kazi kwa usahihi kadri inavyowezekana kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zimeingizwa katika mpango kazi wa mwaka pamoja makadirio ya mwaka. Kadhalika, mpango husika lazima uoneshe seti ya mkataba, gharama kadiriwa kwa kila seti ya mkataba na utaratibu wa manunuzi utakaotumika. Kinyume na kanuni hapo juu nimegundua kuwa bidhaa, kazi na huduma zenye thamani Sh. 2,384,412,108 zilizonunuliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 21 zimefanyika nje ya Mpango wa Mwaka wa manunuzi.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizonunua bidhaa, kazi na huduma nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka ni kama zinavyonekana kwenye Jedwali Na.9-15 hapo chini;

**Jedwali Na.9-15: Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizonunua bidhaa, kazi na huduma nje ya mpango wa manunuzi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Singida | 57,096,380 | 12 | H/W Arusha | 187,916,166 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | H/W Mkalama | 300,007,920 | 13 | H/W Karatu | 388,208,200 |
| 3 | H/W Mafia | 1,301,479,323 | 14 | H/W Ngorongoro | 10,306,000 |
| 4 | H/Mji Masasi | 101,240,000 | 15 | H/Jiji Tanga | 60,040,000 |
| 5 | H/W Bariadi | 429,368,403 | 16 | H/W Babati | 27,574,800 |
| 6 | H/Mji Bariadi | 83,265,215 | 17 | H/Mji Makambako | 27,924,305 |
| 7 | H/W Busega | 17,711,580 | 18 | H/W Iringa | 2,000,000 |
| 8 | H/W Kwimba | 39,960,000 | 19 | H/Mji Mbinga | 49,460,080 |
| 9 | H/W Misungwi | 10,850,000 | 20 | H/W Namtumbo | 38,914,300 |
| 10 | H/W Buchosa | 40,533,287 | 21 | H/W Mbinga | 1,068,750,000 |
| 11 | H/W Missenyi | 2,900,000 | | **Jumla** | **2,384,412,108** |

**Jedwali Na.9-16: Mwenendo wa manunuzi nje ya mpango kwa miaka mitatu**

| Mwaka | Kiasi (Sh.Tz) | Idadi ya Serikali za mitaa |
|---|---|---|
| 2016/17 | 2,384,412,108 | 21 |
| 2015/16 | 1,720,839,381 | 20 |
| 2014/15 | 8,133,314,354 | 5 |

Jedwali Na.9-16 hapo juu nahitimisha kwamba, kiasi cha manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa mwaka wa manunuzi kimepungua kwa Sh.Tz 6,412,474,973 kutoka Sh.Tz 8,133,314,354 kwa mwaka 2014/2015 hadi SH.TZ 1,720,839,381 kwa mwaka 2015/2016 sawa na asilimia 79. Na kuongezekaa kwa SH.TZ 663,572,727 kutoka SH.TZ 1,720,839,381 kwa mwaka 2015/2016 hadi Sh.Tz 2,384,412,108 kwa mwaka 2016/2017 sawa na asilimia 29.

Kitendo cha kufanyika kwa manunuzi yasiyokuwa katika mpango na bila ushindani kinapelekea kuwa na manunuzi yasiokuwa na tija.

Ili Serikali iweze kufikia malengo yake ya manunuzi, napendekeza kwa mamlaka husika kuepuka kufanya manunuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka na kuzingatia Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

### 9.6.8 Bidhaa na huduma zilizolipiwa lakini hazikupokelewa SH.TZ 251,171,899

Agizo Na. 70 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inasema kwamba, itakuwa ni wajibu wa kila Mkuu wa Idara kuhakikisha kwamba mali zote, vifaa na huduma zilizopokelewa zinakaguliwa kwa kulinganishwa na oda, bei, idadi na ubora. Kinyume na Agizo lililonukuliwa, bidhaa zenye thamani ya Sh. 251,171,899 ziliagizwa na kulipiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 5 bila kupokelewa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-17 hapa chini.

**Jedwali Na.9-17: Halmashauri zilizolipia bidhaa ambazo hazijapokelewa**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Liwale | 6,834,400 | 4 | H/W Siha | 10,771,200 |
| 2 | H/W Missenyi | 44,883,100 | 5 | H/W Mbinga | 125,811,560 |
| 3 | H/M Moshi | 62,871,639 | **Jumla** | | **251,171,899** |

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa bidhaa zote zilizonunuliwa zinapokelewa na kutumika kama ilivyopangwa kwa ustawi wa umma.

### 9.6.9 Matengenezo ya Magari yaliyofanyika katika karakana binafsi pasipo kibali cha TEMESA Sh.Tz 234,011,198

Kanuni namba 137 (1) (a), (2) na (3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa 2016 inaelekeza kwamba, TEMESA ifanye ukaguzi wa magari kabla na baada ya huduma kutolewa na kutoa cheti cha uthibitisho. Pale ambapo Mamlaka itashindwa kufanya matengenezo na ukarabati kutokana na kutokuwepo kwa vipuri, ujuzi au rasilimali zinginezo, inaweza kupata huduma hiyo kupitia kwa watoa huduma wengine wenye tuzo za mkataba kwa kushauriana na taasisi inayofanya manunuzi. Kinyume na kanuni iliyonukuliwa hapo juu, katika kipindi cha ukaguzi imebainika kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 zililipa jumla ya Sh. 234,011,198 kwa karakana/gereji binafsi kwa ajili ya

ukarabati na matengenezo ya magari bila ya idhini ya TEMESA (Karakana ya Serikali).

Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanya matengenezo ya magari bila idhini ya TEMESA ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-18 hapo chini.

**Jedwali Na.9-18: Matengenezo ya magari bila idhini ya TEMESA**

| Na. | Jina la Halamshauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Singida | 12,897,400 | 11 | H/W Missenyi | 24,500,002 |
| 2 | H/W Itigi | 15,996,540 | 12 | H/W Ushetu | 10,158,445 |
| 3 | H/M Kigamboni | 62,751,969 | 13 | H/W Same | 5,047,034 |
| 4 | H/W Kisarawe | 14,105,000 | 14 | H/W Bumbuli | 2,683,798 |
| 5 | H/M Lindi | 2,525,528 | 15 | H/Mji Korogwe | 3,133,326 |
| 6 | H/W Bariadi | 13,894,000 | 16 | H/W Lushoto | 920,000 |
| 7 | H/W Bunda | 23,291,878 | 17 | H/W Muheza | 4,540,020 |
| 8 | H/W Kwimba | 10,391,000 | 18 | H/W Pangani | 4,960,000 |
| 9 | H/W Buchosa | 7,178,353 | **Jumla** | | **234,011,198** |
| 10 | H/W Sengerema | 15,036,905 | | | |

Kutokana na kutozingatiwa kwa kanuni ya manunuzi ya umma, inaleta ugumu kuthibitisha iwapo matengenezo na ukarabati wa magari ya serikali umefanywa kwa kuzingatia viwango vinavyohitajika.

Napendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia Kanuni ya 137 na 166 ya kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kuhakikisha kuwa matengenezo na ukarabati yanafanywa na TEMESA. Endapo kutakuwa na uhitaji wa kufanywa na karakana binafsi basi ukarabati na matengenezo hayo yafanyike baada ya kupata kibali kutoka TEMESA.

### 9.6.10 Manunzi ya bidhaa yasiyodhibitishwa Sh. 377,261,492

Ukaguzi nilioufanya kwenye usimamizi wa manunuzi ya bidhaa umebaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. 377,261,492 kwa mwaka 2016/2017 ambazo

hazikurekodiwa kwenye kumbukumbu ya Leja ya Vifaa kinyume na Agizo Na. 54(3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

Hali hii inamzuia mkaguzi kuhakikisha ya kuwa vitu vilivyonunuliwa vilipokelewa na kutumika kama ilivyostahili.

Jedwali Na. 9-19: hapa chini inaonesha orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa amabazo hazikuingiza kwenye leja vifaa vilivyonunuliwa:

**Jedwal Na. 9-19: Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa amabazo hazikuingiza bidhaa kwenye leja**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Urambo | 7,805,260 | 13 | H/W Buchosa | 32,550,718 |
| 2 | H/M Kigamboni | 12,823,830 | 14 | H/Mji Kahama | 17,530,000 |
| 3 | H/W Chalinze | 3,861,900 | 15 | H/W Ngorongoro | 6,435,000 |
| 4 | H/M Morogoro | 21,028,156 | 16 | H/W Bumbuli | 5,509,000 |
| 5 | H/W Kilosa | 20,412,546 | 17 | H/W Lushoto | 5,393,000 |
| 6 | H/W Kilombero | 1,880,000 | 18 | H/W Kilolo | 10,816,574 |
| 7 | H/Mji Ifakara | 2,199,750 | 19 | H/W Mufindi | 10,405,900 |
| 8 | H/W Gairo | 6,042,040 | 20 | H/M Songea | 30,137,300 |
| 9 | H/W Geita | 28,506,855 | 21 | H/W Madaba | 4,659,900 |
| 10 | H/W Chato | 17,761,000 | 22 | H/W Namtumbo | 3,504,000 |
| 11 | H/M Ilemela | 100,136,305 | 23 | H/W Nkasi | 20,758,608 |
| 12 | H/W Misungwi | 7,103,850 | **Jumla** | | **377,261,492** |

Nina shaka huenda vifaa vilivyonunuliwa vilitumiwa kwa matumizi yasiyokusudiwa bila uongozi kugundua na hivyo kupelekea upotevu wa mali za umma.

Nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha kwamba vifaa vyote vilivyonunuliwa vinapokelewa na kuingizwa katika leja kama ushahidi wa matumizi ya fedha za umma

### 9.6.11 Zabuni iliyopitishwa bila kuwa na kibali cha ulipwaji kodi 5,894,349,609

Kanuni Na. 116 (1)(d) ya ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwa madhumuni ya kustahili kushiriki

shughuli za manunuzi, mzabuni atimize majukumu yake ya kulipa kodi, mchango kwa jamii na kuendelea kufuata matwaka ya mwajiri, kulinda mazingira, afya na usalama kwa matakwa ya nchi. Sehemu ya pili ya jedwali Na. 18 la Sheria ya Manunuzi inatoa maelezo ya umuhimu ya kumthaminisha mzabuni au mjenzi ambaye aliweka hati ya kodi au hati ya msamaha wa kodi.

Kinyume na hayo Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti na H/Manispaa ya Kinondoni zilitunuku wazabuni bila kuweka hati sahihi ya kodi kutoka mamlaka ya kodi kuonesha kuwa wazabuni wamelipa kodi zote zinazohusiana na biashara wanazofanya.

Ni maoni yangu kuwa kuwatunuku wazabuni zabuni bila kuhakisha wamelipa kodi zote inasababisha ukwepaji wa kodi na kupoteza mapato ya serikali. Napendekeza menejimenti za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa wazabuni hawatunikiwi zabuni bila kuwasilisha ushahidi wa hati za ulipaji kodi.

## 9.7 UKAGUZI WA KINA WA USIMAMIZI WA MIKATABA

Ukaguzi wa kina wa usimamizi wa mikataba ulifanyika katika mikoa 11. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama kuna thamani ya fedha katika mikataba iliyotekelezwa katika Halmashauri na kuona kama usimamizi wa mikataba ulifanywa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Nimekagua masuala ya utendaji na usimamizi wa mikataba katika Halmashauri 18 (mikoa 11) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama inavyoonekana katika jedwali Na.9-20 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-20: Maeneo yaliyokaguliwa**

| Na. | Mkoa | Halmashauri | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ARUSHA | H/W KARATU | H/W LONGIDO | H/W MONDULI |
| 2. | KAGERA | H/W BIHARAMULO | H/W KARAGWE | H/W MULEBA |
| 3. | KILIMANJARO | H/W HAI | H/W ROMBO | H/W SAME |

| Na. | Mkoa | Halmashauri | |
|---|---|---|---|
| 4. | MBEYA | H/W KYELA | H/W MBEYA |
| 5. | DODOMA | H/W MPWAPWA | |
| 6. | MOROGORO | H/W MALINYI | |
| 7. | MTWARA | H/M MTWARA-MIKINDANI | |
| 8. | MWANZA | H/W BUCHOSA | |
| 9. | NJOMBE | H/MJI NJOMBE | |
| 10. | SINGIDA | H/W MKALAMA | |
| 11. | TANGA | H/W HANDENI | |

Ukaguzi huu ulifanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, Kifungu cha 10 pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIS).

Aidha, ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi Na.11 ya mwaka 2008, ambacho kinanipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi (Thamani ya Fedha) kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija, na ufanisi wa matumizi ya rasilimali katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo. Ukaguzi huu ulihusisha maulizo, uchunguzi, na kutoa taarifa.

Katika sura hii, nimeonesha ukiukwaji wa taratibu za usimamizi wa mikataba uliojitokeza katika Halmashauri 18 na kuhitimisha kwa kutoa mapendekezo kwa Halmashauri zote 18. Ukaguzi uliangalia:

(a) Sababu ya uhitaji wa mradi
(b) Taratibu za zabuni,
(c) Ufanyaji wa tathmini na utoaji wa mikataba, na
(d) Usimamizi wa utekelezaji wa mikataba.

Aidha, mawanda ya ukaguzi yalihusisha ukaguzi wa kandarasi 37 zenye thamani kubwa ambapo mikataba 36 ilikuwa ya ujenzi, na mkataba mmoja ulikuwa wa kuendeleza maeneo ya mijini katika

mji wa Songwe. Sampuli iliyochaguliwa ilikuwa ya mikataba iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 na miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa tangu mwaka wa fedha 2013/2014 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-21** hapo chini.

**Jedwali Na. 9-21: Mawanda ya Ukaguzi wa mikataba**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mikataba |
|---|---|
| | |
| 2013/14 | 3 |
| 2014/15 | 2 |
| 2015/16 | 8 |
| 2016/17 | 24 |
| **Jumla** | **37** |

Nimebaini mapungufu ya kimfumo kwenye kaguzi zote 18 zilizofanyika ambayo yanahitaji kushughulikiwa kikamilifu na Serikali.

Mapungufu yaliyotokana na ukaguzi wa kina wa usimamizi wa mikataba (sehemu ya utendaji) yaliyotolewa katika sura hii yanahusiana na halmashauri 16 za wilaya, halmashauri moja ya mji na halmashauri moja ya manispaa kama inavyoelezwa hapa chini.

### 9.7.1 Kutofanyika kwa tathmini ya athari za kimazingira katika miradi 6 yenye thamani ya Sh. 946,766,050

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwamba, "taasisi inayofanya manunuzi inatakiwa kutathmini athari za kimazingira zinazoweza kusababishwa na mradi katika hatua za awali za maandalizi ya mradi husika na kabla ya kuanza manunuzi". Aidha, sehemu 81(1) ya Sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004, inahitaji tathmini ya athari za kimazingira kuwa inafanyika kama ilivyoainishwa katika jedwali la tatu la Sheria hiyo.

Nimebaini kuwa, halmashauri nne za wilaya zilitekeleza mikataba sita inayofikia jumla ya Sh. 946,766,050 bila kufanya tathmini ya

athari za kimazingira kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.9-22 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-22: Kutofanyika kwa tathmini ya athari za kimazingira katika miradi sita**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Kagera | H/W Biharamulo | LGA/032/2016-2017/HQ/WSDP/W/76 LOT3 | 336,254,200 |
| | | LGA/032/2016 - 2017/HQ/W/65 LOT1 | 157,280,000 |
| Kilimanjaro | H/W Rombo | LGA/HQ/044/CW/01/ 2016/2017 (LOT IV) | 103,614,000 |
| | | LGA/044/HQ/2016/2017/W/013 | 46,170,850 |
| | H/W Hai | LGA/047/206-17/HQ/W/08 | 192,960,800 |
| Arusha | H/W Longido | LGA/006/HQ/2015/2016/W/03 LOT No. 03 | 110,486,200 |
| **Jumla** | | | **946,766,050** |

Kwa maoni yangu, utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira unaziweka Halmashauri katika hatari ya uharibifu wa mazingira hivyo kupoteza manufaa ya mradi kwa jamii na rasilimali za Umma.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri za wilaya husika kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo tathmini ya athari za mazingira inafanywa kikamilifu kabla ya kuanza kwa miradi ili kuepuka hatari zozote zinazoweza kujitokeza.

### 9.7.2 Kutojumuishwa kwa mikataba yenye thamani ya Sh. 1,009,256,370 katika bajeti na mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa

Kanuni ya 69 (7) ya Kanuni za manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwamba, "taasisi inayofanya manunuzi inapaswa kuandaa mpango wa manunuzi kwa mahitaji ambayo yamepitishwa katika bajeti ya mwaka husika wa fedha au kama malipo yatalipwa kwa

mwaka wa fedha unaofuata, malipo ya fedha hizo yawe yametengewa bajeti.
Nimebaini kuwa, Halmashauri mbili za wilaya zilitekeleza mikataba miwili yenye thamani ya Sh. 1,009,256,370 bila kujumuishwa katika bajeti pamoja na mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa kama Jedwali Na. 9-23 linavyoonesha hapo chini.

**Jedwali Na. 9-23: Mikataba isiyojumuishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa na bajeti**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Kagera | H/W Karagwe | KGR/033/2016/2017/W/NT/07 | 184,646,400 |
| | H/W Muleba | LGA/137/2015-2016/MLB/WSDP/W/46-LOT.02 | 824,609,970 |
| **Jumla** | | | **1,009,256,370** |

Kwa maoni yangu, kutekeleza mikataba ambayo haijajumuishwa na kupitishwa katika bajeti ya Halmashauri pamoja na mpango wa manunuzi wa mwaka, kunaweza kusababisha michakato mibovu ya manunuzi na matumizi yasiyopangwa.

Napendekeza Uongozi wa Halmashauri za wilaya husika kuhakikisha katika siku zijazo manunuzi yote yanaenda sambamba na bajeti ya mwaka ya Halmashauri pamoja na mpango wa manunuzi ili kuepuka matumizi yasiyopangwa.

### 9.7.3 Zabuni zenye thamani ya Sh. 1,905,040,527 hazikuchapishwa katika tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA)

Kanuni ya 19 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kuandaa ilani/tangazo kwa zabuni za kitaifa na kimataifa na kuliwasilisha kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kwa ajili ya uchapishaji katika shajara na tovuti ya zabuni ya Mamlaka.

Nimebaini kuwa, Halmashauri tano za wilaya zilitekeleza mikataba saba yenye jumla ya Sh. 1,905,040,527 bila kuchapisha kwenye shajara na tovuti ya Mamlaka (PPRA) kama inavyotakiwa. Jedwali Na. 9-24 hapo chini linaonesha.

**Jedwali Na. 9-24: Zabuni ambazo hazikuchapishwa kwenye tovuti ya mamlaka (PPRA)**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Arusha | H/W Longido | LGA/006/HQ/2016-201701/LOT No.3 | 160,927,338 |
| | | LGA/006/HQ/2015/2016/W/03 LOT 3 | 110,486,200 |
| | H/W Karatu | LGA/002/2015/2016/W/SEDP II/03/LOT4 | 203,216,700 |
| | | LGA/002/2016/2017/W/RF/03 LOT1 | 165,932,119 |
| Kagera | H/W Biharamulo | LGA/032/2016-2017/HQ/WSDP/W/76 LOT3 | 336,254,200 |
| | H/W Muleba | LGA/137/2015-2016/MLB/WSDP/W/46-LOT 02 | 824,609,970 |
| Kilimanjaro | H/W Rombo | LGA/HQ/044/CW/01/2016/2017 LOT IV | 103,614,000 |
| **Jumla** | | | **1,905,040,527** |

Kwa maoni yangu, kwa kutochapisha zabuni katika tovuti na shajara ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Maafisa Masuuli walipunguza wigo wa ushindani.

Napendekeza kwamba, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri husika uhakikishe zabuni zote zinachapishwa katika shajara na kwenye tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kama inavyotakiwa na kanuni.

### 9.7.4 Kutothibitishwa kwa nyaraka za zabuni na Bodi ya Zabuni kabla ya kutangaza Zabuni

Kanuni ya 185(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwamba, " Nyaraka za zabuni zitathibitishwa na Bodi ya Zabuni kabla ya zabuni kutangazwa".

Nimepitia mihutasari ya Bodi ya Zabuni na kubaini kuwa, Halmashauri mbili za wilaya zilitekeleza mikataba minne yenye thamani ya Sh. 824,341,215 pasipo kupitisha nyaraka za zabuni katika Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kuthibitishwa kabla ya kutangazwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-25 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-25: Mikataba ambayo nyaraka za zabuni hazikuthibitishwa na Bodi ya Zabuni**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Tanga | H/W Handeni | LGA/131/2016-2017/W/RF/09 | 142,582,940 |
| | | LGA/131/2016-2017/W/RF/03 | 179,070,900 |
| Singida | H/W Mkalama | LGA/147/2016/2017/W/05 | 300,007,920 |
| | | LGA/147/2016/2017/W/01-LOT 02 | 202,679,455 |
| **Jumla** | | | **824,341,215** |

Kwa maoni yangu, kutangaza zabuni bila idhini ya Bodi ya Zabuni kunazinyima Halmashauri kinga muhimu katika manunuzi, udhibiti na uhakika kuwa mchakato wa manunuzi ya zabuni hizo ulifuata kanuni na sheria.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri husika kuhakikisha kuwa, kwa siku zijazo nyaraka za zabuni zinapitishwa na kuthibitishwa katika Bodi ya Zabuni kabla ya kutangazwa.

### 9.7.5 Ushindani mdogo kwa manunuzi yenye thamani ya Sh 1,193,008,208

Kanuni ya 149 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwamba, "ununuzi wa bidhaa, kazi na huduma zisizo za ushauri kupitia ushindanishaji wa zabuni kimataifa na kitaifa uliozungumziwa katika kanuni hizi, inabidi uzingatiwe kabla njia nyingine za ushindanishaji zabuni zilizozungumziwa katika kanuni

hizi hazijatumika". Aidha, jedwali la saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 linatoa mipaka kwa manunuzi ya ushindani wa dondoo kwa ajili ya kazi zenye thamani ya hadi kufikia Sh. 200,000,000 kwa mkataba.

Kwenye sampuli ya mikataba iliyokaguliwa, nilibaini mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. 1,193,008,208 katika Halmashauri mbili zilizotumia ushindani wa dondoo badala ya mbinu ya ushindani wa kitaifa kununua kazi zenye thamani inayozidi kizingiti kilichotajwa katika jedwali la saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Maelezo ni kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na. 9-26 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-26: Manunuzi yenye ushindani mdogo**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Mtwara | H/M Mtwara-Mikindani | LGA/085/2016-2017/W/06 | 236,460,200 |
| | | LGA/085/2016-2017/W/03 | 617,673,360 |
| Mwanza | H/W Buchosa | LGA/173/SF/2016/2017/W/42 | 338,874,648 |
| **Jumla** | | | **1,193,008,208** |

Kwa maoni yangu, njia ya manunuzi iliyotumika ilipunguza idadi ya Wazabuni walioshindana; hivyo Halmashauri kukosa thamani ya fedha.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri husika kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo mbinu za manunuzi za ushindani wa kitaifa na kimataifa zinapewa kipaumbele kabla mbinu nyingine za manunuzi hazijatumika.

### 9.7.6 Kutosainiwa kwa fomu za tamko la agano na wajumbe wa Kamati ya Tathmini

Sehemu ya 40(6) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 inasema kwamba, “wajumbe wote wa Kamati ya Tathmini wanatakiwa kusaini fomu za maadili zinazotolewa na kanuni

iliyoandaliwa chini ya Sheria hii, ili kuweka wazi kwamba hawana mgongano wa kimaslahi katika mahitaji ya manunuzi".

Mapitio yangu ya taarifa ya tathmini ya mikataba miwili iliyotekelezwa katika Halmashauri mbili yalibaini kuwa, Kamati za Tathmini hhazikuweka bayana maslahi yoyote kwa kusaini tamko la agano kabla ya kuanza kwa tathmini kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 9-27 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-27: Mikataba ambayo fomu za tamko la agano hazikusainiwa**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Arusha | H/W Karatu | LGA/002/2016/2017/W/RF/03 Lot I | 165,932,119 |
| | H/W Longido | LGA/006/HQ/2016-201701/LOT No.3 | 160,927,338 |
| **Jumla** | | | **326,859,457** |

Kwa maoni yangu, kutosaini fomu za tamko la agano Kamati za Tathmini zinajiweka katika hatari ya upendeleo ambayo inaweza kusababisha kutunuku zabuni kwa Mzabuni ambaye hajakidhi vigezo.
Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri husika uhakikishe wajumbe wa Kamati ya Tathmini wanaweka wazi maslahi yao kwa kusaini fomu za tamko la agano kabla ya kuanza mchakato wa tathmini.

### 9.7.7 Kuondolewa kwa Wazabuni wenye bei za chini bila sababu za msingi kulikosababisha hasara ya Sh. 124,139,940

Kanuni ya 17 (2-3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inahitaji taasisi inayofanya manunuzi kabla ya kukataa zabuni zenye bei ya chini kupita kiasi kuomba maelezo ya Wazabuni, kuthibitisha zabuni au sehemu ya zabuni isiyo ya kawaida na kuandika sababu ya kukataliwa kwa zabuni hiyo na mara moja kutoa taarifa kwa Mzabuni anayehusika.

Aidha, Kanuni ya 203 (1) na (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inahitaji zabuni zilinganishwe zenyewe kwa zenyewe ili kubaini kiwango cha chini kilichotathminiwa cha gharama za ununuzi wa bidhaa, kazi au huduma.

Mapitio ya tathmini na mchakato wa kutunuku zabuni yalibaini kuwa, katika mikataba sita iliyotekelezwa kwenye Halmashauri tano, Wazabuni walioomba zabuni kwa bei ya chini waliondolewa katika mchakato kwa sababu zisizo za msingi na kusababisha hasara ya Sh. 124,139,940. Jedwali Na. 9-28 hapo chini linatoa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 9-28: Athari za kifedha na hasara zilizotakana na kuwaondoa Wazabuni wenye bei za chini bila sababu za msingi**

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Zabuni Iliyoshinda (Sh.) | Zabuni ya Chini (Sh.) | Hasara (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| H/W Buchosa | LGA/173/SEDPII/2015/2016/W/09 | 127,362,498 | 115,266,800 | 12,095,698 |
| H/W Longido | LGA/006/HQ/2015/2016/W/03 LOT No. 03 | 110,486,200 | 92,555,440 | 17,930,760 |
| H/W Muleba | LGA/137/2015-2016/MLB/WSDP/W/46-Lot.02 | 824,609,970 | 803,275,646 | 21,334,324 |
| H/W Mkalama | LGA/147/2016/2017/W/05 | 300,007,920 | 266,173,190 | 33,834,730 |
| | LGA/147/2016/2017/W/01, LOT 02 | 202,679,455 | 193,106,357 | 9,573,098 |
| H/W Handeni | LGA/131/2016/2017/W/RF/01/LOT3 | 179,070,900 | 149,699,570 | 29,371,330 |
| **JUMLA** | | | | **124,139,940** |

Kwa maoni yangu, kuwaondoa Wazabuni wenye bei ya chini bila sababu za msingi kulipelekea hasara ya Sh. 124,139,940. Aidha, kulisababisha kuwepo kwa ushindani usiozingatia usawa.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri husika kufuata Kanuni ya 17 na 203 ya Kanuni za manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ili kuongeza uwazi katika ulinganishaji wa Wazabuni. Aidha, Maafisa Masuuli na Bodi za Zabuni wawajibishwe kwa kusababisha hasara ya Sh. 124,139,940.

### 9.7.8 Afisa Masuuli kushindwa kuwapa taarifa Wazabuni walioshindwa zabuni

Kanuni ya 231(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwamba, "Baada ya kupokea taarifa ya uamuzi wa tuzo kutoka Bodi ya Zabuni, Afisa Masuuli anatakiwa, baada ya kuwa amejiridhisha kwamba taratibu sahihi zimefuatwa, atoe notisi ya nia ya kutangaza tuzo ya mkataba ndani ya siku tatu kwa Wazabuni wote walioshiriki katika zabuni husika na kuwapa siku kumi na nne ambazo watatakiwa kuwasilisha malalamiko, kama yapo".

Nimebaini mikataba mitano katika Halmashauri tatu ambapo Maafisa Masuuli hawakutoa notisi za nia ya kutangaza tuzo za mikataba kwa Wazabuni washiriki walioshindwa katika zabuni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.9-29 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-29: Kushindwa kuwapa taarifa Wazabuni walioshindwa tenda**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Arusha | H/W Karatu | LGA/002/2015/16/W/SEDP II/03 LOT 4 | 203,216,700 |
| Mbeya | H/W Kyela | LGA/074/2013/2014/RWSSP/01 Lot 1 | 1,140,256,700 |
| | | LGA/074/2013/2014/RWSSP/01 Lot 2 | 562,260,875 |
| | H/W Mbeya | LGA/078/2016/2017/W/IRR/01 | 239,557,806 |
| | | LGA/078/2015-2016/W/04 | 613,042,214 |
| **Jumla** | | | **2,758,334,295** |

Kwa maoni yangu, kwa kutowapa taarifa Wazabuni walioshindwa zabuni Maafisa Masuuli hawakuzingatia usawa, hivyo kuwanyima

haki zao za kukata rufaa (kama wana malalamiko). Hii pia ilizuia uwazi na usawa katika tathmini na tuzo za mikataba.

Napendekeza kwamba, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri za wilaya husika utoe taarifa kwa Wazabuni wote walioshindwa kabla ya kutangaza mshindi wa tenda.

### 9.7.9 Mapungufu katika kuwapa taarifa Wazabuni walioshindwa kwa mikataba yenye thamani ya Sh. 1,428,630,370

Sehemu ya 60 (3-5) ya Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) na Kanuni ya 231 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013, inahitaji Afisa Masuuli kutoa notisi ya nia ya kumtangaza mshindi wa mkataba (ambayo itakuwa na sababu kwa nini Wazabuni wengine hawakufanikiwa kupata zabuni hizo) kwa Wazabuni wote walioshiriki katika zabuni husika ikiwapa siku saba za kazi kuwasilisha malalamiko yao, kama yapo. Vilevile, kabla ya kutoa notisi ya nia ya kumtangaza mshindi wa mkataba, kuwasilisha uamuzi wa kutunuku kwa Kamati inayohusika na fedha na mipango, kwa ajili ya uchunguzi wa kina.

Mapitio yangu ya notisi za nia ya kutangaza washindi wa zabuni yalibaini mapungufu katika mikataba minne iliyotekelezwa katika Halmashauri tatu kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 9-30 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-30: Mapungufu katika kuwapa taarifa Wazabuni walioshindwa**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|
| KAGERA | H/W BIHARAMULO | LGA/032/2016-17/HQ/W/65.LOT1 | 157,280,000 | Notisi ya nia ya kutangaza mshindi wa mkataba zimetolewa kwa Wazabuni walioshindwa kabla ya Kamati ya Fedha na Mipango kupitia maamuzi ya yaliyofanywa juu ya mshindi wa mkataba huo |
| | | LGA/032/2016-2017/HQ/WSDP/W/76 LOT3 | 336,254,200 | |

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|
| | H/W MULEBA | LGA/137/2015-2016/MLB/WSDP/W/46-Lot.02 | 824,609,970 | Wazabuni walioshindwa zabuni walipewa siku 1 ya kazi kwa ajili ya kuwasiilisha malalamiko yao badala ya siku 7. Aidha, Afisa Masuuli hakutoa sababu za Wazabuni hao kushindwa tZabuni |
| ARUSHA | H/W LONGIDO | HW/LONG/PMU/2015/ SEDP/03 | 110,486,200 | Mzabuni aliyeshindwa zabuni alipewa taarifa zisizo za kweli juu ya kukosa kwake |
| **JUMLA** | | | **1,428,630,370** | |

Kwa maoni yangu, Maafisa Masuuli hawakuzingatia usawa hivyo, kuwanyima haki ya kukata rufaa Wazabuni walioshindwa (kama wana malalamiko) na kuharibu ushindani katika mchakato wa zabuni hizo. Aidha, walizinyima haki Kamati za fedha na mipango kufanya uchunguzi wa kina na kupitisha maamuzi ya kutoa tuzo kwa Mzabuni aliyeshinda kabla ya kuwapa taarifa Wazabuni walioshindwa.

Napendekeza kwamba, katika siku zijazo Maafisa Masuuli wahakikishe notisi za nia ya kutangaza mshindi wa mkataba zinakuwa na sababu za kushindwa kwa Wazabuni wengine walioshiriki katika Zabuni hizo, na kutoa siku saba za kazi kwa Wazabuni walioshindwa kuwasilisha malalamiko yao (kama yapo). Aidha, maamuzi ya kutangaza mshindi wa zabuni kwa mkataba wowote yanatakiwa kuwasilishwa kwenye Kamati ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchunguzi kabla nia ya kumtangaza mshindi haijatolewa.

### 9.7.10 Makosa yaliyobainika katika uhakiki wa mikataba kwa Mwanasheria Mkuu yenye thamani ya Sh. 9,465,625,044

Kanuni ya 59 na 60 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) zinahitaji mkataba unaotokana na kukubalika kwa zabuni husika kuhakikiwa na

Mwanasheria Mkuu au Mwanasheria wa taasisi inayofanya manunuzi kabla mkataba haujasainiwa na pande zote. Afisa Masuuli, mara tu baada ya kupokea maoni kutoka kwa Mwanasheria Mkuu au Mwanasheria wa taasisi inayofanya manunuzi anatakiwa kuingiza marekebisho hayo katika rasimu ya mkataba.

Nimebaini matukio matatu katika Halmashauri mbili ambapo, maoni ya Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria wa taasisi hayakuingizwa katika rasimu za mikataba. Aidha, nimebaini pia matukio mawili katika Halmashauri moja ambapo mikataba ilikuwa haijahakikiwa na Mwanasheria Mkuu au Mwanasheria wa taasisi. Maelezo ni kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na. 9-31 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-31: Makosa yaliyojitokeza katika uhakiki wa mikataba**

| Halmashauri | Namba Ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Makosa Yaliyopatikana |
|---|---|---|---|
| H/W MALINYI (MKOA WA MOROGORO) | LGA/082/205/ 16/W/03 | 70,845,000 | Mikataba ilisainiwa na kutekelezwa bila kuhakikiwa na Mwanasheria wa taasisi husika |
| | LGA/082/2015 /16/W/01 | 96,076,200 | |
| H/W MBEYA (MKOA WA MBEYA) | LGA/078/2014 -2015/C/01 | 8,977,050,004 | Halmashauri hawakuzingatia ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu kwenye majadiliano ya bei, na kwa mujibu wa maoni ya Mwanasheria Mkuu, Mshauri (Consultant) hakuwa na haki kupata sehemu ya faida ya mradi. Vilevile, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishauri kuwa Mshauri |

| Halmashauri | Namba Ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Makosa Yaliyopatikana |
|---|---|---|---|
| | | | atanufaika zaidi na mkataba kuliko mwajiri (Halmashauri) hivyo mwajiri angenufaika zaidi kupitia mikopo ya benki ya biashara |
| H/W HANDENI (MKOA WA TANGA) | LGA/131/2016 - 2017/W/RF/09 | 142,582,940 | Maoni ya Mwanasheria wa Halmashauri kuhusu nguvu maalumu ya kisheria ya mkataba kutosajiliwa na kutokuwa na maazimio ya kampuni hayakuingizwa katika mikataba iliyosainiwa |
| | LGA/131/2016 - 2017/W/RF/03 | 179,070,900 | |
| **JUMLA** | | **9,465,625,044** | |

Kwa maoni yangu, utoaji zabuni kabla ya kuweka maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Wanasheria wa taasisi inaziweka Halmashauri katika hatari za kisheria na inaweza kuhatarisha thamani ya fedha za miradi. Aidha, kutohakiki mikataba kunaweza kusababisha hatari za kisheria na gharama zisizo za lazima.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri za wilaya husika uhakikishe maoni ya Mwanasheria Mkuu na Wanasheria wa taasisi yanaingizwa katika rasimu za mikataba kabla haijasainiwa ili kuepuka matatizo ya kisheria ambayo yanaweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mikataba hiyo. Aidha, Uongozi wa Halmashauri hizi unatakiwa kuhakikisha kwamba mikataba inahakikiwa kabla ya kusainiwa.

### 9.7.11 Kulipwa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa miradi iliyosamehewa Sh. Tz 171,801,364

Aya ya 9.2.2 ya Mkataba wa makubaliano (MoU) kwa ajili ya uanzishaji wa Mfuko wa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (WSDP) pamoja na marekebisho yake ya Juni, 2013 inasema kwamba, "Serikali imekubali kusamehe kodi zote zilizowekwa moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja kwenye matumizi yote yanayostahili ya bidhaa, kazi na huduma za kifedha chini ya WSDP".

Nimebaini mikataba miwili, Na. LGA/004/2016/17/RWSSP/W/14 na Na. LGA/004/2016/17/RWSSP/W/10 katika Halmashauri ya Wilaya Monduli Mkoani Arusha, ambapo kiasi cha VAT Sh. 87,765,679 kililipwa kwa ajili ya miradi ya maji iliyosamehewa kodi. Nimebaini pia mikataba miwili katika Halmashauri za Wilaya Karagwe na Biharamulo yenye namba LGA/033/W/2016/17/W/NT/07 na LGA/032/2016-2017/HQ/WSDP/W/76 LOT 03 ambapo kodi ya ongezeko la thamani (VAT) yenye thamani ya Sh. 84,035,685 ilijumuishwa katika gharama ya miradi ya maji iliyosamehewa kodi.

Kwa maoni yangu, malipo ya VAT kwa miradi iliyosamehewa kodi yanapunguza uwezo wa Halmashauri kugharamia miradi mingine. Aidha, kutofuata MoU kunakatisha tamaa nia za wafadhili kuendelea kutoa ruzuku katika miradi mingine.

Napendekeza kwamba, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri ufuate mkataba wa makubaliano uliosainiwa. Aidha, Afisa Masuuli achukuliwe hatua kwa ulipaji wa VAT katika miradi iliyosamehewa kodi.

### 9.7.12 Mikataba yenye thamani ya Sh. 5,425,064,337 imetekelezwa bila kukatiwa bima

Kifungu cha 7 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) na kifungu cha 14.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) vinahitaji Wakandarasi kukatia bima kutoka tarehe ya kuanza hadi mwisho wa kipindi cha matazamio ya mkataba kwa ajili ya hatari mbalimbali.

Nimebaini katika mikataba Na. LGA/074/2013/2014/RWSSP/01 LOT 1 wenye thamani ya Sh. 1,140,256,700 wa Halmashauri ya Wilaya Kyela na Na. LGA/134/ULGSP/BT/2015/2016/03 wenye thamani ya Sh. 4,284,807,637 wa Halmashauri ya Mji Njombe kuwa imetekelezwa bila kuwa na bima.

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa bima kunaziweka Halmashauri katika hatari ya ucheleweshaji wa ukamilishaji wa mikataba kama matukio yanayokingika yakitokea.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri hizi kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo miradi yote inakatiwa bima kupunguza hatari ya kutokea kwa hasara.

### 9.7.13 Mikataba yenye thamani ya kiasi cha Sh.Tz 5,763,938,985 imetekelezwa bila kuwepo kwa hati za dhamana ya utendaji

Kanuni ya 29 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, inazitaka taasisi zote zinazofanya manunuzi kupewa dhamana ya utekelezaji wa kazi/mkataba kutoka kwa Wazabuni walioshinda zabuni ili kuhakikisha utekelezaji wa mikataba unafanyika kwa uaminifu na malipo yanafanyika kwa wafanyakazi wote, wasambazaji, mafundi na Wakandarasi wasaidizi wa mradi, kama wapo.

Nimebaini matukio matatu katika Halmashauri tatu ambapo mikataba yenye thamani ya Sh. 5,763,938,985 ilitekelezwa bila hati za dhamana. Maelezo ya mikataba hiyo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali Na. 9-32 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-32: Mikataba iliyotekelezwa bila kuwa na hati za dhamana ya utendaji**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Mbeya | H/W Kyela | LGA/074/2013/2014/RWSSP/01 Lot 01 | 1,140,256,700 |
| Mwanza | H/W Buchoosa | LGA/173/SF/2016/2017/W/42 | 338,874,648 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Njombe | H/MJI Njombe | LGA/134/ULGSP/BT/2015/2016/03 | 4,284,807,637 |
| **JUMLA** | | | **5,763,938,985** |

Aidha, ukaguzi wangu umebaini mapungufu katika hati za dhamana zilizowasilishwa na Wakandarasi katika Halmshauri nne zilizotekeleza mikataba minne yenye thamani ya Sh. 1,863,827,124. Maelezo ya mikataba hiyo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali Na.9-33 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-33: Mapungufu katika hati za dhamana zilizowasilishwa**

| Mkoa | Halmashauri | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|
| NJOMBE | H/MJI NJOMBE | LGA/134/ULGSP/BT/2013/2014/02 | 790,000,000 | Hati ya dhamana ya utendaji imeisha muda wake kabla ya kukamilika kwa mkataba |
| KILIMANJARO | H/W SAME | LGA/049/W/2016/2017/04 | 95,660,240 | Hati ya dhamana ya utendaji imeisha muda wake kabla ya kukamilika kwa mkataba |
| DODOMA | H/W MPWAPWA | LGA/023/2016/2017/W/01 | 641,912,684 | Kuwasilisha bima badala ya dhamana ya benki |
| KAGERA | H/W BIHARAMULO | LGA/032/2016-2017/HQ/WSDP/W/76 Lot 03 | 336,254,200 | Hati ya dhamana ya utendaji inalinda miezi 12 tu badala ya 18 |
| **Jumla** | | | **1,863,827,124** | |

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa hati za dhamana za utendaji kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kupoteza rasilimali zake

kwa miradi inayoendelea, endapo Wakandarasi watashindwa kutekeleza mikataba waliyoingia na Halmashauri au endapo watasitisha mikataba hiyo.

Napendekeza kwamba, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri hizi uhakikishe mikataba yote inalindwa kwa hati za dhamana ya utendaji kama inavyoelekezwa katika Kanuni za manunuzi ya Umma, ili kulinda maslahi ya Halmashauri na mafanikio ya utekelezaji wa miradi.

### 9.7.14 Kutotozwa kwa fidia za ucheleweshaji mradi kiasi cha Sh.Tz 119,221,004

Kanuni ya 112(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, inahitaji taasisi inayofanya manunuzi kudai fidia kwa Mzabuni kwa, kuacha kupeleka vifaa, kuacha kutoa bidhaa, au kuacha kutoa huduma au kuchelewa kufanya kazi. Aidha, kifungu cha 23 cha SCC kinataka fidia ya 0.1% ya jumla ya mkataba kutozwa kwa siku kwa kazi iliyocholeweshwa.

Nimebaini katika mikataba miwili yenye Na. LGA/023/2016/2017/W/01 na LGA/023/2016/2017/W/12 katika Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa Mkoani Dodoma, Wakandarasi walichelewa kutekeleza mikataba na Halmashauri haikuwatoza gharama za upotevu wa muda na uharibifu wa rasilimali (liquidated damages) kiasi cha Sh. 119,221,004.
Kwa maoni yangu, kwa kuwa Wakandarasi walichelewa kukamilisha kazi, fidia sawa na Sh. 119,221,004 ilitakiwa kutozwa kutoka kwa Wakandarasi hao.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa, kutoza Sh. 119,221,004 ikiwa ni fidia kutoka kwa Wakandarasi kwa kutokamilisha kazi kwa wakati.

### 9.7.15 Usimamizi duni katika utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. 363,426,440

Kanuni 252 (2) ya Kanuni za manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, inamtaka Msimamizi wa mradi aliyeteuliwa na Afisa Masuuli kusimamia kazi za Kamati ya uchunguzi, kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kila mwezi au ndani ya kipindi kilichowekwa na Afisa Masuuli.

Mapitio yangu ya miradi iliyotekelezwa, yalibaini mikataba mitatu katika Halmashauri tatu ambapo Wasimamizi wa miradi walishindwa kusimamia na kufuatilia miradi ipasavyo na kusababisha kuchelewa kukamilika kwa kazi kama inavyooneshwa katika jedwali Na.9-34 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-34: Usimamizi duni katika utekelezaji wa miradi**

| Mkoa | Halmashauri | Namba Ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Mapungufu Yaliyobainika |
|---|---|---|---|---|
| Kagera | H/W Biharamulo | LGA/032/2016-17/HQ/W/65.LOT1 | 157,280,000 | Msimamizi wa mradi hakuandaa taarifa za maendeleo ya mradi kwa miezi miwili (2) na mradi ulikuwa nyuma ya ratiba |
| Kilimanjaro | H/W Same | LGA/049/W/2016/2017/04 | 95,660,240 | Msimamizi wa mradi hakuandaa taarifa za maendeleo ya mradi kwa miezi minne (4) na mradi ulikuwa nyuma ya ratiba |
| Arusha | H/W Longido | LGA/006/HQ/2015/16/W/03 Lot 3 | 110,486,200 | Mkandarasi hakufanya kazi ya kiasi cha Sh. 53,179,200 na kuitelekeza kazi mnamo tarehe 29/11/2016. |

| Mkoa | Halmashauri | Namba Ya Mkataba | Kiasi (Sh.) | Mapungufu Yaliyobainika |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Malipo ya awali (Advance payment) ya Sh. 5,111,530 hayakurejeshwa. |
| Jumla | | | 363,426,440 | |

Kwa maoni yangu, usimamizi duni katika utekelezaji wa mikataba hiyo, ulisababisha kutomalizika kwa kazi/mikataba. Aidha, kuna hatari ya kuwa na kazi zisizo na ubora kwa kuwa miradi hiyo ilitekelezwa bila usimamizi wa kutosha.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri za Wilaya hizi kuhakikisha Wasimamizi wa miradi wanatekeleza jukumu la usimamizi kama inavyotakiwa. Aidha, Halmashauri hizi zihakikishe kuwa kazi iliyobaki inakamilika ili kupata manufaa yaliyokusudiwa.

### 9.7.16 Kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. Tz 1,656,397,844

Kimsingi, miradi inatakiwa kuanza na kumalizika ndani ya kipindi ambacho kimetajwa katika mikataba iliyosainiwa. Kinyume na hitaji hili, kulikuwa na ucheleweshaji katika utekelezaji na ukamilishaji wa miradi mitatu yenye thamani ya Sh. 1,044,485,160 katika Halmashauri tatu za Wilaya kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9-35 hapo chini.

**Jedwali Na. 9-35: Kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi**

| HALMASHAURI | NAMBA YA MKATABA | KIASI (Sh.) | MUDA WA MKATABA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| H/W BIHARAMULO | LGA/032/2016-2017/HQ/WSDP/W/76 Lot 3 | 336,254,200 | 28/06/2017 hadi 28/12/2017 | Hadi kufikia tarehe 21/08/2017 ukusanyaji wa vifaa na makabidhiano ya mradi vilikuwa havijafanyika |
| H/W KARAGWE | KGR/HWK/033/2016/2017/W/NT/01 | 678,230,960 | 02/03/2017 hadi 01/08/2017 | Hadi kufikia tarehe 29/08/2017 mkataba ulikuwa bado haujakamlika kutokana na kutohamishwa kwa nguzo za umeme zilizotakiwa kuhamishwa kupisha mradi |
| H/W MPWAPWA | LGA/023/2016/2017/W/01 | 641,912,684 | 13/10/2016 hadi 14/10/2017 | Hadi kufikia tarehe 26/01/2018 mkataba ulikuwa haujakamilika |
| **Jumla** | | **1,656,397,844** | | |

Kwa maoni yangu, kuchelewa kwa utekelezaji na ukamilikaji wa miradi hii kunainyima jamii husika faida zilizokusudiwa kwa wakati. Hii inaweza pia kusababisha hatari kwa Halmashauri kuingia gharama za ziada.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri husika ufanye uangalizi wa kutosha kuhakikisha miradi inaanza na kukamilika kwa wakati uliopangwa.

### 9.7.17 Ucheleweshwaji wa malipo kwa kazi iliyofanyika yenye thamani ya Sh.Tz 748,077,772

Vifungu vya mikataba vinahitaji Wakandarasi kuwasilisha makadirio ya thamani ya kazi iliyofanywa kwa kila mwezi, ambayo yatapitiwa na kuthibitishwa na Msimamizi wa mradi ndani ya siku 28. Kushindwa kufanya hivyo, Mkandarasi atatozwa riba kwa kiasi kisicholipwa kwa kutumia kiwango cha riba ya kukopa kibiashara kilichopo kwa wakati huo.

Mapitio yangu ya mkataba Na. LGA/137/2015-2016/MLB/WSDP/W/46-LOT.02 wa Halmashauri ya Wilaya Muleba yalibaini kuwa, Mkandarasi aliwasilisha madai kwa kazi iliyokamilika yenye thamani ya Sh. 558,157,272 mnamo tarehe 20/06/2017. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 13/11/2017 (miezi tano) malipo yalikuwa hayajafanyika. Aidha, mkataba Na. LGA/074/2013/2014/RWSSP/01 LOT 3 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela malipo yenye thamani ya Sh.189,920,500 yalicheleweshwa kwa siku 76.

Kwa maoni yangu, kuchelewa kwa malipo kunaweza kuchelewesha kukamilika kwa miradi hiyo na kuongeza gharama.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri husika kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo malipo yanafanyika kwa wakati kwa kazi zote zilizokamilika ili kulinda maslahi ya pande zote.

**9.7.18 Upungufu wa wafanyakazi katika Kitengo cha Manunuzi na Idara ya Kazi ambao unaathiri utendaji katika kusimamia miradi**

Nimepitia kiwango halisi cha nguvukazi katika Idara ya Kazi na Kitengo cha Manunuzi kulingana na kiwango cha watumishi kilichopangwa na kubaini kuwa, Idara ya Kazi katika Halmashauri ya Wilaya Same hakuna wapimaji na wabunifu wa michoro. Kwa upande mwingine, katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi hajathibitishwa (anaongoza kitengo hicho kwa kukaimu zaidi ya mwaka mmoja bila kuwa barua ya kukaimu toka katika Uongozi wa Halmashauri).

Kwa maoni yangu, upungufu wa wafanyakazi muhimu unazisababishia Idara ya Kazi na Kitengo cha Manunuzi hatari ya kutotekeleza majukumu yao kwa tija na hivyo kupelekea kazi kuwa za kiwango cha chini, na pia kuchelewa kwa ukamilishwaji wa miradi.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuwasiliana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kupata kibali cha ajira kitakachowezesha kujaza nafasi zilizo wazi na kuongeza tija na ufanisi.

### 9.7.19 Kumtangaza mshindi wa zabuni kabla ya idhini ya Kamati ya Fedha na Mipango Sh. 203,216,700

Sehemu ya 60 (4) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 inamtaka Afisa Masuuli wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa, kuwasilisha uamuzi wa mshindi wa zabuni katika Kamati yenye dhamana ya fedha na mipango, kwa ajili ya uchunguzi kabla ya kutoa notisi ya nia ya kutangaza mshindi wa mkataba.

Mapitio yangu katika jalada la mkataba No. LGA/002/2015-16/W/SEDP II/03/LOT4 yamebainisha kuwa, tarehe 23/06/2016 Afisa Masuuli wa Halmashauri ya Wilaya yA Karatu alitangaza mshindi wa mkataba kabla ya uchunguzi wa Kamati ya Fedha na Mipango ambayo ilikutana tarehe 14/07/2016.

Kwa maoni yangu, Afisa Masuuli aliinyima Kamati ya Fedha na Mipango haki ya kutekeleza wajibu wake wa usimamizi. Hii ingeweza kuiweka Halmashauri katika hatari ya kumpa mkataba Mzabuni asiyekidhi vigezo.

Napendekeza kwamba, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri hii uhakikishe Afisa Masuuli anawasilisha maamuzi ya mshindi wa mkataba kwa Kamati ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchunguzi kabla ya kutoa nia ya kumtunuku Mzabuni huyo mkataba.

### 9.7.20 Tofauti kati ya idadi ya zabuni zilizofunguliwa na zilizofanyiwa tathmini

Kanuni ya 202 (3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, inaitaka Kamati ya Tathmini kutathmini zabuni zilizofunguliwa kipindi cha ufunguzi wa zabuni.

Mapitio yangu ya taarifa ya tathmini yenye zabuni Na. LGA/002/2015/2016/W/SEDP II/03 LOT 4 kwa Halmashauri ya Wilaya Karatu yamebaini kuwa, idadi ya zabuni zilizowasilishwa na kufunguliwa kama muhtasari wa ufunguzi wa zabuni unavyoonesha ni tano. Hata hivyo, taarifa ya tathmini ilionesha kuwa zabuni sita zilifanyiwa tathmini.

Kwa maoni yangu, kufanyia tathmini zabuni isiyofunguliwa katika hatua ya ufunguzi wa zabuni ni kuharibu mchakato wa tathmini.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri uhakikishe kwamba zabuni zinazofanyiwa tathmini ni zile tu zilizofunguliwa wakati wa ufunguzi wa zabuni.

### 9.7.21 Kuingia mkataba bila Mwanasheria kushuhudia

Sehemu ya 60(a) ya Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) inasema kwamba "ushuhuda wa kusaini mikataba utafanywa kwa mujibu wa sheria au chombo kingine chochote cha kisheria ambacho kinaanzisha taasisi husika ya manunuzi."

Mapitio yangu ya mkataba Na. LGA/006/HQ/2015/2016/W/03 LOT 3 na LGA/006/HQ/2016-2017/01/LOT 3 katika Halmashauri ya Wilaya Longido yalibaini kuwa, mikataba ilisainiwa bila kushuhudiwa na Mwanasheria. Vilevile, tarehe za kusaini mikataba hazikuainishwa.

Kwa maoni yangu, mikataba iliyosainiwa bila ushahidi wa Mwanasheria haitambuliki kisheria na inaiweka pia Halmashauri katika changamoto kubwa endapo migogoro itatokea.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo, Uongozi wa Halmashauri uhakikishe, mikataba yote inasainiwa kwa kushuhudiwa na Mwanasheria.

### 9.7.22 Usimamizi mbaya wa mkataba uliovunjwa na kusababisha hasara ya Sh. 72,025,634

Nimepitia majalada ya mikataba na kubaini kuwa, tarehe 13/11/2016 Halmashauri ya Wilaya Monduli ilisitisha mkataba wenye namba LGA/004/2016/2017/02 bila kudai Sh. 59,693,990 (10% ya kazi isiyokamilika) kinyume na kifungu cha 61.1 cha GCC na 28.1 cha SCC.

Baada ya hapo, Halmashauri waliingia mkataba mpya wenye thamani ya Sh. 609,271,552 ambao ulisababisha gharama ya ziada ya Sh. 12,331,644 kutoka mkataba ulioingiwa hapo awali. Hivyo kufanya hasara ya jumla ya Sh. 72,025,634.

Kwa maoni yangu, Halmashauri imepata hasara ya Sh. 72,025,634 kwa kutolipwa 10% (Sh. 59,693,990) ya thamani ya kazi isiyokamilika wakati wa kuvunja mkataba wa awali na gharama ya ziada ya Sh. 12,331,644 kwa kuingia mkataba mpya.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri uhakikishe unazingatia vifungu vya mikataba. Aidha, Afisa Masuuli na Msimamizi wa Mradi wachukuliwe hatua kwa hasara waliyosababisha.

### 9.7.23 Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni kukosa sifa za uongozi

Nimepitia muundo wa Bodi ya Zabuni wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba na kubaini kuwa, Afisa Masuuli alimteua Mkuu wa Idara ya Afya ambaye mara nyingi huanzisha manunuzi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri. Hii ni kinyume na Kanuni ya 7 (2) (a) ya Bodi ya Zabuni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 na Sehemu ya 31 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011.

Kwa maoni yangu, kufanya hivyo kunaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi katika mchakato wa manunuzi.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni unafuata Kanuni ya 7(2)(a) ya Bodi ya zabuni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 na Sehemu ya 31 ya Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011.

### 9.7.24 Utayarishaji duni wa BoQs kwa mradi wa umwagiliaji uliosababisha gharama ya ziada ya Sh. 26,059,103

Mapitio yangu ya mkataba Na. LGA/037/2016-2017/MLB/SSIDP/W/01 LOT1 (awamu ya pili) kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba wenye thamani ya Sh. 302,502,470 yalibaini kuwa, Mkandarasi alipaswa kujenga mfereji wenye urefu wa mita 1,573.3 uliochimbwa katika awamu ya kwanza. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa mradi huo katika awamu ya kwanza Mkandarasi alichimba mita 983.3 pekee. Matokeo yake, Halmashauri ilibadili wigo wa kazi ya awamu ya pili kuwa mita 1,360 na bei ya mkataba kuwa Sh. 328,561,674.

Nilitembelea mradi mnamo tarehe 13/11/2017, (siku tano kabla ya tarehe ya kukamilika kwake) nikagundua Mkandarasi amejenga mita 790 tu kati ya mita 1,360 alizotakiwa kujenga katika awamu ya pili ya mradi.

Kwa maoni yangu, utayarishaji duni wa BoQ ulisababisha gharama za ziada kiasi cha Sh. 26,059,100.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo BoQs zinatayarishwa kwa ufanisi ili kuepuka gharama za ziada.

### 9.7.25 Kamati ya Tathmini haikufanya tathmini ya baada ya Wazabuni kupitishwa

Mapitio yangu ya taarifa za tathmini za mikataba No.LGA/HQ/044/CW/01/2016/2017 (LOT IV) na No.LGA/044/HQ/2016/2017/W/013 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo yalibaini kuwa, Kamati ya Tathmini haikufanya uhakiki

unaotakiwa baada ya Wazabuni kupitishwa ili kutathmini ukweli wa nyaraka, uwepo wa vifaa na uzoefu wa Wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya 124 ya Kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

Kwa maoni yangu, Kamati ya Tathmini haikupaswa kupendekeza mshindi wa zabuni kabla ya kufanya uhakiki unaotakiwa baada ya Wazabuni kupitishwa ili kuepuka kuiweka Halmashauri katika hatari ya kuwa na kazi zisizo na kiwango.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo Bodi ya Zabuni inaidhinisha tu Mzabuni anayepatikana baada ya kufanyika kwa uhakiki wa baada ya Wazabuni kupitishwa.

### 9.7.26 Kupokelewa na kuwekwa kwa zabuni na Katibu wa Afisa Masuuli badala ya Katibu wa Bodi ya Zabuni

Nimebaini kuwa, zabuni za Halmashauri ya Wilaya ya Same zilikuwa zikipokelewa na kuhifadhiwa na Katibu wa Afisa Masuuli, na kuwekwa katika Ofisi ya Afisa Masuuli kinyume na Kanuni ya 195 (1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma, 2013 ambayo inahitaji Katibu wa Bodi ya Zabuni kupokea na kuweka zabuni katika kikasha cha zabuni kilichofungwa au katika Ofisi salama kwa niaba ya Bodi.

Kwa maoni yangu, upokeaji na uwekaji wa zabuni unaofanywa na Katibu wa Afisa Masuuli badala ya Katibu wa Bodi, unaweza kusababisha ubadilishwaji wa zabuni hizo, kuondoa baadhi ya zabuni, na hata kufanya marekebisho kwenye zabuni bila kugundulika na Uongozi wa Halmashauri.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri uhakikishe zabuni zinapokelewa na Katibu wa Bodi ya Zabuni na kuwekwa katika kikasha kilichofungwa au katika Ofisi yenye usalama kwa idhini ya Bodi ya Zabuni.

### 9.7.27 Kutopanga muda vizuri katika utekelezaji wa mkataba wenye thamani ya Sh.Tz 95,660,240

Kanuni ya 74(1) ya Kanuni za manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inahitaji kipindi halisi cha mkataba kifanyiwe upembuzi ili Wazabuni wapate muda wa kutosha kukamilisha utoaji wa bidhaa, kazi au huduma.

Nimepitia mkataba Na. LGA/049/W/2016/2017/04 wenye thamani ya Sh. 95,660,240 kwa ajili ya ukarabati wa barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Same na kugundua kuwa, mkataba ulipangwa kuanza tarehe 22/03/2017 na kukamilika tarehe 22/07/2017, kipindi ambacho kilikuwa ni cha mvua kwa taarifa za utabiri wa hali ya hewa. Matokeo yake Mkandarasi alisitisha mkataba kwa miezi miwili (tangu mwezi wa tatu hadi wa tano mwaka 2017).

Kwa maoni yangu, upangaji wa muda wa kutekeleza mkataba usiozingatia msimu wa mvua ulipelekea kuchelewa kwa ukamilishaji wa mradi kwa zaidi ya miezi mitano.
Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha misimu ya mvua inazingatiwa wakati wa upangaji wa tarehe za mikataba ili kuepuka kuchelewesha ukamilishaji wa kazi na huduma kwa jamii.

### 9.7.28 Kukosekana kwa muhtasari wa ufunguzi wa zabuni

Nimepitia mkataba wenye Na. LGA/078/2014/2015/C/01 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na kugundua kuwa hakukuwa na kumbukumbu za kikao cha ufunguzi wa zabuni. Mapitio zaidi ya ufunguzi wa zabuni hizo yamebaini kutokuwepo kwa kumbukumbu yoyote ya mahudhurio ya kikao cha ufunguzi wa zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya 199(1) ya Kanuni ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa muhtasari wa kikao cha ufunguzi wa zabuni kunaashiria kutokuwepo na uwazi kwa

Wazabuni. Vilevile kunaiweka Halmashauri katika hatari ya kupoteza uaminifu. Hii pia inaweza kusababisha kukosekana kwa usawa kwenye mchakato wa tathmini.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba, kwa siku zijazo kikao cha ufunguzi wa zabuni kinafanyika ipasavyo na kumbukumbu zake zinatunzwa kwa rejea zaidi.

### 9.7.29 Mkataba wenye thamani ya Sh. 338, 874,648 umetunukiwa bila tathmini ya zabuni

Mapitio ya mkataba Na. LGA/173/SZ/2016/2017/W/42 wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa na muhtasari wa Bodi ya Zabuni wa tarehe 19/04/2017 yalibaini kuwa, SUMA JKT alinukuu bei ya Sh. 298,874,648 na TBA walinukuu bei ya Sh. 348,943,152. SUMA JKT alishinda zabuni hiyo pasipo na tathmini ya zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya 211 ya Kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Aidha, niligundua kuwa tarehe 19/04/2017 Bodi ya Zabuni iliidhinisha bei ya Sh. 298,874,253 lakini mkataba ulisainiwa kwa Sh. 338, 874,648. Hii ilipelekea gharama za ziada za mradi Sh. 40,000,000.

Kwa maoni yangu, kutunuku mkataba bila tathmini ya zabuni kunazuia ushindani kwa Wazabuni; na kunaiweka Halmashauri katika hatari ya kununua huduma kwa gharama ya juu zaidi.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri ufanye tathmini kikamilifu kabla ya kutangaza mshindi wa zabuni.

### 9.7.30 Usanifu duni wa mradi uliopelekea ucheleweshaji na gharama ya ziada ya Sh. 258,294,791

Kanuni ya 321 (1) ya Kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) inamtaka Mshauri (Consultant) kufanya kazi kulingana na viwango vya taaluma vya sasa na kwa hatua stahiki ili kuepuka kufanya kosa.

Mapitio yangu katika mkataba Na. LGA/134/ULGSP/BT/2015/2016/03 wenye thamani ya Sh. 4,284,807,636.96 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi cha Njombe yalibaini kuwa, mkataba ulitakiwa kuanza tarehe 21/9/2015 na kuisha tarehe 20/8/2016. Hata hivyo, hadi tarehe 17/11/2017 mradi ulikuwa bado haujakamilika.

Zaidi ya hayo, nilibaini ucheleweshaji wa mradi ulisababishwa na usanifu duni wa Mhandisi Mshauri ambao ulileta mabadiliko mengi na kusimama kwa kazi. Hii pia ilisababisha gharama ya ziada ya Sh. 258,294,791.

Kwa maoni yangu, usanifu duni wa mradi ulipelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi na kuongezeka kwa gharama ya Sh. 258,294,791.

Napendekeza kuwa, katika siku zijazo Uongozi wa Halmashauri hii uongeze ubora katika manunuzi yake kwenye eneo la huduma za washauri ili kuepuka gharama za ziada na kuchelewa kwa utekelezaji wa mikataba.

### 9.7.31 Uzembe wa Mshauri uliopelekea kuvunja misingi ya mkataba

Sehemu ya 3 (3.2-3.4) ya hadidu za rejea kwa mkataba Na. LGA/134/ULGSP/BT/2012/2013/03 inahitaji Mshauri wa mradi kusimamia mradi na kutoa taarifa kwa Halmashauri kila wiki, kila mwezi na kila robo mwaka.

Nimepitia mkataba Na. LGA/134/ULGSP/BT/2012/2013/03 wa Halmashauri ya Mji Njombe na kubaini kuwa Mshauri hakutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba (kushindwa kuwasilisha taarifa ya kina na kuweka Mshauri Mkazi). Halmashauri ilimuonya Mshauri kupitia barua Na. NTC/TB/01/234 kuhusu utendaji wake kuwa wa kiwango cha chini. Aidha, nimebaini barua nne kutoka kwa Mkandarasi ambazo zilimtaka Mshauri kutoa maoni ya kitaalam juu ya maulizo yaliyojitokeza eneo la kazi lakini Mshauri hakujibu barua hata moja katika hizo. Hii ilisababisha Mkandarasi

kuomba siku 106 za nyongeza ili kukamilisha kazi, ambazo pia hazikupitishwa na Mshauri (Consultant).
Kwa maoni yangu, Mshauri kushindwa kuandaa taarifa ya maendeleo ya kila mwezi na kutojibu maulizo ya Mkandarasi vilisababisha mradi kuchelewa.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kufuatilia utendaji wa Mshauri dhidi ya masharti yaliyotajwa katika mkataba. Aidha, Halmashauri ya Mji Njombe ichukue hatua dhidi ya Mshauri kadri mkataba unavyotaka.

### 9.7.32 Kushindwa kuzuia Sh. 144,000,000 kutoka kwa Mkandarasi kwa kutohuisha mpango wa kazi

Ukaguzi wangu wa mkataba Na. LGA/134/ULGSP/BT/2013/2014/02 na LGA/134/ULGSP/BT/2015/2016/03 katika Halmashauri ya Mji Njombe ulibaini kuwa, Mkandarasi hakuwasilisha mpango wa kazi uliohuishwa kwa miezi 17 (Awamu 32). Halmashauri ilishindwa kuzuia kiasi cha Sh. 144,000,000 kinyume na kifungu cha 15 na 16 cha SCC ambacho kinahitaji kiasi cha Sh. 4,500,000 kuzuiwa kwa kila awamu ambayo Mkandarasi atashindwa kuhuisha mpango wa kazi.

Kwa maoni yangu, kushindwa kuzuia kiasi hicho cha fedha kunaiweka Halmashauri katika hatari ya ucheleweshaji wa huduma kwa jamii husika na pia upotevu wa fedha iwapo Mkandarasi atashindwa kutekeleza mradi ndani ya kipindi kilichopangwa.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo, kiasi cha fedha kinachotakiwa kwa kila awamu ambayo Mkandarasi atashindwa kuhuisha mpango wa kazi kinazuiwa ili kuepusha hasara kwa Halmashauri inayoweza kujitokeza.

### 9.7.33 Kutelekezwa kwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. 105,942,526.55

Kifungu cha 45.2 na 45.3 cha GCC kinasema kwamba, "Msimamizi wa mradi atakagua taarifa ya kila mwezi ya Mkandarasi na kuthibitisha malipo kwa Mkandarasi ndani ya siku ishirini na nane (28) kuanzia siku ya kupokea cheti cha malipo hayo kutoka kwa Mkandarasi, na kwamba thamani ya kazi iliyofanywa itabainishwa na Msimamizi wa mradi".

Mapitio yangu katika jalada la mawasiliano la mkataba Na. LGA/134/ULGSP/BT/2013/2014/02 katika Halmashauri ya Mji Njombe yalibaini kuwa, Mkandarasi hakufidiwa vifaa vyenye thamani ya Sh. 105,942,526.55 visivyotumika katika awamu ya kwanza ya mkataba kutokana na mabadiliko ya mawanda na matakwa yaliyotolewa na Mshauri. Vifaa hivyo vilinunuliwa kabla mawanda na matakwa ya mkataba hayajabadilika.

Kwa mtazamo wangu, mabadiliko ya mawanda na matakwa ya mkataba yamechangia kutotumika kwa vifaa hivyo vilivyotelekezwa, na pia yamepelekea kutokuelewana kati ya pande zote mbili na kuchelewa kukamilika kwa mradi.

Napendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri kuhakikisha katika siku zijazo, mabadiliko katika mawanda, matakwa na muundo wa mradi yanawasilishwa kwa Mkandarasi kwa wakati. Aidha, Halmashauri inashauriwa kutatua mgogoro baina yake na Mkandarasi na kukamilisha utekelezaji mradi bila kuchelewa zaidi.

### 9.7.34 Kufanyika kwa malipo ya Sh. 204,811,028.20 kinyume na idhini ya Mhandisi Mshauri

Kifungu cha 46.1 cha GCC kinahitaji Halmashauri kulipa kiasi kilichothibitishwa na Msimamizi wa mradi kwa kila cheti husika cha malipo.

Mapitio ya malipo ya kazi zilizotekelezwa kwa mkataba Na. LGA/134/ULGSP/BT/2013/2014/02 na LGA/134/ULGSP/BT/2015/2016/03 yamebainisha kuwa,

Halmashauri ya Mji Njombe ililipa kiasi cha Sh. 204,811,028.20 pungufu ikilinganishwa na fedha iliyoidhinishwa na Mshauri katika malipo 11 kwa awamu ya kwanza na ya pili.

Kwa maoni yangu, kukataa malipo yaliyothibitishwa na Mshauri bila kuwaarifu wahusika kumesababisha mgogoro ambao hatimaye umepekelekea kuchelewa kwa mradi.

Napendekeza katika siku zijazo, Uongozi wa Halmashauri kumpa taarifa Mshauri kuhusu mabadiliko yoyote yatokanayo na kiasi kilichoidhinishwa kwa malipo. Aidha, kukokotoa malipo yote ya awali na kulipa kiasi kilichokatwa (kama kipo) ili kuepuka kukawia zaidi kwa mradi.

## 9.8 Mapungufu yaliyojitokeza kwenye Taarifa ya Mamlaka ya Uzimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwa mwaka 2016/17

Sheria ya Manunuzi Toleo Na, 410 imetoa mamlaka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kufanya ukaguzi wa manunuzi kuanzia kwenye mchakato wa zabuni, utekelezaji wa miradi na kumalizika kwa miradi. Lengo ni kutambua kama manunuzi yanafanyika kwa mujibu wa sheria ya manunuzi.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imeandaa na kuwasilisha ripoti ya ukaguzi na tathmini katika Taasisi 112 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 35 zilizofanya manunuzi. Ripoti hiyo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma imeonesha mambo mengi ambayo pia yamebainishwa katika ripoti yangu. Natambua kazi iliyofanywa na Mamlaka hii ambayo nimeona ni muhimu taarifa yake kujumuishwa katika ripoti yangu kama inavyoonekana hapa chini:

### 9.8.1 Tathimini ya viashiria hatarishi vya rushwa.

Miradi 11 kutoka kwenye taasisi 5 zilizofanya manunuzi zina viashiria hatarishi zaidi ya asilimia 20 ya vigezo vinavyotoa vihatarishi hatari vya rushwa kwenye miradi hiyo. Maelezo ya viashiria hatarishi vya rushwa yanaoneshwa katika Jedwali 9-36 hapo chini:

## Jedwali 9-36 Taasisi za manunuzi zenye viashiria hatarishi

| Taasisi za manunuzi | Maelezo ya miradi | Kabla ya mchakato wa zabuni (% | Tathimini na kutunuku (%) | Usimamizi wa mikataba na ukaguzi (%) | Wastani (% |
|---|---|---|---|---|---|
| H/Msalala | LGA/163/2016/2017/HQ/W/RF/01/LOT 1 for rehabilitation of Kahama – Mwanese - Kabondo roads 16KM | 45 | 17 | 15 | 24 |
| H/W Kahama | LGA/155/2016/2017/W/21 for road maintenance works along Sango road and drain excavation along Bonde la Miwa (Sospeter) Road | 33 | 14 | 21 | 22.66 |
| | LGA/155/2016/2017/W/22 for road maintenance works along petro africa - CDT - Namanga Road (800 M) and drain construction (230) | 33 | 14 | 21 | 22.66 |
| | LGA/155/2016/2017/W/23 for road maintenance works along Kahama motel and Busumabu Road, Mondo Road and Seeke Road | 33 | 14 | 21 | 22.66 |
| | LGA/155/2016/2017/W/25 for road maintenance works along Kapaya - RPS Road | 33 | 14 | 21 | 22.66 |
| | LGA/155/2016/2017/W/05 for supply and installation assorted building materials for clean and waste water system at Kahama TC hospita | 33 | 14 | 21 | 22.66 |
| H/W Moshi | LGA/046/2015/2016/W/10 lot 01 for routine maintenance/spot improvement / period maintenance works along Old Moshi - Kidia, Kiboriloni - Mbokomu, Old Moshi | 33 | 6 | 21 | 20 |

| Taasisi za manunuzi | Maelezo ya miradi | Kabla ya mchakato wa zabuni (% | Tathimini na kutunuku (%) | Usimamizi wa mikataba na ukaguzi (%) | Wastani (% |
|---|---|---|---|---|---|
| | - Mdawi- Kisaseni (1km), Old Moshi - Tela, Mungureni - Tela, Kiboriloni - Kiwalaa (3km), KDC - Kiwalaa (3.8 km), Tema - Mangeni Olimo (6km), Marangu (4km) and Kidia - Kimochi (4.1km) roads<br>33 | | | | |
| | LGA/046/2016/2017/W/01 Lot 09 for routine/ periodic maintenance of Old Arusha road, KwasarakiKindi, Kibashi, Singiti- Nganjeni, Kombo- Kifunyi- Umbwe Primary School, Wereweru- Manushi- KNCU and Manushi Juu KNCU- Somsom roads | 27 | 33 | 21 | 27 |
| H/Mji Masasi | LPO No. 1824 for supply of brand new tractor, 4 disc plough and 12 tons tipping trailler | 42 | 13 | 20 | 24 |
| H/W Kibondo | LGA/041/2015/ 2016/W/56/169/01 for cons and provision of school building facilities at Itab Secondary in Kibondo DC | 8.30 | 23.81 | 36.36 | 22.73 |
| | LGA/041/2015/ 2016/W/09 for reha of 8 toilets of ward 8 District Hospital, Itoele Mabamba Health Centre, 1 toilet at Nyaruyok facility, rehabilitation of Kumuhama and Nyange dispensaries, rehabilitation of OPD at Kifura centre and rehabilitation of placenta pit a Kitahama Bitare Dispensaries at Kibondo DC | 16.67 | 33.33 | 27.27 | 25.71 |

Ni muhimu kujua kwamba viashiria hatarishi vilivyogundulika sio kithibitisho tosha cha rushwa ingawa kadri asilimia inavyoongezeka ndivyo uwezekano wa rushwa unaweza ukatokea. Katika baadhi ya matukio, kadri idadi ya viashiria hatarishi inavyongezeka haimaanishi kuwa mapungufu yanayoonekana hayatokani na uwepo wa rushwa bali ni mapungufu ya kiutendaji.

### 9.8.2 Taasisi za manunuzi zenye utendaji mbovu

Katika uchambuzi wa ripoti, Taasisi za Manunuzi 10 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 6 zina utendaji mbovu katika kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi ambapo utendaji wake upo chini kwa kiwango cha asilimia 60. Halmashauri hizo ni kama zinavyoonekana kwenye Jedwali 9-37 hapa chini.

**Jedwali 9-37: Halmashauri zenye utendaji mbovu kwa mwaka 2016/2017**

| M/za Serikali za Mitaa | Muundo wa kitaasisi | Usahihi katika uandaaji wa mpango wa mwaka wa manunuzi | Usahihiwa mchakatokato wa zabuni | Usahihi wa usimamizi wa mikataba | Usimamizi wa nyaraka za manunuzi | Utekelezaji wa mifumo ya Mamlaka ya usimamizi wa manunuzi | Utatuaji wa malalamiko | Jumla ya alama % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H/W Pangani | 6.15 | 5.80 | 13.11 | 9.10 | 6.50 | 8.00 | 0.00 | 48.66 |
| H/Mji Kahama | 7.83 | 4.15 | 10.12 | 24.50 | 5.00 | 0.00 | 0.00 | 51.60 |
| H/W Kibondo | 6.72 | 8.65 | 12.46 | 15.79 | 6.50 | 2.00 | 0.00 | 52.12 |
| H/W Kasulu | 7.54 | 8.25 | 14.13 | 20.00 | 5.50 | 0.00 | 0.00 | 55.42 |
| H/W Handeni | 5.43 | 7.10 | 11.84 | 32.10 | 1.00 | 0.00 | 0.00 | 57.47 |
| H/Mji Masasi | 6.98 | 6.70 | 16.00 | 23.80 | 5.50 | 0.00 | 0.00 | 58.98 |

Uchambuzi wa ziada unaonesha kuwa Taasisi za Manunuzi 4 kati ya 6 zenye utendaji mbovu zilishakaguliwa miaka iliyopita na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na kupewa mapendekezo ya kuzisaidia ziweze kuzingatia sheria ya manunuzi.

Hata hivyo, Taasisi hizo za Manunuzi hazikutekeleza mapendekezo kwa ufanisi hivyo Mamlaka (PPRA) hai- kuona jitihada zilizofanywa katika utendaji wake. Kumbukumbu zinaonesha kuwa taasisi nyingi za manunuzi zenye utendaji mbovu zilisharipotiwa miaka ya nyuma kama inavyoonesha kwenye jedwali 9-38.

**Jedwali 9-38: Taasisi za Manunuzi zenye mwendelezo wa utendaji mbovu**

| Taasisi za manunuzi | Asilimia za kuzingatia kanuni | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
| H/W Pangani | | | | | 50 | 48.66 |
| H/W Kibondo | 54 | | 48 | 57 | | 52.12 |
| H/W Kasulu | 59 | | 53 | | 56 | 55.42 |
| H/Mji Masasi | | 51.6 | | | | 58.98 |

### 9.8.3 Miradi ya maji iliyokaguliwa

Ripoti ya ukaguzi ya Mamalaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma imehusisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa 26 katika miradi 29 ya maji ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Halmashauri ya Wilaya Kibaha, Halimashauri ya Mji wa Kibaha, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani , Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya mji wa Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Buhingwe, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Ukaguzi unaonesha kuwa mradi mmoja au asilimia 3.4 wenye thamani ya SH.TZ 367,510,000 uliotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe hauridhishi au utendaji mbovu, inaashiria kuwa vigezo vya jumla, malengo ya mradi na thamani ya fedha haitafikiwa.

### 9.8.4 Ukaguzi wa thamani ya fedha.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha kuwa mchakato wa manunuzi na mikataba unazingatia Kifungu cha 7 cha sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016 na Kanuni za manunuzi za mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016.
Kwa mwaka 2016/2016, Mamlaka ya Usimamizi ya Manunuzi ya Umma Ilifanya ukaguzi wa mikataba na ufanisi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 35 zenye jumla ya miradi 115 au asilimia 33.3 yenye thamani ya SH.TZ 24,570,000.

Matokeo ya ufanisi wa miradi yenye thamani ya SH.TZ 1.95 bilioni yanaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za mitaa zipatazo 3 zipo chini ya kiwango kwa asilimia 50 ikimaanisha kwamba utendaji wake haurithishi. Inaonesha kuwa miradi hiyo ina utekelezaji mbovu au usioridhisha inayopelekea malengo ya miradi kutotekelezeka na kutokufikia thamani ya fedha.

Kwa kigezo hiki, hatua za haraka zinahitajika ili kushughulikia mapungufu yaliojitokeza ili hatimaye kupunguza athari zake.

**Jedwali 9-39: Miradi yenye utendaji mmbovu.**

| Na. | Miradi | Taasisi za manunuzi | Kiasi SH.TZ (Bilioni) | Matokeo ya jumla % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi Na. LGA/001/2016/2017/W/WVI /01 Nyongeza ya wodi ya mama wajawazito | H/W Meru | 0.13 | 47.4 |
| 2 | Mradi Na. LGA/001/2016/2017/W /01 ujenzi wa kitengo cha kliniki ya meno | | 0.07 | 47.4 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Mradi Na. LGA/022/2015/2016/HQ/W/10: P03/10 Matengenezo ya mara kwa mara kwa barabara za Lenjulu - Lobilo; Pandambili - Kiteto, Lenjulu - Majawanga, na Majawanga - Chiwe & ujenzi wa miundo mbinu kwa barabara mbalimbali. | H/W Kongwa | 0.15 | 49.8 |
| 4 | Miradi Na. LGA/007/2013/2014/W/01/LOT VII kwa ujenzi wa miundombinu ya maji kijiji cha Likamba | H/W Arusha | 1.60 | 46.0 |
| **Jumla** | | | **1.95** | |

### 9.8.5 Malipo yenye shaka kwa Mkandarasi Sh. 18,750,000

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Kwimba ililipa malipo yaliyotokana na mkataba Na. LGA/096/2016/2017/W/RF/07 kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara za Icheja - Mwandubi (6.4km) matengenezo ya muda maalum (5km), ujenzi wa daraja dogo na mfereji wa barabara ya mjini kupitia kwa mkandarasi Samka yenye thamani ya Sh. 216,860,000. Nilibaini kuwa mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 18,750,000 kwa kazi zisizojulikana.

**Hitimisho**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye utendaji ulio chini ya asilimia 60, zinashauriwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zao za ukaguzi. Kwa hiyo, inatarajiwa kwamba kutokana na matokeo ya kaguzi hizi, taasisi zilizokaguliwa zitachukulia kama fursa ya kuboresha utendaji wao kwa kuzingatia taratibu na kanuni kwa kiwango kinachotakiwa

.

# SURA YA KUMI

## 10.0 USIMAMIZI WA MATUMIZI YA UMMA

### (a) Maelezo ya jumla

Usimamizi wa matumizi ya umma kwa ujumla unasisitiza ufanisi kwenye maeneo matatu ambayo ni nidhamu ya fedha, ufanisi kwenye kupanga matumizi pamoja na ufanisi kwenye utendaji. Nidhamu ya fedha ni kwa serikali kufanya matumizi ambayo yako ndani ya uwezo; ufanisi wa kupanga matumizi inahusu kufanya matumizi sahihi ya fedha za serikali; na ufanisi kwenye utendaji ni utoaji wa huduma za umma kwa ubora na gharama zinazostahili.

Ili kupata matokeo hayo, serikali ilianzisha sheria mbalimbali, kanuni, sera na mifumo ya udhibiti wa ndani inayopaswa kuzingatiwa na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini.

Hata hivyo, mapitio ya jumla yanaonesha kwamba, kuna kasi ndogo ya kufikia malengo tajwa hapo juu. Kwa muda wa miaka miwili mfululizo kumekuwa na mapungufu 15 yanayojirudia kwenye matumizi kama ilivyooneshwa kwenye **Error! Reference source not found.** hapa chini na maelezo zaidi yaliyooneshwa katika **kiambatisho 10-1** cha ripoti hii

**Jedwali Na. 10-1: Mapungufu katika matumizi yanayojirudia kwa miaka miwili inayofuatana**

| Na. | Mapungufu kwenye matumizi | Asilimia ya wastani wa mabadiliko kati ya 2015/2016 na 2016/17 | Na. | Mapungufu kwenye matumizi | Asilimia ya wastani wa mabadiliko kati ya 2015/2016 na 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Malipo yenye nyaraka pungufu | 47.77 | 2. | Malipo ambayo hayakufanyiwa ukaguzi wa awali | 34.03 |
| 3. | Hati za malipo zilizokosekana | 77.21 | 4. | Malipo yasiyostahili | 32.08 |
| 5. | Matumizi yaliyofanywa katika Vifungu visivyohusika | 23.43 | 6. | Malipo batili na yasiyokuwa na manufaa | (47.52) |
| 7. | Matumizi Yasiyokuwamo katika Bajeti | 61.47 | 8. | Matumizi kwenye akaunti ya Amana bila kunukuu stakabadhi zilizoingiza fedha | 43.75 |
| 9. | Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa stakabadhi za mfumo wa kieletroniki | 44.81 | 10. | Matumizi kufanyika zaidi ya kiasi cha amana kilichowekwa | (40.60) |
| 11. | Uhamisho wa ndani wa Fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa | (23.15) | 12. | Mikopo kutoka akaunti ya Amana isiyorejeshwa | 12.74 |
| 13. | Madeni ya miaka iliyopita ambayo hayakulipwa katika mwaka husika | 17.34 | 14. | Malipo yaliyofanywa bila kibali | (0.39) |

| Na. | Mapungufu kwenye matumizi | Asilimia ya wastani wa mabadiliko kati ya 2015/2016 na 2016/17 | Na. | Mapungufu kwenye matumizi | Asilimia ya wastani wa mabadiliko kati ya 2015/2016 na 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15. | Malipo ambayo hayakukatwa Kodi ya Zuio na kuwasilishwa | 23.40 | | | |

Error! Reference source not found.hapo juu linaonesha matokeo ya ukaguzi na asilimia ya wastani wa mabadiliko; ambapo, wastani chanya ukionesha kupungua kwa idadi ya mapungufu licha ya kujirudia; na wastani hasi ukionesha mapungufu yaliyoendelea kutokea huku malipo yenye mapungufu hayo yakizidi kuongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Uchambuzi wa matokeo yenye wastani hasi kwa mabadiliko kwa muda wa miaka miwili mfululizo ni kama inavyoonekana kwenye Kielezo hapo chini;

**Kielelezo Na. 10-1: Uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi yenye ongezeko la asilimia hasi kwa miaka miwili mfululizo**




| | Uhamisho wa ndani wa fedha kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa | Malipo batili yasiyo na manufaa | Matumizi zaidi kwenye akaunti ya Amana |
|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 63 | 40 | 85 |
| 2016/2017 | 78 | 60 | 119 |

Kielelezo hapo juu k inaonesha kuongezeka kwa mwenendo wa uhamisho wa ndani wa Fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa zaidi inaoesha malipo batili na yasiyokuwa na manufaa na matumizi kufanyika zaidi ya kiasi cha amana kilichowekwa.

Hii inamaanisha kuwa fedha za maendeleo na matumizi mengineyo kutoka hazina hazikupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyokusudiwa; hivyo, kusababisha; uhamisho wa ndani wa Fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo pamoja na matumizi kufanyika zaidi ya kiasi cha amana kilichowekwa ili kufanya matumizi muhimu.

Pia, kulikuwa na ongezeko la matumizi yasiyokuwa na manufaa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na misukumo ya nje na malipo yaliyofanywa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na madeni ya kodi la zuio yaliyotokana na kushindwa kwa Mamlaka husika kuzuia kodi hyo kutoka kwa wazabuni. Licha ya baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya jitihada katika kuimarisha udhibiti wa ndani, kuna Mamlaka nyingine ambazo bado zinahitaji mikakati ya ziada ili kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani. Natumaini kuwa idadi na sababu ya hoja za ukaguzi zitaendelea kupungua.

**(b) Mapitio ya matumizi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mara ya kwanza**

Matokeo ya ukaguzi uliofanyika kwenye Mamlaka 14 za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mara ya kwanza yanatoa muonekano wa ufanisi na utendaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Ukaguzi umebainisha mapungufu ambayo yanahitaji usimamizi wa menejimenti za Mamlaka husika ili kuweza kuyaboresha kwa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na kuimarisha mifumo ya udhibiti ya ndani.

Jedwali Na. **10-2** hapa chini linaonesha orodha ya Mamlaka mpya za Serikali za Mitaa na aina ya mapungufu niliyoyabaini wakati wa ukaguzi.

**Jedwali Na. 10-2: Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mara ya kwanza zinazohitaji kuboresha mifumo ya udhibiti ya ndani**

| Na. | Jina la Halmashauri | Mapungufu | Kiasi(Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Chalinze | Malipo yenye nyaraka pungufu | 52,383,631 |
| | | Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa | 29,951,123 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Mapungufu | Kiasi(Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| | | stakabadhi za mfumo wa kieletroniki | |
| | | Matumizi yaliyofanywa katika Vifungu visivyohusika | 43,814,400 |
| | | Matumizi yasiyokuwa katika bajeti | 94,184,392 |
| | | Malipo ambayo hayakufanyiwa ukaguzi wa awali | 46,990,935 |
| | | Mikopo kutoka akaunti ya Amana isiyorejeshwa | 13,030,000 |
| | | Matumizi kwenye akaunti ya Amana bila kunukuu stakabadhi zilizoingiza fedha | 73,996,042 |
| Jumla | | | **354,350,523** |
| 2. | H/Mji Mbinga | Malipo yenye nyaraka pungufu | 1,980,000 |
| | | Malipo yaliyofanywa bila kibali | 12,000,000 |
| | | Matumizi yasiyokuwa katika bajeti | 12,380,000 |
| | | Malipo ambayo hayakufanyiwa ukaguzi wa awali | 162,712,099 |
| Jumla | | | **189,072,099** |
| 3. | H/M Kigamboni | Malipo yenye nyaraka pungufu | 4,062,000 |
| | | Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa stakabadhi za mfumo wa kieletroniki | 144,400,682 |
| | | Masurufu yasiyorejeshwa | 6,790,000 |
| | | Masurufu yaliyochelewa kurejeshwa | 12,817,000 |
| Jumla | | | **168,069,682** |
| 4. | H/W Malinyi | Malipo yenye nyaraka pungufu | 10,398,712 |
| | | Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa stakabadhi za mfumo wa kieletroniki | 46,330,119 |
| | | Malipo ambayo hayakufanyiwa ukaguzi wa awali | 59,939,143 |
| Jumla | | | **116,667,974** |

| Na. | Jina la Halmashauri | Mapungufu | Kiasi(Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| 5. | H/W Madaba | Malipo yenye nyaraka pungufu | 18,642,000 |
| | | Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa stakabadhi za mfumo wa kieletroniki | 8,922,000 |
| | | Matumizi yaliyofanywa katika Vifungu visivyohusika | 10,419,354 |
| | | Matumizi Yasiyokuwa Katika Bajeti | 19,735,000 |
| | | Masurufu yasiyorekodiwa kwenye rejesta | 6,435,320 |
| Jumla | | | **64,153,674** |
| 6. | H/W Kibiti | Malipo yenye nyaraka pungufu | 9,515,940 |
| | | Malipo Yasiyostahili | 14,700,000 |
| | | Matumizi Yasiyokuwa Katika Bajeti | 15,000,000 |
| | | Masurufu yaliyochelewa kurejeshwa | 2,437,000 |
| Jumla | | | **41,652,940** |

Ni matumaini yangu kuwa, udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa nilizozikagua kwa mara ya kwanza utaboreshwa ili kuhakikisha kuwa shughuli za kila siku katika Mamlaka hizi zinaendeshwa kwa ufanisi.

**(c) Mapitio ya usimamizi na udhibiti wa matumizi**

Wakati wa ukaguzi nilibaini matumizi ambayo yalikuwa na ishara za udanganyifu, matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma; kupotea kwa fedha za umma; na matumizi yasiyo na thamani ya pesa. Matumizi ya aina hii yamezuia mawanda ya ukaguzi wangu.

Jedwali Na. 10-3 hapa chini linaonesha aina ya matumizi niliyoyataja hapo juu na kiasi kinachohusika: -

**Jedwali Na. 10-3: Orodha ya aina ya matumizi yasiyofaa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Na. ya Halmashauri | Kiasi(Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| 1. | Malipo yasiyostahili | 36 | 769,479,797 |
| 2. | Malipo batili na yasiyokuwa na manufaa | 17 | 1,011,974,990 |
| 3. | Hati za malipo zilizokosekana | 26 | 477,218,739 |
| 4. | Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na Utoaji wa Stakabadhi za mfumo wa kieletroniki | 93 | 7,421,735,182 |
| 5. | Malipo yenye nyaraka pungufu | 114 | 5,362,908,811 |

Yamefanyika kwa maboresho makubwa kwenye mifumo ya udhibiti wa ndani na kuongeza kasi ya kutekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi ili kukabiliana na mapungufu, natarajia kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa matumizi kwa siku zijazo.

Katika mwaka huu unaotolewa taarifa nilibaini kuwa mapungufu yanayojirudia mara kwa mara yalionekana kwenye maeneo yafuatayo: -

## 10.1 Malipo yasiyostahili Sh.Tz 769,479,797

Ili kuwa na malipo yanayostahili, malipo yanapaswa yahusiane na shughuli zilizokusudiwa na yafuate matakwa ya sheria.

Katika mwaka unaotolewa taarifa, Halmashauri 36 za Serikali za Mitaa zililipa jumla ya Sh.Tz 769,479,797 kwa shughuli mbalimbali, lakini malipo hayo hayakustahili kutokana na: hakukuwa na fedha zilizowekwa kwa ajili ya matumizi hayo; malipo ya aina moja kufanyika mara mbili; kulipa posho kwa kutumia kiwango cha juu zaidi ya kinachokubalika; malipo bila kuzingatia sheria, kinyume na maagizo yaliyotolewa na menejimenti ya programu; au posho na gharama zingine ambazo aina ya malipo yake hayakuwa na manufaa na hayajajumuishwa katika bajeti ya mwaka ya Halmashauri.

Matumizi yasiyostahili yanapelekea matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma, ambapo inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za Halmashauri ikiwa ni za maendeleo au za matumizi ya kawaida.

Nimebaini kuwa kushindwa kwa idara za fedha katika kudhibiti matumizi kama ilivyoidhinishwa kwenye bajeti; na kushindwa kutenga fedha kwenye vifungu sahihi vya matumizi ni sababu kubwa ya matumizi yasiyostahili. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye matumizi yasiyostahili pamoja na kiasi kinachohusika kinaonekana katika **Error! Reference source not found.** chini;

**Jedwali Na. 10-4: Malipo yasiyostahili Sh.Tz 769,479,797**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 9,080,000 | 2 | H/W Meru | 40,851,000 |
| 3 | H/W Arusha | 4,520,000 | 4 | H/W Momba | 10,478,000 |
| 5 | H/W Babati | 63,750,000 | 6 | H/M Mtwara | 5,245,000 |
| 7 | H/W Busega | 9,025,000 | 8 | H/W Mwanga | 1,540,000 |
| 9 | H/W Hanang | 1,040,000 | 10 | H/W Namtumbo | 81,605,813 |
| 11 | H/W Handeni | 4,190,400 | 12 | H/W Ngorongoro | 27,800,000 |
| 13 | H/W Igunga | 5,505,000 | 14 | H/Mji Njombe | 9,340,000 |
| 15 | H/W Kahama | 39,785,532 | 16 | H/W Nyasa | 48,615,750 |
| 17 | H/W Kalambo | 9,000,000 | 18 | H/W Nzega | 13,296,000 |
| 19 | H/W Kaliua | 5,284,000 | 20 | H/Mji Nzega | 3,360,000 |
| 21 | H/W Kibiti | 14,700,000 | 22 | H/W Rombo | 58,449,392 |
| 23 | H/M Kigoma/Ujiji | 8,300,000 | 24 | H/W Same | 11,683,181 |
| 25 | H/W Lushoto | 13,480,000 | 26 | H/W Siha | 14,475,000 |
| 27 | H/W Masasi | 2,200,000 | 28 | H/W Sikonge | 3,566,000 |
| 29 | H/Mji Masasi | 2,330,000 | 30 | H/W Simanjiro | 3,000,000 |
| 31 | H/W Mbinga | 1,010,000 | 32 | H/W Songea | 18,949,000 |
| 33 | H/W Mbogwe | 180,733,529 | 34 | H/M Sumbawanga | 8,647,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 35 | H/W Mbulu | 8,305,400 | 36 | H/W Ukerewe | 26,339,800 |
| | | | | **Jumla** | **769,479,797** |

Narejea mapendekezo yangu niliyotoa kwenye ripoti zilizopita nikizihimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia matakwa ya sheria; kuimarisha udhibiti wa bajeti na kuzingatia vifungu ya bajeti; kurejesha kiasi chote kilicholipwa kimakosa kwenye akaunti za Halmashauri; na kuimarisha udhibiti wa ndani ili kupata thamani ya pesa kwa kiwango cha juu. Mbali na hayo, maafisa wa husika wanapaswa kuwajibika kwa matumizi yasiyostahili.

## 10.2 Matumizi yasiyokuwa na manufaa Sh.Tz 1,011,974,990

Matumizi yasiyokuwa na manufaa ni matumizi yanayofanywa na Halmashauri kwa kulipa gharama za tozo, adhabu au riba kwa kushindwa kuzingatia vipengele ya mikataba ambapo Halmashauri husika haipati faida yoyote kutokana na malipo hayo.

Katika mwaka husika, Halmashauri 17 zililipa kiasi cha Sh.Tz 1,011,974,990 bila kupata manufaa yoyote. Aina ya malipo na kiasi kilichohusika ni kama inavyoonekana kwenye
Jedwali Na. **10-5** hapa chini:-

**Jedwali Na. 10-5: Malipo batili na yasiyokuwa na manufaa Sh.Tz 1,011,974,990**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Aina ya matumizi |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 130,000,000 | Adhabu/riba kwa kushindwa kuzingatia vipengele vya mikataba, ikihusisha faini na fidia kutokana na kesi za kisheria, madai na fidia kwa kuvunja mkataba |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Aina ya matumizi |
|---|---|---|---|
| 2. | H/Mji Babati | 63,824,564 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwa wazabuni kwa mwaka 2013/2014 na 2014/2015 |
| 3. | H/W Bumbuli | 40,000,000 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwenye mikataba ya mwaka 2013 na 2015. |
| 4. | H/W Hanang | 9,812,500 | Gharama zilizotumika kuandaa uchaguzi lakini uchaguzi haukufanyika |
| 5. | H/W Handeni | 277,947,723 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwa wazabuni kuanzia julai 2013 hadi Juni 2015, pia upotevu wa pesa za umma Sh. 197,934,420 kilicholipwa kwa wazabuni nje ya Bohari kuu ya dawa |
| 6. | H/W Kiteto | 44,870,000 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwa wazabuni kwa mwaka Year 2013/2014 to 2016/2017 |
| 7. | H/Mji Kondoa | 2,000,000 | Malipo ya posho ya samani zaidi yaliyosababisha kupotea kwa fedha za serikali |
| 8. | H/W Longido | 10,980,000 | Migogoro ya kazi na malipo zaidi ya posho ya kujikimu kwa Madiwani wakati wa robo ya ya pili ya mwaka 2016/2017 |
| 9. | H/Mji Masasi | 19,360,900 | Mapungufu kutokana na bei za juu zilizotolewa na wasambazaji |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Aina ya matumizi |
|---|---|---|---|
| 10. | H/W Mtwara | 1,320, 000 | Hasara kutokana na kupoka kupokea idadi ndogo ya mabati yakiyonunuliwa |
| 11. | H/W Mtwara | 151,612,400 | Kupotea kwa fedha za Halmashauri baada ya kulipa Ardhi Institute Tabora gharama ya kuthaminisha nyumba za kulipa kodi ya majengo na baadae Mamlaka ya mapato Tanzania kupewa jukumu hilo |
| 12. | H/W Muheza | 26,553,112 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwa wazabuni kati ya mwaka Julai 2013 na Juni 2015. |
| 13. | H/W Nanyumbu | 6,643,560 | Hasara iliyopatikana baada ya kuingia gharama ya kuanzisha kituo cha redio kisichotumika |
| 14. | H/W Pangani | 113,478,820 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwa wazabuni kati ya mwaka Julai 2013 na Juni 2015. |
| 15. | H/W Siha | 6,403,800 | Pesa zilizopotea baada ya kutolewa kwenye akaunti kabla ya muda wa utekelezaji wa shughuli usika |
| 16. | H/W Simanjiro | 74,387,611 | Tozo kwa kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania makato ya kodi la zuio yaliyofanywa kwa wazabuni kati ya mwaka Julai 2012/2013 na 2013/2014 |
| 17. | H/W Tandahimba | 34,100,000 | Halmashauri imepata hasara baada kuingia gharama iliyotumika kufanya kampeni kwa wakulima wa |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Aina ya matumizi |
|---|---|---|---|
| | | | kahawai ili kuhamasisha kuchangia pembejeo na kutengeneza viatabu vya kukusanyia michango hiyo; hata hivyo, Serikali baadae iliagiza pembejeo hizo zitolewe bure. |
| | **Jumla** | **1,011,974,990** | |

Wanasheria wa Halmashauri kushindwa kutasfiri baadhi ya vifungu vya sheria za kodi vinavyoweza kupunguza madeni ya kodi, kutokutoa kodi ya zuio kwenye malipo ya wazabuni, kushindwa kuwasilisha kodi ya zuio Mamlama ya Mapato, na kushindwa kutatua migogoro ya wafanyakazi ndizo sababu kubwa zinazosababisha malipo yasiyo na manufaa. Malipo haya pia yanaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa kodi ya zuio inakatwa na kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mujibu wa matakwa ya sharia; na kuhakikisha kuwa kodi ya zuio iliyolipwa na Halmashauri kwa kushindwa kuzuia kodi hiyo kutoka kwa wazabuni zirejeshwe Halmashauri na wazubuni Husika.

## 10.3 Hati za malipo zilizokosekana Sh. Tz 477,128,739

Agizo la 34(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linamtaka Mweka Hazina wa Halmashauri kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu ziko salama.

Aidha, Agizo la 104 (3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaelekeza kuwa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake vinatakiwa kuwekwa vizuri na kutunzwa kwa muda usiopungua miaka mitano (5).

Kinyume na matakwa ya maagizo hayo, nimebaini hati za malipo zenye thamani ta Sh.Tz 477,128,739 yaliyofanyika kwenye Halmashauri 26 hazikuwamo kwenye makarabrasha husika.

Kwa hiyo, aina na uhalali wa matumizi yaliyofanyika kwenye Halmshauri husika havikuweza kuthibitishwa, hivyo kupelekea kupungua kwa mawanda ya ukaguzi wangu.

Jedwali Na. 10-6 linaonesha Halmashauri ambazo zilitolewa taarifa ya kukosekana kwa hati za malipo.

**Jedwali Na. 10-6: Halmshauri ambazo zilitolewa taarifa ya kukosekana kwa hati za malipo.**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Babati | 17,839,400 | 2 | H/W Mbulu | 2,200,000 |
| 3 | H/Mji Babati | 2,373,099 | 4 | H/W Meatu | 17,360,000 |
| 5 | H/W Bagamoyo | 11,222,880 | 6 | H/W Misungwi | 25,689,427 |
| 7 | H/W Butiama | 35,767,500 | 8 | H/W Mkuranga | 11,745,953 |
| 9 | H/W Hanang | 3,987,000 | 10 | H/W Mwanga | 8,434,147 |
| 11 | H/Mji Handeni | 4,928,125 | 12 | H/W Namtumbo | 27,410,820 |
| 13 | H/M Ilemela | 33,716,963 | 14 | H/W Nanyumbu | 4,310,000 |
| 15 | H/W Kwimba | 2,174,928 | 16 | H/W Newala | 7,334,200 |
| 17 | H/W Kyela | 28,365,200 | 18 | H/W Rombo | 44,437,200 |
| 19 | H/W Mafia | 11,581,886 | 20 | H/W Simanjiro | 1,075,000 |
| 21 | H/W Makete | 5,930,000 | 22 | H/W Tabora | 20,245,690 |
| 23 | H/W Mbogwe | 74,489,707 | 24 | H/W Tandahimba | 20,287,264 |
| 25 | H/W Mbozi | 22,943,600 | 26 | H/W Ukerewe | 31,368,750 |
| | | | | **Jumla** | **477,218,739** |

Narudia mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma kwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza jukumu lao la msingi la kuhifadhi kwa usalama nyaraka muhimu ikiwa ni pamoja na hati za malipo ili kuepuka upotevu.

## 10.4 Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na utoaji wa stakabadhi za mfumo wa kieletroniki Sh.Tz 7,421,735,182

Kifungu Na. 29(4) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 (iliyorekabishwa mwaka 2010) na Kanuni ya 28(1) ya

Kodi ya Mapato ya vifaa vya mfumo wa Kieletroniki, 2012 inahitaji kila mnunuzi kudai na kuhifadhi risiti za kieletroniki au hati ya madai.

Kinyume na matakwa ya sheria zilizotajwa hapo juu na licha ya mapungufu haya kuwa yanajirudia kwa miaka miwili sasa, malipo ya Sh.Tz 7,421,735,182 kwa wazabuni wa bidhaa na huduma yaliyofanywa na Halmashauri 93 yalithibitika kuwa hayana risiti za kieletroniki. Orodha ya Halmashauri husika zimeonyeshwa kwenye **kiambatisho Na.10:2** cha ripoti hii.

Halmashauri kuendelea kulipa wazabuni bila kudai risiti za kieletroniki kunaonesha kuwamo wazabuni wanaofanya nao biashara hawana mashine za kielektroniki au hawadai risiti hizi.

Jedwali Na. 10-7 hapa chini linaonesha Halmashauri zenye manunuzi ya bidhaa na huduma yenye thamani kubwa yasiyo na risiti za kielectroniki.

**Jedwali Na. 10-7: Halmashauri zilizofanya manunuzi bila yasiyoambatana na risiti za kieletroniki**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Sikonge | 551,860,478 |
| 2. | H/M Dodoma | 543,507,333 |
| 3. | H/M Kinondoni | 487,659,674 |
| 4. | H/W Mbarali | 453,714,315 |
| 5. | H/W Hanang | 402,617,980 |

Kwa sasa, Serikali inasisitiza juu ya umuhimu wa kudai risiti za kieletroniki kwa kila manunuzi yanayofanyika. Ni matarajio yangu kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitafanya biashara na wazabuni wasiotoa risiti za kielektroniki na pia watadai risiti zote za kielektroniki ambazo hazikutolewa awali kutoka kwa wazabuni husika.

## 10.5 Malipo ambayo hayakukatwa Kodi ya Zuio Sh.Tz. 156,244,852

Kifungu cha 83A na Aya 4(c) ya Jedwali la kwanza kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2014 kinataka makato ya kodi ya

zuio ya 5% kwa huduma zinazotolewa na 2% kwa manunuzi ya bidhaa.

Kinyume na hayo, kodi ya zuio kiasi cha Sh.Tz 156,244,852 katika mwaka unaokaguliwa hazikukatwa na Halmashauri 21 kwenye malipo ya huduma na bidhaa. Orodha ya Halmashauri hizo na kiasi kilichohusika ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 10-8 hapo chini.

Kukata kodi ya zuio kunapunguza gharama za ukusanyaji wa kodi; huongeza kuzingatia sheria na kupunguza kukwepa kodi; vile vile Serikali hukusanya kodi mapema, kitu ambacho hakijaweza kufanikiwa kutokana na mazingira haya.

**Jedwali Na. 10-8: Kodi ya zuio ambayo haikukatwa Sh.Tz 156,244,852**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 16,461,272 | 2 | H/W Mbarali | 55,097,156 |
| 3 | H/W Arusha | 2,051,780 | 4 | H/W Meru | 3,810,457 |
| 5 | H/W Babati | 1,263,371 | 6 | H/W Momba | 3,129,416 |
| 7 | H/Mji Ifakara | 9,068,243 | 8 | H/M Mpanda | 1,267,203 |
| 9 | H/W Kalambo | 8,178,691 | 10 | H/W Msalala | 5,725,677 |
| 11 | H/W Kilombero | 5,932,129 | 12 | H/M Mtwara | 140,000 |
| 13 | H/W Kilosa | 5,447,064 | 14 | H/W Ngorongoro | 23,549,785 |
| 15 | H/Mji Korogwe | 1,210,830 | 16 | H/W Singida | 1,171,249 |
| 17 | H/W Kyerwa | 4,827,737 | 18 | H/W Tandahimba | 2,519,720 |
| 19 | H/W Lindi | 1,817,073 | 20 | H/W Ukerewe | 3,576,000 |
| 21 | H/Mji Masasi | 526,938 | | | |
| | | | | **Jumla** | **156,244,852** |

Ninashauri Menejimenti za Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuhakikisha zinazingatia matakwa mbali mbali ya sheria, Kanuni, miongozo na maagizo yanayohusiana na makusanyo ya kodi ili kuisaidia Serikali kuongeza mapato.

## 10.6 Malipo ya madeni ambayo hayakuonyeshwa miaka ya nyuma Sh.Tz 1,178,669,460

Malipo yenye thamani ya Sh.Tz 1,178,669,460 yalifanywa na Halmashauri 40 kulipa madeni ya miaka iliyopita. Hata hivyo, hakuna ushahidi ulionionesha kuwa malipo hayo yalikuwa ni sehemu ya madai ya mwaka 2014/2015. Pia, nilishindwa kuthibitisha kwamba yaliingizwa kwenye bajeti ya mwaka husika. Hii ni kinyume na Agizo la 22(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ya LGFM, 2009 linalohitaji kufanya matumizi katika mwaka husika, na hayapaswi kuhairishwa ili yalipwe katika mwaka unaofuata kwa lengo la kuepuka kuwa na matumizi zaidi katika mwaka husika.

Malipo ya madeni ambayo hayakutambuliwa miaka ya nyuma yanabainisha kuwa shughuli zilizopangwa mwaka husika za kiasi sawa na kilichotumika hazikufanyika. Orodha ya Halmashauri zenye malipo ya aina hii ni kama zinavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 10-9 hapa chini: -

**Jedwali Na. 10-9: Madeni ya Miaka Iliyopita Ambayo Hayakulipwa Katika Mwaka Husika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Arusha | 54,549,802 | 21 | H/W Lindi | 22,760,025 |
| 2 | H/W Babati | 3,064,900 | 22 | H/W Meru | 93,185,445 |
| 3 | H/W Biharamulo | 10,923,650 | 23 | H/W Missenyi | 19,074,147 |
| 4 | H/W Bunda | 36,752,800 | 24 | H/W Moshi | 29,145,937 |
| 5 | H/Jiji Dar es Salaam | 121,060,603 | 25 | H/M Moshi | 52,627,800 |
| 6 | H/M Dodoma | 10,697,709 | 26 | H/M Mtwara | 7,197,407 |
| 7 | H/W Hai | 5,449,500 | 27 | H/W Mwanga | 20,685,742 |
| 8 | H/W Hanang | 9,051,653 | 28 | H/Jiji Mwanza | 50,488,161 |
| 9 | H/W Handeni | 46,781,949 | 29 | H/W Ngorongoro | 11,040,000 |
| 10 | H/Mji Handeni | 11,854,460 | 30 | H/W Pangani | 57,592,280 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | H/Mji Ifakara | 7,476,500 | 31 | H/W Rombo | 15,673,400 |
| 12 | H/M Ilala | 126,125,200 | 32 | H/W Rungwe | 45,315,700 |
| 13 | H/W Iringa | 6,762,800 | 33 | H/W Siha | 3,055,500 |
| 14 | H/W Karagwe | 38,950,000 | 34 | H/W Simanjiro | 3,680,000 |
| 15 | H/W Karatu | 29,077,700 | 35 | H/W Songea | 4,532,100 |
| 16 | H/W Kibaha | 7,345,000 | 36 | H/M Songea | 43,827,016 |
| 17 | H/W Kilolo | 17,622,500 | 37 | H/Jiji Tanga | 36,466,527 |
| 18 | H/M Kinondoni | 53,657,304 | 38 | H/W Tunduru | 21,732,700 |
| 19 | H/W Kiteto | 5,376,979 | 39 | H/M Ubungo | 14,473,028 |
| 20 | H/Mji Korogwe | 15,055,210 | 40 | H/W Ushetu | 8,480,326 |
| | **Jumla** | | | | **1,178,669,460** |

Natoa mapendekezo kwa Halmashauri husika kutafuta idhini ya kuhalalisha matumizi yaliyokwishafanyika na kurekebisha taarifa za fedha za miaka husika. Katika siku zijazo Halmashauri zinapaswa kuhakikisha madeni yote yanaingizwa katika rejesta ya madeni na hairuhusu malipo kwa wazabuni ambao hawapo kwenye taarifa ya madeni iliyoidhinishwa.

## 10.7 Matumizi yasiyokuwa katika bajeti na fedha zilizobadilishiwa matumizi Sh. Tz 4,658,384,441

Mamlaka za Serikali za Mitaa 63 zilitumia kiasi cha Sh. Tz 4,658,384,441 kulipia shughuli mabalimbali ambazo hazikuwa kwenye bajeti bila kuwa na kibali cha mamlaka husika. Hii ni kinyume na kifungu cha 43 (5) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2000) kinachozitaka Halmashauri kutumia fedha kama bajeti inavyoruhusu. Matumizi yaliyofanywa nje ya bajeti na fedha zilizobadilishiwa matumizi zinaonesha kuwa shughuli zilizokuwa kwenye bajeti zimeathirika.

Orodha ya Halmashauri pamoja na kiasi kilichotumika kimeoneshwa kwenye **kiambatisho 10:3.**

**Jedwali Na. 10-10: Halmashauri zilizofanya matumizi nje ya bajeti na zilizobadilishiwa matumizi ya fedha kwa kiasi kikubwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Ilemela | 726,319,027 |
| 2 | H/W Geita | 380,000,000 |
| 3 | H/W Meru | 325,329,187 |
| 4 | H/Jiji Mwanza | 269,695,983 |
| 5 | H/Jiji Arusha | 202,608,128 |

Kuandaa bajeti isiyo sahihi na udhibiti duni wa vifungu vya bajeti ndizo sababu zilizopeleka kufanyika kwa matumizi nje ya bajeti na kubadilisha matumizi ya fedha.

Hivyo, ninapendekeza kwa menejimenti za Halmashauri kuzingati matakwa ya kifungu Na. 43 (5) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2000) na kuweka udhibiti imara ili kuzuia malipo yaliyo nje ya bajeti.

## 10.8 Uhamisho wa ndani wa Fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa Sh. Tz 1,240,848,557

Katika kila mwaka wa fedha, fedha zinazopokelewa zinatarajiwa kutumika kulingana na bajeti iliyopitishwa. Hii ni kulingana na Agizo la 23(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inayotaka matumizi yanayofanyika yalipwe kulingana na vifungu vya bajeti na fedha zilizoidhinishwa zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini uhamisho wa kiasi cha Sh. Tz 1,240,848,557 uliofanywa na Halmashauri 17 kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo na fedha hizi hazikurejeshwa kwenye akaunti husika hadi mwisho wa mwaka. Uhamisho wa fedha kwa njia ya mikopo kwenye akaunti za ndani ni matokeo ya mapokezi pungufu na kuchelewa kwa fedha kutoka

Hazina. Uhamishaji wa fedha unaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa ndani ya muda uliotarajiwa.

Orodha ya Halmashauri zenye mikopo kwenye akaunti za ndani ni kama zinavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 10-11 hapa chini: -

**Jedwali Na. 10-11: Uhamisho wa ndani wa Fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 665,000,000 | 2 | H/W Meatu | 30,000,000 |
| 3 | H/Mji Babati | 37,010,328 | 4 | H/W Mpanda | 25,600,000 |
| 5 | H/W Bariadi | 60,000,000 | 6 | H/W Nsimbo | 96,616,865 |
| 7 | H/Mji Bariadi | 9,400,000 | 8 | H/W Serengeti | 6,508,000 |
| 9 | H/W Buchosa | 13,990,964 | 10 | H/M Songea | 14,428,300 |
| 11 | H/W Busega | 65,234,000 | 12 | H/M Sumbawanga | 9,534,000 |
| 13 | H/W Butiama | 32,446,000 | 14 | H/W Tunduru | 16,600,100 |
| 15 | H/M Ilala | 92,480,000 | 16 | H/W Ukerewe | 41,000,000 |
| 17 | H/Mji Masasi | 25,000,000 | | **Jumla** | **1,240,848,557** |

Ninapendekeza kwa Halmashauri kurejesha fedha zilizokopwa kwenye akaunti husika ndani ya mwaka ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwenye akaunti zilizotoa fedha hizi.

## 10.9 Mikopo kutoka akaunti ya Amana isiyorejeshwa Sh. Tz 5,611,768,190

Jumla ya kiasi cha Sh.Tz. 5,611,768,190 zilikopwa kutoka akauti za Amana katika Halmashauri 63 ili kuweza kufanya matumizi mbali mbali ya kawaida. Hata hivyo, mpaka mwisho wa ukaguzi, sikuweza kupata uthibitisho wa maelezo ya kurejeshwa kwa fedha hizo. Hii ni kinyume na matakwa ya Aya 5.19 ya Mwongozo wa Uhasibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 unaoelekeza malipo kwenye akaunti ya Amana kufanyika kwa

lengo lililokusudiwa na kuwe na uthibitisho wa risiti ya mapokezi ya fedha hizo kwenye akaunti hiyo.

Orodha ya Halmashauri pamoja na kiasi husika kimeoneshwa kwenye **kiambatisho 10:4.**

Jedwali Na. 10-12 hapa chini linaonesha Halmashauri 17 zenye kiasi kikubwa cha madeni kwenye akaunti za amana

**Jedwali Na. 10-12: Halmashauri zenye kiasi kikubwa cha madeni kwenye akaunti za amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Masasi | 829,118,058 | 10 | H/M Musoma | 151,633,133 |
| 2 | H/W Mbinga | 380,870,558 | 11 | H/W Nyasa | 134,976,900 |
| 3 | H/M Dodoma | 277,143,371 | 12 | H/W Kalambo | 131,627,146 |
| 4 | H/W Kondoa | 276,085,027 | 13 | H/W Ngara | 126,377,128 |
| 5 | H/W Sumbawanga | 225,933,894 | 14 | H/W Handeni | 114,828,107 |
| 6 | H/W Bumbuli | 219,152,040 | 15 | H/W Muheza | 110,025,785 |
| 7 | H/W Serengeti | 193,855,698 | 16 | H/W Urambo | 109,616,836 |
| 8 | H/W Karagwe | 187,433,961 | 17 | H/W Butiama | 107,789,151 |
| 9 | H/Jiji Arusha | 183,289,182 | **Jumla** | | **5,611,768,190** |

Narudia mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwa menejimenti za Halmashauri kurejesha Sh. Tz 5,611,768,190 zilizokopwa kutoka kwenye akaunti za amana; na kuhakikisha kuwa, siku zijazo malipo yanaambatana na uthibitisho wa risiti ya mapokezi ya fedha iliyotumika kukiri mapokezi ya fedha hizo zilizoingia kwenye akaunti ya Amana.

## 10.10 Malipo yasiyotambulika katika Akaunti ya Amana Sh. Tz 8,388,155,073

Akaunti ya amana ni akaunti ya dhima ambayo hutumiwa kwa ajili ya kuhifadhi fedha za watu tofauti kwa madhumuni tofauti. Matumizi ya fedha hiyo yanatarajia kuwa sawa na lengo kuu la amana hizo. Katika mwaka uliopitiwa 2016/2017, kiasi cha Sh.

Tz 5,284,410,826 zililipwa kutoka kwenye akaunti za Amana za Mamlaka za Serikali za Mitaa 53 ili kutekeleza shughuli mbalimbali lakini hazikuweza kunukuu stakabadhi zilizoingiza fedha hizo.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Sh. Tz 3,103,744,247 zililipwa zaidi ya fedha zilizowekwa katika akaunti ya amana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 26 na kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na matumizi yasiyotambuliwa yameoneshwa katika **kiambatanisho Na. 10:5** cha ripoti hii.

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha udhibiti wa ndani kwenye usimamizi wa akaunti za Amana ikiwa ni pamoja na kurejesha kwenye akaunti ya amana kiasi cha Sh.Tz. 8,388,155,073 kilichotumika bila kutambuliwa.

## 10.11 Malipo bila kibali sahihi Sh. Tz 822,372,229

Agizo la 10 (2) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linahitaji maafisa wenye mamlaka kuhakikisha kwamba matumizi yote ni halali na yamehalalishwa au kuidhinishwa vizuri; kuwe na fedha za kutosha kulipia matumizi yaliyoidhinishwa; matumizi yenye tija na yenye kuleta thamani; na kuwe na ushahidi husika (nyaraka) katika matumizi yote.

Jumla ya Sh. Tz 822,372,229 zililipwa na Mamlaka za serikali za mitaa 17 bila kuwa na kibali sahihi. Hii inajumuisha malipo yaliyofanyika bila kibali cha mkuu wa idara na wakurugenzi watendaji; na malipo yaliyoanzishwa na kuidhinishwa na mtu mmoja. Tazama Jedwali Na. 10-13

**Jedwali Na. 10-13: Malipo yaliyofanyika bila kibali sahihi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Butiama | 8,548,690 | 10 | H/W Meru | 33,850,000 |
| 2 | H/M Dodoma | 40,361,360 | 11 | H/W Musoma | 22,011,227 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | H/Mji Kahama | 23,467,500 | 12 | H/W Rombo | 13,377,600 |
| 4 | H/W Kalambo | 85,064,366 | 13 | H/W Same | 197,964,832 |
| 5 | H/W Kaliua | 4,348,828 | 14 | H/W Siha | 2,187,000 |
| 6 | H/W Kongwa | 4,530,000 | 15 | H/W Sumbawanga | 121,333,567 |
| 7 | H/W Madaba | 19,735,000 | 16 | H/M Temeke | 35,856,059 |
| 8 | H/W Magu | 186,221,400 | 17 | H/W Ukerewe | 11,514,800 |
| 9 | H/Mji Mbinga | 12,000,000 | **Jumla** | | **822,372,292** |

Ukosefu wa idhini na vibali sahihi unaweza kupelekea matumizi yasio sahihi na yasiyo na tija kwa taifa; pia yanaweza kuwa chanzo kikuu cha upotevu wa fedha za umma.

Ninapendekeza kwa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha kwamba malipo yaliyolipwa yamepitishwa na mamlaka sahihi katika ngazi zote ili kupunguza matumizi yasiyoridhisha ya fedha na kupelekea hasara kwa serikali.

## 10.12 Malipo bila kuwa na viambata muhimu Sh. Tz 5,362,908,811

Agizo la 8 (2) (c) na 104 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 linawataka Wahazini na Wakuu wa Idara kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti na kutunza nyaraka za fedha kwa usalama kwenye Idara zao.

Katika mwaka huu wa ukaguzi nilibaini kiasi cha Sh. Tz 5,362,908,811 kulipwa katika Mamlaka 114 bila kuwa na viambata muhimu kama fomu ya posho ya safari iliyoidhishwa, barua ya mwaliko wa mafunzo, orodha ya malipo ya posho, taarifa ya shughuli iliyofanyika, na stakabaadhi ya kukiri mapokezi. Hivyo, sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Orodha ya Halmashauri husika pamoja na kiasi kilicholipwa kwa kila Halmashauri imeoneshwa katika **kiambatanisho 10.6** cha taarifa hi.

Jedwali Na. 10-14 linaomesha Halmashauri zenye malipo yenye thamani ya juu yaliokosa viambata muhimu

**Jedwali Na. 10-14: Halmashauri zenye malipo makubwa yasiyo na viambata muhimu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Rungwe | 247,449,890 | 9 | H/W Newala | 152,350,805 |
| 2 | H/M Ilemela | 234,001,909 | 10 | H/W Longido | 151,744,125 |
| 3 | H/M Kinondoni | 216,110,627 | 11 | H/W Morogoro | 145,938,000 |
| 4 | H/W Mkinga | 212,504,010 | 12 | H/MJI Masasi | 126,547,604 |
| 5 | H/W Kalambo | 198,725,521 | 13 | H/W Magu | 110,809,902 |
| 6 | H/W Ukerewe | 182,048,052 | 14 | H/W Nanyumbu | 104,687,061 |
| 7 | H/W Kwimba | 179,253,232 | 15 | H/W Mbogwe | 104,375,729 |
| 8 | H/M Temeke | 169,616,124 | **Jumla** | | **5,362,908,811** |

Kutokuambatishwa kwa nyaraka kwenye hati za malipo kunaweza kuwa kumetokana na udhibiti mdogo wa ndani wa uhifadhi wa nyaraka za fedha na nyaraka nyingine zinazohusiana na kazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba vitengo vya ukaguzi wa awali vinatumika kwa ufanisi katika kupitia hati za malipo na viambata vyote kabla ya kuidhinishwa na viongozi wa juu. Pia, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa nazishauri kuteua wahusika ambao watakuwa na wajibu wa kuhifadhi na kulinda usalama wa hati za malipo pamoja na vyambata vyake.

## 10.13 Matumizi yaliyolipiwa katika vifungu visivyohusika Sh. 1,777,247,097

Jumla ya Sh. Tz 1,777,247,097 zimebainika kulipwa kutoka kwenye vifungu visivyohusika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 44. Hii ni kinyume na Agizo la 23 (1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaloagiza kwamba, kila malipo yafanywe kulingana na mapato ya kifungu husika na

kwa mujibu wa maelekezo ya bajeti iliyoidhinishwa na fedha zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Mbali na kufanywa kinyume na udhibiti wa bajeti na maagizo, malipo ya matumizi kwa vifungu visivyohusika yanasababisha kuongezeka au kupungua kwa matumizi katika vifungu husika, na hivyo kutokuonyesha uhalisia kwenye taarifa ya mwisho wa mwaka kama inavyo onyesha katika Jedwali Na. 10-15 hapa chini:

**Jedwali Na. 10-15: Matumizi yaliyolipiwa kwenye vifungu visivyo**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Arusha | 18,816,000 | 23 | H/W Makete | 47,106,553 |
| 2 | H/W Bagamoyo | 17,515,340 | 24 | H/W Maswa | 37,554,614 |
| 3 | H/W Bariadi | 33,387,175 | 25 | H/JIJI Mbeya | 5,857,000 |
| 4 | H/W Buchosa | 53,144,500 | 26 | H/W Mbinga | 36,929,000 |
| 5 | H/W Chalinze | 43,814,400 | 27 | H/W Meatu | 146,705,000 |
| 6 | H/W Hanang | 38,234,170 | 28 | H/W Meru | 105,989,260 |
| 7 | H/W Handeni | 12,303,100 | 29 | H/W Missenyi | 7,829,650 |
| 8 | H/MJI Handeni | 10,249,750 | 30 | H/W Misungwi | 32,597,000 |
| 9 | H/M Ilala | 171,800,876 | 31 | H/W Mkalama | 12,256,000 |
| 10 | H/M Ilemela | 66,956,505 | 32 | H/W Mkuranga | 13,822,920 |
| 11 | H/W Iringa | 8,798,352 | 33 | H/W Moshi | 26,504,691 |
| 12 | H/W Itilima | 33,669,000 | 34 | H/M Moshi | 86,521,540 |
| 13 | H/W Kalambo | 47,388,000 | 35 | H/W Mvomero | 18,242,750 |
| 14 | H/W Kigoma | 15,524,190 | 36 | H/W Mwanga | 5,554,140 |
| 15 | H/W Kilindi | 37,470,476 | 37 | H/JIJI Mwanza | 70,496,040 |
| 16 | H/M Kinondoni | 81,599,717 | 38 | H/W Nkasi | 132,640,912 |
| 17 | H/W Kisarawe | 40,193,542 | 39 | H/W Siha | 12,823,000 |
| 18 | H/MJI Korogwe | 23,970,000 | 40 | H/M Songea | 74,530,000 |
| 19 | H/W Longido | 1,713,000 | 41 | H/W Tarime | 9,385,000 |
| 20 | H/W Lushoto | 62,542,100 | 42 | H/W Tunduru | 17,648,280 |
| 21 | H/W Madaba | 10,419,354 | 43 | H/M Ubungo | 20,152,250 |
| 22 | H/MJI Makambako | 9,525,000 | 44 | H/W Urambo | 17,066,950 |
| **JUMLA** | | | | | **1,777,247,097** |

Udhaifu wa mfumo bajeti na mfumo wa hesabu (EPICOR) ndio chanzo kikubwa cha kuwapo kwa malipo yanayofanyika katika vifungu visivyo husika.

Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za serikali za mitaa kutengeneza bajeti yenye uhalisia; ziwasiliane na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuanzisha udhibiti mkubwa wa bajeti katika mfumo wa hesabu (EPICOR); na kama malipo ya matumizi kwa vifungu visivyohusika yanatokea bila kukusudia, basi taratibu za kifedha zifuatwe ili kuhalalisha matumizi hayo.

## 10.14 Malipo ambayo hayakufanyiwa ukaguzi wa awali Sh. Tz 2,182,095,636

Aya 2.4.2 ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 inatamka kuwa hati za malipo na viambata vyake zipitishwe katika idara ya fedha ambapo ukaguzi wa awali utafanyika kuangalia usahihi na uhalali wa taarifa zilizoandikwa kwenye hati ya malipo. Pamoja na Agizo hilo, nilibaini malipo ya Sh. Tz 2,182,095,936 kulipwa bila kufanyiwa ukaguzi wa awali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 kama zilivyo ainishwa katika Jedwali Na. 10-16 hapa chini.

**Jedwali Na. 10-16: Malipo yaliyofayika bila ukaguzi wa awali. Sh. Tz 2,182,095,636**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Buchosa | 249,783,521 | 18 | H/MJI Mbinga | 162,712,099 |
| 2 | H/W Busega | 56,666,724 | 19 | H/W Mbozi | 21,470,000 |
| 3 | H/W Chalinze | 46,990,935 | 20 | H/W Meru | 7,228,000 |
| 4 | H/W Gairo | 12,076,430 | 21 | H/W Mkalama | 32,473,000 |
| 5 | H/W Hanang | 15,634,970 | 22 | H/W Mlele | 29,327,500 |
| 6 | H/W Ileje | 36,185,200 | 23 | H/M Moshi | 112,200,731 |
| 7 | H/W Itilima | 63,364,600 | 24 | H/W Mpanda | 8,542,000 |
| 8 | H/W Kalambo | 403,044,907 | 25 | H/W Mwanga | 17,501,370 |
| 9 | H/W Kongwa | 90,674,300 | 26 | H/W Nanyumbu | 9,360,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | H/MJI Korogwe | 72,620,434 | 27 | H/W Rombo | 4,500,000 |
| 11 | H/W Ludewa | 54,580,000 | 28 | H/W Same | 6,302,480 |
| 12 | H/W Lushoto | 2,655,000 | 29 | H/W Singida | 56,233,000 |
| 13 | H/MJI Makambako | 15,972,000 | 30 | H/M Singida | 96,076,740 |
| 14 | H/W Makete | 25,325,072 | 31 | H/W Sumbawanga | 170,719,478 |
| 15 | H/W Malinyi | 59,939,143 | 32 | H/W Ukerewe | 147,381,522 |
| 16 | H/MJI Masasi | 10,538,767 | 33 | H/W Uvinza | 70,472,386 |
| 17 | H/W Mbeya | 7,790,000 | 34 | H/W Wanging'ombe | 5,753,327 |
| **JULMA** | | | | | **2,182,095,636** |

Malipo yanayofanywa bila ya kupitia kitengo cha ukaguzi wa awali kuna uwezekano mkubwa wa kukosa viambata vya kutosha na mapungufu mengine kama kutoidhinishwa na kuweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa awali na kuhakikisha malipo yote yanaidhinishwa vizuri na idara zote kama zinavyotakiwa na mgawanyiko wa majukumu. Hii ni muhimu kwa usimamizi bora na ufanisi katika matumizi ya rasilimali zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 10.15 Utunzaji wa Rejesta za Amana na Masurufu Wenye Mapungufu

Aya ya 5.19 ya Mwongozo wa Uhasibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 inaeleza kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapokea fedha za Amana za aina mbalimbali. Ili kuhakikisha kunakuwa na udhibiti imara na wa kutosha kwa fedha hizo za amana, inatakiwa kuanzishwa kwa rejista za amana na ziwe na kurasa zinazoonesha kila aina ya Amana; zimepokelewa kutoka wapi na kwa madhumuni gani; tarehe za mapokezi na malipo, kumbukumbu namba na bakaa.

Aya 5.17 ya Mwongozo wa Uhasibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 inasema kuwa rejista ya masurufu ndio muongozo wa kutunza kumbukumbu kwa ufanisi wa urejeshaji wa masurufu. Rejista ya masurufu inapaswa kuwa na taarifa kama vile tarehe masurufu yalipotolewa, aliye pewa masurufu, nambari ya ajira, nambari ya hati ya malipo, kiasi kilichotolewa, tarehe ya kurejesha masurufu na tarehe masurufu yaliporejeshwa.

Kinyume na maagizo ya hapo juu, nilibaini Mamlaka 26 ambazo hazikuandaa rejista ya amana na Mamlaka 16 hazikuandaa vizuri rejista ya masurufu. Kwa hiyo, iliniwia vigumu kubaini mwenendo mzima wa fedha zilizokuwa katika akaunti ya amana na masurufu amabayo hayakurejeshwa.

Ninapendekeza kwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa na kutunza rejister za amana na masurufu kwa kuingiza taarifa zote muhimu kama inavyotakiwa na Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Mitaa, 2009.

Orodha ya Halmashauri husika pamoja na sababu ya kutokutunza rejesta ya amana na masurufu imeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 10:7** cha ripoti hii.

## 10.16 Mapungufu katika usimamizi wa masurufu Sh.Tz 2,081,629,305

Agizo la 40(3) la Memoranda ya fedha Mamlaka za serikali za mitaa ya mwaka 2009 inataka masurufu kurejeshwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kazi kuisha; na Aya 5.17 ya Mwongozo wa Uhasibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 inasema rejesta ya masurufu ndio muongozo wa kutunza kumbukumbu kwa ufanisi wa urejeshaji wa masurufu. Kwa nyongeza, agizo 40 (4) na (5) la Memoranda ya fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inakataza kutoa masurufu kwa mtu yeyote kama atakuwa hajarejesha masurufu ya awali; pia

masurufu yasiyorejeshwa kwa zaidi ya mwezi mmoja baada ya kazi kuisha yanapaswa kupigwa tozo kama kanuni za fedha za serikali zinavyotaka.

Kinyume na maagizo na aya nilizo nukuu hapo juu, nilibaini mapungufu katika kutoa na kurejesha masurufu ya kiasi cha Sh. Tz 2,081,629,305 katika mamlaka 97. Maelezo zaidi yapo kwenye Jedwali Na. 10-17 na **kiambatanisho 10:8** ya ripoti hii.

**Jedwali Na. 10-17: Mapungufu katika kutoa na kurejesha masurufu**

| Idadi ya Mamlaka | Kosa lililo fanyika | Kanuni iliyo kiukwa | Maelezo | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|
| 16 | Masurufu ambayo hayaku rekodiwa kwenye rejista | Aya 5.17 ya Muongozo wa Uhasibu (LAAM), 2009 | Rejista ya masurufu itunzwe kama inavyotakiwa | 196,876,901 |
| 14 | Masurufu kutambulika kama matumizi kabla ya marejesho | Agizo 29(5) Memoranda ya fedha (LGFM),2009 | Mrejesho wa matumizi ya masurufu yafanyike kwa kutumia Journal Voucher. Hati za malipo zisitumike kuhalalisha matumizi ya masurufu. | 336,036,112 |
| 10 | Masurufu yaliyotolewa kabla ya kurejesha ya awali | Agizo 40(4) la Memoranda ya Fedha (LGFM),2009 | Mtu asipewe masurufu kabla ya kurejesha masurufu ya awali. | 558,889,766 |

| Idadi ya Mamlaka | Kosa lililo fanyika | Kanuni iliyo kiukwa | Maelezo | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|
| 57 | Masurufu yasiyorejeshwa na yaliyo rejeshwa baada ya muda mrefu | Agizo 40(3) la memoranda y fedha (LGFM),2009 | Masurufu lazima yarejeshwe ndani ya wiki mbili baada ya shughuli kufanyika; kinyume na hapo, kiasi kinachobakia lazima kikatwe kwenye mshahara wa mtumishi au kupigwa tozo. | 989,826,526 |
| | | **Jumla** | | **2,081,629,305** |

Udhaifu katika kusimamia masurufu ni chanzo kikubwa cha mapungufu, hivyo ninapendekeza kwa menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuweka mfumo imara wa namna ya kutoa masurufu na namna ya kuyarejesha ili kuenda sawa na Agizo la 27 (5) na 40 (1-5) ya memoranda ya fedha ya serikali za mitaa 2009 na aya 5.17 ya Muongozo wa uhasibu 2009.

## 10.17 Mapungufu katika matumizi ya mafuta Sh. Tz 717,518,625

Nilipitia usimamizi wa mafuta na kufanya ulinganisho wa rekodi zilizo kwenye madaftari ya kuratibu safari za magari na umeonesha kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuweka kumbukumbu sahihi za kupokeaji na utoaji wa mafuta. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa taarifa tofauti kati ya madaftari ya kuratibu safari za magari na rejesta ya mafuta. Pia, nimebaini kuwa taarifa kwenye madaftari ya kuratibu safari za magari ziko kinyume na Agizo la 89 (3) (a - e) la Memoranda ya fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambalo linataka daftari la kuratibu safari liwepo kwa kila gari, likionyesha kila safari, tarehe na muda wa safari, mwanzo wa safari na mwisho wa safari, kilometa zinazosomeka kabla ya safari na mwisho wa

safari, jumla ya kilometa ilizotembea katika safari, na mafuta yaliyokuwepo na yaliyopokelewa kwa matumizi ya gari.

Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu yaliyo bainishwa kwenye daftari za kuratibu safari: -

- Manunuzi ya mafuta yenye thamani ya Sh.Tz. 717,518,625 hayakurekodiwa kwenye daftari la kuratibu safari kama inavyo onekana kwenye **Kiambatanisho 10.9**(A)ya ripoti hii.

- Mafuta yenye thamani ya Sh.Tz. 33,399,479 katika mamlaka 5 yaliwekwa kwenye magari ambayo siyo mali ya Halmshauri husika, hivyo sikuweza kuona kama matumizi ya mafuta haya yalikuwa kwa faida ya Halmashauri au vinginevyo. Na hii ilikuwa ni kutokana na kutokupatikana kwa rekodi za magari yaliyohusika na matumizi ya mafuta hayo kama inavyo onyesha katika **kiambatanisho 10.9(B)**

- Kulikuwa na matumizi zaidi ya mafuta yenye thamani ya Sh. 31,876,645 katika Halmashauri 6 ambapo kwa wastani gari zilitumia lita moja kwa kilometa 2 hadi 5 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 10-18 hapa chini: -

**Jedwali Na. 10-18: Mamlaka zenye matumizi Zaidi ya mafuta**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Ikungi | 1,108,254 |
| 2 | H/W Manyoni | 2,800,957 |
| 3 | H/W Msalala | 9,282,356 |
| 4 | H/W Meru | 4,285,713 |
| 5 | H/W Mkalama | 5,366,000 |
| 6 | H/MJI Newala | 9,033,365 |
| | **Jumla** | **31,876,645** |

Matumizi ya mafuta katika Mamlaka za serikali za mitaa yanagharimu fedha nyingi sana; hivyo basi, kutokuwa na uwekaji

na utunzaji mzuri wa madaftari ya kuratibu safari za magari huweza kupelekea mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Pia, kutokuwapo kwa risiti za mafuta na rekodi za matumizi kulipelekea kushindwa kutambua matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa matumizi yasiyofaa ya mafuta. Zaidi ya hayo, kuna usimamizi usioridhisha wa Maafisa wa Usafirishaji katika kuhakikisha vitabu vya kuratibu safari vinasimamiwa vizuri na kukamilishwa kama taratibu na miongozo inavyoagiza.

Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha udhibiti uliowekwa wa kurekodi matumizi ya mafuta ikiwa ni pamoja na kuweka taarifa sahihi katika leja za mafuta, na daftari za kuratibu safari za magari. Kwa kuongeza, lazima kuwe na usimamizi wa kutosha wa madereva ili vitabu vya kumbukumbu viwekwe vizuri kama taratibu na miongozo inavyoagiza.

## 10.18 Matumizi duni ya mfumo wa usimamizi wa fedha (IFMS) katika kuboresha usimamizi wa matumizi

Mageuzi ya sekta ya fedha nchini Tanzania yameanza tangu mwaka 1992. Mfumo wa Usimamizi wa Fedha ulianzishwa mwaka 1996 ikiwa ni sehemu ya Programu ya mageuzi ya huduma Serikalini ili kuimarisha uwezo wa Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara na Wakala katika kuboresha usimamizi wa matumizi. Sehemu kubwa ya shughuli za kifedha za Halmashauri zinafanywa kwa kutumia mfumo wa EPICOR toleo la 9.05 na toleo la 10 kwa baadhi ya Halmashauri. Hata hivyo, tathmini ya ufanisi ya mfumo huo kwenye Halmshauri umebaini changamoto zilizopelekea kuwe na mapungufu kwenye matumizi.

Changamoto zilizobainika na orodha ya Halmashauri yenye changamoto hizo ni kama zinavyoonekana kwenye, zimeelezewa kwenye **Jedwali 10-19** hapa chini.

## Jedwali Na. 10-19: Changamoto za mfumo wa usimamizi wa fedha

| Na. | Changamoto | Na. | Changamoto |
|---|---|---|---|
| 1. | Mfumo unafanya kazi kama chombo cha kudhibiti matumizi ya fedha taslimu hivyo inapokea taarifa za fedha taslimu tu na kutotambua miamala isyohusisha fedha taslimu, hii inapelekea marekebisho kufanywa nje ya mfumo na hesabu za ujumla. | 2. | Mfumo hauna moduli ya madeni inayotumika, hivyo kupelekea Halmashauri kutotumia mfumo kwenye utambuzi wa madeni yanayooneshwa kwenye taarifa za fedha, hii inatoa viashiria vya kasoro na makosa |
| 3. | Mfumo hauna nyenzo zinazowezesha kuvuta taarifa za bajeti wenyewe kutoka kwenye mfumo wa PLANREP (mfumo wa kieletroniki unaotumika kuandaa bajeti) | 4. | Mpango wa manunuzi kwenye mfumo haufanyi kazi hivyo maombi na manunuzi yanayofanyika hayahusishwi na mpango wa manunuzi. |
| 5. | Utaratibu wa kutumia nukuu za bei kwa manunuzi na mikataba haufanyi kazi katika baadhi ya Halmashauri. | 6. | Hati za kurekebisha masurufu yanaidhinishwa nje ya mfumo na marejesho ya masurufu yanafanywa nje ya mfumo |
| 7. | Mfumo wa toleo la 9.05 haufanyi marekebisho hivyo wahasibu huwa wanasafiri hadi Dodoma kila mwisho wa robo mwaka ili kuandaa usuluhishi wa kibenki | 8 | Julai 2016, malipo yalifanywa kupitia akaunti ya amana kutokana na mfumo kuwa bado hautumiki baada ya kufungwa. |
| 9. | Inapotekea makosa wakati wa uhidhinishaji wa malipo inakuwa vigumu kuondoa orodha ya hati za malipo wakati wa marekebisho kwenye mfumo | 10. | Hati za malipo zinaweza kutoka bila kuwa na msimbo wa malipo, hali ambayo hairuhusiwi kwenye udhibiti wa mfumo |

| Na. | Changamoto | Na. | Changamoto |
|---|---|---|---|
| 11. | Mfumo hauruhusu kuchukua viambatisho vya malipo wakati malipo yanapofanyika | 12. | Mfumo kuchelewa kutoa taarifa inapohitajika kama vile usuluhishi wa kibenki. |
| 13. | Mfumo kushindwa kutambua miamala ambayo haijakamilika baada ya mwaka wa fedha kufika mwisho.<br>Hati za madai za miaka iliyopita haziwezi kutolewa ili kutoa marejeo kwa ajili ya malipo<br><br>Hii inazidi kumaanisha kuwa mfumo unafanya kazi kwenye mazingira ya miamala ya fedha taslimu tu | 14. | Masurufu, hati ya manunuzi zinaweza kutoka bila kufunga vifungu vya bakaa ya fedha, ikimaanisha kuwa kama masurufu au hati ya madai yanaweza kutoka lakini bado malipo mengine yanaendelea kufanyika |
| 15. | Mfumo bado hautoi taarifa za fedha, isipokuwa urari wa kihasibu | 16. | Mfumo pia huruhusu malipo kufanyika zaidi ya bajeti |

Changamoto za mfumo zimetokea kutokana na kutokuwapo kwa msaada sahihi na kwa wakati kutoka TAMISEMI pale mfumo unaposhindwa kufanya kazi kutokana na matatizo ya kiufundi; makosa ya binadamu; na vitendo visivyofaa kwenye mfumo.

Kwa maana hiyo, matatizo hayo ya kimfumo husababisha kadhia zifuatazo; madeni ya miaka iliyopita ambayo hayatambuliki hulipwa, masurufu huingizwa moja kwa moja kwenye vifungu vya matumizi, malipo yasiyostahili, mikopo isiyorejeshwa kwenye akaunti ya amana, matumizi kufanyika zaidi ya kiasi kilichowekwa, malipo kufanyika bila kuwa na idhini, kufanya manunuzi nje ya mpango wa manunuzi, malipo yasiyo na bajeti na kubadilishwa kwa matumizi ya fedha.

TAMISEMI ndiye msimamizi wa mfumo huu wa EPICOR, hivyo Halmashauri haziwezi kufanya chochote kuhusiana na uendeshaji wa mfumo. Kwa hiyo, ninapendekeza kwa menejimenti za Halmashauri, ikishirikiana na TAMISEMI na Hazina, kuainisha

mapungufu ya mfumo ili kuweza kupata thamani ya pesa katika mfumo huu pamoja kuimarisha usimamizi wa matumizi.

**10.19 Mapato ya ndani yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa katika shughuli za maendeleo kama bajeti ilivyoidhinishwa Sh. Tz 47,282,133,119**

Maelekezo maalum katika kifungu Na. 6(K) cha Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango Na Bajeti ya mwaka 2016/17 pamoja na uandaaji na utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano (Na. II) wa mwaka 2016/2017-2020/2022 yanazitaka Halmashauri kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya mapato yanapelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na Halmashauri zinapaswa kutoa taarifa ya mapato ya ndani kwenye fomu Na. 4 ya kitabu cha bajeti.

Katika sampuli ya Halmashauri 15, nimebaini kuwa mapato ya ndani yaliyokusanywa ya Sh.Tz. 112, 861,822,563, ambayo asilimia 60 yake ni sawa na Sh.Tz. 67,717,093,537 yalipaswa kuhamishiwa kwenda kwenye akaunti ya maendeleo ili kugharamia miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017. Hata hivyo, Halmashauri hizi zilipeleka kiasi cha Sh.Tz. 20,434,960,418 tu ambayo ni sawa na asilimia 30 ya jumla ya mapato ya ndani yaliyopaswa kuhamishwa; na kushindwa kupekeka Sh.Tz. 47,282,133,119 sawa na asilimia 70 kinyume na matakwa ya maelekezo hapo juu. Angalia Jedwali Na. 10-20.

**Jedwali Na. 10-20: Mapato ya ndani ambayo hayakupelekwa kutekeleza miradi ya maendeleo**

| Na. | Jina la Halmashauri | Makusanyo ya ndani bila kuweka ada za shule,fedha za mfuko wa Afya na kodi ya ardhi (Sh.Tz) | 60% ya mapato ya ndani (Sh.) | Kiasi kilichopelekwa katika shughuli za Maendeleo(Sh. Tz) | % | Kiwango ambacho hakikuwakilisha (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bagamoyo | 2,626,592,090 | 1,575,955,254 | 277,001,877 | 18 | 1,298,953,377 |
| 2 | H/W Buchosa | 956,631,000 | 573,978,600 | 29,184,500 | 5 | 544,794,100 |
| 3 | H/M Ilala | 48,060,029,920 | 28,836,017,952 | 12,965,000,000 | 45 | 15,871,017,952 |
| 4 | H/W Kibiti | 965,120,000 | 579,072,000 | - | 0 | 579,072,000 |
| 5 | H/M Kigamboni | 2,913,460,657 | 1,748,076,394 | 394,958,681 | 23 | 1,353,117,713 |
| 6 | H/W Kilosa | 2,283,979,062 | 1,370,387,437 | 192,008,720 | 140 | 1,178,378,716.96 |
| 7 | H/W Kilwa | 3,051,136,909 | 1,830,682,145 | 43,141,000 | 2 | 1,787,541,145 |
| 8 | H/M Kinondoni | 30,803,952,418 | 18,482,371,451 | 5,399,709,749 | 29 | 13,082,661,702 |
| 9 | H/M Lindi | 1,287,864,000 | 772,718,400 | 166,072,304 | 22 | 606,646,096 |
| 10 | H/W Magu | 1,322,708,229 | 793,624,937 | 202,701,549 | 26 | 590,923,388 |
| 11 | H/W Masasi | 1,471,105,000 | 882,663,000 | 107,322,000 | 12 | 775,341,000.00 |
| 12 | H/Mji Masasi | 1,883,691,658 | 1,130,214,995 | 3,800,000 | 0 | 1,126,414,995 |
| 13 | H/W Misungwi | 1,139,594,925 | 683,756,955 | 82,922,200 | 12 | 600,834,755 |
| 14 | H/W Mkuranga | 4,680,724,614 | 2,808,434,768 | 378,174,052 | 14 | 2,430,260,716 |
| 15 | H/M Ubungo | 9,415,232,081 | 5,649,139,249 | 192,963,786 | 3 | 5,456,175,463 |
| | **Jumla** | **112,861,822,563** | **67,717,093,537** | **20,434,960,418** | **30** | **47,282,133,119** |

Mapitio ya maagizo ya mgawanyo wa mapato ya ndani yanaonyesha kuwa, asilimia 60 ya makusanyo yote yanatakiwa kutumika kwenye shuguli za maendeleo, asilimia 20 kwa ajili ya gharama za kuendesha kata na vijiji; asilimia 10 kwa ajili ya mikopo kwa wanawake na vijana; na asilimia 10 kwa ajili ya shughuli nyingine za Halmshauri. Licha ya kwamba utekelezaji wa shughuli za maendeleo una vyanzo vingine, kwa maoni yangu, sioni uwezekano wa kutekelezeka kwa maagizo hayo kutokana na ukweli kwamba mapato ya ndani yanatumika kugharamia vikao vya Halmashauri, matumizi ya kawaida ya kila siku, matumizi ya dharura na matumizi mengine yanayopaswa kufanywa na Halmashauri kutokana na miongozo inayotolewa na ngazi za juu za Serikali.Huu ni uthibitisho dhahiri kwamba ruzuku ya matumizi

ya kawaida inayotolewa na Serikali kuu haitoshi kugharamia matumizi yote ya kawaida.

Ninashauri TAMISEMI kupitia upya asilimia zilizoainishwa za mgawanyo wa mapato ya ndani ili kuweka viwango ambavyo Halmashauri zitaweza kumudu na kutekeleza.

## 10.20 Mengineyo

### 10.20.1 Mapokezi Pungufu ya Fedha za Ruzuku za Shule Sh. 1,930,944,815

Tarehe 28 Desemba 2015 Serikali ilitoa miongozo ya utekelezaji wa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari. Ruzuku ya elimu inapaswa kutumika kwenye gharama za vitabu, vifaa vya kufundishia, vifaa elekezi, vifaa vya maabara na kemikali, ukarabati, kuongeza uwezo, usimamizi wa shughuli za shule ikijumuisha gharama za vifaa vya ofisi na chakula kama ikiwezeka.

Viwango vya malipo ya ruzuku hii vilivyowekwa na Serikali kwa kila mwanafunzi ni Sh. 6000 na 25,000 kwa shule za msingi na sekondari mtawalia; na fedha hizo zimekuwa zikipelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule. Hata hiyo, mapitio ya fedha za ruzuku zilizopokelewa ndani ya waka 2016/2017 yamebaini kuwa Sh.Tz 1,930,944,815 hazikupelekwa kwenye Halmashauri 28 kama mchanganuo wa mgawanyo wa ruzuku hiyo ulivyooneshwa kwenye **Kiambatisho 10:10** cha ripoti hii.

Serikali haitoi fedha za ruzuku za shule kulingana na namba za wanafunzi waliopo; na hivyo, shule zinashindwa kutekeleza baadhi ya shughuli zilizopangwa kama vile ununuzi wa vitabu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kufanya ukarabati na matengenezo madogo.

Ninapendekeza kwa Wizara husika kuanzisha mbinu itakayowezesha kugawa fedha mashuleni kulingana na idadi ya

wanafunzi waliopo ili kujenga mazingira mazuri ya kufundisha na kusomea na mwishowe kuongeza uwezo wa uelewa kwa wanafunzi.

### 10.20.2 Fedha zisizohamishwa kwenda idara husika Sh. 155,649,000

Serikali kuu ilitoa fedha kwa Mamlaka za Serikali za mitaa kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za kawaida. Fedha hizi zilipaswa kuhamishiwa kwenye akaunti za idara mbalimbali kama vile Elimu, Kilimo, Afya n.k

Hata hivyo, ukaguzi wangu umebaini kiasi cha Sh. 155,649,000 hakikuhamishwa kwenda kwenye akauti za idara husika kutoka kwenye akaunti ya matumizi ya kawaida kwenye Halmashauri mbili zinazooneshwa kwenye Jedwali Na. 10-21 japa chini:-

**Jedwali Na. 10-21: Fedha zisiohamishwa kwenda idara husika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Akaunti ya Idara husika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Buchosa | Elimu na Afya | 89,078,000 |
| 2. | H/W Karagwe | Elimu na Afya | 66,571,000 |
| | | **Jumla** | **155,649,000** |

Kushindwa kuhamisha fedha kumetokana na kutokuwa na udhibiti wa ndani imara kwenye usimamizi wa rasilimali fedha. Pia hali hii inaweza kuwa imeathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutokana na kukosekana kwa fedha.

Ninapendekeza kwa Halmashauri husika kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kulingana na miongozo inayotolewa; na kuhakikisha fedha za matumizi ya kawaida zinahamishwa kwenda kwenye akaunti husika ili kutekeleza shughuli zilizokusudiwa

# SURA 11

## 11.0 USIMAMIZI WA MAPATO

Usimamizi wa mapato unajumuisha shughuli zote ambazo lengo lake kubwa ni kuhakikisha kuwa mapato yote ya serikali kutoka vyanzo mbalimbali yanafanyiwa tathmini sahihi, yanakusanywa kikamilifu na kutolewa taarifa kwa usahihi. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, usimamizi wa mapato hufanywa kwa kufuata sheria ndogo na kanuni za mapato kutoka ya OR-TAMISEMI, matumizi ya mbinu na taratibu sahihi, na uimarishwaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani. Kwa kuwa sio rahisi kwa Serikali Kuu kutimiza mahitaji yote ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kama yalivyoainishwa katika bajeti zao, ni muhimu kwa Mamlaka hizo kukusanya fedha za kutosha kwa kutumia mbinu sahihi za usimamizi wa mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu katika kuendesha shughuli zake. Katika tathmini ya mwaka huu, nimebaini mambo mbalimbali yanayohusiana na usimamizi wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:

## 11.1 Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuwasilishwa na Mawakala Sh.Tz. 3,538,329,470

Kutokana na upungufu wa nguvukazi, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikasimu ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vyake mbalimbali kwa mawakala ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 20, nilibaini kuwa makusanyo ya mapato yenye jumla ya Sh.Tz 3,538,329,470 hayakuwasilishwa na Mawakala kama Jedwali Na. 11.1 linavyoonesha:

**Jedwali Na. 11-1: Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuwasilishwa na Mawakala**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bariadi | 77,141,490 | 12 | H/W Makete | 112,425,378 |
| 2 | H/W Buchosa | 83,834,000 | 13 | H/W Mbogwe | 82,133,300 |

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | H/W Bukombe | 4,987,222 | 14 | H/W Mbulu | 13,000,000 |
| 4 | H/M Dodoma | 49,210,611 | 15 | H/W Meatu | 27,843,157 |
| 5 | H/M Ilemela | 848,496,101 | 16 | H/W Msalala | 7,900,000 |
| 6 | H/W Kalambo | 118,379,800 | 17 | H/W Muheza | 59,598,139 |
| 7 | H/M Kigoma/Ujiji | 709,944,308 | 18 | H/W Njombe | 454,659,030 |
| 8 | H/W Kiteto | 448,895,600 | 19 | H/W Sengerema | 13,639,250 |
| 9 | H/M Lindi | 5,076,800 | 20 | H/W Tabora | 163,784,000 |
| 10 | H/Mji Mafinga | 3,904,500 | | **Jumla** | **3,538,329,470** |
| 11 | H/Mji Makambako | 253,476,784 | | | |

Kutowasilishwa kwa makusanyo kutoka kwa mawakala kumesababishwa na usimamizi dhaifu wa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa; baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zina vifungu katika mikataba yao vinavyotoa muda wa kutathmini utendaji wa mawakala na kutatua changamoto zinazoweza kujitokeza, lakini kinyume chake, tathmini ya utendaji wa mawakala haikufanyika. Vipengele vingine vya mikataba ambavyo havikutekelezwa vinahusu adhabu kwa kuchelewesha makusanyo, uwasilishaji wa amana ambayo ni sawa na makusanyo ya miezi mitatu ya awali, udhamini wa benki au mwingineo ambao Mamlaka husika inaona unafaa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika hazikufanya ufuatiliaji hali iliyosababisha mawakala kutumia mwanya huo kukwepa kulipa madeni yao ya mapato.

Mwenendo wa mawakala ambao hawakuwasilisha mapato yao katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne (4) mfululizo imeonyeshwa katika Jedwali Na. 11-2

**Jedwali Na. 11-2: Mwenendo wa makusanyo ya mapato ambayo hakuwasilishwa na mawakala kwa miaka minne mfululizo**

| Mwaka wa Fedha | Kiasi kisichowasilishwa (Sh.Tz) | % Ongezeko/Upungufu |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 3,538,329,470 | 41 |
| 2015/2016 | 6,035,897,217 | 14 |
| 2014/2015 | 5,304,191,115 | 10 |
| 2013/2014 | 4,843,414,724 | -28 |

Jedwali Na.11.2 linaonesha tatizo la makusanyo ya mapato ambayo hayakuwasilishwa na mawakala kumepungua kwa asilimia 41 katika mwaka wa fedha 2016/2017 ikilinganishwa na mwaka 2015/2016.

Kutokana na changamoto zilizoonekana hapo juu, nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha mifumo wa udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato. Hii ni pamoja na kuboresha utaratibu wa uingiaji mikataba na mawakala na kufanya ufuatiliaji wa makusanyo kwa mawakala. Aidha, Mamlaka hizo ziongeze nguvu katika usimamizi wa makusanyo yanayofanywa na mawakala ikiwa ni pamoja na kuwafanyia tathmini ya kiutendaji kila baada ya kipindi maalum ili kama kuna matatizo katika ukusanyaji yatatuliwe mapema. Aidha, ninasisitiza utekelezaji wa Agizo la 38 (3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009; pia makusanyo yote yawasilishwe mara moja.

## 11.2 Usimamizi usiojitosheleza wa mawakala wa kukusanya mapato kutoka OR-TAMISEMI

Mwawakala ya kukusanya mapato wanakusanya mapato kwa niaba ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kupata kamisheni kutokana na mapato yaliyokusanywa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanya maboresho katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato toka vyanzo vyake.

Faida za kukasimisha ukusanyaji wa mapato, zinaweza kuonekana tu endapo kutakuwa na udhibiti na ufuatijiaji wa karibu wa mawakala ili kupunguza uwezekano wa mawakala kutumia mianya iliyobainika kukusanya mapato mengi na kuwasilisha kidogo. OR – TAMISEMI ina wajibu wa kutoa maelekezo ya namna bora ya kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kukasimisha ukusanyaji kwa mawakala.

Nimefanya mapitio ya taratibu za ufuatiliaji na udhibiti wa mawakala wa kukusanya mapato na kubaini mianya mbalimbali kama ifuatavyo:

- **Kukosekana kwa mwongozo wa usimamizi wa makusanyo kwa kutumia mawakala kutoka OR-TAMISEMI hali iliyopelekea kutokuwa na mikataba inayofanana.**
  Nilifanya mapitio ya mikataba kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na mawakala na kubaini kwamba baadhi inatoa kamisheni ya asilimia 30 wakati mingine inatoa asilimia 20 ya mapato yaliyokusanywa. Baadhi ya mikataba ilikuwa na vipengele/vifungu maalum vya adhabu kwa wakala endapo atashindwa ama kuchelewa kuwasilisha makusanyo kwa wakati, ilhali mikataba mingine haikuwa na vipengele hivyo.

- **Kutofanyika kwa upembuzi yakinifu, wa mapato yanayoweza kupatikana kutoka vyanzo vya mapato haukufanywa.**
  Viwango vya mapato vilivyo katika mikataba vimetokana na taarifa za makusanyo halisi ya miaka ya nyuma badala ya kufanya tahmini ya hali halisi ya chanzo cha mapato katika kipindi husika. Hali hii inaweza kupelekea wakala kupata mapato mengi kuliko inayopata Mamlaka ya Serikali za Mtaa husika.

- Aidha, katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hapakuwa na usimamizi na ufatiliaji wa karibu ikiwa ni pamoja na tathmini ya utendaji na ufuatiliaji wa mawakala wa kukusanya mapato ili kuhakikisha kwamba wametekeleza majukumu yao ipasavyo kwa maslahi ya Mamlaka husika.Kwa mfano, H/Wilaya ya Mbarali

haikuingia mikataba na mawakala wa mapato hali inayotia shaka ni kwa namna gani inawasimamia mawakala wake.

- Agizo la 38(3) la Memoranda ya Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoamua kukasimisha ukusanyaji wa mapato kwa mawakala, kuwataka mawakala aidha kuweka dhamana ya mapato isiyopungua makusanyo ya miezi mitatu, udhamini wa benki, au dhamana yoyote inayokubalika. Kinyume chake baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikudai malipo ya awali ya makusanyo ya miezi mitatu, dhamana ya benki, au hati ya dhamana ama amana yoyote ile ambayo Mamlaka za Serikali za Mitaa ingeona inafaa. Hali hii inaweza kuzisababishia hasara Mamlaka hizo endapo mawakala hawatawasilisha mapato waliyokusanya.

Naishauri serikali kupitia OR-TAMISEMI kurekebisha hali ya sasa kwa kuandaa mkataba ambao utatumika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote ili kuleta ulinganifu; kufanyika kwa upembuzi yakinifu katika vyanzo vyake badala ya kutegemea takwimu za miaka ya nyuma; na Mawakala kuwasilisha dhamana isiyopungua makusanyo ya miezi mitatu, udhamini wa benki, au dhamana yoyote inayokubalika.

## 11.3 Vitabu vya Makusanyo ya Mapato kutowasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi

Agizo la 34 (6)&(7) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linawataka maafisa wote waliopewa vitabu vya kukusanya mapato wawasilishe taarifa ya vitabu vilivyotumika na vile ambavyo havijatumika kila mwisho wa mwezi. Endapo kuna upotevu wowote wa vitabu, itolewe taarifa mapema iwezekanavyo kwa Afisa Masuuli ambaye atatoa taarifa polisi.

Wakati wa ukaguzi wa mapato, jumla ya vitabu 379 vya kukusanyia mapato havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na Mamlaka za Serikali za Mitaa 21 licha ya kuombwa kufanya hivyo.

Kutokana na kukosekana kwa vitabu hivyo vya makusanyo, nilishindwa kuthibitisha kiasi kilichokusanywa mwaka huu kupitia vitabu hivyo ambavyo havikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi.

Mwenendo wa vitabu ambavyo havikuonekana wakati wa ukaguzi kwa miaka minne mfululizo ni kama ilivyooneshwa katika jedwali Na. 11.3 hapa chini.

**Jedwali Na. 11-3: Mwenendo unaoonesha vitabu ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi kwa miaka minne mfululizo**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | Idadi ya vitabu vilivyo kosekana | Asilimia (%) Kuongezeka/Kupungua |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 21 | 379 | 57 |
| 2015/2016 | 57 | 871 | 7 |
| 2014/2015 | 45 | 814 | 72 |
| 2013/2014 | 47 | 474 | -62 |

Jedwali Na.11.3 linaonesha kupungua kwa idadi ya vitabu ambavyo havikuonekana wakati wa ukaguzi kwa tofauti ya vitabu 492 kati ya mwaka 2015/2016 mpaka mwaka 2016/2017. Maelezo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo vitabu vya mapato havikuonekana ni kama ilivyooneshwa katika
Jedwali Na. **11-4** hapa chni.

**Jedwali Na. 11-4: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye vitabu vilivyokosekana**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya Vitabu vya risiti | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya Vitabu vya risiti |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Madaba | 5 | 12 | H/W Longido | 22 |
| 2 | H/W Busega | 1 | 13 | H/W Bumbuli | 2 |
| 3 | H/W Geita | 2 | 14 | H/Mji Mbulu | 2 |
| 4 | H/W Mbogwe | 50 | 15 | H/W Bahi | 78 |
| 5 | H/W Bunda | 6 | 16 | H/Mji Kondoa | 30 |
| 6 | H/W Rorya | 2 | 17 | H/W Kigoma | 16 |
| 7 | H/W Misungwi | 36 | 18 | H/W Nanyumbu | 2 |

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya Vitabu vya risiti | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya Vitabu vya risiti |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | H/W Ukerewe | 6 | 19 | H/W Siha | 27 |
| 9 | H/W Biharamulo | 71 | 20 | H/W Karatu | 6 |
| 10 | H/W Bukoba | 2 | 21 | H/W Mufindi | 3 |
| 11 | H/W Missenyi | 10 | | **Jumla** | **379** |

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuvitafuta vitabu vyote ambavyo havikuonekana wakati wa ukaguzi, na viwasilishwe ofisini kwangu kwa uhakiki. Kwa msisitizo mkubwa, nashauri ofisi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutii Agizo la 34 (6) na (7) la Memoranda ya Fedha katika Serikali za Mitaa, 2009. Pia, nasisitiza kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kupunguza mianya ya ubadhirifu katika ukusanyaji wa mapato.

## 11.4 Kutokutolewa kwa leseni ndogo kwa wakandarasi wajenzi/washauri Sh.Tz. 97,650,000

Aya ya 8 ya Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972 (iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2014) inawataka wakandarasi wajenzi/washauri ambao wamepewa kazi za ujenzi katika maeneo tofauti na makazi yao ya kibiashara wapatiwe leseni ndogo za kuwawezesha kufanya kazi katika maeneo hayo.

Katika ukaguzi wa mwaka 2016/17, nimegundua kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa tatu (3) zilitoa kazi za ujenzi wa barabara kwa wakandarasi wajenzi/washauri wanaotoka nje ya Mamlaka zao bila kuwapatia leseni ndogo za kufanya kazi katika maeneo yao. Matokeo yake jumla ya Sh.Tz 97,650,000 ambazo zingetokana na ada za leseni hizo hazikukusanywa kama Jedwali Na.11.5 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 11-5: Leseni za biashara ambazo hazikukusanywa**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Babati | 45,050,000 |
| 2 | H/Mji Babati | 7,000,000 |
| 3 | H/W Simanjiro | 45,600,000 |
| **Jumla** | | **97,650,000** |

Kushindwa kutoa leseni za biashara ni ishara kwa Mamlaka husika kutofuatilia wakandarasi wa nje wanaotekeleza miradi katika maeneo yao ya kiutawala.

Ninashauri Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa wakandarasi wote wanaotoka nje wanatozwa ada ya leseni ndogo za kufanya kazi. Katika maeneo ya Mamlaka husika. Aidha, zihakikishe kiasi chote kinachodaiwa kinakusanywa kutoka kwa wakandarasi.

## 11.5 Kuchelewa Kupeleka Maduhuli Benki Sh. Tz 296,798,267

Mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali yanatakiwa yawasilishwe benki mara moja kwa sababu za kiusalama.

Agizo la 37(3) na 38(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 inamtaka mtunza fedha kuhakikisha anapeleka benki kwa wakati maduhuli yote yaliyokusanywa. Pia, mweka hazina anatakiwa kuweka taratibu sahihi za kifedha na kihasibu ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na taarifa sahihi za makusanyo yote ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ukusanyaji sahihi wa mapato, utunzaji salama wa mapato hayo pamoja na kupeleka benki kwa wakati makusanyo yote.

Kinyume chake, nilibaini jumla ya Sh.Tz 296,798,267 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 21 ambazo zilikusanywa lakini hazikupelekwa benki kwa wakati kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 11-6 hapo chini.

**Jedwali Na. 11-6: Maduhuli ambayo hayakupelekwa Benki kwa wakati Sh.Tz 296,798,267**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/J Arusha | 6,888,400 | 12 | H/W Lushoto | 3,994,000 |
| 2 | H/W Buchosa | 16,223,828 | 13 | H/W Madaba | 8,867,020 |
| 3 | H/W Bukombe | 24,916,401 | 14 | H/W Magu | 12,945,300 |
| 4 | H/W Bumbuli | 8,516,600 | 15 | H/W Mkalama | 11,451,600 |

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | H/W Bumbuli | 8,516,600 | 16 | H/W Monduli | 18,287,340 |
| 6 | H/Mji Kahama | 30,552,600 | 17 | H/W Muheza | 4,366,000 |
| 7 | H/W Karatu | 7,801,992 | 18 | H/W Ngorongoro | 14,752,800 |
| 8 | H/W Karatu | 7,801,992 | 19 | H/Mji Tunduma | 21,729,400 |
| 9 | H/W Kwimba | 2,555,000 | 20 | H/W Tunduru | 10,265,348 |
| 10 | H/W Liwale | 1,975,400 | 21 | H/W Ukerewe | 70,396,646 |
| 11 | H/W Longido | 3,994,000 | | **Jumla** | **296,798,267** |

Kuna uwezekano wa watumishi wasio waaminifu kuzitumia pesa zilizokusanywa kabla ya kuzipeleka benki, hivyo kupelekea matumizi yasiyoridhisha ya fedha hizo.

Napendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato yake kupitia mfumo wa Mapato (LGRCIS). Aidha, mifumo ya udhibiti wa ndani iimarishwe ili kudhibiti mapato yanapokusanywa kama ilivyoagizwa katika Agizo la 37 (3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009.

## 11.6 Kutokuwapo kwa Madaftari ya Kumbukumbu ya Mapato

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuwa na daftari la kumbukumbu ya mapato ili kutunza taarifa sahihi za mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali na pia, daftari hilo kutumika kufanya makadirio ya makusanyo.

Tathmini niliyofanya mwaka huu ili kujua ufanisi wa taratibu zinazotumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukusanya mapato, hasa ya ndani, imebaini kuwa jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 20 hazikuwa na madaftari ya kutunza kumbukumbu za ukusanyaji mapato au zilikuwa hazihuishi taarifa za madaftari hayo. Hii ni kinyume na Agizo la 23 (3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.11.7

**Jedwali Na. 11-7: Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zisizo na Daftari la mapato**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Biharamulo | 11 | H/W Kibaha |
| 2 | H/W Busega | 12 | H/W Kishapu |
| 3 | H/W Chalinze | 13 | H/W Kwimba |
| 4 | H/Mji Handeni | 14 | H/W Madaba |
| 5 | H/W Igunga | 15 | H/W Mkalama |
| 6 | H/W Igunga | 16 | H/J Mwanza |
| 7 | H/M Ilala | 17 | H/W Sengerema |
| 8 | H/M Ilala | 18 | H/M Tabora |
| 9 | H/M Ilemela | 19 | H/J Tanga |
| 10 | H/W Kibaha | 20 | H/W Ukerewe |

Kutokuwapo na daftari ya kumbukumbu ya mapato kumefanya nishindwe kijiridhisha na usahihi wa mapato yaliyokusanywa, kama vile kodi ya majengo, kodi ya huduma na ushuru wa mabango.

Ninapendekeza kwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe zinaboresha mfumo wa udhibiti wa ndani wa usimamizi wa kumbukumbu za mapato na Waweka Hazina wa Wilaya wanawajibika kusimamia kuanzishwa na kutunza vizuri madaftari ya kumbukumbu za makusanyo kama Agizo la 23 (3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 linavyoelekeza.

## 11.7 Fedha ambazo hazikukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani Sh.Tz 12,191,753,218

Ili kupunguza utegemezi wa fedha toka serikali kuu, pamoja na msukumo kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuongeza mapato na kupunguza gharama za ukusanyaji mapato ili ziweze kutekeleza bajeti inayotakiwa kutekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani; zinatakiwa kuunda mpango mkakati wa ukusanyaji mapato ili ziweze kukusanya mapato yanayotarajiwa kwa wakati na kwenye vyanzo vyake vyote. Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini Mamlaka za Serikali za Mitaa 32 hazikukusanya kikamilifu mapato yaliyotarajiwa kutoka katika vyanzo vyake vyote vilivyopo.

Mwenendo wa mapato ya ndani yasiyokusanywa kwa miaka miwili mfululizo umeoneshwa katika Jedwa Na.11-8

**Jedwali Na. 11-8: Fedha ambazo hazikukusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 32 | 12,191,753,218 |
| 2015/2016 | 91 | 21,130,364,482 |

Maelezo ya kina kwa mapato ambayo hayakukusanywa kwa kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa imeoneshwa katika **Kiambatisho 11:1** cha taarifa hii.

Ninapendekeza kwamba, uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuimarisha na kuboresha usimamizi wa mapato ili kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kuhakikisha wadau wote wanafuata sheria na kanuni katika suala hili. Aidha, nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato kikamilifu kutoka vyanzo vyote vilivyopo ndani ya mamlaka zao ili kufikia malengo waliojiwekea na kupunguza kiwango cha utegemezi kutoka Serikali Kuu katika kugharamia miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida.

## 11.8 Maduhuli Yaliyokusanywa bila ya udhibitisho wa kupelekwa Benki Sh.Tz 2,411,293,357

Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kupeleka benki maduhuli yote yaliyokusanywa kila siku ama siku ya kazi inayofuata. Agizo hili linasaidia kuepukana na ushawishi wa kutumia maduhuli hayo kwa shughuli ambazo hazikupangwa.

Katika ukaguzi, nimebaini kuwa kiasi cha Sh.Tz 2,411,293,357 kilichokusanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 39 hakikuthibitishwa kupelekwa benki kinyume na matakwa ya Agizo lililotajwa hapo juu kama ilivyo katika Jedwali Na.11.9 hapo chini.

**Jedwali Na. 11-9: Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki**

| Na. | Jina la Mamlaka za Serikali za Mitaa | Kiasi (Sh.Tz) | Na. | Jina la Halmashuri | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Busokelo | 3,396,146 | 21 | H/W Arusha | 23,388,000 |
| 2 | H/W Chunya | 9,000,000 | 22 | H/W Rombo | 13,330,000 |
| 3 | H/W Ileje | 4,143,300 | 23 | H/Mji Handeni | 2,767,900 |
| 4 | H/W Mbozi | 6,384,681 | 24 | H/W Babati | 1,247,500 |
| 5 | H/W Iringa | 2,428,763 | 25 | H/Mji Mbulu | 1,304,000 |
| 6 | H/M Iringa | 4,637,244 | 26 | H/W Mpwapwa | 1,638,000 |
| 7 | H/W Kilolo | 151,898,371 | 27 | H/Mji Kondoa | 4,358,300 |
| 8 | H/Mji Mafinga | 2,113,730 | 28 | H/M Singida | 2,016,000 |
| 9 | H/W Geita | 55,474,773 | 29 | H/W Iramba | 64,653,188 |
| 10 | H/W Mbogwe | 1,942,000 | 30 | H/W Manyoni | 5,509,121 |
| 11 | H/W Musoma | 3,756,000 | 31 | H/W Itigi | 6,017,000 |
| 12 | H/J Mwanza | 40,954,086 | 32 | H/W Buhigwe | 5,970,140 |
| 13 | H/M Ilemela | 847,953,399 | 33 | H/W Kigoma | 14,018,125 |
| 14 | H/W Kwimba | 4,854,850 | 34 | H/W Igunga | 690,000 |
| 15 | H/W Misungwi | 140,210,359 | 35 | H/W Tabora | 7,835,000 |
| 16 | H/W Buchosa | 52,387,910 | 36 | H/W Sikonge | 10,912,824 |
| 17 | H/W Ukerewe | 541,391,000 | 37 | H/W Kibaha | 18,591,498 |
| 18 | H/W Karagwe | 89,816,500 | 38 | H/W Kilombero | 96,793,130 |
| 19 | H/W Ngara | 134,690,850 | 39 | H/W Nanyumbu | 25,655,669 |
| 20 | H/W Missenyi | 7,164,000 | | **Jumla** | **2,411,293,357** |

Kutokana na kukosekana kwa taarifa za kupeleka maduhuli benki, sikuweza kujua uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha

mapato ya ndani kilichoripotiwa katika taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

Ninapendekeza kwa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 kwa kuhakikisha kuwa mifumo ya udhibiti wa ndani katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato inaboreshwa na pia makusanyo ambayo hakupelekwa benki yapelekwe mara moja.

## 11.9 Mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa mapato Sh. Tz 17,559,093,875

Uimarishwaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni muhimu sana katika kudhibiti mianya inayoweza kusababisha ubadhirifu wa fedha za Serikali. Agizo la 8(2) (f) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 linawataka Watunza Hazina wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuna mfumo madhubuti ambao unajumuisha uandishi na mapitio ya mara kwa mara ya taratibu za fedha.

Wakati wa Ukaguzi nilibaini mapungufu mengi yanayohusu mfumo wa udhibiti wa ndani unaohusiana na makusanyo ya mapato. Nayo ni; kutokuwapo kwa uwiano kati ya pesa inayokusanywa na pesa iliyowekwa benki, pamoja na kutofautiana kwa hati za madai zinazotolewa na mfumo ambazo huonesha kiasi kikubwa wakati kiasi kilichopokelewa benki ni kidogo. Mengine ni miamala ya mfumo kutokuwa na vifungu vinavyoendana na leja, makusanyo kukusanywa na kutumika kabla ya kwenda benki, makusanyo ambayo hayakuhamishwa kutoka MAXICOM kwenda LGRCIS, na kutokuandaliwa taarifa za usuluhisho wa kibenki katika akaunti ya mapato. Mapungufu haya yote yaliyobainika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 24 yana jumla ya Sh. Tz 17,559,093,875 na yamefafanuliwa katika **Kiambatisho 11:2**

Mapungufu haya yanaashiria udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa mapato. Aidha, yanatengeneza mianya ya ubadhirifu wa mapato hayo.

Napendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato ili kuweza kubaini mianya ya wizi na ubadhirifu mapema na kuchukua hatua stahiki haraka.

## 11.10 Makusanyo ya Kodi ya Matumizi ya Ardhi ambayo haikuwasilishwa Wizara Ardhi Sh. Tz 646,735,470

Waraka Na.CBD 171/261/01/148 wa tarehe 19/11/2012 unazipa uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya kodi za ardhi na kuziwasilisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi kupitia akaunti No.2011000025 iliyopo katika benki ya NMB kabla ya tarehe 5 ya kila mwezi unaofuata.

Katika ukaguzi wa mwaka huu huu nilibaini kuwa jumla ya Sh. Tz 646,735,470 zilizokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 4 hazikurejeshwa Wizarani.

Kutokurejeshwa kwa kodi za ardhi katika muda muafaka kunaweza kusababisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia fedha hizo kwa shughuli ambazo hazikupangwa. Maelezo ya fedha ambazo hazijapelekwa katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi ni kama inavyoonekana katika **Error! Reference source not found.** hapa chini.

**Jedwali Na. 11-10: Orodha ya Makusanyo ya ardhi yasiyopelekwa Wizarani**

| Na | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Arusha | 62,957,667 |
| 2 | H/Mji Babati | 311,338,204 |
| 3 | H/Mji Geita | 72,930,107 |
| 4 | H/W Karatu | 199,509,492 |
| **Jumla** | | **646,735,470** |

Mwenendo wa kodi ya Ardhi iliyokusanywa lakini haikuwasilishwa wizarani kwa miaka miwili mfululizo kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.11-11 hapo chini.

**Jedwali Na. 11-11: Mwenendo wa kodi iliyokusanywa bila kuwasilishwa Wizarani**

| Na | Idadi ya Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Kiasi (Sh.Tz) |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 4 | 646,735,470 |
| 2015/2016 | 11 | 314,180,584 |

Ninashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa zipeleke fedha zote zilizokusanywa kama kodi ya ardhi kwa Wizara ya Ardhi na kuhakikisha siku zijazo zinatekeleza kikamilifu Waraka no. CBD.171/261/01/148 wa 19/11/2012.

## 11.11 Kodi ya Huduma Isiyokusanywa kutoka Kampuni 98

Vifungu Na. 6(1)(n) na 7(1)(a) vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982, iliyorekebishwa mwaka 2000 inataja kodi ya huduma kuwa ni fedha zinazopatikana kutokana na ada kwa kampuni zinazotoa huduma kwa kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mapato ya jumla. Hivyo ni lazima kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya ada ya huduma kwa kampuni zilizopo ndani ya maeneo ya mamlaka husika.

Katika tathmini niliyoifanya nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nane hazikukusanya tozo hizo kutoka kwa kampuni 98 ambazo zipo katika maeneo ya Mamlaka hizo kama inavyoonekna katika Jedwali Na.11-12 hapa chini.

**Jedwali Na. 11-12: Orodha ya idadi ya kampuni zisizokusanya kodi ya huduma**

| Na | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya Kampuni |
|---|---|---|
| 1 | H/W Arusha | 9 |
| 2 | H/W Kakonko | 6 |
| 3 | H/W Karatu | 6 |
| 4 | H/W Kibaha | 25 |

| Na | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya Kampuni |
|---|---|---|
| 5 | H/Mji Kibaha | 20 |
| 6 | H/W Manyoni | 2 |
| 7 | H/J Tanga | 25 |
| 8 | H/W Ushetu | 5 |
| **Jumla** | | **98** |

Kutokukusanywa kwa tozo ya huduma kumesababisha kupotea kwa mapato ya Mamlaka za serikali za Mitaa husika ambapo fedha hizo zingetumika kwenye huduma za kijamii. Aidha, hali hii ilichangia kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka hizo kwa mwaka husika.

Kwa kuwa lengo kuu la Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kutoa huduma kwa jamii, ninashauri Mamlaka hizo kuweka mikakati madhubuti itakayoziwezesha kukusanya tozo ya huduma kutoka kwa kampuni zote za biashara zinazopashwa kulipa tozo hiyo.

## 11.12 Ukosefu wa Sheria Ndogondogo za Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Kifungu cha 80 cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2006 na Kifungu cha 148 cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) iliyorekebishwa mwaka 2006 vinatoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kutunga sheria ndogondogo zitakazowasaidia kutimiza malengo yao ya kukusanya ushuru mbalimbali katika mamlaka zao kwa ufanisi.

Katika ukaguzi uliofanyika, niliweza kubaini jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 11 ambazo hazikuwa na sheria ndogo za kuwawezesha kupata mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali kama vile minara ya simu kama ilivyoonekana katika Jedwali Na.11.13 hapa chini:

**Jedwali Na. 11-13: Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zisizokuwa na sheria ndogo za mapato**

| Na | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa |
|---|---|
| 1 | H/W Bumbuli |
| 2 | H/W Chalinze |

| Na | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa |
|---|---|
| 3 | H/Mji Kibaha |
| 4 | H/W Kibiti |
| 5 | H/W Mbulu |
| 6 | H/W Monduli |
| 7 | H/W Mwanga |
| 8 | H/W Rufiji |
| 9 | H/W Rungwe |
| 10 | H/W Same |
| 11 | H/Mji Tunduma |

Kutokuwepo kwa sheria ndogo kwa aina fulani ya mapato inaashiria kuwa vyanzo vingi vya mapato havikusanywi ipasavyo hivyo Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kushindwa kufikia malengo ya msingi ya utoaji huduma kwa jamii.

Hivyo basi, bado kuna haja ya mamlaka hizo kupanua wigo wa ukusanyaji mapato kwa kuanzisha sheria ndogo kupitia OR-TAMISEMI ambazo zitawawezesha kuongeza mapato yao ya ndani.

## 11.13 Mapungufu katika Mfumo Kukusanya Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Matumizi ya njia za kawaida katika kukusanya mapato kama vile stakabadhi za kuandika kwa mkono na rejesta ya vitabu vya mapato umesababisha uwepo wa mianya ya upoteaji wa mapato na kuchelewa kuwasilisha benki maduhuli yaliyokusanywa hivyo kuathiri Mamlaka husika kutoa huduma za kijamii. Hali hii ilichangia kuanzishwa kwa mfumo wa kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kieletroniki (LGRCIS). Miongoni mwa malengo ya mfumo huu ni kuzuia upotevu wa mapato, kuweka uwazi katika ukusanyaji wa mapato, kusaidia utoaji wa taarifa kamili na uchambuzi kulingana na eneo husika, walipa kodi, ama aina ya mapato. Pia mfumo huu unalenga kusaidia na kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa taratibu za malipo, ukisaidiwa na Mfumo wa Mawasiliano wa Kijiografia(GIS).

Mbali na ukweli kwamba mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kieletroniki (LGRCIS) una moduli zinazoongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato na una mifumo madhubuti ya udhibiti ambayo inahakikisha usalama wa mapato yanayokusanywa, bado kuna dosari mbalimbali katika mfumo huu. Mamlaka za Serikali za Mitaa 61 zilizobainika kuwa na mapugufu zimeonyeshwa katika Jedwali 11.14 hapa chini.

**Jedwali Na. 11-14: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye mfumo wa LGRCIS usio na Ufanisi**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Arusha | 22 | H/W Kakonko | 42 | H/W Mbulu |
| 2 | H/W Babati | 23 | H/W Kaliua | 43 | H/W Meatu |
| 3 | H/Mji Babati | 24 | H/W Karagwe | 44 | H/W Missenyi |
| 4 | H/W Bagamoyo | 25 | H/W Karatu | 45 | H/W Misungwi |
| 5 | H/W Bahi | 26 | H/Mji Kibaha | 46 | H/W Mkuranga |
| 6 | H/Mji Bariadi | 27 | H/M Kigamboni | 47 | H/W Monduli |
| 7 | H/W Biharamulo | 28 | H/W Kigoma | 48 | H/W Mpwapwa |
| 8 | H/W Bukoba | 29 | H/W Kilombero | 49 | H/W Muleba |
| 9 | H/M Bukoba | 30 | H/W Kilosa | 50 | H/J Mwanza |
| 10 | H/W Bumbuli | 31 | H/W Kiteto | 51 | H/W Nanyumbu |
| 11 | H/W Busega | 32 | H/W Kwimba | 52 | H/W Ngara |
| 12 | H/W Busokelo | 33 | H/W Kyela | 53 | H/W Rungwe |
| 13 | H/W Chamwino | 34 | H/W Kyerwa | 54 | H/W Sengerema |
| 14 | H/W Chemba | 35 | H/W Longido | 55 | H/W Shinyanga |
| 15 | H/W Chunya | 36 | H/W Ludewa | 56 | H/M Sumbawanga |
| 16 | H/Mji Handeni | 37 | H/W Manyoni | 57 | H/M Temeke |
| 17 | H/W Igunga | 38 | H/W Mbarali | 58 | H/Mji Tunduma |
| 18 | H/W Ileje | 39 | H/J Mbeya | 59 | H/W Ukerewe |
| 19 | H/M Ilemela | 40 | H/W Mbeya | 60 | H/W Urambo |
| 20 | H/W Iramba | 41 | H/W Mbozi | 61 | H/W Wang'ing'ombe |
| 21 | H/Mji Kahama | | | | |

- LGRCIS ina moduli inayoruhusu kufanya usuluhisho/upatanisho wa taarifa za mapato yaliyokusanywa kupitia mfumo huo na yale yaliyopelekwa kwenye akaunti ya

benki, lakini hapakuwa na ushahidi wowote wa kufanyika upatanisho/usuluhisho wa kila mwezi wa taarifa hizo katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- Baadhi ya marekebisho yaliyofanyika katika hati za madai hayakuripotiwa kwa usahihi ili kuonesha viwango vipya vilivyopitishwa.
- Baadhi ya stakabadhi zilizotolewa na mfumo huu hazikuonekana kwenye daftari la fedha. Aidha, kiasi kilichoripotiwa kwenye stakabadhi hizo hakijulikani.
- Kutokana na changamoto ya upatikanaji wa intaneti na mtandao wa simu katika baadhi ya vijiji, husababisha ugumu kwa wakusanya mapato katika utendaji wao hivyo kulazimika kutunza pesa kwa mda mrefu bila kuzipeleka Benki.
- Katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo katika kipengele cha ardhi yanafanyika nje ya mfumo wa kieletronic (LGRCIS).
- Baadhi ya vyanzo vya mapato bado vinakusanywa kwa kutumia stakabadhi za kawaida kutokana na upungufu/uhaba wa mashine za kukusanyia mapato za kieletroniki ili kufikia maeneo yote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Baadhi ya maeneo katika serikali za mitaa, ukusanyaji ulifanyika bila kutenganisha majukumu; mfano mhasibu alipewa jukumu la kuomba kufanya marekebisho na wakati huohuo alipewa jukumu la kuidhinishamarekebisho hayo; hii ni tofauti na miongozo ya fedha inavyotaka, anayeomba anatakiwa awe tofauti na anaye idhinisha.
- Kutokutunzwa kwa taarifa za msingi za wateja katika mfumo kwa ajili ya utambuzi, mteja mmoja anaweza kuwa na namba zaidi ya moja na pia hakuna kizuizi kwa watumishi wa serikali za mitaa katika kutengeneza namba za utambuzi katika mfumo.
- Katika baadhi ya mashine, kiasi kilichoripotiwa kukusanywa kwa kutumia mashine hizo hakilingani na kiasi kilichoripotiwa katika mfumo; kuna nyakati ambazo mfumo hauwezi kuzitambua mashine hizo za kukusanyia mapato. Pia

upungufu wa mashine za kukusanyia mapato (POS) umeendelelea kuonekana katika mwaka wa ukaguzi. Orodha ya upungufu wa mashine za kukusanya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na.11-15

**Jedwali Na. 11-15: Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye upungufu wa machine za kieletroniki (POS)**

| Na. | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mtaa | Idadi ya mashine pungufu |
|---|---|---|
| 1 | H/Mji Bariadi | 29 |
| 2 | H/W Chemba | 91 |
| 3 | H/W Igunga | 37 |
| 4 | H/W Iringa | 120 |
| 5 | H/W Karagwe | 36 |
| 6 | H/W Kwimba | 89 |
| 7 | H/W Mwanga | 108 |
| 8 | H/W Nzega | 116 |
| | **Jumla** | **626** |

- Mfumo wa mapato hauwezi kuchapisha ankara za wateja zenye kujitosheleza kwa taarifa zilizokamilika.
- Uchunguzi wa ukaguzi katika mfumo umebainisha kuwa dashibodi ya mfumo hauonyeshi mashine ambayo hutumiwa kukusanya mapato kutoka kwa vyanzo vidogo.

Nazishauri kwa msisitizo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa mafunzo ya mfumo wa kukusanya mapato kwa njia za kieletroniki ili kuondoa matatizo yalioanishwa katika ripoti hii na kuendelea kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kushirikiana kwa karibu na OR-TAMISEMI

## SURA YA KUMI NA MBILI

## 12.0 USIMAMIZI WA MALI

Usimamizi wa mali ni utaratibu maalum wa utumiaji, uendeshaji, uendelezaji, ufutaji na uuzaji wa mali kwa gharama nafuu kwa lengo la kuwa na usimamizi bora kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Usimamizi wa mali unajumuisha kuweka usawa wa gharama, fursa na vihatarishi wakati wa kutumia mali hizo katika kufikia malengo ya taasisi.

Usimamizi wa mali pia unasaidia taasisi kutathmini mahitaji, matumizi na utendaji wa mifumo ya usimamizi wa mali. Pia, usimamizi wa mali unasaidia matumizi ya mbinu linganifu katika usimamizi wa mali katika vipindi tofauti vya matumizi ya mali hizo.

Ukaguzi wa usimamizi wa mali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ulibaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo:

### 12.1 Mali za Kudumu zilizoachwa kwa muda mrefu na zisizotengenezeka

Agizo la 45 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (LGFM) 2009 linataka mali zote ambazo hazihitajiki tena, hazitengenezeki, zilizochakaa au chakavu zitambuliwe na zifutwe kwa idhini ya Kamati ya Fedha, na hatimaye, Baraza la Madiwani. Zaidi ya hayo, Aya 26 ya Viwango vya Kimataifa vya Uaandaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma namba 21 inazitaka taasisi kufanya tathmini kila mwaka na kuripoti kama kuna dalili yoyote kwamba mali inaweza kupungua thamani yake kutokana na uchakavu na taasisi inatakiwa kukadiria thamani ya mali inayoweza kurejesheka.

Mapitio ya taarifa za matengenezo, utunzaji na ufutaji wa magari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa uligundua kwamba, magari na mali nyinginezo zimeachwa kwa muda mrefu bila kutengenezwa; na menejimenti hazijachukua hatua zozote za kutathmini kiwango cha uchakavu; ili kuweza kujua ni kwa

kiwango gani Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapata faida kutokana na ama kukarabati au kuuza mali hizo. Orodha ya mali hizo kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeainishwa katika **Kiambatanisho No.12:1**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kusimamia na kufanya matengenezo ya mali zote zilizopo chini ya mamlaka yake na kuhakikisha kwamba mali zote zinafanya kazi na zinatumika. Kuendelea kuacha mali kwa muda mrefu bila matengenezo kunapelekea kupanda kwa gharama za matengenezo na kupungua kwa thamani ya mali husika kutokana na uchakavu; hivyo kupunguza kiasi cha mapato ambacho kingepatikana endapo mali hizi zingeuzwa mapema.

Inapendekezwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kubaini na kufanya tathmini ya uchakavu wa mali zake ili kufanya maamuzi ya ama kuzifuta au kuzikarabati.

## 12.2 Kutotunza Daftari la Mali za Kudumu

Agizo la 103(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa 2009 linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutunza daftari la kumbukumbu za mali inazomiliki au ilizokodisha kwa kipindi fulani. Zaidi ya hayo, Agizo la 103 (2) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 linataka uwepo wa kumbukumbu muhimu kama vile taarifa ya ongezeko la mali, tarehe iliyonunuliwa, gharama na aina ya fedha zilizotumika kufanya manunuzi, eneo mali iliko, bei, maelezo ya mali zilizofutwa/kuuzwa ikiwa ni pamoja na tarehe ya kuuzwa, gharama za mauzo, na namba ya utambulisho ya mali husika.

Kinyume na agizo la hapo juu, ukaguzi ulibaini kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa 26 hazikutunza daftari la mali za kudumu; na Mamlaka zingine zinatunza daftari la mali za kudumu lakini hazina taarifa zote muhimu.

Taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa zisizotunza daftari la mali za kudumu na zile zenye daftari lisilo na taarifa zote muhimu zimeainishwa katika Jedwali Na 12-1 hapa chini;

**Jedwali Na. 12-1: Idadi ya Halmashauri zisizotunza daftari la mali la kudumu**

| S/N | Region | Name of Council | Register Not Available | Incomplete Register |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mara | H/W Musoma | v | |
| 2 | | H/W Tarime | v | |
| 3 | | H/Jiji Musoma | v | |
| 4 | Mwanza | H/W Kwimba | | v |
| 5 | Dodoma | H/W Chemba | | v |
| 6 | Kigoma | H/W Kasulu | v | |
| 7 | Tabora | H/W Nzega | | v |
| 8 | Tabora | H/W Kaliua | v | |
| 9 | Dodoma | H/W Chamwino | v | |
| 10 | Dodoma | H/W Kondoa | | v |
| 11 | Dodoma | H/W Mpwapwa | v | |
| 12 | Kigoma | H/W Kasulu | v | |
| 13 | Geita | H/W Mbogwe | v | |
| 14 | Mara | H/W Musoma | | v |
| 15 | Arusha | H/W Meru | | v |
| 16 | Kilimanjaro | H/W Siha | | v |
| 17 | Morogoro | H/Jiji Morogoro | v | |
| 18 | Njombe | H/W Ludewa | v | |
| 19 | Ruvuma | H/W Madaba | | v |
| 20 | Ruvuma | H/W Mbinga | | v |
| 21 | Ruvuma | Mbinga Tc | | v |
| 22 | Rukwa | H/W Mpanda | | |
| 23 | Njombe | H/W Njombe | v | |
| 24 | Ruvuma | H/W Songea | v | |
| 25 | Pwani | H/W Mafia | | v |
| 26 | Morogoro | H/W Malinyi | | v |

Ninapendekeza kwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuhakikisha kwamba daftari la mali za kudumu linatunzwa na kuhuishwa mara kwa mara kama inavyotakiwa na Agizo 103 (1) na (2) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa (LGFM), 2009.

## 12.1 Ardhi na Majengo yasiyo na Nyaraka za Umiliki Sh. Tz 3,557,465,000

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kwamba baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliwasilisha taarifa ya fedha ya ardhi na majengo yenye thamani ya Sh.Tz 3,557,465,000 ambazo hazikuwa na nyaraka za umiliki. Katika mazingira hayo, nilishindwa kuthibitisha kuwapo, umiliki, thamani halisi na uhalali wa ardhi na majengo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nane kama inavyoonekana katika jedwali Na.12-2 hapa chini:

**Jedwali Na. 12-2: Ardhi na Majengo yasiyo na Nyaraka za Umiliki**

| Mkoa | Jina la H/W | Aina ya Mali | Thamani (Sh.Tz) |
|---|---|---|---|
| Kagera | H/M Bukoba | Hati Miliki | 2,198,000,000 |
| Mara | H/W Serengeti | Hati Miliki | 1,359,465,000 |
| Dodoma | H/W Mpwapwa | Hati Miliki | - |
| Mara | H/W Serengeti | Hati Miliki | - |
| Rukwa | H/W Mpanda | Hati Miliki | - |
| Mbeya | H/W Rungwe | Hati Miliki | - |
| Rukwa | H/M S'wanga | Hati Miliki | - |
| Dar Esalaam | H/M Ubungo | Hati Miliki | |
| **Jumla** | | | **3,557,465,000** |

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata nyaraka za umiliki wa mali zao, kwa mfano, hati miliki za ardhi na majengo. Aidha, thamani ya ardhi na majengo ioneshwe katika taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uaandaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma Na. 17 ili taarifa zao za fedha ziweze kuonesha ukweli na uhalisi wa utendaji wao wa kifedha.

## 12.3 Magari yasiyo na Bima

Agizo la 95 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 linawataka Maafisa Usafiri kuhakikisha kuwa magari yote

yanawekewa bima dhidi ya majanga yasiyotarajiwa na pia kuhakikisha malipo ya bima yanafanyika pindi muda unapowadia.

Kinyume na agizo hilo hapo juu, nilibaini wakati wa ukaguzi kwamba baadhi ya magari ya Mamlaka ya Serikali za Mtaa hayakuwekewa bima kama inavyoonekana katika Jedwali Na 12-3 hapa chini

**Jedwali Na. 12-3: Idadi ya Halmashauri zenye magari yasiyokua na Bima**

| Region | S/No. | Name of Council | Number of Vehicles not insured |
|---|---|---|---|
| Shinyanga | 1. | H/W Kishapu | 8 |
| | 2 | H/W Shinyanga | 13 |
| Mwanza | 3 | H/W Kwimba | 25 |
| Manyara | 4 | H/W Mbulu | 8 |
| Singida | 5 | H/W Mkalama | 4 |
| Singida | 6 | H/J Singida | 5 |
| Arusha | 7 | H/W Meru | 6 |
| Tanga | 8 | H/W Mkinga | 4 |
| Songwe | 9 | H/W Ileje | 16 |
| Iringa | 10 | H/Mji Iringa | 16 |
| Songwe | 11 | H/W Momba | 15 |
| Mbeya | 12 | H/W Rungwe | 4 |

Kutokana na kukosekana kwa bima, Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ziko katika hatari ya kuingia katika hasara endapo kutatokea majanga yasiyotarajiwa.

Ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuhakikisha kuwa magari yote yanawekewa bima, ikiwa ni pamoja na pikipiki na mitambo kama inavyotakiwa na Agizo la 95 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009.

## 12.4 Mali ambazo hazina namba za utambulisho Sh.Tz 53,147,580,819

Agizo la 63(5) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ya mwaka 2009 linataka mali zote zinazomilikiwa na Halmashauri kuwa na namba za utambulisho; pia namba hizo za utambulisho ziaandikwe katika daftari la kumbukumbu za mali.

Kinyume na agizo hilo hapo juu, ilibainika wakati wa ukaguzi kwamba baadhi ya mali zinazomilikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 5 hazikuwekewa namba za utambulisho kwa ajili ya kuzitambua kwa urahisi. Hivyo basi, sio rahisi kutofautisha kati ya mali zinazomilikiwa na Halmashauri pamoja na mali kama hizo zinazomilikiwa na taasisi zingine ambazo zimehifadhiwa katika eneo la Halmashauri husika kama inavyoonekana katika jedwali Na.12-4 hapa chini: -

**Jedwali Na. 12-4: Orodha ya halmashauri zenye mali zisizo na namna ya utambulisho**

| Kumb Na. | Mkoa | halmashauri | Sh.Tz |
|---|---|---|---|
| 1 | Shinyanga | H/W Maswa | - |
| 2 | Tabora | H/W Urambo | 11,440,000.00 |
| 3 | Arusha | H/W Arusha | 132,075,320.00 |
| 4 | Ruvuma | H/W Songea | 53,004,065,499 |
| 5 | Pwani | H/W Kibaha | - |
| **Jumla** | | | **53,147,580,819** |

Nazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba zinaweka namba za utambulisho kwenye mali zilizokuwepo pamoja na zile zilizonunuliwa katika mwaka huu wa fedha unaokaguliwa ambazo hazijawekewa namba za utambulisho kama inavyoelezwa kwenye Agizo la 63(5) ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009.

## SURA YA KUMI NA TATU

## 13.0 UKAGUZI MAALUM

### 13.1 Mambo muhimu yaliyobainika kwenye Ukaguzi Maalum

Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na Kanuni ya 79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum endapo atapata maombi kutoka kwa mtu yeyote, Taasisi, Mashirika ya Umma, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa au chombo kingine chochote.

Sheria pia inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa maamuzi yake binafsi atakapoona inafaa kufanya ukaguzi maalum. Kwa mwaka 2016/2017, nilifanya kaguzi maalum mbili; ulioombwa na Waziri Mkuu na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuhusu mambo yaliyojitokeza katika ujenzi wa Soko jipya la Mwanjelwa Katika Jiji la Mbeya pamoja na ukaguzi Maalum unaoendelea wa usuluhishi wa kiasi salia na kiasi sawa cha fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 zilizounganishwa na mfumo wa malipo a TISS uliopo TAMISEMI –DODOMA.

Ukaguzi wa ujenzi wa Soko la Mwanjelwa ulifanyika kulingana na hadidu za rejea zilizoandaliwa mahususi kwa ajili ya kuongoza ukaguzi huo. Ukaguzi ulifuata viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa sekta ya Umma na ulifanyika ili kutoa taarifa walioomba ukaguzi huo kwa waliyoiomba ili waweze kuchukua hatua stahiki.

Ufuatao ni muhtasari wa mambo muhimu na mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi maalum wa ujenzi wa soko la Mwanjelwa.

#### 13.1.1 Kusaini mikataba ya mikopo kutoka benki ya CRDB bila kupata idhini kutoka OR-TAMISEMI Sh. Tz bilioni 16.062

Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilikopa jumla ya Sh. Tz bilioni 16.062 katika awamu tatu (awamu ya kwanza wa Sh. Tz bilioni 13 na wa awamu ya tatu wa Sh.Tz bilioni 3.062) bila kupata idhini kutoka

kwa Waziri mwenye dhamana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama inavyotakiwa katika Kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2002). Pia, timu ya ukaguzi ilishindwa kuthibitisha kama H/Jiji la Mbeya ilipata idhini ya mkopo wa awamu ya pili wa Sh. Tz bilioni 3.5 kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa sababu ya kukosekana nyaraka halisi za idhini ya mkopo huo. Nakala za nyaraka zilizowasilishwa kwa wakaguzi zinatia shaka kwa vile Ofisi ya Rais-TAMISEMI haikuwa na kumbukumbu za mkopo huo.

### 13.1.2 Kusaini mkataba wa Mkopo wa Sh. Tz bilioni 13 na Benki ya CRDB kabla ya kupata dhamana ya Wizara ya Fedha

Halmashauri ya Jiji la Mbeya iliingia mkataba na Benki ya CRDB wa kuchukua mkopo kabla ya kupata dhamana ya kukopa fedha hizo kutoka Wizara ya Fedha kama mdhamini wa Mkopo. Dhamana ya mkopo wa awamu ya kwanza wa Sh. Tz bilioni 13 ilitolewa tarehe 17/06/2009; wakati mkataba wa mkopo huo kati ya H/Jiji la Mbeya na Benki ya CRDB ulisainiwa tarehe 02/05/2008 ikiwa ni zaidi ya mwaka mmoja tangu kuingia mkataba.

### 13.1.3 Hasara iliyotokana na kuchukua mkopo kabla shughuli za ujenzi hazijaanza rasmi Sh. Tz 3,360,423,611

Nimepitia nyaraka mbalimbali na kubaini kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipata hasara ya kiasi ya Sh. Tz 3,360,423,611 kwa kuingia mkataba wa mkopo wa Sh. Tz bilioni 13 kabla ya kuanza kwa mradi wa ujenzi wa Soko. Hasara iliyotokea ilisababishwa na tozo ya riba ya mkopo, ijapokuwa fedha za mkopo huo bado zilikuwa zimehifadhiwa kwenye akaunti inayomilikiwa na benki ya CRDB badala ya kuwekwa kwenye akaunti ya ujenzi iliyofunguliwa benki ya CRDB maalum kwa ajili ya shughuli hiyo tu.

### 13.1.4 Uchukuaji wa Mkopo usiozingatia Mpango Mkakati wa Biashara uliopelekea H/Jiji la Mbeya kuchukua mkopo zaidi ya kiasi kilichokusudiwa Sh. Tz 5,517,600,000 (39%)

Kipengele cha 6.3 cha Mpango Mkakati wa Biashara kinachohusu mtaji wa uwekezaji kinaonesha kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilitarajia kukopa kiasi cha Sh. Tz 14,044,400,000 kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Soko jipya la Mwanjelwa.

Kinyume na kipengele kilichonukuliwa hapo juu, H/Jiji la Mbeya ilikopa kiasi cha Sh. Tz 19,562,000,000. Hali hii inadhihirisha kuwa Mpango Mkakati wa Biashara haukutumika kama dira ya kufanikisha utekelezaji wa mradi huu na kusababisha kuchukuliwa Mkopo kiasi cha Sh. Tz 5,517,600,000 (39%) zaidi ya kiasi kilichokusudiwa.

### 13.1.5 Malipo kwa Wakandarasi

**a) Malipo kwa Mkandarasi yanayozidi kazi alizofanya Sh. Tz 1,140,288,750**

Mshauri Mwelekezi (MD Consultant) alithibitisha malipo ya Sh. Tz 590,000,000 kwa Mkandarasi Mjenzi wa kwanza M/s Tanzania Building Works Ltd kwa kazi ambazo hakuzifanya. Pia, kiasi cha Sh. Tz 112,208,200 kililipwa zaidi ya kiasi kilichopo kwenye BoQ. Vilevile, Kiasi cha Sh. Tz 67,796,250 kililipwa kwa Mkandarasi Mjenzi wa pili, M/s Nandra Engineering & Construction, kwa kazi ambazo hazikufanyika; na kiasi cha Sh. Tz 370,284,300 kililipwa zaidi ya kiwango cha kazi kilichoainishwa kwenye BoQ.

**b) Hasara kutokana na kurudia kazi zilizofanywa na mkandarsi mjenzi M/s Tanzania Building Works Ltd Sh. Tz 304,470,500**

Mshauri Mwelekezi alielekeza Mkandarasi Mjenzi M/S Nandhra Engineering Construction Co. Ltd kurudia kazi zenye thamani ya Sh. Tz 304,470,500 ambazo zilikwishafanywa na mkandarasi wa kwanza, M/s Tanzania Building Works Ltd, bila kutoa sababu ya kurudiwa kwa kazi hizo. Hii ikapelekea kuongezeka kwa gharama zisizokuwa na ulazima za jumla ya Sh. Tz 304,470,500.

c) **Hasara iliyotokana na mabadiliko na nyongeza za kazi zilizotokana na uzembe na kukosekana weledi Sh. Tz 3,161,636,499**

Kutozingatiwa kwa hatua stahiki katika usanifu wa mradi huu, kumesababisha usanifu uwe na mahitaji makubwa ya mabadiliko na kazi za nyongeza. Mapungufu hayo yaliyojitokeza yangeweza kuonekana wakati wa kujadili ripoti ya awali ya usanifu na kurekebishwa kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi. Hasara ya Sh. Tz 2,807,902,779 ilitokana na kuwapo kwa kazi za nyongeza alizopewa mkandarasi wa pili, ambapo pia kazi nyingine hazikuwepo kwenye BoQ tangu mwanzo. Na, kiasi cha Sh. Tz 353,733,720 kililipwa kwa Mshauri mwelekezi ikiwa ni nyongeza ya gharama za ushauri.

### 13.1.6 Ongezeko la gharama lililotokana na kuvunjwa kwa mkataba wa awali Sh. Tz 5,816,523,387

Halmashauri ya Jiji la Mbeya iliingia mkataba na mkandarasi mjenzi M/s Tanzania Builiding Works Ltd kwa ajili ya Ujenzi wa Soko Jipya la Mwanjelwa kwa gharama ya Sh. Tz 10,670,072,917.50. Mkandarasi alivunja mkataba akiwa ameshafanya kazi kwa asilimia 80; na alikuwa amekwishalipwa kiasi cha Sh. Tz 8,881,871,802. Hivyo basi, ilitarajiwa kuwa kazi ya asilimia 20 iliyobakia ingeweza kukamilishwa kwa gharama isiyozidi Sh. Tz 1,788,201,115.

Ili kumaliza kazi iliyokuwa imebakia ya asilimia 20, H/Jiji la Mbeya liliingia tena mkataba na M/s Nandhra Engineering Construction Co. Ltd Sh. Tz 7,224,875,097 sawa na asilimia 81 ya kiasi kilicholipwa kwa mkandarasi wa awali ambaye alishakamilisha kazi kwa asilimia 80. Mkandarasi Mjenzi M/s Nandhra Engineering Construction Co. Ltd bado anadai kiasi Sh. Tz 379,776,488 kutokana na kazi ambazo alikuwa hajalipwa.

### 13.1.7 Hasara iliyosababishwa na kutokumshirikisha Mshauri Mwelekezi katika mchakato wa kumpata Mkandarasi M/s Nandhra Engineering Construction Co. Ltd Sh. Tz 682,798,733.

Baada ya kupitia nyaraka mbalimbali, ilibainika kuwa Mkandarasi Mjenzi M/s Nandhra Engineering Construction Co. Ltd alipewa mkataba wa ujenzi wenye thamani ya Sh. Tz 5,300,000,000 wakati Mshauri Mwelekezi alikadiria kuwa kazi hiyo ya ujenzi ingefanywa kwa Sh. Tz 4,617,201,267, na hivyo, kuisababishia hasara ya Sh. Tz 682,798,733. Mkataba ulisainiwa pasipo kurejewa kwa makadirio yaliyofanywa na Mshauri Mwelekezi.

### 13.1.8 Malipo ya awali kulipwa kinyume na kifungu cha mkataba Sh. Tz 1,000,000,000

Kiasi cha Sh. Tz 2,600,510,937 kililipwa kwa mkandarasi Mjenzi M/s Tanzania Building Works Ltd ikiwa ni malipo ya awali badala ya Sh. Tz 1,600,510,937, kinyume na Kifungu Na. 53 cha Mashart ya Jumla ya Mkataba baina ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Mkandarasi Mjenzi. Mkandarasi alirudisha kiasi cha Sh. Tz 200,000,000 na kubakia deni la Sh. Tz 800,000,000. Kutokana na kuvunjwa kwa mkataba, marejesho ya deni hilo ni ya mashaka.

### 13.1.9 Tozo ya kuchelewa kumaliza kazi kutotozwa kwa M/s Tanzania Building Works Ltd Sh. Tz 1,033,912,388

Mkandarasi Mjenzi M/s Tanzania Building Works Ltd alicheleweshakazi kwa siku 353. Hivyo, kwa mujibu wa makubaliano, mkandarasi alipaswa kulipa tozo (liquidated damages) ya jumla ya Sh. Tz 1,067,207,291 kwa kuchelewa kumaliza kazi. Hata hivyo, kiasi cha Sh. Tz 33,294,903 kilikuwa kimeshalipwa kwa H/Jiji la Mbeya kama tozo; bado kiasi cha Sh. Tz 1,033,912,388.37 hakijalipwa na Mkandarasi.

### 13.1.10 Kutokuwapo kwa uwezekano wa kulipa deni la mkopo kwa kutumia mapato yatokanayo na Soko la Mwanjelwa na mapato ya ndani

Ukaguzi ulibaini kuwa H/J la Mbeya ingeweza kukusanya kiasi cha Sh. Tz 293,641,908 kwa mwezi iwapo soko lote lingepata wapangaji. Ukitoa gharama za uendeshaji, kiasi cha Sh. Tz 260,309,508 ndicho ambacho kingesalia kwa ajili ya marejesho ya mkopo kutoka Benki ya CRDB.

Katika upitiaji wa jinsi ya kulipa mkopo, nilibaini kuwa H/Jiji ilitakiwa kulipa kiasi cha Sh. Tz 356,309,077 kwa mwezi ikiwa ni marejesho ya mkopo.

Pia, nilibaini kuwa H/J la Mbeya inapaswa kurejesha wastani wa Sh. Tz 57,000,000 kwa mwezi kwa Bodi ya Mikopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mkopo uliokopwa mwaka 2004 kwa ajili ya ujenzi wa Hostel na Ukumbi wa Mkapa.

Hata hivyo, H/Jiji la Mbeya ina mkopo mwingine kutoka Benki ya CRDB wa Mradi wa Viwanja vya Sistila uliokopwa mwaka 2015, ambapo, wanapaswa kurejesha wastani wa kiasi cha Sh. Tz 48,926,810 kwa mwezi. Hivyo, H/Jiji la Mbeya inapaswa kujeresha jumla ya Sh. Tz 462,413,887 kwa mwezi kwa mikopo yote iliyokopa.

Hali hii inadhihirisha kuwa H/Jiji la Mbeya haina uwezo wa kurejesha deni la Mkopo wa CRDB kwa kutumia mapato yatokanayo na upangishaji wa Soko Jipya la Mwanjelwa wala kwa kutumia mapato yake ya ndani.

### 13.1.11 Hasara ambayo Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipata kwa kuchukua mkopo benki ya CRDB badala ya NSSF Sh. Tz 5,138,762,054

Baada ya kupitia nyaraka mbalimbali zinazohusiana na ujenzi wa Soko Jipya la Mwanjelwa, ilibainika kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulionesha nia ya kuikopesha H/Jiji la

Mbeya kwa riba ndogo ya 11%. Hata hivyo, Halmashauri iliamua kuchukua mkopo kutoka benki ya CRDB kwa riba kubwa kati ya 14.5% na 16%. Uamuzi wa kuchukua Mkopo wa Benki ya CRDB badala wa NSSF ulipelekea kupatikana kwa hasara ya Sh. Tz 5,138,762,054.

### 13.1.12 Kughushiwa kwa mikataba ya upangaji na kutofuata matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma

Baada ya kupitia mikataba mbalimbali ya upangaji, nilibaini kuwa baadhi ya mikataba imeghushiwa, kwani baadhi yake imefanyiwa mabadiliko mbalimbali bila ya kuridhiwa na pande zote mbili za mkataba. Mabadiliko yaliyofanyika katika mikataba ni kufuta baadhi ya taarifa au kutumia wino wa kufutia (correction fluid).

Pia, nilibaini mapungufu mbalimbali yakiwemo kutokuwapo kwa ushindani wakati wa utangazaji wa zabuni; kutofanyika kwa upembuzi yakinifu ili kupata bei za upangishaji kwa kila chumba; kupangisha watu/taasisi bila kupitia mchakato wa Manunuzi ya Umma; na kutowajulisha waliokosa vyumba/vizimba pamoja na sababu za kukosa kwao kinyume na Kifungu 77(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni ya 110 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

### 13.1.13 Mapungufu yaliyobainika katika mikataba ya upangishaji wa Soko Jipya la Mwanjelwa

Nilipitia mikataba mbalimbali ya upangaji na kubaini mapungufu mbalimbali yakiwemo wahusika kutoandika tarehe ya kusaini mkataba, kutosaini mikataba, mikataba yote kutokuwa na kipengele cha tozo ya kushindwa/kuchelewa kulipa kodi kila mwezi, na kipengele cha jinsi ya kutatua migogoro iwapo pande mbili zikishindwa kufuata mkataba.

**13.1.14 Mkopo wa Viwanja vya Sistilla kutumika kulipia riba ya mkopo wa Mradi wa Soko la Mwanjelwa na kuisababishia H/Jiji hasara ya Sh. Tz 5,000,000**

H/Jiji la Mbeya iliingia mkataba na Benki ya CRDB tarehe 26/11/2012 wa Mradi wa Viwanja wa Sistila uliosainiwa tarehe 20/02/2013. Halmashauri ilikopa Sh.Tz Bilioni 1.5, na ilipanga kiasi cha Sh.Tz milioni 500 kutoka fedha hizo kitumike kulipa riba ya Mkopo wa Mradi wa Ujenzi wa Soko Jipya la Mwanjelwa. Mkopo huu wa viwanja vya Sistilla ulikuwa na riba ya asilimia kumi na tano (15%), wakati mkopo wa mradi wa Soko la Mwanjelwa riba yake ilipungua hadi kufikia asilimia kumi na tatu (13%). Hii lipelekea H/Jiji la Mbeya kupata hasara ya Sh.Tz 5,000,000 inayotokana na tofauti iliyopo kati ya riba ya asilimia 13 na 15.

**13.1.15 H/Jiji la Mbeya kushindwa kukusanya kodi ya pango Sh.Tz 1,225,158,063**

Nilipitia taarifa ya upangishaji wa Soko Jipya la Mwanjelwa na taarifa ya madeni ya kodi ya pango na kubaini kuwa, H/Jiji la Mbeya kupitia kwa Msimamizi wa Mradi UTT-PID imeshindwa kukusanya kodi ya pango ya jumla ya Sh.Tz 1,225,158,063 kutoka kwa wapangaji wa Soko Jipya la Mwanjelwa kutokana na wapangaji hao kuacha kufanya biashara sokoni hapo. Kushindwa kwa msimamizi wa uendeshaji wa Soko la Mwanjelwa UTT- PID kufuatilia madeni ya pango kunadhihirisha kuwa hana uwezo wa kutosha kusimamia uendeshaji wa Soko Jipya la Mwanjelwa.

Soko linajumuisha vyumba 447 vya maduka na bucha lakini hadi kufika wakati wa ukaguzi (Aprili 2017), vyumba 321 sawa na asilimia 72 ya vyumba vyote vilikuwa vimefungwa na hakuna biashara yoyote iliyokuwa inaendelea. Wapangaji wa vyumba hivyo wameshindwa kufungua kwa madai kuwa bei ya upangishaji ni kubwa ikilinganishwa na ile ya soko katika eneo la Mwanjelwa.

## 13.2 Masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi Maalum wa usuluhishi wa kiasi salia na kiasi sawa cha fedha za Mamlaka za serikali za mitaa 46 zilizounganishwa na mfumo wa malipo ya TISS uliopo TAMISEMI-DODOMA

### 13.2.1 Kiasi ambacho hakikusuluhishwa katika daftari la mapato na matumizi na kilichosalia kwenye benki

Agizo la 29 (2) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009 linamtaka Mweka Hazina kuhakikisha kuwa usuluhishi unafanyika, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa akaunti mbalimbali sanjari na kufanya usuluhishi kati ya daftari la fedha na taarifa za benki kila mwezi na kufanya masahihisho ipasavyo.

Pia Agizo la 31 (1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka Afisa Masuuli kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi kabla au ifikapo tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha. Agizo la 31 (6) (f) linaeleza zaidi kwamba taarifa za fedha zinazowasilishwa zinapaswa kuambatana na taarifa za usuluhishi wa benki na ziwasilishwe kwa maafisa wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili waweze kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha.

Zaidi ya hayo, Aya ya 56 ya Kiwango cha 2 cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma kinazitaka taasisi kubainisha kipengele cha salio la fedha taslim na kiasi salia na kiasi sawa cha fedha, na kuwasilisha usuluhishi huo kwenye taarifa ya mtiriko wa fedha na kiasi hicho hicho kiwekwe kwenye Taarifa ya Mizania ya Hesabu.

Kupitia Waraka Na. CA.3 / 244/01 wa tarehe 3 Mei 2016, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilielekezwa kubadilisha mfumo wake wa malipo na kutumia mfumo wa malipo moja kwa moja katika akaunti za walipwaji kwa kupitia mtandao wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (TISS). Mfumo huu umebadilisha ufanyaji

wa malipo kwa njia ya hundi na badala yake malipo yanafanywa moja kwa moja kwenye akaunti za wateja kwenye benki zao. Mpangilio huu unahitaji Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinazotumia TISS kufungua akunti za fedha kwenye Benki ya Tanzania (BoT).

Sura ya 2 (4) ya Muongozo wa kutumia TISS uliotolewa na OR-TAMISEMI kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa mwezi Aprili 2016, inawataka watumishi wa kitengo cha usuluhishi katika idara ya malipo (CPO) katika OR-TAMISEMI kufanya usuluhishi wa benki kwa fedha zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizowekwa au kulipwa kupitia akaunti zao za BoT.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi maalum, nilibaini yafuatayo ambayo hayakusuluhishwa:

**a) Kiasi cha SH.TZ 3,075,198,442.10 hakikusuluhishwa kwenye vitabu vya hesabu**

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliwasilisha taarifa za mwisho za fedha kwa mwaka wa fedha ulioshia Juni 30, 2017 kwa ajili ya ukaguzi. Taarifa hizo za fedha zilijumuisha taarifa za mtiririko wa fedha ambazo baada ya ukaguzi na uchambuzi kwenye mfumo wa TISS na Epicor, ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 29 kati ya 46 zilionesha tofauti ya kiasi salia chenye jumla ya shilingi bilioni 3 kutoka kwenye taarifa zilizokuwa zimewasilishwa na OR-TAMISEMI kupitia taarifa ya usuluhishi wa hesabu zilizotolewa ndani ya mfumo wa Epicor kwa tarehe 30 Juni 2017. Kupitia taarifa ya usuluhishi iliyotokana na Mfumo wa Epicor mnamo Juni 30, 2017, kiasi ambacho hakikusuluhishwa kwenye vitabu vya hesabu ni kama ilivyooneshwa katika **Jedwali 13.0-1** hapa chini na mchanganuo wa kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kama zinavyooneshwa katika Kiambatisho 13:1 cha ripoti hii.

**Jedwali Na. 13.0-1: Kiasi ambacho hakikusuluhishwa kwenye vitabu vya hesabu kufikia 30 Juni, 2017 SH.TZ 3,075,198,442.10**

| AKAUNTI YA BENKI | BAKAA YA FEDHA TASLIM KWA MUJIBU WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA (SH.TZ) | BAKAA YA FEDHA TASLIM KWA MUJIBU WA TAARIFA ZA USULUHISHI WA BENKI (SH.TZ) | TOFAUTI YA BAKAA TASLIM (SH.TZ) |
|---|---|---|---|
| | **(A)** | **(B)** | **(B-A)** |
| Mfuko Mkuu | -290,056,775.47 | -411,115,185.17 | -121,058,409.70 |
| Maendeleo | 15,545,805,746.65 | 13,253,320,069.87 | -2,292,485,676.78 |
| Matumizi ya kawaida | 75,314,298.74 | -178,388,427.29 | -253,702,726.03 |
| Amana | 10,332,398,778.34 | 7,391,387,413.09 | -2,941,011,365.25 |
| Sekta ya elimu | 517,141,107.97 | 62,185,709.53 | -454,955,398.44 |
| Sekta ya Afya | 2,063,301,497.50 | 1,643,813,408.32 | -419,488,089.18 |
| Mfuko wa barabara | 4,545,610,957.42 | 4,894,227,993.52 | 348,617,036.10 |
| Sekta ya maji | 785,870,374.00 | 841,993,897.98 | 56,123,523.98 |
| Mishahara | 299,899,101.05 | 3,302,661,764.25 | 3,002,762,663.20 |
| **JUMLA** | **33,875,285,086.20** | **30,800,086,644.10** | **-3,075,198,442.10** |

**b) Tofauti kati ya kiasi salia cha Benki kwa mujibu wa Barua toka OR-TAMISEMI kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kiasi salia halisi kilichopo benki kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu**

Mapitio ya taarifa za benki za OR-TAMISEMI zinazohusiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 zinazotumia mfumo wa TISS kupitia akaunti tisa zilizopo Benki Kuu kwa tarehe 30 Juni, 2017, ikilinganishwa na takwimu za kiasi halisi kilichopo benki kwa kila akaunti na kwa mujibu wa taarifa za benki kutoka Benki Kuu na kama ilivyoripotiwa na OR-TAMISEMI kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CA. 3/244/01/298 tarehe 29 Januari, 2018 ilionesha kuwepo kwa tofauti ya SH.TZ 1.2 bilioni kati ya kiasi halisi kilichopo kwenye akaunti Benki Kuu

dhidi ya kiasi salia kilichoripotiwa na OR-TAMISEMI kama inavyoonekana katika **Jedwali 13-2** hapa chini:

**Jedwali Na. 13.0-2: Tofauti kati ya salio halisi la Benki Kuu na salio kwa mujibu wa barua ya OR-TAMISEMI kwenda kwa Mamlaka za serikali za mitaa**

| Na. | Akaunti ya Benki | Salio kwa mujibu wa barua ya OR-TAMISEMI kwenda kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa | Salio halisi kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| | | (A) | (B) | (B) -(A) |
| 1 | Mfuko Mkuu | (333,223,831.55) | 203,217.85 | 333,427,049.40 |
| 2 | Sekta ya maji | 8,780,144,311.87 | 6,642,949,856.12 | (2,137,194,455.75) |
| 3 | Mfuko wa barabara | 46,690,161,647.74 | 51,355,922,346.06 | 4,665,760,698.32 |
| 4 | Mishahara | 1,584,784,286.68 | 1,241,429,383.78 | (343,354,902.90) |
| 5 | Mtumizi ya kawaida | 4,123,738.65 | 557,278,405.63 | 553,154,666.98 |
| 6 | Amana | 9,815,806,717.15 | 9,089,322,964.83 | (726,483,752.32) |
| 7 | Sekta ya Afya | 3,932,663,503.66 | 3,457,155,208.79 | (475,508,294.87) |
| 8 | Sekta ya Elimu | 712,025,370.48 | 275,006,288.33 | (437,019,082.15) |
| 9 | Maendeleo | 23,130,797,391.74 | 22,927,135,037.85 | (203,662,353.89) |
| | | **94,317,283,136.42** | **95,546,402,709.24** | **1,229,119,572.82** |

**c) Kiasi cha SH.TZ 1,384,751,218.84 hakikusuluhishwa kwenye kiasi salia cha benki**

Mapitio ya ripoti za usuluhishi wa kibenki yaliyotokana na mfumo wa Epicor mnamo tarehe 30 Juni, 2017 yalibainisha kuwa, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 37 kati ya 46, kiasi salia cha benki kwa mujibu wa taarifa za benki kwa tarehe Juni 30, 2017 kilitofautiana na taarifa za kibenki zilizotolewa na OR-TAMISEMI

kupitia barua yenye kumb. Na. CA.3/244/01/298 ya tarehe 29 Januari, 2018 ambayo ilipekea tofauti ya SH.TZ 1.3 bilioni ukilinganisha na kiasi halisi kilichopo benki na kiasi kilichoripotiwa kwa mujibu wa barua ya OR-TAMISEMI. Nilipitia na kuhakiki kiasi salia cha benki cha taarifa ya usuluhishi kwa kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho 13:2** cha ripoti hii

### 13.2.2 Kiasi cha SH.TZ 256,097,975.956 hakikuondolewa kwenye akaunti yenye fedha zilizoshindwa kwenda kwa wateja (unapplied) na hazikurudishwa kwenye akaunti husika za Mamlaka za Serikali za Mitaa mpaka kufikia 30 Juni, 2017

Malipo yaliyokataliwa kutoka benki za biashara hupelekwa kwenye akaunti maalum inayoitwa akaunti yenye fedha zilizoshindwa kwenda kwa wateja (unapplied account) iliyopo BOT. Akaunti hii hutumika kuhifadhi fedha zilizokataliwa kutokana na mapungufu mbalimbali wakati wa malipo yaliyofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama vile; nambari ya utambulisho ya benki kukosewa, malipo yaliyojirudia, akaunti ya mlipwaji kutotumika, akaunti zilizofungwa, majina kutofautiana, na nambari ya akaunti na jina kutofautiana.

Sehemu ya XXIV ya Waraka wa Fedha Na. 7 wa 2016/2017 uliotolewa tarehe 19 Mei, 2017 unawataka Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotumia mfumo wa TISS kuhakikisha kwamba taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo na waingizaji wa taarifa zinapaswa kuwa sahihi na hakika. Kabla ya kibali chochote cha malipo katika mfumo, Mweka Hazina anapaswa kuchunguza kikamilifu na kuthibitisha usahihi wa maelezo ya mlipaji ikiwa ni pamoja na namba ya akaunti ili kuepuka fedha kupelekwa katika akaunti isiyohusika au kurejeshwa kitu ambacho kinaweza kuleta usumbufu kwa watu wanaostahili kulipwa fedha hizo.

Hata hivyo, baada ya kufanya usuluhishi wa kibenki ilibainika kuwa, akaunti yenye fedha zilizoshindwa kwenda kwa wateja Na.9921210201 ilikuwa na jumla ya SH.TZ 256,097,976 ambazo

zilikuwa zimekusanyika kutoka tarehe 9 Mei 2016 hadi 30 Juni 2017 bila kufanyiwa usuluhisho na kurejeshwa kwenye akaunti husika za OR-TAMISEMI zilizopo Benki kuu.

Kwa kuongezea, wakati wa ukaguzi Machi, 2018 nilibaini ongezeko la kiasi cha fedha kwenye akaunti yenye fedha zilizoshindwa kwenda kwa wateja hadi kufikia kiasi cha SH.TZ 1,182,842,247 kwa mujibu wa salio la tarehe 01 Machi, 2018, pia kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye mfumo wa TISS kwenye akaunti hiyo. Hii ni ongezeko la SH.TZ 926,097,975.95 sawa na 362% ikilinganishwa na salio la Juni 30, 2017 wakati kiasi kilichosalia kilikuwa ni SH.TZ 256,097,975.95.

### 13.2.3 Masuala ambayo hayakufanyiwa usuluhishi katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki

Mapitio ya taarifa ya usuluhishi wa benki kutoka kwenye mfumo unaotumika kufanya usuluhishi unaoitwa "Treasury Management Software" (TMS) yalibainisha kuwepo kwa vifungu vya mapato na matumizi ambavyo havikusuluhishwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017. Kulikuwa na malipo yaliyofanywa katika vitabu vya fedha na hayakuwepo kwenye taarifa za benki kiasi cha SH.TZ 1,192,098,194,636.97; Mapato kwenye daftari la fedha lakini hayapo kwenye taarifa za benki kiasi cha SH.TZ 1,428,998,791,332.52 na kiasi cha SH.TZ 1,424,205,225,514.80 ni Malipo yaliyofanyika benki na hayapo kwenye vitabu vya fedha kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 13-4.**

**Jedwali Na. 13.0-3: Masuala ambayo hayakufanyiwa usuluhishi katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki**

| Akaunti ya benki | Mapato kwenye taarifa za Benki lakini hayapo kwenye daftari la fedha (SH.TZ) | Malipo kwenye taarifa za Benki lakini hayapo kwenye daftari la fedha (SH.TZ) | Mapato kwenye daftari la fedha lakini hayapo kwenye taarifa za Benki (SH.TZ) | Malipo kwenye daftari la fedha lakini hayapo kwenye taarifa za Benki (SH.TZ) |
|---|---|---|---|---|
| Mfuko Mkuu | 23,785,316,568.27 | (16,444,552,351) | 26,608,410,800 | (17,102,506,595) |
| Maendeleo | 40,037,500,445.72 | (24,961,134,245) | 54,361,330,428 | (14,790,019,201) |
| Matumizi ya kawaida | 4,182,754,526.50 | (660,501,647) | 3,958,021,187 | (217,529,260) |
| Amana | 17,349,165,073.09 | (1,856,748,534) | 31,047,285,368 | (12,704,551,729) |
| Sekta ya Elimu | 84,584,860,130.32 | (72,299,914,683) | 59,901,182,957 | (36,030,902,260) |
| Sekta ya Afya | 24,982,934,155.53 | (3,952,144,431) | 25,890,229,470 | (837,041,194) |
| Mfuko wa barabara | 11,383,267,087.54 | (51,419,323,906) | 11,137,975,036 | (1,387,980,740.71) |
| Sekta ya Maji | 7,687,215,426.11 | (7,361,704,446) | 9,764,628,614 | (2,548,152,316.19) |
| Mishahara | 1,210,212,212,101.72 | (1,208,325,611,677) | 1,206,329,727,468 | (1,106,479,511,337) |
| **Total** | **1,424,205,225,514** | **(1,387,281,635,924)** | **1,428,998,791,332** | **(1,192,098,194,636)** |

### 13.2.4 Malipo yaliyofanyika kwenye akaunti za OR-TAMISEMI zilizopo BoT lakini hayakuwepo kwenye vitabu vya kumbukumbu ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ni kawaida kwa salio la benki kutokana na rekodi za uhasibu za taasisi kutofautiana na taarifa halisi ya benki kutokana kuwepo kwa tofauti ya muda. Usuluhishi wa kibenki husaidia kugundua tofauti yoyote kati ya rekodi za uhasibu za taasisi na taarifa za benki zinazotokana na tofauti ya muda wa kufanyika na kurekodi miamala husika.

Mapitio ya malipo katika vitabu vyote vya fedha vya Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 ambazo zilitumia mfumo wa TISS kwa malipo, katika akaunti za OR-TAMISEMI zilizopo Benki Kuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017, na taarifa za benki za akaunti tisa za benki za OR-TAMISEMI ambazo zipo Benki kuu zinazotumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote kufanya malipo; nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 26 katika akaunti tano kati ya tisa za OR-TAMISEMI zilizopo benki Kuu zilionekana kuwa na malipo yenye jumla ya SH.TZ 12,703,711,998.32 lakini malipo haya hayakuwepo kwenye daftari za fedha za Mamlaka za Serikali za mitaa husika. Hii ni kinyume na Agizo la 29 (2) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambalo linamtaka Mweka Hazina kuhakikisha kuwa usuluhishi unafanyika, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa akaunti mbali mbali sanjari na kufanya usuluhishi kati ya daftari la fedha na taarifa za benki kila mwezi na kufanya masahihisho ipasavyo.
Pia, hii ni kinyume na Kanuni ya 162 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004) ambayo inahitaji salio la benki kwa kila akaunti kusuluhishwa na daftari la fedha angalau kila mwezi. Angalia **Kiambatisho 13:3** cha hii ripoti.

Muhtasari wa malipo yaliyopo katika Benki lakini hayakuwepo kwenye vitabu vya fedha vya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 13-5 hapo juu. Zaidi ya hayo, ukaguzi wa taarifa za benki na daftari za fedha ulibainisha kuwa ilikuwa ni ngumu kutambua mapato yaliyopokelewa kwenye taarifa ya benki lakini hayapo kwenye daftari la fedha kutokana na kutokuwepo kwa namba au taarifa tambulishi inayoweza kutofautisha mapato yatokanayo na Mamlaka za Serikali za Mitaa moja na nyingine kwenye taarifa hizi mbili yaani ya daftari la fedha na taarifa ya benki.

### 13.2.5 Uwepo wa malipo yaliyofanyika mara mbili yenye jumla ya SH.TZ 328,320,201.65

Mfumo wa malipo ya moja kwa moja katika akaunti za walipwaji kwa kupitia mtandao wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (TISS) unahusisha akaunti za benki tisa (9) za kila Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 zilizopo benki kuu. Akaunti hizi zinatumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinazotumia mfumo wa TISS. Pia, usimamizi wa kifedha unafanywa kupitia Epicor kama ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa TISS isipokuwa malipo kwa njia ya hundi yalibadilishwa kwenda mfumo wa malipo ya moja kwa uhamisho wa fedha wa elektroniki licha ya kwamba TISS na Epicor hazijaunganishwa moja kwa moja (Direct intergrated). Katika mwaka wa fedha 2016/2017, kulikuwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 zilizotumia mfumo wa TISS.

Mapitio ya taarifa tisa (9) za benki kwa akaunti za OR-TAMISEMI zilizopo benki kuu kwa mwaka 2016/2017 yalibaini kuwepo kwa malipo yaliyofanyika mara mbili yenye jumla ya SH.TZ 328,320,201.65. Pamoja na kiasi hiki, malipo ya jumla ya SH.TZ 139,069,961.42 yalilipwa mara mbili kwa watu 17 na makampuni mbalimbali kupitia akaunti zao za benki katika mabenki ya kibiashara. Kiasi kilichobaki cha SH.TZ 189,250,240.23 ilikuwa ni uhamisho mara mbili wa fedha kati ya akaunti za OR-TAMISEMI zilizopo Benki Kuu.

### 13.2.6 Usimamizi wa mradi wa utekelezaji wa TISS usioridhisha

Sehemu ya 5 ya mwongozo wa uendeshaji wa miradi ya TEHAMA wa Wakala wa Mifumo wa Serikali (e-GA) unaelekeza namna ya upangaji na usimamiaji wa miradi inayohusu teknolojia inavyopaswa kuwa. Mpango huo unapaswa kubainisha kazi za mradi ambazo zinahitajika kufanywa na malengo yanayotarajiwa. Hii itajumuisha mawanda ya mradi, utekekelezaji wa mradi na kazi zinazopaswa kufanyika. Sehemu ya 4 ya mwongozo huo inahitaji meneja wa mradi kutambua na kuteua timu ya watu wenye ujuzi sahihi na utaalam binafsi ili waweze kufanya kazi pamoja na kwa usimamizi mdogo, kufanya mikutano na vikao vya mara kwa mara kwa lengo la kutaka kujua

kama malengo na kusudio la mradi linatekelezwa na kufafanua majukumu ya kila mmoja kwa uwazi. Sehemu ya 6 inafafanua kuwa jinsi mradi unavyoendelea, unapaswa kufuatiliwa kwa makini ili kubaini kama unaendelea vizuri, kubaini viashiria vya hatari au tatizo, na taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya mradi zinapaswa kuandaliwa na kupelekwa kwa wadau.

Timu ya ukaguzi ilipitia na kuchambua ripoti zilizotolewa na wataalam wawezeshaji kutoka Wizara ya Fedha wakati wa utekelezaji wa mfumo wa TISS kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 46. Uchambuzi wetu ulibaini kuwepo kwa mapungufu katika kutatua changamoto zitokanazo na mfumo hasa katika ofisi ya kitengo cha malipo (CPO). Kitengo hiki kimekuwa kikisaidiwa na watumishi kutoka Wizara ya Fedha pale wanapohitajika kutoa msaada, hivyo kupelekea kuwepo kwa ugumu wa utatuzi wa mapungufu kutokana na muda mchache wanaopata watumishi kutoka Wizara ya Fedha na vilevile imepelekea ugumu wa kutatua mapungufu ya mfumo kwa wakati. Kulikuwa na changamoto 20 zilizotajwa na mtaalam kutoka Wizara ya fedha tangu Mei 30, 2016, lakini ni changamoto 6 kati ya changamoto 20 zilizokuwa zimetatuliwa mpaka kufikia 28 Februari 2018.

**Mapendekezo**
**TAMISEMI wanashauriwa kufanya yafuatayo:**

i. Kuhuisha mfumo wa Epicor kulingana na mahitaji ya mtumiaji ya usuluhishi wa kibenki hasa kwa kuweka namba ya kumbukumbu ya kila muamala unaofanyika, tarehe za muamala, jina ya mlipwaji, jina la watoa fedha na Fungu au utambulisho wa Mamlaka za Serikali za Mitaa; pia kuwasiliana na benki kuu waweze kuandaa taarifa za benki zinazolingana na taarifa za daftari la fedha ili kurahisisha ulinganifu wa taarifa kati ya Benki (TISS) na Epicor (GL) kupitia Programu ya usuluhishi inayofanyika kwa njia ya TMS.

ii. kuhakikisha malipo ambayo hayakwenda kwa mteja yanayorejeshwa na benki za biashara yanaelekezwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ambako shughuli za malipo zilianzia; na kuzisisitiza Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zenye malipo yao kwenye akaunti ya fedha ambazo hazikutumika, kuhakikisha zinafanya marekebisho kwa wakati kwenda kwenye akaunti za benki husika ili vitabu vya fedha vionyeshe taarifa sahihi.

iii. Kutoa mafunzo stahiki kwa watumiaji wa mfumo, kushughulikia mapungufu yatokanayo na uelewa wa mfumo husika, kurekebisha mfumo wa EPICOR kuruhusu kwa muamala wa mapato na matumizi kuingia kwenye daftari la fedha, mara baada muamala wa benki kuu unapokuwa umekamilika katika akaunti ya TISS. (Miamala kati ya mifumo miwili yaani Epicor na TISS inapaswa kuunganishwa ili kuwezesha mifumo yote miwili kuhuishwa na kutoa taarifa kwa pamoja)

iv. Itumike programu ya kuhamisha mafaili (uploaders) kufanya miamala ya kupeleka mapato kwenye daftari la fedha mara baada ya fedha kupokelewa benki. Pia udhibiti uimarishwe ili kuzuia uanzishaji wa miamala ya uhamishaji wa fedha kutoka kwenye vyanzo vya ndani vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa au akaunti za amana katika mabenki ya kibiashara nje ya mfumo wa EPICOR

v. Kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinaweza kutambua malipo na mapato yote yaliyofanyika kwenye akaunti zao zilizopo Benki kuu.

vi. Kuwapatia watumiaji wa Epicor na TISS mwongozo na vifaa vya mafunzo kama msingi wa maarifa ili kuwawezesha kudhibiti nyaraka katika mifumo ya Epicor na TISS.

vii. Kuandaa mpango/mfumo wa utekelezaji ili kukamilisha masuala yote yaliyojitokeza wakati wa majaribio na kufanya tathmini ya ukubalikaji wa mfumo kwa watumiaji kwenye mifumo wa Epicor na TISS iliyohuishwa.

# SURA YA KUMI NA NNE

## 14.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Ripoti hii inaonesha jitihada tulizozifanya kwa nchi yetu kwa kutimiza wajibu wa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha usimamizi wa fedha za Umma na uwazi unaongezeka katika kuongoza sekta ya Umma.

Wakati wa uandaaji wa ripoti hii, kila Afisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa alitumiwa ripoti za ukaguzi kwa ajili ya kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo katika kurekebisha mapungufu yaliyobainika katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kisha kuuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kama inavyoelekezwa katika Kifungu Na. 40(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.12 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2013) na Kanuni ya 86 na 94 za Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Aya zifuatazo zinatoa majumuisho ya yatokanayo na ukaguzi kwa mwaka 2016/2017 na kutoa mapendekezo yanayopaswa kutekekelezwa.

### 14.1 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi zilizopita

Kama ilivyoelezwa hapo juu, baada ya Maafisa Masuuli kuwasilisha mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kifungu Na. 40 (1) na (2) kinamhitaji Mlipaji Mkuu wa Serikali kuziunganisha na kuwasilisha Ripoti Jumuifu ya Mpangokazi wa Utekelezaji na Mapendekezo ya CAG kwa Waziri husika ambaye ataiwasilisha mbele ya Bunge katika kikao kinachofuata na nakala kutumwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia, Kifungu Na. 40 (4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 kinahitaji Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujumuisha utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka husika.

Wakati wa ukaguzi nilijadiliana na menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu hoja za ukaguzi na ripoti za ukaguzi wa kawaida na kaguzi maalum. Pia nilifuatilia kuona utekelezaji wa

ahadi na kama mpango kazi unapelekea hoja za miaka ya nyuma kutekelezwa.

Licha ya kufanyika kwa mawasiliano, Menejimenti na Mlipaji Mkuu wa Serikali walishindwa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi kwenye Mmamlaka za Serikali za Mitaa; kwani kati ya mapendekezo 14 niliyoyatoa kwenye Ripoti Jumuifu ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, hakuna pendekezo liliotekelezwa kikamilifu. Asilimia 64 yalikuwa yakiendelea kutekelezwa na asilimia 36 hayakushughukiwa kabisa. Sambamba na hilo, kati ya mapendekezo 12,643 niliyotoa kwenye ripoti 171 za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2015/2016, asilimia 34 ya mapendekezo yalitekelezwa, asilimia 25 yalikuwa yakiendelea kutekelezwa, asilimia 25% hayakushughukiwa kabisa na asilimia 16 yalipitwa na wakati.

Aidha, hakuna majibu yaliyopatikana kuhusiana na mapendekezo yatokanayo na kaguzi maalum zilizofanyika miaka mitano iliyopita kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 39.

Vilevile, kati ya maagizo 748 yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kwa mwaka 2015/2016, asilimia 31 yalitekelezwa, asilimia 34 yapo katika hatua za utekelezaji na asilimia 35 hayajatekelezwa.

Hii inathibitisha kutokuwapo kwa jitihada za kutosha kutoka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Iwapo mapendekezo na maagizo hayo hayatafanyiwa kazi, yatasababisha kuendelea kutokea kwa mapungufu kama hayo miaka ijayo.

**Mapendekezo**

- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuweka mikakati na mipango madhubuti kuhusiana na mapungufu yote yaliyojitokeza ili kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo yote ya ukaguzi unafanikiwa. Mikakati hiyo inatakiwa iwe na uhalisia

kiutekelezaji; itekelezwe kwa muda uliopangwa na iweke bayana namna ya utekelezaji.

- Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inapaswa kuongeza ufuatiliaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhakikisha kuwapo kwa mikakati na mipango endelevu ya kuhakikisha kuwa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ambayo hayajatekelezwa yanatekelezwa kwa muda uliopangwa.

## 14.2 Mapungufu katika udhibiti na utekelezaji wa Bajeti

### (i) Ruzuku za Serikali

Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2016/2017 ilikuwa jumla ya Sh.Tz trilioni 5.9, ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa kiasi cha Sh.Tz trilioni 4.9, na ya matumizi ya miradi ya maendeleo kiasi cha Sh.Tz trilioni 1. Hata hivyo, kiasi kilichopokelewa kilikuwa jumla ya Sh.Tz trilioni 4.9 kikijumuisha trilioni 4.4 kwa matumizi ya kawaida na Sh.Tz milioni 564 kwa miradi ya maendeleo.Hivyo, kiasi cha Sh.Tz trilioni 1 sawa na 17% hakikupokelewa. Upokeaji wa ruzuku pungufu ukilinganisha na bajeti unashusha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao kila siku. Pia, kudhoofisha ukamilishaji wa miradi ya maendeleo, hivyo kudidimiza ukuaji wa uchumi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2016/2017 unaonesha kuwa, kati ya fedha zilizokuwepo kiasi cha Sh.Tz trilioni 5.3, jumla ya Sh.Tz trilioni 5.1 kilitumika; ambapo Sh.Tz trilioni 4.6 kilitumika kwa matumizi ya kawaida na Sh.Tz bilioni 529 kilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo, hivyo kiasi cha shilingi bilioni 200 hakikutumika.

Nilielezwa na menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa, kutotumika kwa kiasi hicho kumesababishwa na ucheleshwaji wa fedha za ruzuku kutoka Hazina.

**(ii) Mapato ya ndani**

Mapato ya ndani ni fedha ambazo zimekadiriwa na kukusanywa kugharamia shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Usimamizi sahihi wa mapato husababisha kuboresha ukusanyaji, hivyo kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Wakati wa ukaguzi, Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 zilipanga kukusanya SH.TZ bilioni 627 kutokana na mapato ya ndani. Hata hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya Sh.Tz bilioni 520 hivyo kupelekea makusanyo pungufu ya SH.TZ bilioni 107 sawa na asilimia 17 ya kiasi kilichokadiriwa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliripoti kuwa, hali ya hewa isiyoridhisha iliyojitokeza mara kwa mara kuwa ndiyo ilipelekea kushuka kwa ushuru wa mazao ambao hutegemea hali nzuri ya hewa. Vyanzo vikubwa vya kukusanya mapato kwa Serikali za Mitaa ni ushuru wa huduma, ada za masoko, ushuru wa mazao, ushuru wa huduma maalumu, ada ya leseni na vibali vya biashara.

**Mapendekezo:**

- Ninahimiza Wizara ya Fedha, kupitia Hazina, kutoa fedha kwa wakati kulingana na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili fedha zitumike kwa shughuli zilizopangwa, hivyo kupunguza kiwango cha shughuli ambazo hazijatekelezwa.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa, kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zinapaswa kuwasiliana na Hazina juu ya athari za kutolewa fedha pungufu hadi kusababisha kutokufikia malengo yaliyokusudiwa.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuibua na kutumia vyanzo vingine vya mapato ili kupunguza athari za upungufu wa fedha za ruzuku na na kupunguza utegemezi toka ushuru wa mazao ambacho ndio chanzo kikuu cha mapato ya ndani. Hii ni kwa sababu chanzo hiki kinategemea sana hali ya hewa.

## 14.3 Mapungufu katika Udhibiti wa Ndani na utawala bora

Ili kuboresha na kudumisha yatokanayo na ukaguzi, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kudumisha ufanisi kwenye mfumo wa udhibiti wa ndani kama ulivyoainishwa kwenye Agizo Na. 10 na 25(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

Wakati wa ukaguzi imeonekana kuwa kuna kujirudiarudia kwa mapungufu yahusuyo mfumo wa udhibiti wa ndani wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, hususani kukosekana kwa sera ya mambo yahusuyo teknolojia, ambapo inaweza kupelekea kuwa na usimamizi usioridhisha na kutokuwapo kwa udhibiti madhubuti wa vifaa kama kompyuta na mifumo wa ndani wa kompyuta. Pia, husababisha watumishi kutojengewa uwezo wa masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Vilevile, nilifanya tathmini kuhusu kuwapo kwa Kamati ya Ukaguzi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na majukum yake. Nilibaini kuwa, kwa kiwango kikubwa, Kamati hizi zinashindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu kutokana na kukosekana kwa rasilimali pamoja na wajumbe kukosa maarifa ya namna ya kutekeleza majukumu yao.

**Mapendekezo**

Nashauri iwepo sera madhubuti ya usimamizi wa masuala yahusuyo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Pia, watumishi wanatakiwa kujengewa uwezo kwenye masuala ya teknolojia. Zaidi, Kamati za Ukaguzi zinapaswa kuwezeshwa kikamilifu ili kuweza kutimiza majukumu yao ipasavyo.

## 14.4 Mapungufu katika Usimamizi wa Mapato

Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina uwezo wa kukusanya mapato ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za utawala na maendeleo, bali hutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. Ukaguzi unaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kufanya vibaya kwenye ukusanyaji wa mapato kutokana na ukusanyaji usioridhisha wa madeni ya mapato kutoka kwa wadaiwa, mzunguko mdogo wa fedha na kukosekana kwa mbinu

madhubuti za ukusanyaji wa mapato. Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 zilishindwa kukusanya mapato kwa asilimia 17 kutoka kwenye vyanzo vyake ikilinganishwa na upungufu ya asilimia 10 kwa mwaka 2015/2016. Wakati huohuo, makusanyo kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato si ya kuridhisha kwa kuwa wameshindwa kukusanya jumla ya Sh.Tz 3,538,329,470.

Ukusanyaji usioridhisha wa mapato unasababishwa na kukosekana kwa jitihada madhubuti ndani ya Idara ya Fedha, hali isiyoridhisha ya hewa, pamoja na mfumo usioridhisha wa ukusanyaji mapato ambapo sio tu unaathiri ukusanyaji wa madeni ya mapato bali pia unapelekea kuwapo kwa takwimu zisizo sahihi zihusuzo wadaiwa kwenye taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa .

Ukusanyaji wa mapato usioridhisha unapelekea kudhoofisha upatikanaji wa huduma za msingi kwa jamii.

**Mapendekezo**

Nakazia mapendekezo niliyotoa miaka ya nyuma kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha inaboresha ukusanyaji wa mapato, kuwezesha wadau kufuata sheria na kanuni mbalimbali. Pia, nahimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia ipasavyo vyanzo vya mapato vilivyopo ili kuongeza mapato kufikia malengo yaliyokusudiwa, hivyo kupunguza utegemezi toka Serikali Kuu.

## 14.5 Udhaifu katika Usimamizi wa Rasilimali Watu

Usimamizi mzuri wa rasilimali watu kwa vitendo ni nguzo kuu ya kuimarisha usimamizi wa udhibiti wa ndani. Upungufu wa wafanyakazi na kukosekana kwa ujuzi huathiri muundo, utekelezaji na ufuatiliaji wa udhibiti wa ndani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Moja ya changamoto kubwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani Halmashauri za Wilaya, ni jinsi ya kuwavutia na kuwalinda wafanyakazi wenye ujuzi na Umahiri kwenye maeneo yote ya uongozi. Vilevile nafasi nyingi za Wakuu wa Iidara zinakaimiwa na watumishi ambao hawajathibitishwa kujaza nafasi hizo. Kuwapo

kwa watumishi wanaokaimu nafasi za ukuu wa idara kunasababishwa na kuwapo kwa watumishi wasio na sifa zinazokidhi pamoja na mamlaka teuzi kuchelewa kuteuwa watumishi wanaostahili kujaza nafasi hizo. Pia, muundo wa utumishi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa mpya 14 zilionesha Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 zina maofisa 67 wanaokaimu ukuu wa idara na vitengo. Maofisa wanaokaimu wanashindwa kutekeza majukumu yao kikamilifu kwa sababu ya kutokuwa na mamlaka ya kutoa maamuzi sahihi kwa mujibu wa majukumu ya kazi walizopewa.

Pia, nilitathmini idadi ya watumishi  katika Serikali za Mitaa 161 na niliona uhaba wa watumishi 155,013 sawa na asilimia 32 ya idadi inayohitajika ya watumishi 477,829. Uchambuzi kwa miaka mitatu mfululizo unaonesha kupungua kwa rasilimali watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa japokuwa kuna mapendekezo niliyowahi kuyatoa kuhusiana na suala hili miaka iliyopita.

Kazi iliyofanyika hivi karibuni ya kuhakiki sifa za kitaaluma za watumishi wa umma imeongeza upungufu wa watumishi,hususani idara na vitengo muhimu zaidi katika shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa kama elimu, afya na kilimo.Idara hizi zimeathirika zaidi kutokana na upungufu huo.

Kufuatia upungufu niliouelezea, ufanisi na ubora wa utoaji wa huduma kwa Mamlaka za Serikali za Serikali za Mitaa utaathiriwa kwa sababu watumishi waliopo sasa wanawajibika kufanya kazi zaidi hivyo ubora na umakini utapungua.

**Mapendekezo**

Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zinashauriwa kupanga vizuri na kupunguza idadi ya watumishi wanaokaimu nafasi za ukuu wa idara na vitengo kwa kuwathibitisha au kuteua wengine wapya wenye sifa kwenye nafasi hizo. Sambamba na hilo, nasisitiza kuwa Serikali ihakikishe upungufu wa watumishi kwa mujibu wa ikama ya

utumishi unapatiwa ufumbuzi ili kuongeza na kuboresha huduma zinazotolewa kwa jamii.

## 14.6 Mapungufu katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Miradi ya Maendeleo ni miradi ya uwekezaji wa muda mrefu inayohitaji kiasi kikubwa cha fedha katika kuanzisha, kutekeleza, kuboresha na kuendeleza rasilimali mali.

Uchunguzi uliofanywa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa ukaguzi umebaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 zilibakiwa na kiasi cha shilingi bilioni SH.TZ .265.1 sawa na asilimia 33 ya fedha iliyokuwepo.Nimeona jitihada kidogo za kuridhisha katika matumizi ya ruzuku ya miradi ya maendeleo, ambapo kwa mwaka 2015/2016 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilibakia na kiasi cha shilingi bilioni SH.TZ 213 sawa na asilimia 36 ya jumla fedha zilizokuwepo.

Kuwapo wa fedha zilizobakia mwisho wa mwaka kunamaanisha kwamba, kuna kasi isiyoridhisha katika kutekeleza miradi ya maendeleo au fedha hizo zilichelewa kutolewa na Hazina.

**Mapendekezo**

Ninapendekeza kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zianzishe utaratibu wa ufanisi ambao utahakikisha kwamba miradi yote ya maendeleo iliyopangwa kwa kutumia rasilimali inatekelezwa na kukamilika kwa kuzingatia muda na gharama ili kuongeza upatikanaji wa huduma bora kwa jamii na Taifa.

## 14.7 Mapungufu katika Kuzingatia Sheria za Manunuzi na usimamizi wa ya mikataba

Ukaguzi wa manunuzi ya bidhaa na huduma kwa mwaka wa fedha 2016/17 ulifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 zilitumia jumla ya SH.TZ trilioni 1.36 kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma. Kuongezeka kwa matumizi ya manunuzi kunasababishwa na kuanzishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 14 ambazo zimekaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka wa

2016/17. Serikali ilitoa fedha kugharamia matumizi ya miradi ya maendeleo, manunuzi vya bidhaa na huduma na gharama za matengenezo ili kuendeleza shughuli za kila siku katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zimesababisha uwepo wa shughuli nyingi za manunuzi.

Maelezo ya jumla ya mchakato wa manunuzi na usimamizi wa mkataba wakati wa ukaguzi yameonesha mapungufu yaliyoendelea kutokea mara kwa mara katika mchakato wa manunuzi na usimamizi wa mikataba. Mapungufu hayo yanaweza kuwa na athari ya kifedha, hasa kwa kuwa yanaweza kusababisha matumizi yasiyo na tija.

Mapungufu yaliyobainishwa kwa miaka mitatu mfululizo yanahusiana na kutofuatwa kwa taratibu sahihi za manunuzi; nukuu tatu za bei au zabuni za ushindani kutotumika kuwezesha uteuzi wa muuzaji kulingana na mchakato wa ushindani na wa haki. Wakati mwingine, bidhaa na huduma zilipatikana bila kibali cha bodi ya zabuni, bidhaa au huduma hazikuwa na kipaumbele, hivyo, kutokuwekwa kwenye mpango wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, bidhaa na huduma zilinunuliwa nje ya orodha iliyoidhinishwa na kutambulika na Wakala wa Manunuzi Serikalini; na, mara kwa mara, bidhaa na huduma hazikuthibitishwa kupokelewa.

Hali hii ina athari kwenye matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo, mara nyingi, bidhaa au huduma zinapatikana kwa bei kubwa zaidi na thamani ya fedha haikupatikana kutokana na kutokuwapo kwa udhibiti inaohakikisha kuwa michakato ya ushindani na ya haki inafanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutochukuliwa tahadhari katika suala hili kutapelekea kuwapo kwa matumizi ya manunuzi yasiyo na tija kila mwaka.

**Hitimisho**

Mapungufu yaliyoainishwa yanahitaji hatua za haraka na zinazozingatia kanuni za usawa, uwazi, ukamilifu, na ufanisi wa

gharama katika mchakato wa ununuzi unaotumika mara kwa mara. Pia, ihakikishwe kuwa watumishi wa idara ya manunuzi wana sifa wanazopaswa kuwa, nazo kwa mujibu wa Kifungu Na. 37(2) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (2011). Zaidi, Bodi ya Manunuzi ijumuishe timu sahihi ya wajumbe ili kuwezesha kufanyika kwa manunuzi yanayoendana na thamani ya fedha iliyotumika.

## 14.8 Mapungufu katika kusimamia matumizi

Usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma kwa ujumla unasisitiza utekelezaji wa mambo matatu, yaani nidhamu ya fedha, ufanisi kwenye ugawaji wa fedha, na ufanisi katika uendeshaji. Nidhamu ya matumizi ya fedha ina maana serikali kutotumia zaidi ya kiasi kilichopangwa kutumika. Ufanisi kwenye ugawaji wa fedha humaanisha serikali kutumika kwenye mambo sahihi. Na ufanisi katika uendeshaji unamaanisha kuwa upatikanaji wa huduma zenye ubora na kwa gharama nafuu.

Ili kufikia utekelezaji wa mambo matatu yaliyotajwa hapo juu, serikali ilianzisha sheria mbalimbali, kanuni, sera na mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo kila Mamlaka za Serikali za Mitaa inahitajika kutekeleza.

Kwa ujumla, utekelezaji unaonesha kasi isiyoridhisha, kwani kwa miaka mingi kunakuwa na mapungufu yanayofanana.Mapungufu hayo yanajumuisha; matumizi yasiyo na nyaraka sahihi, kukosekana kwa hati za malipo, madeni yatokanayo na uhamisho wa fedha kutorudishwa, na matumizi kufanyika nje ya vifungu vya matumizi vinavyostahili. Pia, kuna mapungufu ya matumizi katika akaunti ya amana ambapo malipo yalifanyika bila kuonesha kibali cha malip; na mara nyingine, kiasi kilichokopwa katika akaunti ya amana kilisalia bila kulipwa kwa muda mrefu, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa za akaunti ya amana.

Kuna maendeleo kidogo katika eneo la uwekaji wa viambatisho kwenye hati za malipo. Pia, tatizo la kukosekana kwa hati za malipo pindi zinapohitajika kwa ukaguzi limepungua idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokuwa na mapungufu hayo zimepungua kutoka 146 kwa mwaka 2015/2016 na kuwa 130 kwa

mwaka 2016/2017. Pia, kiasi cha fedha kupungua kutoka Sh.Tz bilioni 12.9 mpaka Sh.Tz bilioni 5.8. Vilevile, kuna mabadiliko chanya kwenye matumizi yaliyolipwa kwa vifungu visivyo sahihi, kwani kiasi kimepungua kutoka Sh.Tz bilioni 3.3 2015/2016 hadi Sh.Tz bilioni 1.7 kwa mwaka 2016/2017 na idadi ya hoja za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupungua kutoka 62 (2015/2016) hadi 44 (2016/2017).

Ingawa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikifanya jitihada na juhudi katika kurekebisha mfumo wa udhibiti wa ndani, pia kuna baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa bado zinahitajika kufanya maboresho ya mifumo yao ya udhibiti wa ndani. Nina matumaini kuwa idadi na aina za mapungufu ya ukaguzi vitaendelea kupungua; na kwamba, hii inaweza kuwa mwanzo wa mwenendo mzuri katika kaguzi zijazo.

**Mapendekezo**

Napendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa ziboreshe mifumo wa udhibiti wa ndani hususani utunzaji wa nyaraka za matumizi, kuandaa bajeti yenye uhalisia, kuwasiliana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuboresha udhibiti wa bajeti kwenye mfumo wa malipo (Epicor) na iwapo kwa bahati mbaya matumizi yamefanyika nje ya vifungu sahihi, idhini ya mapitio ya bajeti ifanyike ili kurekebisha makosa ambayo yanaathiri usahihi wa Taarifa za Fedha.

## 14.9 Usimamizi usioridhisha wa Mali

Natia shaka jinsi rasilimali za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyosimamiwa. Licha ya ukweli kwamba viwango vya uandaaji wa hesabu pamoja na maagizo vinaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhifadhi vyema kumbukumbu za rasilimali mali, bado kuna mapungufu katika kutambua na kuthaminisha mali za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sababu mojawapo ni kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina rejista zinazotunza taarifa ya mali na zingine kutoandaliwa kama inavyotakiwa kiasi cha kusababisha hupelekea mali nyingi kutokuwa na thamani lakini bado zinatumika. Kuwapo kwa magari chakavu pasipo kutolewa maamuzi ya ama yauzwe ama

yatengenezwe; kutoorodheshwa kwa mali za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye taarifa za fedha; kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa bidhaa zilizopo ghalani na pia kuwepo kwa kiwango kikubwa cha fedha za wadaiwa wa muda mrefu.

**Mapendekezo**

Kwa kuboresha zaidi taarifa za fedha; ninazikumbusha Mamlaka za Serikali za Mitaa zote kuandaa na kuhifadhi vyema rejista za mali zisizohamishika kwa mujibu wa Mwongozo wa Fedha wa Serikali za Mitaa, 2009 na zinapaswa kusahihishwa mara kwa mara kwa kurekodi taarifa zote muhimu kwa mali zote; kuharakisha uuzaji wa mali ambazo hazitumiki na zinaonekana kuongeza gharama za kuziendesha ama kuzitengeneza kwa mujibu wa sera na taratibu za uuzaji wa mali za Umma; pia kuharakisha mchakato wa ulipwaji wa madeni ya wadai ya muda mrefu na kufuatilia wadaiwa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili waweze kulipa madai yao na kuwezesha malipo kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 14.10 Mapendekezo kwa Serikali kupitia Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008

Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa mapendekezo kwa lengo la kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyo na tija; kuongeza ukusanyaji wa mapato; kuzuia hasara zinazohusu mali na fedha za umma zinazosababishwa na uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu na rushwa. Mapendekezo hayo yatatayarishwa na kuwasilishwa kwa Waziri husika kama nitakavyoona inafaa kwa kuboresha usimamizi wa mali na fedha za umma ikiwa ni pamoja na kurekebisha Kanuni, Miongozo au Maagizo yanayotolewa kupitia sheria zinazotambulika.

Katika kutekeleza jukumu langu la ushauri chini ya sheria iliyotajwa hapo juu, napendekeza Serikali ichukue tahadhari kwa kuzingatia na kuyapatia ufumbuzi masuala yafuatayo:

a) Kuboresha makusanyo yatokanayo na kodi ya majengo na ada za mabango
b) Uwekaji wa mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kuwepo kwa mazingira ya rafiki ya mfumo
c) Sheria na kanuni zinazopaswa kuangaliwa ili kuona uwezekano wa kufanyiwa mabadiliko

**a) Kuboresha makusanyo yatokanayo na kodi ya majengo na ada za matangazo kutoka kwenye mabango**

Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (CAP 290) (kama ilivyorekebishwa mwaka 2000) iliyoanzishwa na Kifungu Na. 38 cha Sheria ya Fedha ya 2016 imeipa jukumu Mamlaka ya Mapato Tanzania kukadiria, kutathmini, kukusanya na kuweka rekodi ya ukusanyaji wa kodi za majengo.

Pia Kifungu Na. 74 cha Sheria ya Fedha ya 2016 kinabadilisha Sheria za Mamlaka ya Mjini ya mwaka 1983 (CAP 289) kwa kufuta kifungu Na. 16 cha Sheria mama.

Marekebisho ni kama ilivyoelezwa hapo chini:

- Kifungu Na. 16 (1) kinahitaji, Waziri (Waziri wa Fedha na Mpango) kwa ushirikiana na Waziri anayehusika na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na baada ya kupata uwakilishi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuweka viwango kwa ajili ya eneo hilo ndani ya Tanzania Bara;

- Kifungu Na. 16 (2) kinahitaji, mapato yaliyokusanywa chini ya Sheria lazima yawekwe katika akaunti maalum inayopaswa kufunguliwa na Waziri (Waziri wa Fedha na Mpango) katika Benki ya Tanzania (BoT) kwa manufaa ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- Kifungu Na. 16 (3) kinahitaji, mgawanyo na usambazaji wa mapato yaliyowekwa katika akaunti iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) kuwa unapaswa kufanywa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa kanuni

zilizotolewa na Waziri baada ya kushauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa mwaka 2016/2017, Mamlaka ya mapato Tanzania iliweza kukusanya jumla ya SH.TZ 23,443,673,850 ikiwa ni kodi ya majengo kutoka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 32. Hata hivyo, nilishindwa kuthibitisha utekelezaji wa taratibu zilizowekwa na Waziri za kutoa fedha za kodi zilizokusanywa na kiasi kilichotolewa kwa kila Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Pia, Sura ya 31A (1) ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2017), inaipa TRA mamlaka ya ziada ya kukadiria, kutathmini, kukusanya na kupokea ada za matangazo kutoka kwenye mabango.

Zaidi ya hayo, marekebisho yaliyofanywa mwaka 2017 kwa Sheria ya Mamlaka ya 1983 (Sura 289) imefuta Kifungu Na. 16 (2) na kuingiza vifungu vipya; (2) na (2A) ambavyo vinatoa maelekezo kuwa kiwango cha fedha kinachokusanywa na TRA kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu na ugawaji wa fedha za mapato yaliyokusanywa kupelekwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na bajeti yake.

**Mapendekezo**

Ili kuongeza makusanyo, nashauri Serikali yafuatayo:

a) Kuanzisha utaratibu ambapo TRA itashirikiana na Wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mitaa kutambua na kugawa ankara kwa ajili ya mali zinazopimwa pamoja na mabango. Hii ni kutokana na TRA kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha kuwezeza kukusanya kwa kiwango cha juu kodi hizo kutoka katika Miji, Manispaa na Majiji.
b) Kurekebisha kifungu Na. 16 (3) cha Sheria ya Miji ya mwaka 1983 (Imebadilishwa 2016) ambacho kwa maoni yangu kinakinzana na Kifungu Na.16 (2) ya Sheria ya Miji ya 1983 (iliyorekebishwa 2017) kinachohitaji Waziri kutoa kanuni za

kuongoza ugawaji wa mapato yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Serikali za Mitaa wakati Sura ya 16 (2) inaelekeza kuwa mapato yaliyokusanywa kurejeshwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na bajeti yake.

c) Kupitia Kifungu Na. 6 (1) cha Sheria ya Miji ya mwaka 1983 (iliyorekebishwa 2017) kuzifikiria Halmashauri za Wilaya kama eneo linaloweza kukutumika kukusanya kodi za majengo ili TRA iwe na mamlaka ya kukusanya na kuwajibika kukusanya pia kwenye Wilaya.

**b) Uwekaji wa mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kuwepo kwa mazingira ya rafiki mfumo**

Nilitathmini mazingira ya Teknolojia ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusiana na uendeshaji wa mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) na kutambua uwepo wa udhaifu mkubwa kama vile kutokuwa na uanzishwaji wa kamati za uendeshaji wa ICT, kukosekana kwa mpango wa mfumo na mipango ya kimkakati ya ICT, kukosekana kwa mpango wa kuondoa athari zitokanazo na mfumo wa ICT, mipango endelevu ya mfumo wa ICT na Sera ya ICT.

Kwa maoni yangu, mazingira ya uendeshaji wa ICT katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hayajawahi kuwa rafiki na hayaendani na uwekezaji wa serikali unaoendelea katika upatikanaji na uwekaji wa mifumo mbalimbali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mantiki hiyo, masuala muhimu yaliyopo kwenye mifumo kama vile utawala bora wa mifumo, usiri, uaminifu na upatikanaji wa habari za Mamlaka za Serikali za Mitaa hayashughulikiwi vizuri katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hivyo huhatarisha uhakika wa taarifa zote za fedha na usimamizi zinazozalishwa kutoka mifumo hii.

Wakati wa tathmini sikuweza kuthibitisha kama Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwa ndio watumiaji wa mwisho zilipata fursa

ya kutoa maoni yao na mapendekezo juu ya usahihi wa mifumo iliyopo na mazingira halisi ya uendeshaji kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mfano, nilishuhudia uwepo wa mifumo kama vile Lawson, BEMIS, LGRCIS, Planrep, MIS na zaidi ambayo haijaunganishwa au kuingiliana na mifumo mikuu ya Serikali kama vile Epicor. Mifumo isiyo tegemezi na mifumo pishanishi ni vigumu kuisimamia na hupelekea udurufu wa kazi zinazofanana hivyo kupelekea kuongezeka kwa hatari ya makosa wakati wa kuunganisha taarifa kutoka kwenye mifumo tofauti.

Zaidi ya hayo, nilibaini kutokuwepo kwa mafunzo ya kutosha kuhusu uendeshaji wa mifumo hii na kutokuwepo kwa uboreshaji wa mifumo inayosababishwa na ukosefu wa fedha za kujenga uwezo. Watumiaji wengi wa mifumo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa hawajahudhuria mafunzo. Mafunzo ya muda mfupi ambayo yalifanyika kwa namna isiyokidhi malengo ya mifumo ilipelekea kuwepo kwa pengo la ujuzi kwa masuala ya ICT. Wakaguzi wa Ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao ni sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wana ufahamu mdogo juu ya mifumo hii. Pia nilibaini kuwa, baadhi ya badilifu (modules) za mifumo zilizo na leseni ya matumizi hazijaboreshwa au hazitumiki kutokana na kutokuwepo kwa ujuzi na uwezo kwa watumiaji na pia kwa kiwango kikubwa taarifa za hesabu bado zinaandaliwa nje ya mfumo.

**Mapendekezo**

Ninapendekeza Serikali kuhakikisha kuwa changamoto za mazingira ya ICT zinashughulikiwa kikamilifu ili kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakabiliana na uwekezaji wa Serikali katika ICT ili kukuza uaminifu katika usimamizi wa fedha na uandaaji sahihi wa taarifa.

Zaidi ya hayo, Serikali iwe ikizifanyia kazi changamoto zinazoonekana wakati wa kujaribu mfumo kwenye maeneo ya majaribio kabla ya mfumo kuanza kutumika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote na kuandika somo walilolipata kwa ajili ya

maamuzi ya baadae wakati wa ununuzi wa mifumo mipya. Wakati wa uchunguzi na majaribio, Serikali inashauriwa kuwashirikisha kwa karibu Mamlaka za Serikali za Mitaa kama mtumiaji wa mwisho na mnufaika wa mifumo.

Serikali inapaswa kuzingatia pia upatikanaji wa mifumo ambayo inaweza kuunganishwa au kuingiliana na Mfumo Mkuu ili kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo hii.

Pia ninaishauri Serikali wakati mchakato wa bajeti kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga uwezo ili kupunguza pengo la ujuzi na kuongeza matumizi sahihi na kamili ya mifumo hii.

**c) Changamoto zilizopo kwenye Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake, pamoja na kanuni za bodi za zabuni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Katika ukaguzi wa manunuzi nilibaini baadhi ya mapungufu ambayo kwa mtazamo wangu yalikuwa yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na mianya iliyopo kwenye sheria za manunuzi. Yafuatayo ni baadhi ya mianya niliyoibaini:

**(i) Kanuni Na. 166 (1) na (2) za Kanuni za Manunuzi ya Umma**

Kanuni hii inahusiana na manunuzi madogomadogo ambapo Kanuni ndogo Na. 166 (1) inatanabaisha kuwa manunuzi madogo yanaweza kufanywa na Taasisi kwa kununununua moja kwa moja kutoka maduka makubwa, maduka au maduka ya madawa, au sehemu zinazofanana na hizo ikiwa gharama za manunuzi hayo hayazidi ukomo wa SH.TZ 5,000,000 uliowekwa kwenye jedwali la saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma.

Kanuni ndogo ya 2 pia inaelezea kuwa mchakato wa manunuzi madogomadogo hauhitaji yafuatayo:

(a) Nyaraka za maombi ya manunuzi;
(b) Maombi ya zabuni;
(c) Ufunguzi wa zabuni;
(d) Nukuu ya mshindi wa zabuni; au
(e) Nyaraka za mkataba uliosainiwa.

Zaidi ya hayo, Kanuni kidogo ya 4 inaelekeza kuwa Taasisi inaweza kulipa malipo madogomadogo kwa kutumia fedha taslimu, masurufu au kadi za manunuzi.

Kanuni tajwa hapo juu zimepelekea kuwepo kwa mianya kwenye manunuzi ya Umma hususani:

- Manunuzi ya bidhaa na huduma kufanyika kwenye maduka ya rejareja na maduka ya vinywaji kwa kudhania na kuamini ya kuwa neno "maduka makubwa, maduka au maduka ya madawa, au sehemu zinazofanana na hizo" yanajumuisha maduka ya rejareja na maduka ya vinywaji. Kuna haja ya kutolewa ufafanuzi wa ziada kuhusiana na neno "sehemu zinazofanania" ili kuwe na uelewa wa pamoja ni sehemu gani sahihi ambayo taasisi zinapaswa kwenda kufanya manunuzi madogomadogo.

- Kuna hatari ya kugawanya kiwango cha manunuzi ili manunuzi yasizidi ukomo wa SH.TZ 5,000,000 ili kukwepa manunuzi kwa njia ya ushindani.

- Manunuzi toka kwa wauzaji holela kunapelekea kuwepo kwa manunuzi ya bidhaa zisizokuwa na ubora kwa gharama kubwa; na mara nyingi bei za bidhaa zinazotozwa huenda hazitokani na ushindanishi wa bei.

- Manunuzi madogomadogo yanainyima fursa Taasisi husika kukusanya mapato yatokanayo na malipo yanayofanyika kwa hundi yakiwemo ushuru wa huduma na kodi ya zuio.

- Utumiaji wa fedha taslimu na masurufu kwa manunuzi madogomadogo unaweza kupelekea uwepo kwa manunuzi yasiyo na tija na yasiyopangwa.

**(ii) Kanuni Na. 58 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma,2013**

Kanuni hii inatoa mwongozo wa kuidhinisha manunuzi kupitia azimio la bodi ya zabuni, yaani maamuzi ya bodi ya zabuni bila kufanyika kikao bali zinazungushwa nyaraka kwa wajumbe wa bodi

ya zabuni ili wasome na kuidhinisha au kutoa sababu kimaandishi kuelezea kutokubaliana na yaliyomo kwenye nyaraka hizo. Nusu ya wajumbe wa bodi ya zabuni inakidhi akidi na inawakilisha Bodi nzima ya zabuni kwenye uidhinishaji wa manunuzi kwa njia ya kuidhinisha manunuzi kupitia azimio la bodi ya zabuni.

Kanuni ndogo ya 1 inaelezea kuwa, maamuzi ya Bodi ya Zabuni yanaweza kufanywa na Bodi ya Zabuni pasipo kuwepo kikao kupitia uidhinishaji manunuzi kwa njia ya azimio la bodi ya zabuni

Hatahivyo kuna mianya hutokea wakati wa kutekeleza Kanuni hii ikiwepo ifuatayo:

(a) Hakuna ukomo wa kiwango cha udhinishaji wa manunuzi kupitia uidhinishaji manunuzi kwa njia ya azimio la bodi ya zabuni, ambapo wakati mwingine manunuzi yanahusisha kiasi kikubwa cha fedha yaliyopitishwa kupitia njia hiyo. Kwa kutumia uidhinishaji manunuzi kwa njia ya azimio la bodi ya zabuni, inaminya fursa kwa Bodi ya Zabuni kupitia kwa ukaribu na kwa pamoja mchakato wa manunuzi.

(b) Hata hivyo, kanuni ndogo ya 3 inaelekeza kuwa mjumbe yeyote wa Bodi ya Zabuni ana haki ya kuomba maamuzi yaliyofanyika huko nyuma kujadiliwa kwenye kikao cha Bodi ya Zabuni lakini inaweza isiwezekane ikiwa akidi ya wajumbe wa Zabuni ilikosa uadilifu, ujuzi au haikuzingatia sheria na kanuni za manunuzi ya Umma.

(c) Kanuni ndogo ya 4 inaelezea kuwa “nusu ya wajumbe wa Bodi ya Zabuni watakaunda akidi ya maamuzi ya Bodi nzima ya Zabuni”. Nashauri kuwa uwiano wa wajumbe wanaopaswa kuunda akidi unatakiwa kuzidi nusu ya wajumbe ili kupunguza hatari ya kuwepo kwa maamuzi yasiyo sahihi.

**(iii) Uhitaji wa kulinganisha Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma**

Kwa sasa kuna sheria mbili za manunuzi ya Umma zinazotumika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni Sheria ya Manunuzi

ya Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake pamoja na Kanuni za Bodi za zabuni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014.

Nimekuja kuona kuwa kuna kanuni mbili zinazokinzana kuhusiana na ushiriki wa mwakilishi wa idara nufaika na manunuzi wakati wa tathimini ya Zabuni za Idara husika.

Kifungu Na. 39(1)(e) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2011, inaeleza kuwa idara nufaika kwenye Taasisi inayofanya manunuzi inatakiwa iwe na mwakilishi kwenye timu ya tathimini ya Zabuni kwa Idara husika. Maelekezo haya yanakinzana na Kanuni ya 27(3) ya Kanuni za Bodi za zabuni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 inayoeleza kuwa mwakilishi wa idara nufaika na manunuzi husika hatakiwa kuwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya kutathimini Zabuni.

Hili mojawapo ya jambo linalooonesha ukinzani kwenye matumizi ya Sheria za manunuzi. Hivyo nashauri Serikali kuondoa mwingiliano wa Sheria na Kanuni kwenye manunuzi ya Umma.

**(iv) Ongezeko la muda kwenye Mikataba**

Kifungu Na. 77(3) cha Sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 kinaelekeza kuwa ongezeko la muda litaongezwa na Afisa Masuuli kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa kwenye kanuni za manunuzi ya umma.

Kanuni ya 111 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inaongelea kuhusu ongezeko la muda kwenye mikataba, na kanuni ndogo ya kwanza (1) inaelekeza kuwa amri ya ongezeko la muda kwenye mikataba linaweza kutolewa pekee na Afisa Masuuli na sababu zilizopelekea ongezeko hilo zinapaswa kuainishwa kwenye kumbukumbu za kutekeleza Mradi.

Hata hivyo, Kanuni haijaeleza bayana ukomo wa muda na ukomo wa idadi kwenye ongezeko la muda linalopaswa kutolewa na Afisa Masuuli kwenye Mkataba. Hii hupelekea kuwe na mwanya kwa Mkandarasi kupewa muda wa nyongeza kuzidi muda wa mwanzo

mkataba. Hivyo kupelekea kuchelewa kutekeleza shughuli za mikataba husika na hupelekea ongezeko la bei kwenye mikataba.

# VIAMBATISHO

## 2.0 HATI ZA UKAGUZI

### Kiambatisho 2.0:1: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Hati inayoridhisha

| Na. | Jina la Halmashauri | Na. | Jina la Halmashauri | Na. | Jina la Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 42 | H/M Musoma | 83 | H/W Kondoa |
| 2 | H/W Arusha | 43 | H/W Mvomero | 84 | H/Mji Kondoa |
| 3 | H/W Babati | 44 | H/W Mwanga | 85 | H/W Kongwa |
| 4 | H/W Bagamoyo | 45 | H/Jiji Mwanza | 86 | H/Mji Korogwe |
| 5 | H/W Bahi | 46 | H/W Nachingwea | 87 | H/W Kwimba |
| 6 | H/W Bariadi | 47 | H/W Namtumbo | 88 | H/W Kyela |
| 7 | H/Mji Bariadi | 48 | H/Mji Nanyamba | 89 | H/W Kyerwa |
| 8 | H/W Biharamulo | 49 | H/W Nanyumbu | 90 | H/W Lindi |
| 9 | H/W Buhigwe | 50 | H/W Newala | 91 | H/M Lindi |
| 10 | H/W Bukoba | 51 | H/W Nkasi | 92 | H/W Liwale |
| 11 | H/W Bukombe | 52 | H/Mji Newala | 93 | H/W Ludewa |
| 12 | H/W Bumbuli | 53 | H/W Ngara | 94 | H/W Nsimbo |
| 13 | H/W Bunda | 54 | H/W Ngorongoro | 95 | H/W Nyang'hwale |
| 14 | H/Mji Bunda | 55 | H/W Njombe | 96 | H/W Nyasa |
| 15 | H/W Busega | 56 | H/Mji Njombe | 97 | H/W Nzega |
| 16 | H/W Busokelo | 57 | H/W Iringa | 98 | H/Mji Nzega |
| 17 | H/W Butiama | 58 | H/M Iringa | 99 | H/W Rorya |
| 18 | H/W Chalinze | 59 | H/W Itigi | 100 | H/W Ruangwa |
| 19 | H/W Chamwino | 60 | H/W Itilima | 101 | H/W Rufiji |
| 20 | H/W Chato | 61 | H/Mji Kahama | 102 | H/W Rungwe |
| 21 | H/W Chemba | 62 | H/W Kakonko | 103 | H/W Same |
| 22 | H/W Chunya | 63 | H/W Kalambo | 104 | H/W Sengerema |
| 23 | H/Jiji Dar es Salaam | 64 | H/W Kaliua | 105 | H/W Serengeti |
| 24 | H/M Dodoma | 65 | H/W Karagwe | 106 | H/W Shinyanga |
| 25 | H/W Gairo | 66 | H/W Karatu | 107 | H/M Shinyanga |
| 26 | H/W Geita | 67 | H/W Kasulu | 108 | H/W Sikonge |
| 27 | H/Mji Geita | 68 | H/Mji Kasulu | 109 | H/W Singida |
| 28 | H/W Hai | 69 | H/W Kibaha | 110 | H/M Singida |
| 29 | H/W Hanang | 70 | H/Mji Kibaha | 111 | H/W Songea |
| 30 | H/Mji Handeni | 71 | H/W Kibiti | 112 | H/M Songea |
| 31 | H/Mji Ifakara | 72 | H/W Kibondo | 113 | H/W Madaba |
| 32 | H/W Igunga | 73 | H/M kigamboni | 114 | H/W Mafia |
| 33 | H/W Ikungi | 74 | H/W Kilindi | 115 | H/Mji Mafinga |
| 34 | H/M Ilala | 75 | H/W Kilolo | 116 | H/W Magu |

| Na. | Jina la Halmashauri | Na. | Jina la Halmashauri | Na. | Jina la Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 35 | H/W Ileje | 76 | H/W Kilombero | 117 | H/Mji Makambako |
| 36 | H/M Ilemela | 77 | H/W Kilosa | 118 | H/W Makete |
| 37 | H/W Iramba | 78 | H/W Kilwa | 119 | H/W Malinyi |
| 38 | H/W Mufindi | 79 | H/M Kinondoni | 120 | H/W Manyoni |
| 39 | H/W Muheza | 80 | H/W Kisarawe | 121 | H/W Masasi |
| 40 | H/W Muleba | 81 | H/W Kishapu | 122 | H/Mji Masasi |
| 41 | H/W Musoma | 82 | H/W Kiteto | 123 | H/W Maswa |
| 124 | H/W Mbarali | 139 | H/W Morogoro | 153 | H/W Tabora |
| 125 | H/Jiji Mbeya | 140 | H/M Morogoro | 154 | H/W Tandahimba |
| 126 | H/W Mbeya | 141 | H/W Moshi | 155 | H/Jiji Tanga |
| 127 | H/Mji Mbinga | 142 | H/M Moshi | 156 | H/W Tarime |
| 128 | H/W Mbozi | 143 | H/W Mpanda | 157 | H/Mji Tarime |
| 129 | H/W Mbulu | 144 | H/M Mpanda | 158 | H/M Temeke |
| 130 | H/Mji Mbulu | 145 | H/W Mpimbwe | 159 | H/Mji Tunduma |
| 131 | H/W Meatu | 146 | H/W Mpwapwa | 160 | H/W Tunduru |
| 132 | H/W Missenyi | 147 | H/W Msalala | 161 | H/M Ubungo |
| 133 | H/W Mkalama | 148 | H/W Mtwara | 162 | H/W Ulanga |
| 134 | H/W Mkinga | 149 | H/M Mtwara | 163 | H/W Urambo |
| 135 | H/W Mkuranga | 150 | H/W Songwe | 164 | H/W Ushetu |
| 136 | H/W Mlele | 151 | H/W Sumbawanga | 165 | H/W Uvinza |
| 137 | H/W Momba | 152 | H/M Sumbawanga | 166 | H/W Wang'ing'ombe |
| 138 | H/W Monduli | | | | |

## Kiambatisho 2.0:2: Halmashauri zenye hati yenye shaka na isiyoridhisha pamoja na misingi ya hati hizo

| | |
|---|---|
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Hati Isiyoridhisha** | |
| **1.** | **Hamashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji** |
| **i.** | **Amana/fedha ambayo haijapokelewa benki na haina viambatisho SH.TZ 219,220,242**<br>Fedha taslimu na zilizosalia Benki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 zimejumuisha kiasi cha SH.TZ 219,220,242 ambacho kilikuwa hakijapelekwa benki na wala hakikuwepo kwa mtunza fedha, na menejimenti haikuweza kutoa nyaraka na maelezo kuniwezesha kujiridhisha ukweli wa fedha hizo zilipo. |
| **ii.** | **Mali, Mitambo na Vifaa (PPE) vimeoneshwa zaidi kwa SH.TZ 12,407,891,777**<br>Maelezo ya ziada Na. 42 ya taarifa ya fedha yameonesha thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa kuwa ni SH.TZ 68,247,558,197; ingawa, mapitio yangu ya taarifa ya uthamini wa mali umebaini kwamba thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa ilikuwa SH.TZ 55,839,666,420 na hivyo kupelekea thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa kuoneshwa zaidi kwa SH.TZ 12,407,891,777. |
| **iii.** | **Thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa isiyothibitishwa SH.TZ 2,891,630,014**<br>Thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa chini ya maelezo ya ziada Na. 42 ya taarifa za fedha imejumuisha kiasi cha SH.TZ 2,891,630,014 kuwa ni thamani ya mali zilipokelewa kutoka Mpango wa Kuendeleza Majiji na Miji Tanzania (TSCP); Mali hizo ni magari, malori na mashine ya kuchimbua, buldoza na mitambo ya ujenzi wa barabara. Hata hivyo, hapakuwa na misingi ya uthamini shaji wa mali hizo ili kuniwezesha kuthibitisha thamani iliyooneshwa. Kutokuwepo kwa ufafanuzi na nyaraka za kuthibitisha thamani ya mali iliyooneshwa ni vigumu kuthibitisha endapo kiasi kilichooneshwa ni sahihi au la. |
| **iv.** | **Tofauti isiyotolewa maelezo ya thamani ya kazi za ujenzi zinazoendelea SH.TZ 1,698,670,766**<br>Thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa chini ya maelezo ya ziada Na. 42 ya taarifa za fedha imejumuisha kiasi cha SH.TZ 1,613,085,572 kikiwa thamani ya kazi za ujenzi zinazoendelea. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuweza kuendana na |

thamani ya kazi za ujenzi zinazoendelea iliyooneshwa kwenye maelezo ya ziada Na. 46 ya taarifa ya fedha ambayo ni kiasi cha SH.TZ 3,311,756,338, hivyo kupelekea uwepo tofauti isiyo na maelezo ya jumla ya SH.TZ 1,698,670,766.

**v. Fedha taslim zilizokusanywa na wakala wa kukusanya mapato hazijawasilishwa SH.TZ 17,173,700**

Ukaguzi niliofanya umebaini kuwa, fedha kiasi cha SH.TZ 4,943,400 na SH.TZ 12,230,300 zilizokusanywa kupitia mashine mbili za kukusanyia mapato (POS) ambazo zilikabidhiwa kwa Major Car Accessories (ID 20050000628) na Amri Said (ID.200500001785) kwa mtiririko huo hazikupelekwa benki wala kuonehswa katika Taarifa za Fedha za Halmashauri. Aidha, mashine hizo mbili za kukusanyia mapato hazikuweza kuthibitishwa uwepo wake. Kwa hiyo, thamani ya wadaiwa wa Halmashauri katika taarifa zake za fedha imeoneshwa pungufu kwa SH.TZ 17,173,700.

**vi. Wadaiwa wa maduhuli kwenye Mfumo wa Taarifa ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Serikali za Mitaa (LGRCIS) ambao hawakuingizwa kwenye taarifa za fedha SH.TZ 709,944,308**

Mapitio ya orodha ya wadaiwa kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Serikali za Mitaa (LGRCIS) ya tarehe 29 Juni, 2017 umebaini kuwa, kulikuwa na bakaa ya kiasi cha SH.TZ 709,944,308 ambacho hakijawasilishwa Halmashauri kutoka kwa wakusanyaji mapato walioajiriwa na kupewa mashine za kukusanyia mapato. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kiasi hicho cha mapato hakijawasilishwa na hakijaoneshwa wala kutolewa maelezo kwenye taarifa ya fedha.

**vii. Malipo ya posho yenye nyaraka pungufu SH.TZ 71,465,000**

Malipo ya posho kiasi cha SH.TZ 71,465,000 yamejumuishwa katika matumizi ya mwaka ya Halmashauri. Sikuweza kupata nyaraka husika au ufafanuzi kuthibitsha uhalali na usahihi wa matumizi hayo. Kwa hiyo, ilikuwa vigumu kujiridhisha kama kiasi hicho cha fedha kilioneshwa kwa usahihi na kilitumika kwa shughuli zilizoidhinishwa na Halmashauri.

**viii. Fedha za ruzuku za maendeleo kwa Serikali za Mitaa (LGCDG) kumetumika kwa shughuli zisizofahamika SH.TZ 133,312,200**

| | |
|---|---|
| | Katika mwaka wa ukaguzi, Halmashauri ilipokea kiasi cha SH.TZ 271,165,000 kutoka Hazina kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo zilizopangwa kutekelezwa kupitia fedha za ruzuku za maendeleo kwa Serikali za Mitaa. Hata hivyo, nilibaini kuwa menejimenti ya Halmashauri ilibadili matumizi ya fedha hizo kiasi cha SH.TZ 133,312,200 kwenda kwenye shughuli zisizofahamika ambazo hazikupangwa kwenye bajeti ya fedha za ruzuku za maendeleo kwa Serikali za Mitaa. Hivyo, mawanda ya ukaguzi wa matumizi hayo yalikwazwa. |
| **ix.** | **Tofauti ya takwimu linganifu kwenye taarifa ya fedha**<br>Mapitio ya taarifa ya fedha yamebaini kwamba, kuna tofauti kubwa kati ya takwimu linganifu za mwaka unaoshia tarehe 30 Juni, 2016 na zile zilioneshwa kwenye mwaka husika unaoshia tarehe 30 Juni, 2017. Hakuna marekebisho ya taarifa ya fedha ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 yaliyofanyika kurekebisha tofauti hiyo. |
| **x.** | **Kutosahihishwa kwa makosa ya mwaka uliopita**<br>Kiwango cha 3 Aya 47 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS 3), inahitaji marekebisho ya makosa makubwa ya kipindi kilichopita yafanyike kwenye kipindi husika katika seti ya kwanza ya Taarifa za Fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi baada ya makosa hayo kugundulika. Kinyume na matakwa ya viwango tajwa, takwimu za kulinganisha kwenye taarifa ya fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 zimejumuisha makosa ya kipindi kilichopita ambayo hayakurekebishwa. Hii inajumuisha Mali, Mitambo na Vifaa kuoneshwa pungufu kwa SH.TZ 380,000,000 na kuoneshwa pungufu kwa bakaa ya ruzuku ya matumizi ya kawaida kwa SH.TZ 3,115,351,810. Kutokana na kukosekana kwa marekebisho, Mali/mtaji iliyooneshwa kwenye taarifa za fedha za Halmashauri kwa tarehe 1 Julai, 2016 na twakwimu zake za kulinganisha zilipotoshwa. |
| **2.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma** |
| **i.** | **Uwasilishaji usio sahihi wa mali/mtaji (Net Asset/Equity) katika Taarifa ya Mizania ya hesabu ya mwaka unaoushia tarehe 30 Juni, 2017**<br>Kulingana na kiwango cha kwanza cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS 1), Taarifa ya Mizania ya Hesabu kwa taasisi za Umma inatakiwa kufafanua Mali/mtaji kama mjumuisho wa mtaji ulichangiwa, jumla ya faida/hasara iliyojumuishwa na akiba. Hata hivyo, Taarifa ya Mizania ya hesabu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kuishia tarehe 30 Juni, 2017 haikuandaliwa vizuri ambapo sehemu ya Mali/mtaji zilijumuisha tu faida iliyojumuishwa |

kwa mwaka wa ukaguzi ambayo ni SH.TZ 11,168,376,000 wakati ilipaswa kujumuisha, faida jumuifu kiasi cha SH.TZ 4,028,937,000; faida inayotokana na kuthaminisha mali ya SH.TZ 6,892,739 na faida ya mwaka ambayo ni SH.TZ 246,699. Matokeo yake, uwasilishwaji wa Mali/mtaji katika Taarifa ya Mizania ya hesabu ni wa kupotosha.

ii. **Tofauti ya SH.TZ 5,896,523,000 kati ya bakaa ya ruzuku ya mali za kudumu iliyooneshwa kwenye taarifa ya fedha iliyowasilishwa tarehe 13 Disemba 2017 na Taarifa za Fedha zilizorekebishwa na kuwasilishwa tarahe 2 Machi 2018 haina maelezo ya ufafanuzi**

Taarifa ya Mizania ya hesabu kwa Halmashauri ya Wilaya Kigoma hadi tarehe 30 Juni, 2017 iliyopokelewa tarehe 13 Disemba 2017 imeonesha bakaa ya ruzuku ya mali za kudumu ya SH.TZ 5,913,081,000. Hata hivyo, taarifa za fedha zilizorekebishwa na kuwasilishwa tarehe 2 Machi 2018 imeonesha bakaa ya ruzuku ya mali za kudumu kuwa ni SH.TZ 11,809,604,000. Hii ilisababisha tofauti isiyokuwa na maelezo ya SH.TZ 5,896,523,000 ambayo inasababisha shaka juu ya usahihi wa bakaa iliyooneshwa.

iii. **Ongezeko lisilo sahihi kwenye takwimu linganifu ya jumla ya mali iliyooneshwa kwenye Taarifa ya Mizania ya hesabu hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 kiasi cha SH.TZ 27,082,000**

Nilibaini kuwa takwimu linganifu za jumla ya mali iliyooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizorekebishwa na kuwasilishwa tarahe 2 Machi 2018 imeongezwa kimakosa ambapo kiasi kilichooneshwa ni SH.TZ 26,334,396,000, wakati ukokotozi niliofanya utafikia kiasi cha SH.TZ 26,361,478,000 na kusababisha tofauti ya SH.TZ.27,082,000. Hivyo, kiasi linganifu cha mali/mtaji pia kimeoneshwa pungufu kwa kiasi cha SH.TZ 27,082,000 kutokana na kosa hili.

iv. **Tofauti isiyo na maelezo inayotokana na mabadiliko ya takwimu linganifu kwenye maelezo ya ziada ya taarifa ya fedha**

Mapitio ya maelezo ya ziada Na. 28 ya taarifa ya fedha kuhusu Mali, Mitambo na Vifaa yamebaini kwamba kwa mwaka 2015/2016, magari yalioneshwa katika thamani halisi ya manunuzi ya SH.TZ 1,014,438,000. Hata hivyo katika mwaka 2016/2017, thamani halisi ya magari iliyooneshwa ni SH.TZ.785,000,000 na kusababisha tofauti ya SH.TZ 229,438,000 isiyokuwa na maelezo ya ufafanuzi.

Vile vile, maelezo ya zaida Na. 40 ya taarifa ya fedha juu ya bakaa ya ruzuku ya mali za kudumu imejumuisha uchakavu jumuifu wa SH.TZ 5,201,022,000. Hata hivyo, takwimu linganifu ya uchakavu uliojumuishwa kwa kipindi husika ulikuwa SH.TZ 5,091,081,000 na kusababisha tofauti ya SH.TZ 109,941,000 isiyokuwa na ufafanuzi.

Zaidi ya hayo, mali zilizoongezeka na kuoneshwa kwenye maelezo ya ziada Na. 40 ya taarifa ya fedha ilikuwa ni SH.TZ 1,186,466,000. Hata hivyo, maelezo ya ziada Na. 28 ya taarifa ya fedha inajumuisha mali zilizoongezeka zilizopakana kupitia ruzuku ni SH.TZ 1,209,701,000 ambayo pia inaelezwa katika taarifa ya matumizi ya mali za kudumu. Kwa kuwa mali zilizoongezeka zilizopatikana kupitia ruzuku zinapaswa kuwa sawa katika maelezo ya ziada Na. 28 na Na. 40. Haikuwa wazi kwangu ni kwa jinsi gani kiasi hicho kilivyofikiwa.

**v. Ukokotozi usio sahihi wa bakaa kati ya faida ya mwaka na mtaji kwa kipindi kinachoishia 30 Juni, 2017 SH.TZ 3,250,003,000**

Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji kwa mwaka unaoishia 30 Juni, 2017 imeonesha salio anzia kati ya faida ya mwaka na mtaji wa SH.TZ 4,028,937,000 wakati faida ya mwaka ni SH.TZ 246,699,000 ambayo inaleta jumla ya SH.TZ 4,275,636,000. Ingawa, bakaa kati ya faida ya mwaka na mtaji imeoneshwa kuwa ni SH.TZ 1,025,633,000 na kusabibisha tofauti ya SH.TZ 3,250,003,000 ambayo haikutolewa maelezo.

**vi. Upungufu wa matumizi usiothibitishwa katika Taarifa za Fedha zilizorekebishwa SH.TZ 122,920,000**

Kwenye taarifa ya fedha ya Halmashauri ambayo iliwasilishwa tarehe 13 Desemba, 2017, Halmashauri imeonesha kiasi cha SH.TZ 439,669,000 kama gharama za mafunzo. Ingawa kwenye taarifa ya fedha iliyorekebishwa na kuwasilishwa tarehe 2 Machi, 2018 gharama za mafunzo zilipunguzwa na kufikia SH.TZ 316,749,000 bila kuwa ufafanuzi wa mabadiliko yaliyofanywa, hiyo ilisababisha kupungua kwa matumizi kwa kiasi cha SH.TZ 122,920,000

**vii. Kuoneshwa zaidi kwa Mali za Kifedha SH.TZ 27,082,000**

Maelezo ya ziada Na. 36 ya taarifa ya fedha yanafafanua Taarifa ya Mizania ya Hesabu iliyoonesha Mali nyingine za kifedha kiasi cha SH.TZ 54,164,000. Ingawa kiasi halisi cha fedha kilichowekezwa Bodi ya Mkopo ya Serikali za Mitaa hadi

kufikia tarehe 30 Juni, 2017 ni SH.TZ 27,082,000 na kusababisha kuoneshwa zaidi kwa Mali za kifedha kwa SH.TZ 27,082,000.

**viii. Kuoneshwa zaidi kwa madeni ya Halmashauri kwa kiasi cha SH.TZ 27,082,000**

Madeni ya muda mrefu yamejumuisha kiasi cha SH.TZ 27,082,000 ambacho ni kiasi kinachopaswa kumaliziwa kufikia kima cha chini cha akiba ya lazima kinachohitajika na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 ili Halmashauri iweze kustahili kukopa. Kiasi hiki hata hivyo, hakikuwa na ufafanuzi sahihi na nyaraka za kuthibitsha kuwa kiasi hicho kina vigezo vya kutambuliwa kama deni chini Kiwango cha 19 aya ya 22 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma. Kutokuwepo kwa ufafanuzi na nyaraka za kuthibitisha kiasi kinachodaiwa na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, ni vigumu kuthibitisha kuwa kiasi hicho kimeoneshwa kwa usahihi kwenye taarifa za fedha za Halmashauri.

**ix. Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakuwasilishwa na wakusanyaji SH.TZ 14,018,125**

Wadaiwa na malipo kabla ya huduma ya SH.TZ 130,972,000 yaliyooneshwa kwenye taarifa ya fedha hayajumuishi jumla ya SH.TZ 14,018,125 iliyooneshwa kama mapato ya Halmashauri na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali za Mitaa (LGRCIS) lakini mapato haya hayajawasilishwa na wakusanya mapato. Mapitio yangu ya rejesta ya wadaiwa yamebaini kuwa, wakusanya mapato hawawakuingizwa kwenye rejesta ya wadaiwa hivyo kupotosha bakaa ya Wadaiwa na malipo kabla ya huduma kwa kiasi cha SH.TZ 14,018,125.

**x. Kukosekana kwa vitabu vya kukusanyia maduhuli**

Kodi za ndani zinazofikia jumla ya SH.TZ 146,105,000 zilizooneshwa kwenye taarifa ya fedha, hazijumuishi mapato yanayotokana na kutolewa kwa vitabu saba (7) vya wazi vya kukusanyia mapato ambavyo havikuonekana kipindi cha ukaguzi. Hivyo, kukosekana kwa vitabu saba (7) vya wazi vya kukusanyia mapato imekuwa vigumu kuthibitisha usahihi na ukamilifu wa kodi za ndani zilizooneshwa kwenye taarifa ya fedha ya Halmashauri.

**3. Halmashauri ya Wilaya Pangani**

**i. Mapato mengine ya ndani yameoneshwa zaidi kwa SH.TZ 52,520,229**

- **Mkopo kwa wanawake na vijana umetambuliwa kama mapato mengine ya ndani SH.TZ 29,662,850**

Mapato mengine ya ndani chini ya maelezo ya ziada Na.16 yanajumuisha madai ya kiasi cha SH.TZ SH.TZ 32,262,850 ambayo ni madeni yasiyolipwa na vikundi vya wanawake na vijana. Deni lisilolipwa linajumuisha kiasi cha mkopo SH.TZ 29,662,850 ambacho kimetambuliwa kama mapato yasiyopokelewa kimakosa katika mwaka huu. Hii imeonesha zaidi mapato mengine ya ndani kwa SH.TZ 29,662,850. Mapato halisi ambayo hayajapokelewa ni SH.TZ 2,600,000 tu.

- **Kutothibitishwa kwa mapato mengine ya ndani ambayo hayajapokelewa SH.TZ 22,857,379**

  Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka unaoishia 30 Juni, 2017 na maelezo ya ziada Na. 16 zimeonesha mapato mengine ya ndani ya SH.TZ 575,947,618. Pia taarifa ya mtiririko wa fedha umeonesha mapato mengine ya ndani ya SH.TZ 520,827,389; hii inamaanisha kuna mapato yasiyopokelewa ya SH.TZ 55,120,229. Mapato ambayo hayajapokelewa yalioneswhwa kwenye maelezo ya ziada Na. 16 ni mkopo wa jumla wa vikundi vya wanawake na vijana ambao ni SH.TZ 32,262,850. Hii inasababisha tofauti ya SH.TZ 22,857,379 isiyothibitika kupokelewa.

**ii. Matumizi yameoneshwa zaidi kwa SH.TZ 175,216,412**

- **Kuoneshwa zaidi kwa madeni ya bidhaa na huduma yasiyolipwa SH.TZ 125,226,361**

  Mapitio ya maelezo ya ziada Na. 18, Urari wa hesabu na viambatisho vya taarifa ya fedha yamebaini kuwa, jumla ya gharama za huduma na bidhaa zimejumuisha bidhaa na huduma nyingine kiasi cha SH.TZ 495,871,462 ambazo zinahusisha madeni ya bidhaa yasiyolipwa ya SH.TZ 134,613,001. Hata hivyo, uhakiki uliofanywa kwenye orodha ya madeni ya bidhaa na huduma iliyoambatishwa umebaini kuwa SH.TZ 9,386,640 tu ndio madeni ya bidhaa na huduma yasiyolipwa kwa mwaka huu wa ukaguzi na kiasi kilichobaki cha SH.TZ 125,226,361 kilikuwa tayari kimetambuliwa kama madeni yasiyolipwa mwaka uliopita.

- **Mkopo kutoka Bodi ya Mikopo kwa Serikali za Mitaa umetambuliwa kama matumizi kwenye Taarifa ya mapato na matumizi SH.TZ 49,990,051**

  Maelezo ya ziada Na. 20 ya taarifa ya fedha, yameonesha kima cha chini cha lazima cha akiba ni SH.TZ 11,844,752 na SH.TZ 38,145,299 na kuwa na jumla ya SH.TZ 49,990,051. Huu ni mkopo ambao umeoneshwa kwenye Taarifa

ya Mizania ya Hesabu na maelezo ya ziada Na. 29 ya taarifa ya fedha; hivyo matumizi yameongezwa zaidi kwa SH.TZ 49,990,051.

iii. **Malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma Utumishi wa Umma SH.TZ 3,558,922**

Jumla ya SH.TZ 1,983,240 zililipwa kama mishahara kwa watumishi ambao utumishi wao ulisafikia ukomo kwa sababu ya utoro. Aidha, jumla ya SH.TZ 1,656,240 zililipwa kama makato ya kisheria kwa taasisi tofauti. Malipo haya yangeweza kuepukwa iwapo tu watumishi wangeondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali mara tu utumishi wao unapofikia ukomo.

iv. **Shughuli za uwekezaji zimeoneshwa pungufu kwenye Taarifa ya Mtiririko wa Fedha SH.TZ 21,460,490**

Taarifa ya Mtiririko wa Fedha kwa mwaka unaoshia tarehe 30 Juni, 2017 imeonesha kiasi cha SH.TZ 793,535,524 kama gharama ya shughuli za uwekezaji kwa ajili ya manunuzi ya Mali, Mitambo na Vifaa. Hata hivyo, mapitio yaliyofanywa kwenye maelezo ya ziada Na. 22 ya taarifa ya fedha inayoelezea matumizi ya mali za kudumu na chanzo cha fedha yameonesha, Jumla ya Mali, Mitambo na Vifaa zilizoongezeka ni SH.TZ 814,996,014 na kusababisha tofauti ya SH.TZ 21,460,490. Hivyo, gharama za Uwekezaji zilizooneshwa kwenye Taarifa ya Mtiririko wa Fedha zilipunguzwa kwa kiasi hicho.

v. **Makosa ya mwaka wa nyuma hayajarekebishwa kwenye kipindi husika yalipotokea SH.TZ 2,444,744,591**

Katika mwaka 2015/2016, Halmashauri ilionesha mali zilizoongezeka katika maelezo ya ziada Na. 36 ya taarifa ya fedha zenye thamani ya SH.TZ 2,444,744,591. Hata hivyo, marekebisho yamefanywa kwenye maelezo ya ziada Na. 32 inayohusiana na bakaa ya ruzuku ya mali za kudumu mwaka 2016/2017 badala ya mwaka husika.

vi. **Marekebisho yasiyothibitika yaliyofanywa kabla ya tarehe 1 Julai, 2015 SH.TZ 3,138,616,795**

Halmashauri ilipitisha marekebisho ya SH.TZ 3,138,616,795 kwenye Taarifa kuhusu Mabadiliko ya Mtaji. Hata hivyo, kiasi hicho hakikufafanuliwa wala kuwa na nyaraka kuthibitisha usahihi wake.

| | |
|---|---|
| **vii.** | **Kuoneshwa zaidi kwa mapato yasiyopokelewa kutokana na kuuza huduma SH.TZ SH.TZ 2,075,000**<br>Maelezo ya ziada Na. 13 na 23 ya taarifa ya fedha na urari wa mahesabu vimeonesha mapato yasiyopokelewa kutokana na kuuza huduma ya SH.TZ 5,885,000. Hata hivyo kiasi hicho kinajumuisha madai ya miaka ya nyuma ya SH.TZ 2,075,000 ambayo tayari yalishatambuliwa vipindi vilivyopita. |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye hati yenye shaka** | |
| **1.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga** |
| **i.** | **Vitabu vinane (8) vya kukusanyia maduhuli havikuonekana**<br>Vitabu vinane (8) vya kukusanyia maduhuli vilitolewa kwa wakusanyaji maduhuli mbalimbali lakini havikutolewa kwa ajili ukaguzi pale vilipotakiwa. Kwa kukosekana kwa vitabu hivi vya wazi vya kukusanyia maduhuli, nimeshindwa kuthibitisha kiasi cha maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo; hivyo mawanda ya ukaguzi yalikwazwa. |
| **ii.** | **Malipo yasiyokuwa na nyaraka za kutosha SH.TZ 67,969,400**<br>Ukaguzi wa hati za malipo na nyaraka zake husika umebaini malipo yenye thamani ya SH.TZ 67,969,400 hayakuambatanishwa na vielelezo vya kutosha kama hati za kukiri malipo, hati za madai, fomu za malipo kwa kufanya kazi muda wa ziada na taarifa za kazi walizofanya ili kuthibitisha uhalali wa malipo. |
| **2.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa** |
| **i.** | **Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakuthibitika kupelekwa benki SH.TZ 41,321,410**<br>Ukaguzi wa nyaraka za makusanyo ya maduhuli ya Halmashauri na vitabu vya kukusanyia maduhuli ulibaini, maduhuli yenye thamani ya SH.TZ 41,321,410 hayakupelekwa benki. Hii ni kinyume na Agizo 37(2-3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambayo inahitaji fedha zote zilizokusanywa kulipwa katika akaunti ya benki ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kila siku au siku ya pili ya kazi. |
| **ii.** | **Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakuwasilishwa Makao Makuu ya Halmashauri na wakusanyaji SH.TZ 11,066,500**<br>Kinyume na Agizo 37(2-3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, maduhuli kiasi cha SH.TZ 11,066,500 yalikusanywa lakini hayakuwasilishwa kwa Mtunza Fedha Mkuu wa Halmashauri. |

| | |
|---|---|
| | **Fedha zilizosalia kwenye malipo mbalimbali hazijarejeshwa benki SH.TZ 11,923,000**<br>Mapitio ya hati za malipo, orodha za walipwaji, stakabadhi, nyaraka za benki, na taarifa za benki yamebaini jumla ya SH.TZ 11,923,000 ambazo hazikulipwa baada ya kulipa posho kwa madiwani na washiriki wengine wa vikao mbalimbali, ambazo hazikurejeshwa benki. |
| **3.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe** |
| **i.**<br><br><br><br><br><br>**ii.** | **Kukosekana kwa vitabu 50 vya kukusanyia maduhuli**<br>Ukaguzi wa maduhuli, ulibaini kukosekana kwa vitabu 50 vya kukusanyia maduhuli, vitatu ni vitabu vya wazi (HW5) na vingine 47 ni vitabu vya tozo vyenye thamani ya SH.TZ 6,190,000. Kukosekana kwa vitabu vya wazi (HW5) kumenifanya nishindwe kufahamu kiasi cha fedha kilichokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo. Hii inamaanisha mawanda ya ukaguzi wangu yalikwazwa.<br><br>**Kukosekana kwa hati za malipo na malipo yenye nyaraka pungufu SH.TZ.168,743,687**<br>Katika mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri ilishindwa kuwasilisha kwa ukaguzi hati za malipo pamoja na nyaraka zake kwa matumizi yenye jumla ya SH.TZ 74,489,707. Hii ni kinyume na Agiza la 104 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aidha, kulikuwa na malipo yenye nyaraka pungufu ya SH.TZ 94,253,980 ambayo kwa ujumla yamekwaza mawanda yangu ya ukaguzi kutokana na kushindwa kuthibitisha sababu na uhalali wa malipo yaliyofanyika. |
| **4.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi** |
| **i.** | **Madeni yasiyokuwa na vielelezo SH.TZ 106,043,843**<br>Vielelezo vya bakaa ya madeni yenye thamani ya SH.TZ 106,043,843 iliyoripotiwa kwenye taarifa ya fedha havikuwasilishwa na menejimenti ya Halmashauri; hii ni kinyume na Agizo 31 (6) (h) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Kutokana na kukosekana kwa nyaraka hizo, nilishindwa kuthibitisha uhalali na usahihi wa bakaa ya madeni iliyooneshwa katika taarifa za fedha. |

ii. **Kukokesekana kwa hati za malipo SH.TZ 25,689,427**

Hati za malipo na viambatisho vyake vya SH.TZ 25,689,427 havikuwepo kwenye mafaili husika kinyume na Agizo la 104 (1) na (2) la Memoranda ya Fedha ya mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Kukosekana kwa viambatisho hivyo kulinifanya nishindwe kuthibitisha uhalali, dhumuni na aina ya malipo hayo hivyo mawanda ya ukaguzi wangu yalikwazwa.

## 5. Halmashauri ya Wilaya ya Longido

i. **Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao hawakuwa kwenye utumishi wa Umma SH.TZ 7,088,000**

Katika mwaka wa ukaguzi, jumla ya SH.TZ 4,371,364 zililipwa kama mishahara kwa watumishi waliokwishakoma utumishi wa Umma kwa sababu ya mbali mbali ambazo zinajumuisha utoro, kufukuzwa, kufariki na kustaafu. Hii ni kinyume na Agizo 79 (8) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aidha, jumla ya SH.TZ 1,656,240 zililipwa kwa taasisi tofauti kama makato ya kisheria ya wafanyakazi hao. Malipo haya yangeweza kuepukwa ikiwa wafanyakazi ambao hawako tena katika utumishi wa Umma wangeondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali mara tu wanapokoma utumishi wa Umma

ii. **Kukosekana kwa vitabu vya wazi ishirini na mbili (22) vya kukusanyia maduhuli**

Vitabu vya wazi ishirini na mbili (22) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ajili ukaguzi vilipohitajika. Hivyo kiasi cha maduhuli kilichokusanywa hakikuweza kufahamika. Kuna uwezekano mkubwa wa maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo kutumika vibaya.

iii. **Malipo batili na yasiyokuwa na manufaa SH.TZ 10,980,000**

Halmashauri ilifanya malipo batili na yasiyokuwa na manufaa ya jumla ya SH.TZ 10,980,000 yaliyotokana na kulipa fidia kwa ajili ya migogoro ya kiutumishi na kulipa zaidi posho za kujikimu kwa madiwani kwa robo ya pili ya mwaka 2016/2017. Serikali haikupata manufaa yoyote kwa kufanya matumizi haya.

iv. **Malipo yenye nyaraka pungufu SH.TZ 31,122,646**

| | |
|---|---|
| | Nimebaini hati za malipo za SH.TZ 31,122,646 hazikuwa na vielelezo husika vya malipo kinyume na Agizo la 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambayo inamtaka Mweka Hazina wa Halmashauri kudumisha mfumo bora wa uhasibu na kuhakikisha kuwa nyaraka na viambatisho vyote zinahifadhiwa kwa usalama. Kutokana na kukosena kwa nyaraka husika, uhalali wa malipo haya haukuweza kuthibitishwa |
| **v.** | **Malipo zaidi ya posho SH.TZ 19,470,000**<br>Halmashauri ilifanya malipo zaidi kwa kiasi cha SH.TZ 19,470,000 kama posho za kujikimu kwa madiwani na maafisa mbalimbali wa Halmashauri. Hii ina maana kwamba shughuli zilizopangwa zenye thamani hiyo hazikutekelezwa. |
| **6.** | **Halmashauri ya Wilaya Lushoto** |
| **i.** | **Marekebisho yasifafanuliwa katika Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji SH.TZ 646,373,899**<br>Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji ya Halmashauri imeonesha marekebisho ya kiasi cha SH.TZ 646,373,899 kwenye bakaa anzia ya faida jumuifu ili kurekebisha hasara iliooneshwa pungufu kwa mwaka 2014/2015 ambayo ilitokona na kuthaminisha mali za Halmashauri. Hata hivyo, marekebisho hayo hayajaambatishwa na jedwali husika kuthibitisha usahihi wa kiasi kilichorekebishwa. Kutokana na kutokuwepo kwa jedwali la marekebisho, nimeshindwa kuthibitisha kiasi cha Mtaji kilichooneshwa kama kilikokotolewa kiusahihi na hivyo kutolewa taarifa. |
| **ii.** | **Madeni kuoneshwa pungufu kwa kiasi cha SH.TZ 103,399,586**<br>Tarehe 22 Septemba, 2017 TARURA iliwasilisha madai ya kiasi cha SH.TZ 103,399,586 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa barua yenye kumb. Na. TAR./LDC/W/2017/2018/11 kudai fedha za matazamio zilizokatwa kutoka malipo ya wakandarasi mbalimbali ambao walifanya kazi na Halmashauri kabla ya kuuanzishwa kwa TARURA Julai, 2017. Hata hivyo, maelezo ya ziada Na. 18 ya taarifa ya fedha, yanaonesha kiasi cha SH.TZ 9,356,005 kama deni la fedha za matazamio, hii inaashiria kwamba kiasi cha SH.TZ 103,399,586 hakijajumuishwa kwenye jumla ya madeni ya SH.TZ 636,818,122. Hivyo mtaji halisi na faida jumuifu imeoneshwa zaidi kwa kiasi hicho. |
| **iii.** | **Kutooneshwa maelezo ya ziada ya fedha zilizotolewa benki zaidi ya kiasi kilichopo SH.TZ 127,903,136** |

| | |
|---|---|
| | Taarifa ya Mizania ya Hesabu imeonesha fedha zilizotolewa benki zaidi ya kiasi kilichopo kwa SH.TZ 127,903,136 chini ya madeni ya muda mfupi. Kiasi hiki kimerejewa na maelezo ya ziada Na. 10 ya Taarifa ya Fedha. Hata hivyo, maelezo ya zaida Na. 10 yaliyorejewa yanahusiana na gharama za matengenezo ya SH.TZ 2,549,384,450 ambayo yameoneshwa kwa usahihi kwenye taarifa ya Mapato na Matumizi. Kukosekana kwa maelezo ya zaida, usahihi wa Taarifa ya fedha zilizotolewa benki zaidi ya kiasi kilichopo haukuweza kuthibitishwa. |
| **7.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Rombo** |
| **i.** | **Malipo yasiyokuwa na vielelezo SH.TZ 110,561,833**<br>Halmashauri ilifanya matumizi ya kiasi cha SH.TZ 110,561,833 ambayo vielelezo vyake sahihi havikuwasilishwa, vielelezo hivyo ni hati za malipo, hati za madai na stakabadhi ya kukiri malipo. Hivyo, ilikuwa vigumu kujiridhisha kuhusu aina na uhalali na kama matumizi yaliyofanywa yalikuwa kwa shughuli za Halmashauri<br><br>**ii. Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki SH.TZ 13,330,000**<br>Ukaguzi wa kumbukumbu za makusanyo ya Halmashauri na vitabu vya kukusanyia mapato umebaini kuwa, maduhuli ya kiasi cha SH.TZ 13,330,000 hayakupelekwa benki. Hii ni kinyume na Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. |
| **iii.** | **Malipo yasiyostahili kutoka kwenye akaunti ya Amana SH.TZ 39,692,000**<br>Jumla ya SH.TZ 39,692,000 ililipwa kutoka akaunti ya amana kugharamia shughuli za kawaida za Halmashauri. Hakuna ushahidi ulitolewa kuthibitisha kuwa fedha za shughuli hizo zilihifadhiwa kwenye akaunti ya amana au marekebisho yamefanywa kuyatambua matumizi hayo kwenye taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri. Hii imesbabisha kuoneshwa pungufu kwa matumizi kwenye taarifa ya mapato na matumizi kwa kiasi hicho. |
| **8.** | **Halmashauri ya Manispaa Bukoba** |
| **i.** | **Kushindwa kuthibitisha umiliki wa majengo na ardhi SH.TZ 2,198,000,000**<br>Taarifa ya fedha imejumuisha mali zenye thamani ya SH.TZ 2,198,000,000 ambazo Halmashauri ilizipata kwa kuhamishwa umiliki wa shule ya sekondari Omumwani kutoka CCM kwenda Halmashauri ya Manispaa Bukoba bila |

| | |
|---|---|
| | gharama yoyote. Niliomba taarifa kutoka kwa menejimenti ambazo zingeniwezesha kujiridhisha juu ya umiliki wa mali zilizohamishwa na wajibu wa Halmashauri juu ya madeni yanayotokana na mali hizo; njia sahihi iliyotumika kupata thamani itakayooneshwa kwenye taarifa za fedha kulingana na mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma; na kutambuliwa kwa mali/madeni yaliyohamishwa pamoja na ufafanuzi wa mambo hayo kwenye taarifa za fedha. Sikupewa taarifa nilizoomba kuandika taarifa hii (Februari, 2018) |
| **9.** | **Halmashauri ya Mji wa Babati** |
| **i.** | **Malipo batili na yasiyo na manufaa yaliyotokana na madai ya kodi yalipwa na Halmashauri badala ya wakandarasi SH.TZ 92,448,954.72**<br>Halmashauri ilikuwa na deni la kodi la SH.TZ 92,448,954.72 lililotokana na kodi ya zuio kutoka kwa wakandarasi na wazabuni mbalimbali. Kiasi hicho chote kililipwa na Halmashauri. Hata hivyo, kati ya fedha zilizolipwa, SH.TZ 63,824,564 hazikuzuiwa na Halmashauri wakati wa kufanya malipo kwa wazabuni hivyo zililipwa kutoka kwenye akaunti ya amana na maendeleo. Hii ni kinyume na kufungu cha 83 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya 2013) ambayo inazihitaji Halmashauri kuzua kodi kutoka kwenye malipo ya watoa huduma na wazabuni. Kodi hii ya zuio ilipaswa kulipwa na watoa huduma na sio Halmashauri. Hivyo, haya ni matumizi yasiyo na manufaa na Serikali imepata hasara kwa kulipa kodi ya zuio badala ya wazabuni kufanya malipo hayo. |
| **ii.** | **Makusanyo ya maduhuli hayakuthibitika kupelekwa benki SH.TZ 6,466,000**<br>Jumla ya SH.TZ 6,466,000 zilikusanywa na wakusanya maduhuli mbalimbali lakini hazikuthibitika kupelekwa benki kama inavyohitajika na Agizo la 37 (2) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Kutokana na kukosekana kwa vielelezo vya kupelekwa benki, sikuweza kuthibitisha uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha mahuduli kilichokusanywa na kutolewa taarifa. Aidha, maduhuli ya Halmashauri yanaweza kutumiwa vibaya na kusababisha hasara ya fedha za Umma. |
| **iii.** | **Kukosekana kwa hati za malipo SH.TZ 2,373,099** |

| | |
|---|---|
| | Halmashauri ilifanya malipo yenye thamani ya SH.TZ 2,373,099 ambayo hayakuwa na hati za malipo kinyume na Agizo la 104 la Memoranda ya Fedha ya mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aina na uhalali wa matumizi yaliyofanywa na Halmashauri hayakuthibitishwa. |
| **iv.** | **Malipo kwa fedha taslimu yasiyo na vielelezo SH.TZ 5,200,000**<br>Malipo ya fedha taslimu kiasi cha SH.TZ 5,200,000 yalifanyika kwa walipwaji mbalimbali kutoka akaunti tofauti bila kuwa na nyaraka sahihi. Huku ni kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi. Hivyo, kukosekana kwa nyaraka za malipo, uhalali wa malipo haukuweza kuthibitishwa. Pia, kuna uwezekano kwamba kiasi hicho kilitumiwa kwa madhumuni binafsi |
| **v.** | **Malipo yenye nyaraka pungufu SH.TZ 9,281,300**<br>Halmashauri ililipa kiasi cha SH.TZ 9,281,300 bila ya kuwa na vielelezo au kuwa na nyaraka pungufu. Kokosekana kwa nyaraka za malipo, uhalali wa matumizi haukuwezwa kuthibitishwa. |
| **10.** | **Halmashauri ya Manispaa ya Tabora** |
| **i.** | **Madeni yameoneshwa pungufu kwenye taarifa ya fedha SH.TZ 93,746,020**<br>Ukaguzi wa taarifa za fedha (Maelezo ya ziada Na. 23 ya taarifa za fedha: taarifa ya Madeni) na viambatisho vingine umebaini kuwa, Halmashauri imeonesha deni la jumla ya SH.TZ 4,857,583,953 ambalo linajumuisha SH.TZ 890,759,149 ambazo ni kiasi kisicholipwa kwa Mkandarasi Masasi Construction Ltd. Hata hivyo uchambuzi wa nyaraka zinazohusiana na deni hilo umebaini kwamba, kiasi anachodai mkandarasi hadi tarehe 30 Juni, 2017 ni SH.TZ 984,505,169 hivyo deni la kiasi cha SH.TZ 93,746,020 halijatambuliwa kwenye taarifa za fedha. |
| **ii.** | **Kukosekana kwa hati za malipo SH.TZ 20,245,690**<br>Ukaguzi wa matumizi kwa mwaka 2016/2017 ulibainisha kuwa, hati za malipo na viambatisho vyake vyenye thamani ya SH.TZ 20,245,690 havikupatikana katika makabrasha husika wala kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. kwa hiyo sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika. |
| **iii.** | **Malipo yenye nyaraka pungufu ya SH.TZ 29,035,641** |

| | |
|---|---|
| | Ukaguzi wa hati za malipo kwa mwaka wa 2016/2017 umebaini kiasi cha SH.TZ 29,035,641 kulipwa bila kuwa na viambatisho vya kutosha. Hivyo sikuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi yaliyofanyika. |
| **iv.** | **Kukosekana kwa viambatisho vya kurejeshwa masurufu ya jumla ya SH.TZ 44,368,130**<br>Niliangalia urejeshwaji wa masurufu ya kiasi cha SH.TZ 44,368,130 na kubaini kurejeshwa kwa masurufu hayo mpaka tarehe 30 June, 2017. Hata hivyo viambatisho vya kurejeshwa kwa masurufu haya havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi licha ya kuviomba mara kadhaa. Hii ni kinyume na Agizo la 104 (2) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sikuweza kuthibitisha matumizi ya fedha zilizolipwa kama masurufu. |
| **11.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe** |
| **i.** | **Tofauti isiyokuwa na maelezo kati** ya **manunuzi ya bidhaa na huduma katika ya taarifa ya mapato na matumizi na taarifa ya mtiririko wa fedha SH.TZ 187,164,254.89**<br>Taarifa ya mapato na matumizi inaonesha manunuzi ya bidhaa na huduma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 June, 2017 kuwa ni SH.TZ 2,264,182,894.33 ambayo inakinzana kwa kiasi cha SH.TZ 187,164,254.89 na kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha ambacho ni SH.TZ 2,451,347,149.22. Kiasi cha manunuzi ya bidhaa na huduma kilichooneshwa kwenye mtiririko wa fedha ni kikubwa kwa sababu Halmsahauri ililipa madeni ya nyuma. Hata hivyo, hakuna ushahidi ambao ungeniwezesha kuthibitisha tofauti hiyo ilitokana na kulipa kwa madeni; hivyo usahihi wa kiasi cha manunuzi ya bidha na huduma haukuweza kufahamika. |
| **ii.** | **Matumizi ya kawaida yalilipwa kutoka akaunti ya Amana badala ya akaunti ya matumizi mengeneyo SH.TZ 569,117,349.28**<br>Halmashauri ililipa jumla ya SH.TZ 569,117,349.28 kutoka akaunti ya amana kugharamia matumizi mbalimbali ya kawaida. Kiasi hicho hakikuidhinishwa na Kamati ya Fedha kwa kuwa matumizi hayo hayakuwa kwenye bajeti. Aidha miamala hii haikuwekwa kwenye msimbo wa matumizi husika kulingana na mifumo ya Epicor. Kwa hiyo, kiasi cha SH.TZ 569,117,349.28 hakikujumuishwa kwenye jumla ya matumizi yaliyooneshwa kwenye taarifa ya mapato na matumizi, na matokeo yake faida ya mwaka iliyoripotiwa haikuwa sahihi. |

| 12. | Halmashauri ya Wilaya ya Meru |
|---|---|
| i. | **Upungufu wa nyaraka za malipo yenye jumla ya SH.TZ 29,181,454**<br>Nimebaini hati za malipo za SH.TZ 29,181,454 hazikuambatishwa na nyaraka husika za malipo kinyume na Agizo la 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambalo linamtaka Mweka hazina kudumisha mfumo bora wa uhasibu na kuhakikisha nyaraka zote zinahifadhiwa kwa usalama. Kukosekana kwa viambatisho hivyo kulinifanya nishindwe kuthibitisha uhalali matumizi hayo. |
| ii. | **Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki SH.TZ 36,267,082**<br>Halmashauri ilishindwa kuthibitisha kupelekwa benki kwa maduhuli ya kiasi cha SH.TZ 36,267,082 yaliyokusanywa. Hii ni kinyume na Agizo la 37 (3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Kutokuwepo kwa nyaraka za kupeleka benki fedha taslim iliyokusanywa, uhalali na usahihi wa maduhuli yalioonеshwa kwenye taarifa ya mapato na matumizi haukuthibitishwa. Aidha, mapato ya Halmashauri yanaweza kutumiwa vibaya na kuwa upotevu wa fedha za umma. |
| iii. | **Malipo ya mishahara yaliyolipwa kwa watumishi waliokoma Utumishi wa Umma SH.TZ 128,044,000**<br>Katika mwaka wa fedha uliokaguliwa, jumla ya SH.TZ 66,438,474.28 zililipwa kama mishahara kwa watumishi waliokwishakoma utumishi kwa sababu ya utoro, kufukuzwa, kufariki na kustaafu. Hii ni kinyume na Agizo 79 (8) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aidha, jumla ya SH.TZ SH.TZ 61,605,525.72 zililipwa kama makato ya kisheria kwa taasisi tofauti. Malipo haya yangeweza kuepukwa ikiwa watumishi ambao hawako tena katika utumishi wa Umma wangeondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali mara tu wanapokoma utumishi wa Umma. |
| iv. | **Malipo ya kodi ya ongezeko la thamani kwa mzabuni asiyesajiliwa SH.TZ 10,340,850**<br>Halmashauri ililipa jumla ya SH.TZ 67,790,000 ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani kwa ajili manunuzi ya samani za ofisi. Hata hivyo imebainika kwamba, mzabuni ambaye amelipwa malipo pamoja na kodi ya ongezeko la thamani sio mzabuni aliyesajiliwa kwa kodi ya ongezeko la thamani. Zaidi ya hayo, taarifa kutoka TRA ilibainisha kuwa namba ya utambulisho wa mlipa kodi 105-746-644 iliyo kwenye ankara ya mzabuni Na. 0815 haikuwa inatumika tena na kiasi |

| | |
|---|---|
| | cha kodi ya ongezeko la thamani havikuwasilishwa TRA. Serikali ilipoteza SH.TZ 10,340,850 kwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani kwa mzabuni asiyestahili.<br><br>**v. Malipo zaidi ya posho vikao SH.TZ 6,791,000**<br>Halmashauri ililipa kiasi cha SH.TZ 50,000 kama posho ya kikao kila mtu wakati wa mikutano ya madiwani kinyume na waraka Na. PM/P/1/567/59 wa tarehe 16 Agosti 2012 ambao umeeleza kuwa posho ya vikao vya madiwani ni SH.TZ 40,000 kwa mtu; hivyo kusababisha malipo zaidi ya posho kiasi cha SH.TZ 6,791,000 ambacho kingeweza kuepukwa ikiwa kiwango sahihi kingetumika.<br><br>**vi. Malipo ya posho ya vikao kwa wajumbe ambao hawakuhudhuria vikao SH.TZ 2,100,000**<br>Nilibaini kuwa Halmashauri ilifanya malipo ya posho ya vikao kwa wajumbe ambao hawakuhudhuria vikao kama inavyoonesha daftari la mahudhurio. Haya ni matumizi mabaya ya makusudi kwa fedha za Serikali ambayo yamesababisha hasara ya SH.TZ 2,100,000.<br><br>**vii. Kukosekana kwa vitabu vitatu (3) vya kukusanyia maduhuli**<br>Vitabu vya wazi vitatu (3) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwangu kwa ukaguzi vilipohitajika; Hivyo kukosekana kwa vitabu hivyo nilishindwa kuthibitisha maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo. Kuna uwezekano mkubwa maduhuli yalikusanywa kupitia vitabu hivyo kutumika vibaya. |
| **13.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe** |
| | **i. Kukosekana kwa vitabu sita (6) vya kukusanyia maduhuli**<br>Vitabu vya wazi sita (6) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ukaguzi. Hivyo kutokana na kukosekana kwa vitabu hivyo nilishindwa kuthibitisha usahihi wa maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo. Kuna uwezekano mkubwa wa maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo kutumika vibaya.<br><br>**ii. Kukosekana kwa hati za malipo SH.TZ 31,368,750** |

| | |
|---|---|
| | Halmashari ilifanya malipo yenye thamani ya SH.TZ 31,368,750 ambayo hati zake za malipo na vielelezo havikupatikana kinyume na Agizo la 104 la Memoranda ya Fedha ya mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Hivyo nilishindwa kuthibitisha sababu na uhalali wa malipo yaliyofanyika. |
| **iii.** | **Kutotambua thamani ya uchakavu kwa mali isiyoshikika SH.TZ 24,060,000**<br>Halmashauri ina Mali isiyoshikika yenye thamani ya SH.TZ 60,150,000; kutokana na sera ya uhasibu ya Halmashauri, ilikadiriwa mali hii kudumu kwa miaka mitano (5); hivyo kiwango cha kushuka thamani kwa mwaka kilipaswa kuwa ni SH.TZ 12,030,000. Hata hivyo Halmashauri haikutambua kushuka kwa thamani kwa kiasi cha SH.TZ 24,060,000 kwenye faida au hasara kwa muda wa miaka miwili. |
| **14.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Siha** |
| **i.** | **Maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu batili vya leseni za biashara na vileo SH.TZ 5,834,000**<br>Nilibaini kuwa, hakukuwa na kumbukumbu ya vitabu viwili vya leseni kwenye rejesta ya vitabu vya stakabadhi za kukusanyia maduhuli. Pia hakukuwa na maelezo ya maduhuli yaliyokusanywa kutokana na kwa leseni za biashara 64 zilizotolewa kwa jumla ya SH.TZ 4,910,000. Hii inaashiria kwamba vitabu vya leseni vyenye Na. 2180301-2180400 na Na. 2179001-2179100 ni vitabu batili na vilitumika kutoa leseni kwa wamiliki wa biashara wakati mapato yake yalipokelewa na maafisa husika kwa faida zao binafsi.<br><br>Pia, leseni za vileo ishirini na saba (7) zilitolewa kutoka kwenye vitabu vitano (5) lakini hapakuwa na kumbukumbu kwenye rejesta ya vitabu vya stakabadhi za kukusanyia maduhuli wala ushahidi wa mapato yaliyokusanywa. Hii inaashiria kwamba, vitabu vya leseni vyenye Na. 1001 - 1050, 1351 - 1400, 1851 - 1900, 4950 - 4500 na 3000 – 3050 ni batili na maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo yametumika vibaya. |
| **ii.** | **Vitabu kumi na moja (11) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi**<br>Vitabu kumi na moja (11) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi pale vilipohitajika. Hivyo, maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo hayakuweza kutambulika. Kuna uwezekano wa matumizi mabaya ya mapato ya Halmashauri kwenye sehemu za kukusanyia. |

**iii. Vitabu vitatu (3) vya leseni za biashara havikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi**

Kitabu kimoja (1) cha leseni za biashara kilichotolewa kwa Halmashauri hakikupatikana na hapakuwa na kumbukumbu ya kitabu hicho kwenye rejesta ya vitabu vya stakabadhi za kukusanyia maduhuli. Aidha, vitabu viwili ambavyo kumbukumbu zake zipo kwenye rejesta ya vitabu vya stakabadhi za kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi pale vilipohitajika. Kutokuwepo kwa vitabu hivi, uhalali wa utoaji wa leseni za biashara kwa wafanya biashara haukuwezwa kuthibitishwa.

**iv. Upotoshwaji wa vivuli vya leseni (Carbon slipping) kwenye ukusanyaji wa mapato ya leseni za biashara uliosababisha matumizi mabaya SH.TZ 4,933,000**

Katika ukaguzi wa leseni halisi themanini (80) nilibaini kuwa kiasi cha SH.TZ 6,158,000 kilikusanywa lakini maafisa husika wa ukusanyaji maduhuli na kutoa leseni za biashara waliandika kiasi pungufu cha SH.TZ 1,225,000 kwenye vivuli vya leseni na kupeleka benki kiasi hicho. Kwa hiyo, kiasi cha SH.TZ 4,933,000 kilitumika vibaya kutokana na udanganyifu wa vivuli vya leseni (Carbon slipping) kulikofanywa na maafisa wa Halmashauri.

**v. Mapato kutoka maeneo yaliyopangishwa hayakupelekwa benki SH.TZ 7,980,000**

Halmashauri ilikusanya kiasi cha SH.TZ 30,680,000 kama pango la jumla ya ekari 767 kwa shughuli za kilimo. Hata hivyo, kiasi cha SH.TZ 22,700,000 kilithibitika kupelekwa benki na kubaki kiasi cha SH.TZ 7,980,000. Kukosekana kwa nyaraka za kibenki na ushahidi wa kuwepo fedha taslimu, kuna uwezekano wa kiasi ambacho hakikupelekwa benki kuwa kimetumiwa vibaya na wakusanyaji mapato wa Halmashauri.

**vi. Majina na stakabadhi za uwongo zilizonukuliwa kwenye Leseni za Biashara**

Nimebaini kwamba, leseni za biashara arobaini na mbili (42) ambazo zimetolewa kwa maduka mbalimbali zilinukuliwa majina na namba za stakabadhi ambazo si za kweli na kiasi kilichooneshwa katika leseni hizo pia sio sahihi. Hii inaonyesha matumizi mabaya ya mapato ya Serikali kupitia udanganyifu wa leseni za Biashara.

**vii. Leseni za biashara zimetolewa bila kuoneshwa kiasi kilicholipwa**

| | |
|---|---|
| | Nimebaini kwamba, leseni za biashara kumi na moja (11) zilitolewa kwa maduka mbalimbali bila kuonesha kiasi cha mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye leseni husika, kwa upande mwingine ilibainika kuwa leseni moja ya biashara ilitolewa bila maelezo yoyote yalioandikwa kwenye nakala iliyobaki kwenye kitabu cha leseni. Kutoa leseni ya biashara bila kuonesha kiasi cha mapato kwenye nakala ya leseni inayobaki kwenye kitabu inaonesha matumizi mabaya ya mapato ya Halmashauri. |
| **viii.** | **Kiasi kisicholipwa hakujarejeshwa kwenye akaunti SH.TZ 2,412,500**<br>Halmashauri ilibakiwa na posho zisizolipwa kiasi cha SH.TZ 2,412,500 ambazo ushahidi wa kupelekwa benki haukutolewa na fedha taslimu hazikuwepo. Fedha ya Umma inaweza kuwa zimetumika vibaya. |
| **ix.** | **Malipo ya posho kwa maafisa ambao sio waajiriwa wa Halmashauri SH.TZ 3,500,000**<br>Menejimenti ya Halmashauri ililipa Maafisa wa ukaguzi elimu posho kiasi cha SH.TZ 2,600,000 baada ya kujaza fomu za kudai posho za Halmashauri. Mapitio ya orodha ya malipo ya mishahara na tange ya watumishi yamebaini kwamba hapakuwa na Maafisa wa Ukaguzi katika Halmashauri. Aidha menejimenti ya Halmashauri ililipa kiasi cha SH.TZ 900,000 kwa Mkaguzi Mkuu Elimu wa Wilaya kama posho za simu kutoka mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 wakati mlipwaji hakuwa anastahili malipo hayo, hivyo kufanya jumla ya SH.TZ 3,500,000 kulipwa kwa maafisa ambao si watumishi wa Halmashauri. Haya ni matumizi yasiyofaa ambayo yalisababisha kuoneshwa zaidi kwa kiasi cha ujira, mishahara, na stahili nyinginezo za watumishi kwa SH.TZ 3,500,000. |
| **15.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Handeni** |
| **i.** | **Malipo ya mishahara yaliyolipwa kwa watumishi waliokoma Utumishi wa Umma SH.TZ 3,845,032**<br>Katika mwaka wa fedha uliokaguliwa, jumla ya SH.TZ 2,188,792 zililipwa kama mishahara kwa watumishi waliokwishakoma utumishi kwa sababu ya utoro, kufukuzwa, kufariki na kustaafu. Hii ni kinyume na Agizo 79 (8) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aidha, jumla ya SH.TZ 1,656,240 zililipwa kama makato ya kisheria kwa taasisi tofauti. Malipo haya yangeweza kuepukwa ikiwa wafanyakazi ambao hawako tena katika utumishi wa Umma wangeondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali mara tu wanapokoma utumishi wa Umma. |

| | |
|---|---|
| **ii.** | **Maduhuli yaliyokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali hayakupeleka benki SH.TZ 18,928,500**<br>Halmashauri ilishindwa kutoa vielelezo vya kuthibitisha kupeleka benki kiasi cha SH.TZ 18,928,500 zilizokusanywa. Hii ni kinyume na Agizo la 37 (3) la Memoranda ya Fedha ya mamlaka za Serikali za Mitaa, ya mwaka 2009. Kutokuwepo kwa vielelezo vya kupeleka benki au fedha zilizokusanywa, uhalali na usahihi wa maduhuli ya vyanzo vya ndani kilichoripotiwa katika taarifa ya fedha haikuweza kuthibitishwa. Aidha, maduhuli ya Halmashauri yanaweza kutumiwa vibaya na kuwa hasara ya fedha za umma. |
| **iii.** | **Malipo yenye nyaraka pungufu SH.TZ 84,534,100**<br>Jumla ya SH.TZ 84,534,100 zililipwa bila kuwa na viambatanisho vilivyojitosheleza. Hii ni kinyume na Agizo la 8 (2) (c) ya Memoranda ya Fedha ya mamlaka za Serikali za Mitaa, ya mwaka 2009. Kukosekana kwa viambatanisho hivyo kulinifanya nishindwe kuthibitisha uhalali matumizi hayo. |
| **iv.** | **Malipo batili na yasiyo na manufaa yanayotokana na Halmashauri kulipa madai ya kodi badala ya wazabuni SH.TZ 80,013,303**<br>Halmashauri ilitathminiwa deni la kodi la jumla ya SH.TZ 140,975,737 na Mamlaka ya Mapato ya Tanzani (TRA) kwa muda kati ya mwezi Julai 2013 na mwenzi June 2015. Deni lilihusisha kiasi cha SH.TZ 95,538,862 kama kodi ya zuio kutoka kwa wazabuni na tozo ya SH.TZ 45,436,874 kwa kutozingatia sheria za kodi. Hadi wakati wa ukaguzi Halmashuri ilishalipa kiasi cha SH.TZ 80,013,303 na deni linalobaki ni SH.TZ 60,962,434. Kwa maoni yangu malipo hayo ni malipo yasiyo na manufaa kwa kuwa hapakuwa na ushahidi wa Halmashauri kuzuia kiasi hicho kutoka kwa watoa huduma wakati wa kufanya malipo. Kodi ya zuio ilipaswa kulipwa na watoa huduma na sio Halmashauri. Kwa hiyo, haya ni malipo yasiyo na manufaa kwa Serikali kwa kuwa imelipa deni lisilopaswa kulipwa na Serikali. |
| **16.** | **Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro** |
| **i.** | **Malipo batili na yasiyo na manufaa yaliyotokana na madai ya kodi yalipwa na Halmashauri badala ya wakandarasi SH.TZ 74,387,610.70**<br>Halmashauri ililipa jumla ya SH.TZ 140,309,394.52 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama kodi ya zuio kutoka kwa wakandarasi na wazabuni mbalimbali. Hata hivyo kati ya fedha zilizolipwa, kiasi cha SH.TZ 74,309,394.52 hakikuwa |

kimezuiwa na Halmashauri wakati wa kufanya malipo kwa wakandarasi na wazabuni. Hii ni kinyume na kufungu cha 83 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya waka 2008 (kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya 2013) ambayo inazihitaji Halmashauri kuzua kodi kutoka kwenye malipo ya watoa huduma na wakandarasi. Hivyo, haya ni matumizi yasiyofaa na Serikali imepata hasara kwa kulipa kodi ya zuio badala ya wazabuni na wakandarasi kulipa kosi hiyo.

**ii. Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakuthibitika kupelekwa benki SH.TZ 7,810,700**

Jumla ya SH.TZ 7,810,700 zilikusanywa na wakusanya maduhuli lakini sikuweza kuthibitisha makusanyo hayo kupelekwa benki na makusanyo hayo hayakuwepo kwenye ofisi za Halmashauri kinyume na Agizo 37(2-3) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Kutokuwepo kwa nyaraka za benki na kutokuwepo kwa makusanyo hayo kwa mtunza fedha kumenifanya kushindwa kuthibitisha uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha maduhuli yanayotokana na vyanzo vya ndani yaliyokusanywa na kuripotiwa kwenye taarifa ya fedha. Aidha, maduhuli ya Halmashauri yanaweza kutumiwa vibaya na kuwa hasara ya fedha za umma.

**iii. Kukosekana kwa Hati za Malipo SH.TZ 1,075,000**

Halmashari ilifanya malipo ya jumla ya SH.TZ 1,075,000 ambayo hati zake za malipo na vielelezo havikupatikana kinyume na Agiza la 104 la Memoranda ya Fedha ya mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo nilishindwa kuthibitisha sababu na uhalali wa malipo yaliyofanyika.

**iv. Malipo yenye nyaraka pungufu SH.TZ 5,060,828**

Malipo ya SH.TZ 5,060,828 yalifanyika bila kuwa na viambatanisho vilivyojitosheleza. Kukosekana kwa viambatanisho hivyo kulinifanya nishindwe kuthibitisha uhalali matumizi hayo.

**v. Vitabu viwili (2) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ukaguzi**

Vitabu vya wazi viwili (2) vya kukusanyia maduhuli havikuwasilishwa kwa ukaguzi. Hivyo kukosekana kwa vitabu hivyo nilishindwa kuthibitisha kiasi cha maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo. Kuna uwezekano mkubwa maduhuli yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo kutumika vibaya.

**Kiambatisho 2.0:3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne mfululizo**

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | | | | | |
| 1 | H/Jiji Arusha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 2 | H/W Arusha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 3 | H/W Karatu | Hati inayoridhisha | Hati isiyoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 4 | H/W Longido | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 5 | H/W Meru | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 6 | H/W Monduli | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 7 | H/W Ngorongoro | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| PWANI | | | | | |
| 8 | H/W Bagamoyo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 9 | H/W Chalinze | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 10 | H/W Kibaha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 11 | H/Mji Kibaha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 12 | H/W Kibiti | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 13 | H/W Kisarawe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 14 | H/W Mafia | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15 | H/W Mkuranga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 16 | H/W Rufiji | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| DAR ES SALAAM | | | | | |
| 17 | H/Jiji Dar es Salaam | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 18 | H/M Ilala | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 19 | H/M kigamboni | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 20 | H/M Kinondoni | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 21 | H/M Temeke | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 22 | H/M Ubungo | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| DODOMA | | | | | |
| 23 | H/W Bahi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 24 | H/W Chamwino | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 25 | H/W Chemba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 26 | H/M Dodoma | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 27 | H/W Kondoa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 28 | H/Mji Kondoa | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 29 | H/W Kongwa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 30 | H/W Mpwapwa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| GEITA | | | | | |
| 31 | H/W Bukombe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 32 | H/W Chato | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 33 | H/W Geita | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 34 | H/Mji Geita | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 35 | H/W Mbogwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 36 | H/W Nyang'hwale | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| IRINGA | | | | | |
| 37 | H/W Iringa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 38 | H/M Iringa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 39 | H/W Kilolo | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 40 | H/Mji Mafinga | - | - | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 41 | H/W Mufindi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| KAGERA | | | | | |
| 42 | H/W Biharamulo | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 43 | H/W Bukoba | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 44 | H/M Bukoba | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 45 | H/W Karagwe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 46 | H/W Kyerwa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 47 | H/W Missenyi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 48 | H/W Muleba | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 49 | H/W Ngara | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| KATAVI | | | | | |
| 50 | H/W Mlele | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 51 | H/W Mpanda | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 52 | H/M Mpanda | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 53 | H/W Mpimbwe | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 54 | H/W Nsimbo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| KIGOMA | | | | | |
| 55 | H/W Buhigwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 56 | H/W Kakonko | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 57 | H/W Kasulu | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 58 | H/Mji Kasulu | - | - | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 59 | H/W Kibondo | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 60 | H/W Kigoma | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati isiyoridhisha |
| 61 | H/M Kigoma/Ujiji | Hati inayoridhisha | Hati isiyoridhisha | Hati isiyoridhisha | Hati isiyoridhisha |
| 62 | H/W Uvinza | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| KILIMANJARO | | | | | |
| 63 | H/W Hai | Hati inayoridhisha | Hati isiyoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 64 | H/W Moshi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 65 | H/M Moshi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 66 | H/W Mwanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 67 | H/W Rombo | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 68 | H/W Same | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 69 | H/W Siha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| LINDI | | | | | |
| 70 | H/W Kilwa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 71 | H/W Lindi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 72 | H/M Lindi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 73 | H/W Liwale | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 74 | H/W Nachingwea | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 75 | H/W Ruangwa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| MANYARA | | | | | |
| 76 | H/W Babati | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 77 | H/Mji Babati | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 78 | H/W Hanang’ | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 79 | H/W Kiteto | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 80 | H/W Mbulu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 81 | H/Mji Mbulu | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 82 | H/W Simanjiro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| MARA | | | | | |
| 83 | H/W Bunda | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 84 | H/Mji Bunda | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 85 | H/W Butiama | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 86 | H/W Musoma | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 87 | H/M Musoma | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 88 | H/W Rorya | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 89 | H/W Serengeti | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 90 | H/W Tarime | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 91 | H/Mji Tarime | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| MBEYA | | | | | |
| 92 | H/W Busokelo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 93 | H/W Chunya | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 94 | H/W Kyela | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 95 | H/W Mbarali | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 96 | H/Jiji Mbeya | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 97 | H/W Mbeya | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 98 | H/W Rungwe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| MOROGORO | | | | | |
| 99 | H/W Gairo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 100 | H/Mji Ifakara | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 101 | H/W Kilombero | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 102 | H/W Kilosa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 103 | H/W Malinyi | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 104 | H/W Morogoro | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 105 | H/M Morogoro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 106 | H/W Mvomero | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 107 | H/W Ulanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| MTWARA | | | | | |
| 108 | H/W Masasi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 109 | H/Mji Masasi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 110 | H/W Mtwara | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 111 | H/M Mtwara | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 112 | H/Mji Nanyamba | - | - | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 113 | H/W Nanyumbu | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 114 | H/W Newala | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 115 | H/Mji Newala | - | - | - | Hati inayoridhisha |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 116 | H/W Tandahimba | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| MWANZA | | | | | |
| 117 | H/W Buchosa | - | - | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 118 | H/M Ilemela | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 119 | H/W Kwimba | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 120 | H/W Magu | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 121 | H/W Misungwi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 122 | H/Jiji Mwanza | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 123 | H/W Sengerema | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 124 | H/W Ukerewe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| NJOMBE | | | | | |
| 125 | H/W Ludewa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 126 | H/Mji Makambako | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 127 | H/W Makete | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 128 | H/W Njombe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 129 | H/Mji Njombe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 130 | H/W Wang'ing'ombe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| RUKWA | | | | | |
| 131 | H/W Kalambo | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 132 | H/W Nkasi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 133 | H/W Sumbawanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 134 | H/M Sumbawanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| RUVUMA | | | | | |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 135 | H/W Madaba | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 136 | H/W Mbinga | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 137 | H/Mji Mbinga | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 138 | H/W Namtumbo | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 139 | H/W Nyasa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 140 | H/W Songea | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 141 | H/M Songea | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 142 | H/W Tunduru | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| SHINYANGA | | | | | |
| 143 | H/Mji Kahama | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 144 | H/W Kishapu | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 145 | H/W Msalala | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 146 | H/W Shinyanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 147 | H/M Shinyanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 148 | H/W Ushetu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| SIMIYU | | | | | |
| 149 | H/W Bariadi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 150 | H/Mji Bariadi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 151 | H/W Busega | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 152 | H/W Itilima | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 153 | H/W Maswa | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 154 | H/W Meatu | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| SINGIDA | | | | | |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 155 | H/W Ikungi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 156 | H/W Iramba | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 157 | H/W Itigi | - | - | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 158 | H/W Manyoni | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 159 | H/W Mkalama | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 160 | H/W Singida | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 161 | H/M Singida | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| SONGWE | | | | | |
| 162 | H/W Ileje | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 163 | H/W Mbozi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 164 | H/W Momba | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 165 | H/W Songwe | - | - | - | Hati inayoridhisha |
| 166 | H/Mji Tunduma | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| TABORA | | | | | |
| 167 | H/W Igunga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 168 | H/W Kaliua | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 169 | H/W Nzega | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 170 | H/Mji Nzega | - | - | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 171 | H/W Sikonge | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 172 | H/W Tabora | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 173 | H/M Tabora | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 174 | H/W Urambo | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| TANGA | | | | | |

| Mkoa | Jina la Halmashauri | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 175 | H/W Bumbuli | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 176 | H/W Handeni | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 177 | H/Mji Handeni | - | - | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 178 | H/W Kilindi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 179 | H/W Korogwe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 180 | H/Mji Korogwe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 181 | H/W Lushoto | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 182 | H/W Mkinga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 183 | H/W Muheza | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 184 | H/W Pangani | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati isiyoridhisha |
| 185 | H/Jiji Tanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

**Kiambatisho 2.0:4: Mamlaka za Serikali za Miataa yenye masuala mengine yanayoambatana na hati ya Ukaguzi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Masuala ya Msisitizo | Masuala Mingineyo | Taarifa nyinginezo | Mambo muhimu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | V | | | |
| 2 | H/W Arusha | V | | | |
| 3 | H/W Babati | V | | | |
| 4 | H/Mji Babati | V | V | | |
| 5 | H/W Bumbuli | V | | | |
| 6 | H/W Bunda | V | | | |
| 7 | H/W Busokelo | V | | | |
| 8 | H/W Chamwino | V | | V | |
| 9 | H/W Chunya | V | | | V |
| 10 | H/M Dodoma | V | | V | |
| 11 | H/W Geita | V | | | |
| 12 | H/W Hai | V | | | |
| 13 | H/W Hanang | V | V | | |
| 14 | H/W Handeni | V | | | |
| 15 | H/Mji Handeni | V | | | |
| 16 | H/W Igunga | | V | | |
| 17 | H/W Ileje | V | V | | |
| 18 | H/M Ilemela | V | | | |
| 19 | H/W Iramba | V | | | |
| 20 | H/M Iringa | | V | | |
| 21 | H/W Itilima | V | | | |
| 22 | H/W Kalambo | | V | | |
| 23 | H/W Kaliua | | | V | |
| 24 | H/W Karatu | V | | | |
| 25 | H/W Kibondo | V | | V | |
| 26 | H/W Kigoma | | | V | |
| 27 | H/M Kigoma/Ujiji | V | | V | |
| 28 | H/W Kilindi | | V | | |
| 29 | H/W Kishapu | V | | | |
| 30 | H/W Kiteto | V | | | |
| 31 | H/W Kondoa | V | | | |
| 32 | H/Mji Kondoa | | | V | |
| 33 | H/W Korogwe | V | | | |

| Na. | Jina la Halmashauri | Masuala ya Msisitizo | Masuala Mingineyo | Taarifa nyinginezo | Mambo muhimu |
|---|---|---|---|---|---|
| 34 | H/Mji Korogwe | V | V | | |
| 35 | H/W Kyela | V | | | V |
| 36 | H/W Kyerwa | V | V | | |
| 37 | H/W Lindi | | | | V |
| 38 | H/W Liwale | | V | | |
| 39 | H/W Ludewa | V | | | |
| 40 | H/W Madaba | V | | | |
| 41 | H/W Magu | V | | | |
| 42 | H/W Manyoni | | | | V |
| 43 | H/W Masasi | V | | | V |
| 44 | H/Mji Masasi | V | | | V |
| 45 | H/W Maswa | V | | | |
| 46 | H/Jiji Mbeya | V | | | |
| 47 | H/W Mbeya | V | V | | V |
| 48 | H/W Mbinga | V | | | |
| 49 | H/Mji Mbinga | V | | | |
| 50 | H/W Mbogwe | V | | | |
| 51 | H/W Mbozi | V | | | |
| 52 | H/Mji Mbulu | V | | | |
| 53 | H/W Meru | V | | | |
| 54 | H/W Mkalama | V | V | | V |
| 55 | H/W Mkinga | V | | | |
| 56 | H/W Momba | V | V | | |
| 57 | H/W Monduli | V | | | |
| 58 | H/W Morogoro | | V | | |
| 59 | H/M Morogoro | | V | | |
| 60 | H/W Mpanda | V | | | |
| 61 | H/W Msalala | V | | | |
| 62 | H/W Mtwara | V | | | |
| 63 | H/M Mtwara | V | | | |
| 64 | H/W Muleba | V | | | |
| 65 | H/W Nanyumbu | V | | | |
| 66 | H/W Newala | V | | | |
| 67 | H/Mji Newala | V | V | | |
| 68 | H/W Ngara | V | V | | |

| Na. | Jina la Halmashauri | Masuala ya Msisitizo | Masuala Mingineyo | Taarifa nyinginezo | Mambo muhimu |
|---|---|---|---|---|---|
| 69 | H/W Ngorongoro | | V | | |
| 70 | H/Mji Njombe | | V | | |
| 71 | H/W Nkasi | | | V | |
| 72 | H/W Nyang'hwale | V | | | |
| 73 | H/W Rombo | V | | | V |
| 74 | H/W Rorya | V | V | | |
| 75 | H/W Rufiji | V | | | |
| 76 | H/W Sengerema | V | | | |
| 77 | H/W Serengeti | V | | | |
| 78 | H/W Shinyanga | V | V | | |
| 79 | H/M Shinyanga | | | V | |
| 80 | H/W Siha | V | | | |
| 81 | H/W Simanjiro | | V | | |
| 82 | H/W Singida | V | | | |
| 83 | H/W Songwe | V | | | |
| 84 | H/M Sumbawanga | V | | | |
| 85 | H/Jiji Tanga | V | | | |
| 86 | H/W Ulanga | V | | | |

# 3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

## Kiambatisho 3:1:Utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya jumla

| Na. | Mapendekezo | Hali halisi ya utekelezaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyo tekelezwa | Yanayoendelea kutekelezwa | Yasiyo tekelezwa |
| 1. | Mapendekezo ya miaka ya nyuma ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa | | √ | |
| 2. | Makosa katika Mchakato wa Bajeti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa | | √ | |
| 3. | Tathmini ya mfumo wa uthibiti wa Ndani na Masuala ya Utawala | | √ | |
| 4. | Udhaifu katika usimamizi wa mapato kutoka vyanzo vya mapato ya Halmashauri | | √ | |
| 5. | Udhaifu katika usimamizi wa raslimali fedha | | √ | |
| 6. | Udhaifu katika usimamizi wa raslimali watu | | √ | |
| 7. | Udhaifu katika usimamizi wa matumizi | | √ | |
| 8. | Udhaifu katika usimamizi wa mali | | | √ |
| 9. | Kutokufuata Sheria za manunuzi | | | √ |
| 10. | Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo | | √ | |
| 11. | Mapungufu yaliyobainika wakati wa uchaguzi mkuu uliofanyika Octoba,2015 | | | √ |
| 12. | Mapunguzi katika usimamizi wa fedha za ruzuku zilizotumwa shuleni moja kwa moja | | | √ |
| 13. | Kukosekana kwa mpango endelevu wa ukamilishaji wa miradi ya maendeleo | | √ | |
| 14. | Changamoto zitokanazo na uchangiaji toka kwenye mapato ya ndani kwa Halmashauri | | | √ |
| **Jumla** | | **0** | **9** | **5** |

**Kiambatisho 3:2: Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyosalia kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

| Na. | Jina La Halmashauri | Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Mapendekezo yaliyopitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 95 | 32 | 15 | 20 | 28 |
| 2 | H/W Arusha | 169 | 66 | 4 | 33 | 66 |
| 3 | H/W Babati | 66 | 22 | 13 | 12 | 19 |
| 4 | H/Mji Babati | 87 | 21 | 17 | 15 | 34 |
| 5 | H/W Bagamoyo | 79 | 29 | 30 | 20 | 0 |
| 6 | H/W Bahi | 38 | 6 | 10 | 2 | 20 |
| 7 | H/W Bariadi | 76 | 31 | 14 | 7 | 24 |
| 8 | H/Mji Bariadi | 117 | 28 | 49 | 14 | 26 |
| 9 | H/W Biharamulo | 72 | 16 | 25 | 11 | 20 |
| 10 | H/W Buchosa | 48 | 9 | 9 | 14 | 16 |
| 11 | H/W Buhigwe | 36 | 8 | 5 | 11 | 12 |
| 12 | H/W Bukoba | 104 | 30 | 24 | 22 | 28 |
| 13 | H/M Bukoba | 63 | 13 | 16 | 12 | 22 |
| 14 | H/W Bukombe | 31 | 9 | 1 | 17 | 4 |
| 15 | H/W Bumbuli | 94 | 3 | 40 | 46 | 5 |
| 16 | H/W Bunda | 38 | 14 | 8 | 11 | 5 |
| 17 | H/W Busega | 82 | 24 | 36 | 9 | 13 |
| 18 | H/W Busokelo | 65 | 22 | 33 | 10 | 0 |
| 19 | H/W Butiama | 28 | 4 | 12 | 12 | 0 |
| 20 | H/W Chamwino | 22 | 7 | 9 | 4 | 2 |
| 21 | H/W Chato | 45 | 29 | 4 | 9 | 3 |
| 22 | H/W Chemba | 38 | 6 | 4 | 5 | 23 |
| 23 | H/W Chunya | 79 | 39 | 13 | 18 | 9 |
| 24 | H/Jiji Dar es salaam | 30 | 12 | 9 | 8 | 1 |
| 25 | H/M Dodoma | 95 | 58 | 11 | 6 | 20 |
| 26 | H/W Gairo | 59 | 15 | 27 | 0 | 17 |
| 27 | H/W Geita | 41 | 1 | 27 | 12 | 1 |
| 28 | H/Mji Geita | 51 | 28 | 16 | 3 | 4 |
| 29 | H/W Hai | 83 | 32 | 16 | 3 | 32 |
| 30 | H/W Hanang | 86 | 18 | 15 | 12 | 41 |

| Na. | Jina La Halmashauri | Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Mapendekezo yaliyopitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 31 | H/W Handeni | 80 | 33 | 7 | 27 | 13 |
| 32 | H/Mji Handeni | 36 | 21 | 12 | 2 | 1 |
| 33 | H/W Igunga | 65 | 25 | 25 | 13 | 2 |
| 34 | H/W Ikungi | 105 | 19 | 16 | 12 | 58 |
| 35 | H/M Ilala | 61 | 31 | 22 | 5 | 3 |
| 36 | H/W Ileje | 140 | 94 | 31 | 4 | 11 |
| 37 | H/M Ilemela | 220 | 46 | 57 | 91 | 26 |
| 38 | H/W Iramba | 101 | 11 | 33 | 33 | 24 |
| 39 | H/W Iringa | 85 | 50 | 11 | 0 | 24 |
| 40 | H/M Iringa | 78 | 60 | 12 | 0 | 6 |
| 41 | H/W Itigi | 29 | 8 | 8 | 10 | 3 |
| 42 | H/W Itilima | 78 | 25 | 29 | 15 | 9 |
| 43 | H/Mji Kahama | 99 | 36 | 15 | 6 | 42 |
| 44 | H/W Kakonko | 57 | 5 | 9 | 32 | 11 |
| 45 | H/W Kalambo | 149 | 54 | 27 | 62 | 6 |
| 46 | H/W Kaliua | 80 | 59 | 14 | 3 | 4 |
| 47 | H/W Karagwe | 89 | 18 | 37 | 16 | 18 |
| 48 | H/W Karatu | 220 | 17 | 18 | 152 | 33 |
| 49 | H/W Kasulu | 130 | 32 | 22 | 52 | 24 |
| 50 | H/Mji Kasulu | 9 | 6 | 1 | 2 | 0 |
| 51 | H/W Kibaha | 33 | 19 | 5 | 1 | 8 |
| 52 | H/Mji Kibaha | 49 | 10 | 13 | 13 | 13 |
| 53 | H/W Kibondo | 19 | 9 | 8 | 2 | 0 |
| 54 | H/W Kigoma | 57 | 8 | 12 | 20 | 17 |
| 55 | H/M Kigoma/ujiji | 78 | 5 | 11 | 50 | 12 |
| 56 | H/W Kilindi | 49 | 8 | 27 | 7 | 7 |
| 57 | H/W Kilolo | 80 | 49 | 19 | 0 | 12 |
| 58 | H/W Kilombero | 87 | 47 | 12 | 0 | 28 |
| 59 | H/W Kilosa | 43 | 16 | 13 | 0 | 14 |
| 60 | H/W Kilwa | 60 | 9 | 14 | 16 | 21 |
| 61 | H/M Kinondoni | 135 | 123 | 4 | 8 | 0 |
| 62 | H/W Kisarawe | 56 | 8 | 30 | 18 | 0 |
| 63 | H/W Kishapu | 154 | 45 | 4 | 84 | 21 |
| 64 | H/W Kiteto | 102 | 40 | 16 | 3 | 43 |
| 65 | H/W Kondoa | 64 | 25 | 11 | 11 | 17 |
| 66 | H/W Kongwa | 42 | 0 | 1 | 21 | 20 |

| Na. | Jina La Halmashauri | Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Mapendekezo yaliyopitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 67 | H/W Korogwe | 141 | 25 | 63 | 33 | 20 |
| 68 | H/Mji Korogwe | 65 | 6 | 17 | 26 | 16 |
| 69 | H/W Kwimba | 123 | 44 | 27 | 30 | 22 |
| 70 | H/W Kyela | 118 | 26 | 64 | 24 | 4 |
| 71 | H/W Kyerwa | 58 | 20 | 12 | 3 | 23 |
| 72 | H/W Lindi | 85 | 42 | 15 | 21 | 7 |
| 73 | H/M Lindi | 45 | 7 | 7 | 10 | 21 |
| 74 | H/W Liwale | 64 | 25 | 31 | 0 | 8 |
| 75 | H/W Longido | 162 | 15 | 26 | 76 | 45 |
| 76 | H/W Ludewa | 19 | 10 | 0 | 2 | 7 |
| 77 | H/W Lushoto | 57 | 19 | 6 | 7 | 25 |
| 78 | H/W Mafia | 70 | 0 | 19 | 47 | 4 |
| 79 | H/Mji Mafinga | 38 | 33 | 2 | 2 | 1 |
| 80 | H/W Magu | 98 | 20 | 36 | 28 | 14 |
| 81 | H/Mji Makambako | 78 | 14 | 27 | 22 | 15 |
| 82 | H/W Makete | 81 | 51 | 13 | 17 | 0 |
| 83 | H/W Manyoni | 160 | 62 | 38 | 21 | 39 |
| 84 | H/W Masasi | 59 | 6 | 13 | 32 | 8 |
| 85 | H/Mji Masasi | 50 | 7 | 16 | 27 | 0 |
| 86 | H/W Maswa | 95 | 50 | 17 | 2 | 26 |
| 87 | H/W Mbarali | 51 | 22 | 13 | 16 | 0 |
| 88 | H/Jiji Mbeya | 97 | 82 | 14 | 1 | 0 |
| 89 | H/W Mbeya | 81 | 11 | 65 | 5 | 0 |
| 90 | H/W Mbinga | 46 | 2 | 16 | 28 | 0 |
| 91 | H/W Mbogwe | 62 | 20 | 14 | 23 | 5 |
| 92 | H/W Mbozi | 62 | 22 | 1 | 30 | 9 |
| 93 | H/W Mbulu | 76 | 23 | 13 | 8 | 32 |
| 94 | H/W Meatu | 75 | 17 | 50 | 6 | 2 |
| 95 | H/W Meru | 66 | 6 | 4 | 54 | 2 |
| 96 | H/W Missenyi | 86 | 9 | 31 | 23 | 23 |
| 97 | H/W Misungwi | 140 | 8 | 40 | 72 | 20 |
| 98 | H/W Mkalama | 72 | 22 | 13 | 3 | 34 |
| 99 | H/W Mkinga | 131 | 79 | 24 | 10 | 18 |
| 100 | H/W Mkuranga | 73 | 35 | 27 | 10 | 1 |
| 101 | H/W Mlele | 34 | 0 | 23 | 0 | 11 |
| 102 | H/W Momba | 89 | 54 | 17 | 11 | 7 |

| Na. | Jina La Halmashauri | Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa | Mapendekezo yasiyotekelezwa | Mapendekezo yaliyopitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 103 | H/W Monduli | 78 | 32 | 2 | 25 | 19 |
| 104 | H/W Morogoro | 37 | 8 | 5 | 1 | 23 |
| 105 | H/M Morogoro | 23 | 5 | 17 | 0 | 1 |
| 106 | H/W Moshi | 103 | 9 | 12 | 49 | 33 |
| 107 | H/M Moshi | 56 | 4 | 4 | 37 | 11 |
| 108 | H/W Mpanda | 85 | 48 | 14 | 23 | 0 |
| 109 | H/M Mpanda | 60 | 22 | 25 | 12 | 1 |
| 110 | H/W Mpwapwa | 47 | 5 | 16 | 10 | 16 |
| 111 | H/W Msalala | 81 | 53 | 9 | 7 | 12 |
| 112 | H/W Mtwara | 58 | 15 | 6 | 34 | 3 |
| 113 | H/M Mtwara | 71 | 25 | 4 | 42 | 0 |
| 114 | H/W Mufindi | 61 | 32 | 6 | 1 | 22 |
| 115 | H/W Muheza | 111 | 24 | 68 | 12 | 7 |
| 116 | H/W Muleba | 78 | 27 | 22 | 7 | 22 |
| 117 | H/W Musoma | 52 | 5 | 4 | 41 | 2 |
| 118 | H/M Musoma | 79 | 15 | 14 | 30 | 20 |
| 119 | H/W Mvomero | 45 | 19 | 11 | 0 | 15 |
| 120 | H/W Mwanga | 81 | 12 | 14 | 34 | 21 |
| 121 | H/Jiji Mwanza | 163 | 26 | 34 | 93 | 10 |
| 122 | H/W Nachingwea | 26 | 9 | 15 | 1 | 1 |
| 123 | H/W Namtumbo | 62 | 22 | 28 | 11 | 1 |
